

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA ISHIRINI

Kikao cha Ishirini na Tisa - Tarehe 13 Julai, 2010

(Mkutano ulanza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ZifuataZo Ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Fedha na Uchumi kwa Mwaka wa Fedha, 2010/2011.

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizikaguliwa za Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wkaguzi Tanzania kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2009 [*The Annual Report and Audit Accounts of The National Board of Accountants and Auditors (NBA) Tanzania for the Financial Year ended 30th June, 2009*].

MHE. ABDALLAH O. KIGODA, MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:

Taarifa ya Kamati ya Fedha na Uchumi Kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Fedha na Uchumi kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 pamoja na maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

MHE. KABWE ZUBERI ZITTO - MSEMADI WA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI:

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Fedha na Uchumi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Bodi ya Mfuko wa Barabara kwa mwaka wa 2006/2007 na 2007/2008 [*The Annual Report and Audited Accounts of The Roads Fund Board for the Financial Years 2006/2007 and 2007/2008*]).

MASWALI NA MAJIBU

Na. 211

Wananchi Wa Nkungwe Kupatiwa Mtumbwi

MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa Wilaya ya Kigoma Vijijini walioko Kijiji cha Nkungwe wako karibu na mto mkubwa sana ambapo wakati wa masika huja sana maji. Na ka kuwa wananchi hao hushindwa kwenda mashambani kutafuta chakula na pia wengine hupoteza maisha yao kwa kuchukuliwa na maji ya mto huo wakati wanapovuka kwa miguu.

Je, kwa nini Serikali isiwaonee huruma wananchi hao na kuwapatia mtumbwi mkubwa wa kuweza kuvuka katika mto huo wakati wa masika?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sijapata Fadhili Nkayamba, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba wananchi wa Kijiji cha Nkungwe wapo karibu na mto mkubwa unaoitwa Luiche. Aidha, ni kweli kuwa mto huo unapojaa maji wakati wa masika, wananchi hao wanapata adha na shida kuvuka katika mto huo mkubwa wakienda mashambani kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa eneo hili kupitia Programu ya Sekta ya Kilimo na Umwagiliaji Wilaya (*DASIP*) wameibua mradi wa ujenzi wa daraja ili kutumika kuhudumia wananchi wengi.

Hali halisi imeonyesha kuwa daraja likijengwa litahudumia wananchi wengi zaidi badala ya kutumia mtumbwi. Katika mwaka 2009/2010 kikundi kilichoibua mradi huo kupitia *DASIP* kilipatiwa shilingi milioni 28 kuendeleza ujenzi wa daraja Hata hivyo, ujenzi haujaanza kwa sababu imeonekana kuwa gharama halisi ya ujenzi kuwa shilingi milioni 77.

Katika mwaka 2010/2011, Halmashauri kupitia Programu ya Maendeleo ya Kilimo Wilaya (*DADP*) imetenga shilingi milioni 40 ili kujenga daraja hilo. Aidha, wananchi wenyewe watachangia shilingi milioni 9. Daraja hili linategemewa kujengwa mwaka huu wa fehda 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza wananchi wa Kijiji cha Nkungwe, Kigoma Vijijini kwa kuibua mradi mzuri ambao ukikamilika utawasaidia katika maendeleo yao hususan katika masuala ya kilimo. (*Makofit*)

MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kuweza kutekeleza hayo, kwa kuweza kuwapatia milioni 28 na baadaye mwaka huu 2010/2011 watawapatia milioni 40 kwa ajili ya kujenga daraja hilo.

Kwa hiyo, napenda kumpongeza Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Jakaya Mrisho Kikwete na sasa hivi tunaenda kwa ari zaidi, nguvu zaidi na kasi zaidi ili tuweze kuleta maendeleo katika Jimbo la Kigoma Kaskazini. Kwa hiyo, ndugu zanguni hata wanawake tunaweza CCM hoyeee.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Sijapata Fadhili Nkayamba na mimi nakubaliana na Mheshimiwa Sijapata kwamba wanawake jeshi kubwa, habari ndio hiyo.

Na. 212

Uhaba Wa Eneo La Kulisha Mifugo

MHE. MCH. LUCKSON MWANJALE aliuliza:-

Kutokana na kukosekana kwa eneo la kulishia mifugo, kumekuwa ni kero kubwa kwa wananchi wa Kata ya Ilengo na Kata ya Ulenje:-

Je, kwa nini Serikali isiwaruhusu wananchi wa Kata hizo kulisha mifugo yao katika eneo ambalo liko wazi katika Milima ya Mporoto?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvu naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale, Mbunge wa Mbeya Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Ilengo inapakana na Hifadhi ya Taifa ya Kitulo na ina jumla ya ng'ombe 4,228, mbuzi 1,173, kondoo 52, nguruwe 941 na kuku 7,000. Kata ya Ulenje inapakana na Hifadhi ya Misitu ya Mlima Mporoto na ina ng'ombe 2,503, mbuzi 1,592, kondoo 135, nguruwe 646 na kuku 10,000.

Jumla ya mifugo katika Kata zote mbili zinahitaji wasatani wa hekta 8,000 za malisho.

Hata hivyo, hadi sasa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya Vijijini imetenga hekta 54.8 kwa ajili ya ufugaji, eneo ambalo halitoshelezi mahitaji halisi ya idadi ya mifugo iliyopo. Kwa kutambua kero za wafugaji, katika Bajeti ya 2010/2011, Halmashauri imetenga shilingi milioni 10 ili kuendelea na mpango wa matumizi bora ya ardhi jambo ambalo litasaidia kupunguza tatizo la eneo la malisho katika Kata tajwa na Wilaya nzima kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kero ya uhaba wa maeneo ya malisho, wafugaji wa Kata za Ilengo na Ulenje wamekuwa wakiingiza mifugo katika Hifadhi ya Kitulo na Mlima Mporoto na Hifadhi ya wanyama ya Kitulo jambo ambalo ni kinyume cha sheria ya Msitu Na.14 ya mwaka 2002 kifungu 26 (n) na sheria ya Hifadhi ya wanyama pori Na.5 ya mwaka 2009 kifungu cha 21 ambazo zote zinatakaza kuingiza mifugo katika maeneo ya Hifadhi. Kwa kuzingatia sheria hizo, haitawezekana Serikali kuwaruhusu wafugaji kuingiza na kuchungia maeneo ya hifadhi ya Mlima Mporoto na Hifadhi ya Kitulo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuhimiza Halmashauri zote nchini kutenga maeneo ya ufugaji kwa kila Kijiji ili kuondoa kero kwa wafugaji nchini. Aidha, wafugaji wanahimiza kufuga mifugo kulingana na uwezo wa ardhi na malisho, ikiwa ni pamoja na kupanda malisho katika maeneo yao ili kupunguza migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi, uharibifu wa mazingira na kuzuia kuenea kwa magonjwa ya mifugo.

MHE. MCH. LUCKSON MWANJALE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana naomba niulize swalí moja tu la nyongeza. Kwa kuwa wananchi wa Kata ya Ilungu walikuwa wanategemea kulisha mifugo yao katika eneo ambalo limechukuliwa na *TANAPA* au katika shamab lile la *Kitulo National Park*. Je, ni lini Serikali itawafidia wale wananchi kwa sababu miaka karibu mitano imepita hawajapata fidia yao na hawana mahali pa kwenda mpaka sasa hivi.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba hili tatizo mimi nalifahamu, *actually* Hifadhi ya Kitulo inaanizishwa nilikuwa katika Bodi ya *TANAPA* na tulienda pale tukazungumza na wale wananchi na ilikuwa wapewe fidia na utaratibu wa Serikali ni kwamba Hifadhi za Taifa zinapoanzishwa wale watu ambao wanakuwa katika yale maeneo huwa wanalipwa. Kwa hiyo, nina amini kwamba ni taratibu tu zainafanywa na Serikali na wananchi hawa wanatakiwa kufidiwa, naomba tu *TANAPA* ambao ndio wanahuksika wachukue hatua za haraka kufanya tathmini ili wananchi hao walipwe haki zao.

MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa swalí la msingi linahusiana na uhaba wa malisho na kwa kuwa Wilaya ya Bukombe

asilimia 40 tu ya malisho ndio linafaa kwa ufugaji, wanatumia kwa makazi na kwa Kilimo.

Wananchi wa Wilaya hususani ya Bukombe katika maeneo yaliyo mwambao na Hifadhi ya Kigosi Myowosi wanapata shida sana mahali pa kulishia mifugo yao na kwa kuwa tumepitisha sheria hapa ya malisho, Serikali inasema nini kuhusiana na maeneo na malisho katika maeneo yetu yale kwa sababu Vijiji havina uwezo wa kutenga eneo. Hili linatakiwa litengwe na Serikali. Serikali Kuu inasema nini kusaidia hapo?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu upo ambao Wizara ya Maendeleo ya Makazi imekuwa ikifanya kupima maeneo ili kuwepo na *land use plan* katika Vijiji.

Kwa sasa hivi mpaka sasa tumeshapima hekta milioni 1.4 na katika mwaka huu wa fedha wametenga tena hela kupima maeneo mengine.

Naamini sehemu kama za Bukombe ambapo kuna matatizo ya ardhi, naamini Wizara itapima ardhi ili kuweza kutenga maeneo ambayo wafugaji wanatakiwa kufuga na hasa ukizingatia ni karibuni tu mwaka huu tumeweza kuitisha sheria ya vyakula vya mifugo na malisho.

Kwa hiyo, naamini kwamba jambo litafanyiwa kazi na Serikali.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali inasema kila wakati kwamba wafugaji waoteshe nyasi. Je, ni lini Serikali italeta mbegu za nyasi na kuhamasisha wananchi na kuwafundisha kuotesha katika maeneo ambayo nyasi zimeisha?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tunahimiza, kwanza ili kuboresha mifugo.

Kuna njia mbili za kufanya. Kwanza kabisa ni kuwa na malisho halafu vile vile kuwa na mifugo ambayo ni bora ambayo inapatikana kwa njia ya uhamilishaji na hii, tukitumia hii njia kwanza tutapunguza sana uharibifu wa mazingira kwa sababu ng'ombe mmoja ambaye ni bora na anapata zalisho kwa njia ya uhamilishaji anaweza kuwa na kilogram mpaka 800 ili mradi tu apate malisho mazuri na ya kutosha.

Sasa jambo hiloWizara yangu imelitambua na tunazo mbegu za kutosha, tunazalisha katika mashamba kwa mfano pale Kongwa katika Wilaya yako. Kuna mbegu nyingi tu na pale Kibaha.

Kwa hiyo, anayezihitaji mwananchi tunaomba awasiliane na Wizara yetu. Kuhusu nini cha kuwafundisha wafugaji, tunao Maafisa Ugani ambao wapo katika Vijijini vingi na angalau katika kila Kata wapo, tunaomba hao Maafisa Ugani, Mheshimiwa Mbunge

uwasiliane nao ili waweze kuwasaidia wananchi ili waweze kuwapatia elimu namna ya kupanda hizo mbegu na kupata malisho ya wanyama.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wilaya ya Mpwapwa na Kongwa kuna vituo vya utafiti wa mifugo na malisho na kwa kuwa vituo hivi vinafanya kazi katika mazingira magumu na haswa katika suala zima la utafiti wa mifugo na malisho.

Je, Naibu Waiziri atakubaliana na mimi kwamba ipo haja ya kuviimrisha vituo hivi vya Kongwa malisho na kituo cha utafiti cha Mpwapmwa kwa kuitengea Bajeti ya kutosha?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mhehsimiwa Lubeleje ambaye ni rafiki yangu na huwa tunafuatana kwenda katika vituo hivi vya utafiti. Ni kweli kwamba hali ya kifedha ama ya Bajeti, vituo hivi vilikuwa vinategewa ilikuwa ndogo. Lakini tumeendelea kuviimrisha na Mheshimiwa Lubeleje wewe ni shaidi ambaye umefuutilia bajeti.

Mwaka huu tumeongeza na tunaendelea kuboresha Bajeti ya hivyo vituo ili viweze kufanya kazi kwa hali nzuri. Kwa hiyo, ni kwamba hata mwaka huu tumetenga fedha nyingi kwa ajili ya kazi za maendeleo katika vituo hivyo na kuvinunulia vitu kama matrekta, magari vile vile na kuboresha maabara zao.

Kwa hiyo, ni kwamba Serikali inaendelea kuboresha na hasa ukizingatia kwamba hivi vituo viko katika Wizara ya Mifugo ambayo ipo katika utaratibu wa **KILIMO KWANZA**.

Na. 213

Mkakati wa kudhibiti na kuwezesha walemvu

MHE. RIZIKI OMAR JUMA aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwa na wimbi kubwa la walemvu wanaozurura barabarani na kuomba msaada ili waweze kujikimu kimaisha na kwa kuwa walemvu ni sehemu ya jamii na wakiwezeshwana wanaweza:-

Je, Serikali ina mikakati gani kabambe ya kudhibiti na kuliwezesha kundi hili ili hatimaye waweze kujajiri wenywew?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia mahitaji maalum ya kundi la watu wenyewe ulemavu na vile vile kurekebisha upungufu uiojitokeza katika sheria zilizokuwepo. Serikali imepitisha Sheria ya watu wenyewe ulemavu Na. 9 ya mwaka 2010 yaani *The Persons with Disability Act 2010* hapa Bungeni katika kikao cha 19 na kusainiwa na Mheshimiwa Rais hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Watu Wenye Ulemavu inalenga, pamoja na malengo mengine, kuwawezesha watu wenyewe ulemavu kupata fursa sawa ya ajira kama Watanzania wengine na hatimaye kuwapatia uwezo wa kujitegemea na hivyo kuondokana na tatizo la kuzurura na kuomba barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa sheria hii ambao utaanza mara baada ya kanuni kuandaliwa, utaweka taratibu na misingi ambayo itasisitiza na kuwawezesha watu wenyewe ulemavu kupata haki mbalimbali ikiwemo kupata elimu ya kujitemea, kutobaguliwa kutokana na hali zao na kupata fursa sawa katika masuala mengi ikiwa ni pamoja na uvezeshwaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua kuwa kazi ni muhimu katika Maendeleo ya binadamu na kwamba inamwawezesha mtu kujitegemea, Wizara inaendesha vyuo vinne ambavyo vinalenga kuwawawezesha watu wenyewe ulemavu wanaokosa fursa sehemu nyingine ili waweze kupata ujuzi wa fani mbalimbali na Kujitegemea kimaisha. Vyuo vitatu vinavyoendesha mafunzo kwa sasa ni Yombo (Dar es Salaam), Mirongo (Mwanza) na Singida. Matengenezo ya Chuo cha Luanzari (Tabora) yamekamilika na maandalizi yanafanyika ili kuandaa wakufunzi ili kuanza mafunzo katika mwaka huu wa 2010/2011.

Aidha, Wizara ina mipango ya kuvifufua vyuo vingine vitatu vya Masiwani (Tanga), Mbeya na Mtapika (Masasi) ambavyo vilifungwa kutokana na ufinyu wa fedha za kuviendesha. Mwaka 2010/2011 jumla ya Shs. 210,000,000/= zimetengwa ili kuanza na kuendeleza ukarabati vyuo vifuatavyo:-

Chuo cha Ufundı cha Wanawake wasioona Singida Sh. 60,000,000/=, chuo cha watu wenyewe ulemavu cha Yombo Sh. 100,000,000/= na chuo cha walemau Masiwani Tanga sh.50,000,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo yanayotolewa katika vyuo hivi ni pamoja na useremala, uunganishaji vyuma, ushonaji nguo, ukarani na kompyuta, umeme wa majumbani, ushonaji viatu, utengenezaji batiki na useketaji (ufumaji), kilimo, ufugaji na ujenzi. Aidha, kwa kuzingatia maelekezo ya sera ya Taifa ya Maendeleo na huduma kwa watu wenyewe ulemavu, Serikali kwa kushirikiana na wadau inaendelea kuhamasisha jamii ili wawatambue watu wenyewe ulemavu kama sehemu ya jamii na kuwahusisha katika mipango ya maendeleo ya jamii na taifa kwa ujumla.

MHE. RIZIKI OMAR JUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwanza naomba nichukue

nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri na kuishukuru Serikali kwa maandalizi mazuri ya kuwajali Ndugu zetu wenyе ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Sheria ipo tayari, lakini Kanuni bado hazijakuwa tayari tunazisubiri. Lakini kwa uzoefu tulionao Sheria ya UKIMWI tulichukua miaka miwili mpaka Kanuni zikapatikana. Je, ni lini Kanuni hizi ambazo zinasubiriwa na Sheria zitakuwa tayari ili ziweze kufanya kazi hasa ukizingatia kundi hili muhimu sana ambalo unalishughulikia?

Swali la pili, Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa idadi kubwa ya walemavu tunayo katika Mikoa, Wilaya na Vijiji. Lakini sina hakika kama Serikali inawatambua walemavu wote ambao tunao na kwa sababu inaandaa mazingira ya kuwaweka vizuri.

Je, ni lini Serikali itachukua hatua ya kufanya sensa ya kuwatambua walemavu wetu ambao tunao mikoani mwetu na Wilayani? Nakushukuru.

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi kwamba Kanuni tumeanza kuziandaa. Ni kweli kwamba Kanuni za Sheria ya UKIMWI bado hazijatoka, lakini nataka nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tuko katika hatua za mwisho na Kanuni hizo zinazohusiana na Sheria ya Walemavu pia na zenyewe tunazishughulikia. Naamini atakaporudi Bungeni Mungu akimjalia atakuta ziko tayari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la idadi ya watu wenyе ulemavu, ni kweli kabisa kwamba Serikali hatuna hasa ile idadi kamili na kuweza kuwatambua katika maeneo yanayohusika. Lakini katika mpango mkakati ni kwamba tumeanzisha daftari la watu wenyе ulemavu ambalo litatoa takwimu sahihi zitakazosaidia kupanga mipango yao ya maendeleo kuanzia ngazi ya Taifa hadi ngazi ya Kijiji. Kwa hiyo, tunalifanyia kazi. Ahsante. (*Makofi*)

MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa kati ya mwaka 1985 na mwaka 1994 Serikali ilikuwa imewapa mafunzo walemavu wasioona kufanya kazi ya *telephone operator* na kwa mujibu wa Sheria ya mwaka 1982 ambayo sasa imefutwa Serikali zenyewe ikawa zenyewe ikawa mwajiri mkuu wa walemavu hao. Lakini kwa bahati mbaya tulipoingia kwenye mfumo wa mtandao Ofisi nyingi zimeweka kompyuta, walemavu hao hawawezi tena kutumia kompyuta japo walikuwa wamefundishwa kuwa *telephone operators*.

Je, Serikali ina mkakati gani hawa watu ambao wanakisiwa kuwa zaidi ya 150 ambao wamekosa kazi kwa ajili ya kuingia kwenye mtandao waweze nao kupata haki au kwa kupewa semina upya kwa njia hii ya kisasa au kuweka mtandao wa kisasa wa kompyuta ambao ni *user frindly* kwa watu wasioona?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kuna baadhi ya walemvu ambao walikuwa *telephone operator* na wenyewe walikuwa wanatumia hizi simu za teknolojia ya zamani na ni kweli kabisa kwamba sasa tunaenda katika mambo ya Sayansi na Teknolojia na mambo mengine.

Nataka kusema tu ni kwamba si kweli kwamba baadhi ya wasioona hawawezi kutumia kompyuta, kama Mheshimiwa Mbunge ameweza kutembelea kwenye maonyesho mbalimbali katika upande wetu wa Ustawi wa Jamii wapo kabisa walemvu wa macho na kuna kompyuta maalum ambazo wanazitumia.

Lakini kama nilivyosema katika jibu langu nimesema mafunzo yanayotolewa katika vyuo vyetu hivi ni pamoja na ukarani na mafunzo ya kompyuta. Kwa hiyo, wale ambao walikuwa na ufundi wa kuwa *telephone operator*, kwa ile *system* ya zamani, naamini kabisa tutawafanyia programu tuweze kuona na wenyewe wanawezeshwa ili waweze kujua mambo ya kompyuta na hatimaye waweze kuajirika na kuendelea kutumia hizi nyaya za kisasa.

Na. 214

Uwepo wa madini ya Uranium na vito Liwale

MHE. HASSAN C. KIGWALILO aliuliza:-

Imebainika kuwa madini aina ya uranium na vito vyta aina mbalimbali vinapatikana huko Liwale:-

- (a) Je, ni maeneo gani kwenye Wilaya ya Liwale yenye madini hayo?
- (b) Madini aina ya Uranium yana madhara gani kwa binadamu na athari hizo zinadhibitiwa vipi?
- (c) Je, Serikali ina mkakati gani ya kutoa elimu ya tahadhari kwa wananchi wa Liwale pindi madini hayo yatakapoanza kuchimbwa ili kuwaondolea hofu wananchi?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo, Mbunge wa Liwale, lenye sehemu (a), b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Mwenyekiti, madini ya *Uranium* yanapatikana eneo la mto Madaba, Wilaya ya Liwale lenye miamba ya Karoo Kaskazini na *Seleous Reserve*.

Madini mengine yanayopatikana katika Wilaya ya Liwale ni vito vya aina ya *garnet* yanayopatikana katika eneo la Ngarumahiga, *Sapphire* katika eneo la Ngarumahinga Nambwa na *Bismuth* katika eneo la Majiorwe na *Malembo River*.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, madini ya uranium yakiwa katika hali yam bale (*ore*) ya upili (*secondary ore*) inavyopatikana katika eneo la Madaba hayana madhara kwa binadamu kwa kuwa madini yamejifungia na elementi ya oksijeni kuwa *uransium oxides* (*uraninite*, *uranyl vanadate* (*Francevillite & Natronite*) na kadhalika. Mbale ya *uranium oxide* inatenganishwa kupata metali ya *uranium*. *Uranium oxide* ndiyo inayopatikana kwa wingi hapa nchini na itahifadhiwa baadaye inategemewa kutengenezwa kuchenjuliwa na kusafirishwa nje kama (*yellow cake*).

(c) Baada ya ugunduzi wa *uranium* hapa nchini na makampuni kujitokeza katika utafutaji wa madini ya uranium, Serikali imeanza mchakato wa kutunga sheria/kanuni kwa ajili ya kusimamia shughuli za utafutaji, uchimbaji, utunzaji, usafirishaji na biashara ya madini yatoayo mionzi hatarishi. Taarifa muhimu zimekusanya kutoka katika nchi zenye uzoefu zinazochimba madini ya uranium na taasisi zinazosimamia masuala ya mionzi.

Aidha, mawasiliano na wadau mbalimbali yanaendelea zikiwemo Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia; *Tanzania Atomic Energy Commission* na kampuni zinazojihusisha na utafutaji wa uranium nchini ili kuendelea na mchakato wa kutunga sheria/Kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali imejipanga kutoa elimu kwa wataalam wake na wananchi wanaokaa katika maeneo yote yenye mashapo na uranium ili kuondoa hofu ya mionzi. Hata hivyo mwilingiliano wa mionzi kwa watu wanaofanya kazi kwenye migodi ya uranium ni kidogo na unaoweza kudhibitiwa.

MHE. HASSAN C. KIGWALILO: Ahsante kwa majibu mazuri. Kwa kuwa katika jibu lako umesema Serikali inajiardaa. Je, unaweza kutoa *time frame* ya kuonyesha lini kazi ya kutoa elimu itaanza rasmi ili wananchi wa Liwale waweze kupata elimu hiyo wasibabaike kabla?

Swali la pili, kwa kuwa *uranium* pia inahusika na mambo ya umeme na Liwale sasa hivi inapata msukosuko wa umeme hamwezi mkaona kwamba muweke mikakati ya kuona *uraniam* iliyoko Liwale ikawasaidia wana Liwale wenyewe?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye maeneo haya ambayo *uranium* imepatikana, tumeanza kufanya kazi ya kutoa elimu tayari. Isipokuwa labda niseme kwamba labda inawezekana kazi hiyo haijaanza kwa sababu elimu imezingatia yale maeneo ambayo uchimbaji unabainika kwamba utaanza kwa siku za karibuni kwa maana ya mwakani au mwaka kesho kutwa 2012.

Kwa hiyo, elimu hii imeanza Namtumbo, imeanza Bahi, na Manyoni, kwa sababu haya ndiyo maeneo ambayo kimsingi tunatarajia tutaanza uchimbaji mwaka 2012 hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu utafiti bado unaendelea wa upatikanaji wa *urani um* kwenye maeneo ya Liwale kama ilivyo maeneo ya Mbinga upande wa pili. Kwa sababu yote yako kwenye ule mwamba mmoja wa *South Selous Basin* kule, basi pale ambapo tutafikia hatua ambapo tunadhani wananchi wanahitaji elimu kwa sababu uwepo wa *uranium* kule katika hali nyingine inaweza ikaleta matatizo namna fulani.

Tutapeleka elimu hiyo japo tunaamini kwamba katika maeneo yote ya *uranium* kwa muda utakavyoruhusu tutapeleka elimu ya masuala ya *uranium* pamoja na kwamba kama ingekuwa na athari au hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la pili la mambo ya umeme. Hili tumelizungumzia nadhani mwaka huu mwanzoni wakati nikijibu swali la Mheshimiwa Mzee Philemon Ndesamburo. Tulichosema ni kwamba kwa nchi zinazoendelea mwisho wa matumizi wa *uranium* ni kwenye kuichenjua na kuifikisha kwenye hatua inayoitwa *yellow cake*.

Baada ya hapo inasafirishwa kwa sababu inabidi ichenjuliwe kwa hatua ya juu zaidi kwa *process* inayoitwa *nuclear in reachment* sasa ikishafikia hatua hiyo inatumukizwa kwenye ma-nuclear re-actor yale ndiyo unapata *nuclear fuel* ambayo inakwenda kutumika kama umeme ama kwenye matumizi yale makubwa makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala la kutengeneza *nuclear re-actor*, *nuclear re-actor* lina gharama kubwa sana, moja. Lakini la pili hata *maintenance* yake ni gharama kubwa sana na hapa Afrika ukiondoa Afrika Kusini ambao wana *nuclear re-actor* moja nadhani. Hatuna sisi *nuclear re-actors*.

Kwa hiyo, sisi wote tunaochimba huwa tunafikia hatua ya *yellow cake* na kuipeleka nje, inauzwa kama *yellow cake*, kama nishati hiyo ambayo pia biashara yake ni kubwa sana. Lakini kama ninavyosema kwa huko mbele kwa sababu huu utaalam huu wa kuzalisha umeme wa *uranium* umeanza tangu mwaka 1958 na kama ilivyo kwa teknolojia zote kadri siku zinavyokwenda tunazidi kuboresha ujuzi.

Mimi naamini kwamba na sisi nchi zinazoendelea ndani ya miaka 20, 30 tutakuwa na uwezo na utaalam wa ku-process *nuclear yellow cake* mpaka kuifikia kwenye *fuel* na kuwa na umeme wa *nuclear* kama ilivyo kwa nchi zilizoendelea kwa hivi sasa.

Na. 215

Bei ya zao la Kahawa na Chai

MHE. MWADINI ABBAS JECHA (K.n.y. MHE. SAVELINA S. MWIJAGE) aliuliza:-

Kwa kuwa wakulima katika Mkoa wa Kagera wanapata riziki zao kutokana na kilimo cha Kahawa na chai kwani mazao hayo ndiyo yamewawezesha watoto wengi kwenda shule na kwa kuwa inaeleweka kuwa Serikali imedhibiti soko la Kahawa kwa muda mrefu sasa na wakulima hawana haki ya kujadili soko huria kitu kinachowakatisha tamaa ya kuendeleza zao hilo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuangalia upya bei ya mazao hayo, kwani kwa sasa bei ya Kahawa ni kama robo ya thamani ya dola moja ya Marekani?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Savelina Silvanus Mwijage, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2008/2009 wastani wa bei ya Kahawa ya (robusta) mnadani ilikuwa dola za Kimarekani 1.49 sawa na shilingi 2,235. Kahawa ya maganda ilinunuliwa kwa shilingi 800 kwa kilo. Mwaka 2009/2010 bei ya mnadani ilikuwa dola 1.25 sawa na shilingi 1,875 na bei kwa mkulima ilikuwa shilingi 450/= bei ambayo ni zaidi ya robo ya dola moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango inayotekeliza na Serikali ili kuboresha bei ya kahawa ni pamoja na kufungua masoko ya wakulima kupitia vyama vyaya ushirika na makampuni binafsi. Aidha, mkulima anayo fursa ya kuuza kahawa yake mnadani iwapo anazalisha kahawa ya kutosha au kuuza kahawa yake moja kwa moja kwenye masoko ya nje kwa kutumia utaratibu wa *Direct Export*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango mingine ya Serikali ni kutoa bei elekezi kupitia Bodi ya Kahawa ili imsaidie mkulima kufahamu hali ya soko. Kushiriki katika maonyesho ya kikanda na kimataifa ili kuitangaza Kahawa ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu zao la chai, bei ya chini yaani (*minimum price*) ya majani mabichi ya chai hupangwa na wadau. Kwa mfano, Rungwe bei ya soko iliyopo ni shilingi 160, Mufindi shilingi 145, Lushoto shilingi 130, Karagwe shilingi 110 na Muheza shilingi 110. (*Makofii*)

Tofauti hii ya bei inatokana na tofauti ya uimara wa vyama vyaya wakulima katika kujadiliana bei na wadau. Sababu nyingine ni kwamba wakulima kuwa na ubia au (hisia) katika viwanda vyaya kusindika majani wanayozalisha kwa mfano viwanda vyaya Rungwe na Lushoto.

Kwa upande wa Mufindi, ongezeko la bei linatokana na uamuzi wa mwenye kiwanda kuongeza bei. Vyama vyaya wakulima kwa maeneo ya Karagwe na Muheza vinashauriwa kujenga umoja wenye nguvu katika kujadiliana na wenye viwanda.

MHE. MWADINI ABBAS JECHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa suala la kahawa linaonekana kuwa na fursa nyingi za soko. Lakini wengi wa wakulima wa zao hili wanalamika kwamba bei yao wanauza zao hili hairidhishi.

Je, Serikali huchukua hatua gani kuwaelimisha wakulima wa kahawa wa vijiji ili nao wawe na fursa linganifu ya kuchangamkia soko la Kahawa ili waweze kupata bei nzuri ya zao hilo?

Lakini swali la pili, kwa kuwa soko la chai linaonekana halivutii wakulima hasa kutokana na udhaifu wa vyama vyta wakulima katika kujadiliana bei ya zao hilo na wadau.

Je Serikali imechukua hatua gani kuvielimisha vyama vyta wakulima ili nao waweze kuwa na nguvu ya kimajadiliano na wadau ili hatimaye kuwe na bei nzuri ya chai hiyo waendelee kulizalisha zao hilo?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme kwamba bei ya mazao haya yanatokana na nguvu ya soko kusema kweli Serikali haipangi bei lakini kuitia Bodi ya Mazao haya ya Chai na Kahawa na mazao mengine kuitia Bodi zake zile Serikali inatoa bei elekezi kwamba tusishuke chini ya hapa, chini ya bei fulani kwa kilo au kwa kipimo fulani.

Kwa hiyo, ninachoshauri ni kwamba wadau hawa waweze kukaa na wakulima pamoja na wenye viwanda waweze kukaa na kupanga bei nzuri. Ila sasa nichukue tu mfano nzuri kwa mfano kiwanda hiki cha Mufindi mwenye kiwanda ameongeza bei ili aweze kuwapa wakulima wake, wale wakulima wanaoleta chai pale bei nzuri.

Kwa hiyo, niweze kuwashauri wale wenye viwanda kwamba ili mkulima aweze kupeleka zao bora la chai na mazao mazuri haya yaweze kwenda kwenye viwanda ni lazima wapewe bei mzuri.

Kwa hiyo, nawashauri wenye viwanda kusema kweli waweze kutoa bei nzuri lakini pia wadau wanavyokaa pale pamoja na vyama vyao waweze kwenda pale na kujadiliana vizuri kusudi waweze kuwa na bei nzuri ambayo ina manufaa kwa mkulima.

Kusema kweli elimu hii tunaitoa sisi kama Wizara kuitia Halmashauri zetu lakini kuitia kwenye Bodi zetu hizi za mazao haya kusudi mkulima aweze kupata bei nzuri.

Lakini katika viwanda vile ambavyo wenye hisa, kuna baadhi ya wakulima wenye hisa katika viwanda vile tunawashauri waweze kukaa vizuri na kupanga bei nzuri ili mkulima aweze kufanikiwa, maana siyo wakulima wote ambao wana hisa na viwanda vile, kusudi wakulima wale waweze kupata bei nzuri ya mazao haya. (*Makofii*)

Uboreshaji wa Miundombinu ya Kilimo

MHE: CASTOR R. LIGALAMA aliuliza:-

Kwa kuwa, ili KILIMO KWANZA kiweze kuwa na tija ni lazima kiendane na uboreshaji wa miundombinu ya kilimo kama vile barabara na upatikanaji wa umeme; na kuwa kuna mikoa sita ambayo inategemewa sana kwa uzalishaji wa mazao ya chakula:-

(a) Je, Serikali inafanya jitihada gani katika kuboresha barabara na kuipatia umeme Mikoa hiyo ili izalishe kwa tija?

(b) Je, Serikali itakuwa tayari kuwasaidia wakulima wa Kilombero ili waweze kupanda mpunga kitaalam kwa kufuata vipimo na kuwapatia majembe ya kupandia?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Castor Raphael Ligalama, Mbunge wa Kilombero, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa michango ya sekta nyingine za uchumi kwa sekta ya Kilimo ili kuiwezesha ikue kwa kasi itakayoiwezesha kutoa mchango unaotakiwa katika kuondoa umasikini nchini. Ndio maana dhana ya KILIMO KWANZA ikabuniwa ambapo NGUZO zake zinaainisha michango ya kila sekta katika kuendeleza sekta ya kilimo. Nguzo ya tisa ya KILIMO KWANZA, inaainisha mchango wa sekta ya miundombinu katika maendeleo ya kilimo hususan huduma za barabara, umwagiliaji, nishati na masoko.

Kutokana na azma hiyo, Serikali inatekeleza miradi mbalimbali nchini ikiwemo mikoa sita ilioainishwa kwa ajili ya uwezekano mkubwa wa kuzalisha kwa uhakika na kwa wingi mazao ya chakula.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tayari inawasaidia wakulima wa Kilombero katika kuwajengea uwezo wa kuzalisha zao la mpunga ili waongeze tija na uzalishaji. Msaada wanaopata wakulima wa Kilombero ni sehemu ya utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*ASDP*) kuitia Mipango ya Wilaya ya Kuendeleza Kilimo (*DADPs*).

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuitia mipango hiyo, Wizara inashirikiana na Halmashauri ya Kilombero kuitia Skimu ya Njagi kufundisha wakulima Kanuni Bora za kilimo cha mpunga. Wakulima 96 wa mpunga wanafaidika na mafunzo hayo. Aidha, mashamba darsa 10 ya kilimo cha mpunga yameanzishwa katika vijiji vya Miwanganini, Msolwa, Ujamaa, Chita, Merera, Mkangawalo na Zingali, ambapo jumla ya wakulima 250 wanashiriki.

Vile vile jumla ya wakulima 430 wamepatiwa mafunzo ya kuwa Wagani-Kazi wa kilimo cha mpunga na watasaidiana na wataalam wa Ugani kuendeleza kilimo hicho. (*Makofi*)

MHE: CASTOR R. LIGALAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nina shukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu Waziri, anakiri kwamba nguzo ya tisa ya KILIMO KWANZA inazungumzia kuoanisha sekta nyingine katika Maendeleo ya Kilimo. Je, Wizara itakubaliana na mimi kwamba katika hatua fulani ya kupanga mipango itabidi hizo Wizara nyingine za Miundombinu, Maji na Umwagiliaji, Viwanda Biashara na Masoko pamoja na Nishati na Madani, wakae pamoja ili kuainisha vipaumbele?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; katika Wilaya yangu ya Kilombero katika Chuo cha Katrin, kimeteuliwa kuwa *Centre of Excellence* katika utafiti wa mpunga na vile vile tunazalisha na kutoa Maafisa Ugani pale. Je, Serikali itakuwa tayari kukikarabati Chuo kile ambacho kilijengwa mwaka 1964?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Ligalama, Mbunge wa Kilombero, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku zote Serikali inapopanga Bajeti, huwa inakutana pamoja na ndio inapopanga vipaumbele vya Bajeti. Inapopanga vipaumbele vya Bajeti, tunaposema kwamba Wizara ya Kilimo inahitaji ipelekewe pembejeo kiasi fulani, Mawaziri wote wanakubaliana na Serikali kwa ujumla inakubaliana. Kwa hiyo, suala hili la kiwamba Wizara ya Miundombinu, Wizara ya Nishati na Madini wakae pamoja, kusema kweli ni kwamba wanakaa pamoja na ndio maana barabara hizo tunazozitengeneza ni kwa ajili ya kutoa mazao kutoka maeneo ya uzalishaji na kuyapeleka maeneo ya watumiaji. Kwa hiyo, inazingatiwa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti kwa mfano barabara hii inayojengwa sasa hivi inayotoka Sumbawanga kuja Tunduma, imesaidia sana katika kuhakikisha kwamba mazao yanayozalishwa kule pamoja na kusafirisha wananchi wanaokaa kule lakini mazao yanayozalishwa kule yaweze kuletwa kwenye maeneo haya mengine ya soko na maeneo Ambayo hayana chakula. Kwa hiyo, siku zote Wizara hizo zinakaa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na kukarabati chuo hiki; kusema kweli ninakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge, kwamba zoezi hili linaendelea kwa sababu ni azma yetu kwamba ifikapo 2012/2013 tuweze kukamilisha ile azma yetu na kuwa na Maafisa Ugani 15,000 kwa ngazi zote kwa maana ya kusema kwamba kwenye vijiji tunakuwa na Maafisa Ugani, kwenye Kata pamoja na kwenye Tarafa na kuwapatia vitendea kazi ili waweze kufanya kazi yao ya ugani sawasawa.

Hati za Kumiliki Nyumba Kutolewa Katika Halmashauri

MHE. DIANA M. CHILOLO aliuliza:-

Kwa kuwa, Hati ya muda mrefu ya Kumiliki nyumba au shamba hutolewa ofisi za kanda ambapo kwa Kanda ya Kati Ofisi hizo zipo Dodoma. Na kwa kuwa, wananchi wengi hawana uwezo wa fedha za nauli, malazi na chakula kwenda Dodoma kufuata Hati hizo:-

Je, ni lini Serikali itapeleka huduma hiyo karibu na wananchi katika ofisi za Halmashauri ili kuwapunguzia wananchi gharama? (*Makofi*)

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshaanza kuchukua hatua madhubuti za kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (*CCM*), Ibara ya 42(c), inayoelekeza kuwa Serikali iendelee kurahisisha taratibu za upatikanaji wa Hatimiliki za ardhi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeanzisha Ofisi sita za Ardhi za Kanda, zinazoongozwa na Makamishna Wasaidizi wa Ardhi. Ofisi hizo ni za Kanda ya Kati – Dodoma, Kanda ya Ziwa – Mwanza, kanda ya Mashariki – Dar-es-Salaam, Kanda ya Kaskazini – Moshi, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini – Mbeya na hivi karibuni imeanzhishwa Kanda ya Kusini Mashariki kwa ajili ya mikoa ya Mtwara na Lindi ambapo Ofisi ya Kanda ipo Mtwara.

Aidha, Wizara imeimarisha Ofisi za Msajili wa Hati katika Kanda zote ili shughuli ya utoaji wa Hati na kusajiliwa zifanyike katika ngazi ya Kanda.

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida mchakato wa kusajili hati za kumiliki ardhi unaanzia kwenye ngazi ya Halmashauri inayohusika ambapo muombaji wa Hati miliki hutakiwa kulipia ada ya umilikishwaji, kisha Afisa Ardhi Mteule wa Halmashauri hutayarisha hatimiliki ya kiwanja hicho na kisha kuituma kwa Kamishna Msaidizi wa ardhi wa Kanda kwa ajili ya kusainiwa na kusajiliwa katika Ofisi ya Msajili wa Hati Msaidizi wa Kanda. Maafisa hawa wawili (Kamishna wa Ardhi Msaidizi na Msajili wa Hati Msaidizi) hukaa kwenye jengo moja ili kurahisisha utoaji wa Hatimiliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu uliopo sasa haumlazimishi mwananchi kufuatilia Hati yake katika Ofisi za Kanda, kwani baada ya Hati Miliki kusajiliwa pale

kwenye Kanda, hurejeshwa kwa Afisa Ardhi Mteule Hatimiliki ili aje aichukue hapo Wilayani. Kutokana na kuanzishwa kwa Ofisi za Ardhi za Kanda, muda wa kusajili Hati umefupishwa na kuwa chini ya miezi mitatu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inayo nia ya dhati ya kusogea huduma karibu zaidi na wananchi hadi ngazi za Halmashauri, lakini kutokana na uwezo mdogo kifedha na uhaba wa wataalam katika ngazi ya Halmashauri na Kanda.

Mheshimiwa mwenyekiti, mwisho ninapenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Chilolo kwa kufuatilia kwa makini haki za wananchi wa Singida katika suala la utoaji wa Hatimiliki.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la kwanza. Kwa kuwa lengo la Serikali ni kupeleka huduma hii katika Halmashauri zote nchini. Na kwa kuwa, Halmashauri tayari zina Ofisi na tayari zina Maafisa Ardhi wateule. Je, ni fedha nyingi kiasi gani ambazo zinakwamisha zoezi hili kupelekwa kwenye Halmashauri ili wananchi waondokane na adha wanayoipata ya kusubiri Hati hizo kwa muda mrefu pamoja na kuondoa mianya ya rushwa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili. Kwa kuwa hata upatikanaji wa viwanja kuna tatizo, kwani Maafisa Ardhi hutoa kipaumbele kwa matajiri na kwa baadhi ya viongozi na wananchi wa kawaida kupata tabu ama kuombwa rushwa.

Je, Mheshimiwa Waziri analifahamu hili? Na kama analifahamu. Je, yupo tayari kutoa kauli ya utawala kwa Maafisa ardhi wenye tabia hiyo? (*Makofii*).

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Chilolo, Mbunge mwenzangu, dada yangu kutoka Mkoa wa Singida, kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la ni kwa nini huduma hii haijafika katika Halmashauri na ni kwa nini kuna upungufu wa viwanja mpaka vinatolewa kinamna namna, linaanzia pale kwenye Halmashauri penyewe. Kwa sababu ili kazi hii ifanyike ni lazima Halmashauri ziwe na wataalam, ziwe na Kasma kwa ajili ya kazi hiyo, fedha za kufanya kazi hii na ziwe na vitendea kazi. Halmashauri nyingi mambo haya hawana mpaka leo tunapozungumza, kuna Halmashauri 45 hazina Maafisa Ardhi kabisa.

Sasa hii kazi ukiipeleka kwenye Halmashauri, ataifanya nani? Halmashauri nyingi kama sio zote, haziweki fungu la Ofisi ya Ardhi, hakuna. Idara nyigine zina mafungu, Elimu ina fungu, Maji kuna fungu, Afya kuna fungu, ukija kwenye ardhi hawaweki. Liko tatizo ambalo tukishalitatua pale kwenye Halmashauri, sisi tuko tayari kupeleka huduma hii mahali hapo. Amesema Nitoe kauli ya wataalam pale kwenye Halmashauri ambao

wanagawa ardhi kwa kutumia njia zisizofaa. Jambo la kwanza ninazishauri Halmashauri, zipime viwanja vingi. Upungufu wa viwanja ndio unasabisha haya madhara mengine.

Halafu Pili, tuwasimamie hawa watumishi. Mkuu wa Mkoa wa Dar-es-Salaam, ameonyesha mfano. Jinsi ambavyo Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, unaweza ukasimamia Halmashauri inapofanya maovu ili waweze kufanya mambo mema. Kwa hiyo, mfano wa Dar-es-Salaam, uzingatiwe na ufuatwe na Wakuu wa Mikoa yote na Wakuu wa Wilaya wote, kwa sababu Halmashauri ziko kwenye himaya zao. (*Makofî*)

Na. 218

Vyuo Kuzuia Wanafunzi Kufanya Mitihani

MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI K.n.y. MHE: CHARLES M. KAJEGE aliuliza:-

Kwa kuwa, kwa muda mrefu sasa baadhi ya vyuo nchini vimekuwa vikiwazuia wanafunzi ambao hawajamaliza kulipa ada za vyuo hivyo kufanya mitihani ya kumaliza mihula au kumaliza kozi zao:-

Je, Serikali inalitambua tatizo hilo na inachukua hatua gani madhubuti?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Charles Muguta Kajege, Mbunge wa Mwibara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali inatambua tatizo la baadhi ya Vyuo kuwazuia wanafunzi ambao hawajamaliza kulipa ada za mafunzo kufanya mitihani ya kumaliza mihula au kumaliza kozi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa ulipaji ada za mafunzo umewekwa na Mabaraza na Bodi ya Vyuo husika. Aidha, utaratibu hupitishwa na kuidhinishwa na vyombo shirikishi ambavyo pia wanafunzi hushiriki. Nia ya kuweka taratibu hizi ni kuhakikisha kuwa wanafunzi wanalipa ada kama walivyowekeana mikataba ya kulipa na vyuo husika.

Kabla ya wanafunzi kudahiliwa, hutakiwa kuingia mkataba na chuo kuwa atalipa ada yote ya chuo kabla ya kuruhusiwa kuingia darasani. Serikali kwa kushirikiana na vyuo na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, imekuwa inatoa elimu kwa Umma na hasa wanafunzi juu ya umuhimu wa kulipa ada.

Aidha, Serikali imekuwa inaruhusu rufaa kwa wale wanafunzi ambao wameshindwa kabisa kulipia gharama za uchangiaji wa elimu ya juu. Ikumbukwe kuwa vyuo huendeshwa kwa kutegemea ada za wanafunzi kama mapato ya ndani.

Kutokana na ukweli kwamba gharama za utoaji elimu ya juu ni mkubwa tunaomba wananchi waikubali Sera ya uchangiaji wa elimu ya juu ili kutoa fursa kwa wanafunzi wengi zaidi kupata elimu ya juu.

MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri na yenye usafaha ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa pengine Serikali izingatie na iliangalie suala hili kwamba, mwanafunzi anapokuwa ameshasoma na amefikia kipindi cha kufanya mitihani na anazuiwa kufanya mitihani kwa sababu tu hajamalizia ada. Hasa ukizingatia kwamba hata Sera ya *CCM* inawajali sana wananchi wake. Hivyo kupitia kwa vijana hawa ambao wanasoma katika mazingira magumu na wametoka katika familia tofauti tofauti, zingine ni familia zisizokuwa na uwezo kabisa, ni kwa nini Serikali isitoe maelekezo kwenye vyuo hivi? (*Makofi*)

Wanafunzi waruhusiwe kufanya mitihani, lakini kupewa matokeo au vyeti vyao ndio sasa waweze kukamilisha suala la ada?

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri na baada ya hapo ninaomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulipaji wa ada ndio unawezesha Vyuo Vikuu na Vyuo vingine vya elimu ya juu viweze kutekeleza majukumu yao. Kila mwanafunzi anapokwenda kwenye Chuo Kikuu, anawekeana mkataba na Chuo Kikuu kwamba atalipa ada kwa utaratibu ule ambao amepewa, kama ni mkopo au *scholarship* au atalipa mwenyewe.

Sasa inapofika mahali ambapo mwanafunzi amekuwa na matatizo ya kupata fedha kwa ajili ya kukamilisha ada yake, ni muhimu kwamba mwanafunzi yule aende kwenye uongozi wa Chuo Husika, awe na mpango yake mwenyewe, akieleze chuo anao mpango gani wa kuweza kulipa ada hiyo; na hakuna chuo ambacho kitamkataza kufanya mitihani kama amekubaliana na chuo ni jinsi gani atakamilisha ada yake. (*Makofi*)

Na. 219

Matengenezo ya Barabara ya Mwanangwa Mpaka Salawi

MHE. JACOB D. SHIBILITI aliuliza:-

Barabara ya Mwanangwa – Misasi Busongo – Mwawile – Salawi, ilifanyiwa matengenezo makubwa hasa eneo la Mwawile – Mwagiligili mwaka 2003 lakini kwa sasa eneo hilo lina hali mbaya sana:-

Je, ni lini Serikali itaifanyia matengenezo kama ya awali ili iendelee kuitika?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jacob Dalali Shibili, Mbunge wa Misungwi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilifanyia matengenezo makubwa barabara ya Mwanangwa – Misasi – Busongo – Mwawile – Salawi ili iweze kuitika wakati wote.

Kwa kuzingatia azma hiyo, Wizara yangu kuitia wakala wa barabara imetenga jumla ya shilingi milioni 432,400 kuitia mfuko wa barabara (*Road Funds*) katika mwaka wa 2010/2011 kwa ajili ya kuifanyia matengenezo makubwa barabara hiyo ikiwa ni pamoja na maeneo ya Mwawile na Mwagiligili ambayo yameharibika kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niongeze tu kwamba hivi sasa Mkandarasi anayeitwa *Meli Contractors Ltd.* wa Shinyanga, tayari ameshaanza kazi ya matengenezo ya barabara hiyo kwa mkataba wa shilingi milioni 308. Kazi imeanza tarehe 9 Julai, 2010 na inatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, 2010.

Kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba barabara hiyo itaendelea kuitika kwa kipindi chote cha mwaka baada ya kufanyiwa matengenezo hayo.

MHE. JACOB D. SHIBILITI: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ninaomba niulize swali moja la nyongeza. Lakini kabla ya swali la nyongeza nianze tu kwa kumpongeza Naibu Waziri, Waziri mwenyewe na Wizara kwa ujumla kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Lakini pia wapokee shukrani za wananchi wa Mwawile, Mwagiligili, Buhingo Busongo kwa kazi inayoendelea kwa sasa hivi kwa kweli wanakubaliana na wewe kwamba kazi zinaenda vizuri na wanakupongeza sana na wanakutakia maisha mema na wananchi wako wa huko unakotoka basi waweze kukuchagua tena uje uweze kuendelea kutusaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi kwenye swali. Kwa kuwa barabara hii ya Mwanangwa, Misasi, hadi Salawe imekuwa ikitumia pesa nyingi sana.

Je, Serikali ina mpango gani sasa kuitengeneza kwa kiwango cha lami hata kama ni kwa *portion* kuanzia Mwanangwa Msasi baadaye Misasi Buhingo ili angalau barabara hiyo sasa iweze kudumu kwa muda mrefu zaidi?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nishukuru sana kwa pongezi hizo alizozitoa kwetu na kwa Serikali kwa ujumla jinsi ambavyo tumetekeleza ilani ya Uchaguzi na hususan kwenye jimbo lake na mimi nimshukuru tu kwa msukumo alionao wa kusimamia miundombinu ya barabara katika eneo lake na naye tumtakie kila la heri na mimi amenitakia kila heri huko ninakotoka. Nataka nimwambie ninatoka ni Chilonwa, nadhani wapiga kura wamesikia kama alivyonitakia Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuhusu swalii lake ya kwamba eneo la barabara hii ili lisiweze kutumia fedha nyingi mara kwa mara ianze kufikiriwa kutengenezwa kwa kiwango cha lami.

Kimsingi nakubaliana naye kwamba ukitengeneza barabara kwa kiwango cha lami inadumu kwa muda mrefu. Lakini kutokana tu ufinyu wa Bajeti ndiyo unatufanya tuwe tunafanya matengenezo kidogo kidogo kwa kiwango cha changarawe na mahala pengine kwa njia tu ya udongo,

Lakini adhima ya Serikali ni kuhakikisha kwamba hapo baadaye kama uwezo Serikali itakuwa umeimarika basi barabara hizi ziweze kufikiriwa kwa kutengeneza kiwango cha lami. Kwa hiyo, tuombe uzima tu na tutakiane heri. Kwa kadri tutakavyokuwa tunaendelea tukirudi hapa tena suala lake linaweza likafikiriwa.

Na. 220

Upatikanaji wa Vyombo vya Usafiri Majini

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM aliuliza:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya upatikanaji wa meli na boti za uhakika na za kudumu katika maeneo yanayounganisha wasafiri katika bandari ya Hindi na kwenye maziwa kama vile Dar es Salaam - Mafia, Tanga, Pemba, Dar es Salaam - Mtwara maeneo yote yanayounganisha Bandari zote Ukanda wa Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa na Ziwa Tanganyika?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mbunge wa Mtambile, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kujiondoa kwenye shughuli za moja kwa moja katika biashara ya usafiri, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali kwa lengo la kuboresha usafiri wa meli na boti katika maeneo ya bahari na maziwa nchini ili wananchi wapate huduma salama za usafiri.

Mikakati hiyo ni pamoja na kuweka mazingira mazuri ya kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje kwa kujenga miundombinu ya uhakika kama vile magati yatakayowezesha na kurahisisha huduma ya usafiri wa majini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada za Serikali za kupata wawekezaji, tayari mwekezaji kampuni ya *Coastal Fast Ferries* ameshaleta nchini boti mbili ziitwayo Kilimanjaro I na Kilimanjaro II ambazo zinatarajiwa kuwasili nchini mwanzoni mwa mwezi Julai, 2010, boti zote zitatumika katika Bahari ya H indi baina ya Visiwa vya Unguja na Pemba na Bandari ya Dar es Salaam, Tanga na Mtwara.

Aidha, Shirika la Meli la Zanzibar limeshaanza taratibu za awali za kununua meli mbili (2) mpya ikiwemo meli moja ya abiria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa usafiri katika maziwa Serikali kupitia kampuni ya Huduma za Meli (*MSCL*) yenye Makao Makuu mjini Mwanza ambayo hutoa huduma za usafiri katika Ziwa Victoria, Nyasa na Tanganyika inayo mikakati ya kuzifanya matengenezo meli zake ambazo ni chakavu kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha kutoka Serikalini na nchi wahisani pamoja na kuendelea kuwavutia wawekezaji katika sekta ya usafiri wa majini kutoka ndani na nje ili kutoa huduma katika maziwa hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuweka mazingira mazuri ya kukaribisha wawekezaji katika sekta hii ya usafiri wa majini ili wananchi waendelee kupata huduma ya usafiri iliyokuwa bora na yenye usalama kwa watu na mali zao.

Aidha, Serikali kupitia mamlaka ya usafiri wa nchi kavu na majini (*SUMATRA*) imeendelea kufanya ukaguzi meli na boti zinazotoa huduma ya usafiri katika Bahari, Maziwa na Mito ili kuhakikisha ubora wa vyombo vyote vya usafiri majini kwa lengo la kulinda usalama wa watu na mali zao.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nina swalii moja dogo la nyongeza. Mheshimiwa Waziri amezungumzia zaidi ya mkakati wa kupatikana kwa Bodi hizo Dar es Salaam, Zanzibar, Pemba na Mtwara, lakini sijamsikia Mheshimiwa Waziri akigusia suala la kupatikana kwa Boti kuelekea kisiwa cha Mafia. Anasemaje, juu ya tatizo hili sambamba na wananchi wale wa Ukerewe ambao wanacho kilio kikubwa na cha siku nyingi?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba nimetaja baadhi ya sehemu ambazo zitahudumiwa na Boti hizi ambazo sasa hivi mipango yake imeshabainika kwamba zitapatikana.

Lakini jibu la ujumla nimesema tu kwamba Serikali itaendelea kuhamasisha sekta binafsi katika upatikanaji wa vyombo hivi vya usafiri. Kwa hiyo, katika uhamasishaji tutazingatia pia na visiwa vya Mafia na Ukerewe na kadhalika. (*Makofi*)

MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuwa wawekezaji hawa wanaohudumia maziwa ya Tanganyika, Nyasa na Victoria na hususan ziwa Nyasa wameshindwa kutupa meli za uhakika kwenye ziwa hilo na meli zilizopo zinajaa sana na ni chakavu sana. Watu walishakufa kwa sababu ya kuzama na meli pale Makonde katika ziwa Nyasa miaka michache iliyopita.

Je, Serikali mnaendelea kungoja wawekezaji mpaka muone watu wamekufa wengine baada ya meli nyingine imezama ziwa Nyasa ndiyo mtachukua hatua?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme la hasha, Serikali haidhamirii hivyo hata kidogo na napenda tu kwa niaba ya Serikali niwape pole wananchi wa Ludewa kwa hayo majanga yaliyotokea siku hizo zilizopita katika shida ya usafiri wa majini na adha wanayoipata kwa ujumla. Lakini niseme tu kwam ba kama nilivyoeleza katika jibu la msingi kwamba Serikali ilishajiondoa katika biashara hii ya moja kwa moja ya usafiri majini.

Lakini hiyo haimaanishi kwamba haihusiki na maisha na usalama wa raia wake. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba pamoja na jitihada za Serikali hizi za kuihusisha sekta binafsi katika suala hili la usafiri majini lakini vilevile Serikali itaendelea kuchukua hatua za dharura za kuhakikisha kwamba wananchi wake hawaathiriki zaidi ya hayo yaliyotokea huko ziwa Nyasa.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tumemaliza maswali ya siku ya leo. Sasa nianze na wageni, na nitaomba wageni nikiwataja mchukue fursa hiyo kusimama.

Kwanza katika wageni ambaو tunao katika ukumbi huu asubuhi hii ya leo ni pamoja na wageni wa Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo, ambaو ni Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali (*Pay Master General*). Hawakuandikwa kwa majina, nashukuru sana karibu sana Katibu Mkuu. Gavana wa Benki Kuu na Wasaidizi wake, Mheshimiwa Gavana Ndulu karibu sana. (*Makofi*)

Manaibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, karibuni sana. Mhasibu Mkuu wa Serikali, Wakurugenzi na Makamishna wa Idara mbalimbali za Wizara ya Fedha na Uchumi, karibuni sana. Tunaye pia Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Wasaidizi wake, karibuni sana. (*Makofi*)

Lakini pia tuna Wakuu wa Mashirika mbali mbali na taasisi mbalimbali ambazo ziko chini ya Wizara ya Fedha na Uchumi. Pia katika wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo, wako viongozi wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Kilosa ambaو ni Wenyeviti na Makatibu wa Kata, wapo viongozi wa CCM Wilaya wenyeviti na makatibu wa Kata twende kwa mikono. Naomba wale viongozi watano wa CCM Wilaya ya Kilosa wasimame. Karibuni sana. Hawa viongozi ni Gervasi Makoye, Raphael Chayeka, Kassim Lila, Jackson Lifukwe na Lukano Abeid. Lakini pia tunao Wenyeviti 27, na Makatibu wa Kata kutoka katika Jimbo la Kilosa, wasimame wote kwa pamoja, hawa ndiyo wapiganaji wenyewe,

niwahakikishie Mheshimiwa Mustafa Mkulo anafanya kazi nzuri hapa Bungeni anatupa ushirikiano wa kila aina msibabaishwe na mavuvuzela. (*Kicheko/Makofi*)

Maafisa kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu ni pamoja na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali Mheshimiwa Ludovick Utoh na maafisa wengine wote wa ofisi hii waliofutana naye, naomba wasimame wote kwa pamoja, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia, ni mtoto wake kutoka Antlanta Georgia, ambaye anasoma huko anaitwa Abdallah Mtulia, karibu sana B wana Abdallah, hawakuandika unasoma nini natumaini na wewe unasoma udaktari pia, *like father like son*. Lakini yupo mtoto wa rafiki yake ambaye anatoka Maryland Marekani ambaye pia anasoma, anaitwa Ramadhani Athuman, karibu sana Bungeni tunakutakia kila la heri katika masomo yako huko Marekani ukishamaliza urudi nyumbani. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Joyce Masunga, ni Chiku Said ambaye ni Mama Mlezi na ndiye anayemtunzia nyumba na wanaye kwa kipindi chote cha miaka mitano, ahsante karibu sana. Hapa Bungeni maarufu anaitwa *Maziwa fresh*. Jesca Japheth mke wa Dereva wake Bwana Juma Lazaro, karibu sana Jesca. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Aloyce Kimaro, ni Festo Samson, Msaidizi wa Mheshimiwa Mbunge, karibu sana nikwambie tu Vunjo huko kuna shughuli. Wageni wa Naibu Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya vijana, Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, ni dada zake wawili amba ni wajasiriamali, Prisca Laya na Maria Odemba, karibuni sana Prisca na Maria.

Lakini tunayo timu ya waandishi na watangazaji wanane, kutoka redio *Kili FM stereo Moshi* ikiongozwa na Ndugu Exaud Maria wamekuja kutembelea Bunge karibuni sana Ndugu zangu kutoka *FM studio Moshi* natumaini dada yangu Chonya hajambo.

Pia tuna wanafunzi 50 na walimu watano kutoka shule ya Sekondari ya Makole iliyopo Dodoma, nadhani wapo *Basement*. Tunao wanafunzi 30 na walimu wanne kutoka shule ya msingi ya Kiwanja cha Ndege iliyopo hapa hapa Dodoma. Pia natumaini watakuwa *Basement*. Wanafunzi 30 na walimu wawili kutoka shule ya Azimio Sekondari iliyopo hapa hapa Dodoma.

Tunao wageni wa Mwenyekiti wa Bunge, nao ni Meneja wa Maendeleo ya Wafugaji Dr. Justice Mumba, kutoka Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, karibu sana karibu Mumba.

Lakini pia tunaye Meneja wa huduma za Utalii Ndugu Veronica Ufunguo, kutoka Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, karibuni sana.

Lakini mwisho ninaye mgeni wangu maalum anaitwa Sunday, asimame, huyo ni Ndugai *Junior*, karibu sana *Sunday* yuko *Form One, Tabora Boys Secondary School*. Katika mtihani wa Darasa la Saba matokeo yaliyopita katika mkoa wa Dodoam alikuwa wa pili Kimko, *like father like son. (Kicheko/Makofi)*

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2010/2011 Wizara ya Fedha na Uchumi

MWENYEKITI: Niwaombe wanaotaka kuchangia Hoja hii karibu nafunga orodha, mlete majina moja kwa moja.

WAZIRI WA FEHDA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato, Matumizi ya Kawaida na Maendeleo ya Wizara ya Fedha na Uchumi kwa mwaka wa Fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile Mkutano Mkuu wa CCM umekamilisha shughuli zake karibuni na kuweka historia ndani ya Chama hicho kwa kufanya Uchaguzi wa viongozi wa Kitaifa kwa njia ya Amani na Utulivu, chini ya misingi ya Kidemokrasia napenda awali ya yote kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, Mwenyekiti wa CCM na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa tena kwa kura nyingi sana kuwa mgombea wa kiti cha Urais kwa tiketi ya CCM. (*Makofi*)

Ushindi huo wa kishindo ni ishara kukubalika kwake kutokana na kazi nzuri aliyowafanyia Watanzania katika kipindi cha kwanza cha awamu ya nne. Ninamtakia heri, afya njema na ushindi mkubwa katika Uchaguzi Mkuu ujao wa mwezi wa kumi mwaka huu. (*Makofi*)

Vilevile napenda kumpongeza Mheshimiwa Dr. Bilali kwa kuchaguliwa na kupitishwa na mkutano Mkuu wa CCM kuwa mgombea mwenza wa kiti cha Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi, hekima busara, utaalam na uzoefu wake vitasaidia sana katika kushauri Kuhusu utekelezaji wa sera nzuri za CCM. Naye ninamtakia afya njema na ushindi mkubwa wa CCM kwenye uchaguzi mkuu ujao.

Kadhalika, napenda kumpongeza Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa kuchaguliwa kuwa mgombea wa Urais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi (CCM). Kutokana na umahiri na uzoefu wake katika nafasi ya Makamu wa Rais ni dhahiri ushindi mkubwa kwake na kwa CCM utapatikana katika Uchaguzi Mkuu unaokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pondezi hizo, sasa napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe Mwenyekiti, Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Kamati za Bunge, kwa kuendesha majadiliano ya bajeti ya mwaka 2010/2011 kwa umakini tangu yalipoanza hadi sasa. Aidha, nawashukuru Wajumbe wa Kamati mbalimbali za Bunge kwa michango na ushauri waliota wakati wa kupitia makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara, Idara na Mikoa. Michango na ushauri wao utaendelea kuboresha utendaji wa Serikali katika kutoa huduma kwa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, nitumie nafasi hii kuwashukuru kwa namna ya pekee Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi chini ya Mwenyekiti Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda Mbunge wa Jimbo la Handeni kwa maoni, ushauri na mapendekezo waliyoyatoa. Wizara imezingatia ushauri na mapendekezo ya Kamati katika kuandaa hotuba hii, pia napenda kueleza kuwa maoni hayo pamoja na yale yatakayotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa kujadili hoja hii yataendelea kuzingatiwa wakati wa utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niwashukuru Naibu Mawaziri wa Wizara ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Omari Yussuf Mzee na Mheshimiwa Jeremiah S. Sumari kwa ushirikiano mkubwa walionipa katika kutekeleza majukumu yangu na pia maandalizi ya bajeti hii. Aidha, nawashukuru wafanyakazi wote wa Wizara na Taasisi zake, chini ya uongozi wa Katibu Mkuu Alhaji Ramadhani M. Khijjah na Naibu Makatibu Wakuu Bwana John M. Haule, Bwana Laston T. Msongole na Dr. Servacius B. Likwelile, Makamishna na Wakurugenzi kwa kazi nzuri wanayoifanya bila kuchoka. Vile vile, nawashukuru wafanyakazi wa Benki Kuu chini ya uongozi wa Gavana Profesa Benno Ndulu na wafanyakazi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania chini ya uongozi wa Kamishna Mkuu Bw. Harry Kitilya kwa kazi nzuri na ushirikiano wao mkubwa. Naomba ushirikiano walionipa uendelee ili Wizara iendelee kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee naomba Bunge lako Tukufu lipokee shukrani kwa Profesa Benno Ndulu aliyoeta ushauri wa kitaalamu uliowezesha nchi yetu kukabili msukosuko wa kiuchumi kwa umakini mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005. Katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005, Wizara ya Fedha na Uchumi imeelekezwa kujikita katika kufanya mambo makuu yafuatayo:-

Kusimamia Uchumi Jumla; kusimamia Bajeti ya Serikali; Kuhakikisha sekta za kipaumbele zinapatiwa rasilimali fedha; kuboresha sekta ya fedha; kuboresha huduma kwa wastaa fu na kusimamia Mashirika ya Umma. Katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi mafanikio mengi yamepatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miaka mitano (2005 – 2009) uchumi umeendelea kuimarika na Pato la Taifa likuwa kwa wastani wa asilimia 7.2 kwa mwaka katika kipindi hicho. Ukuaji huu wa uchumi ulichangiwa zaidi na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi katika sekta za:-

Viwanda; ujenzi; fedha na mawasiliano na uchukuzi. Kutokana na idadi ya watu Tanzania Bara kukadiriwa kuwa milioni 39.3 katika mwaka 2009, pato la wastani la kila Mtanzania lilikadiriwa kuwa Shilingi 682,737.70 mwaka huo sawa na Dola za Kimarekani 517.6 ikilinganishwa na Shilingi 441,030.20 mwaka 2005, sawa na Dola za Kimarekani 392.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hicho, Wizara ya Fedha na Uchumi, kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*), imechukua hatua mbalimbali za marekebisho ya sera za kodi na kubuni vyanzo vipyta ya mapato kwa lengo la kupanua wigo wa kodi. Hatua hizi ni pamoja na kuhimiza ulipaji kodi kwa hiari na kusimamia Sheria za kodi ambazo zimesaidia kuweka mazingira mazuri zaidi ya uzalishaji na kurahisisha ukusanyaji wa kodi na kuongeza mapato ya ndani. Kufuatia maboresho katika mfumo mzima wa ukusanyaji kodi, mapato ya ndani ya Serikali yameongezeka kwa asilimia 121 kutoka Shilingi bilioni 2,124.8 mwaka 2005/2006 hadi Shilingi bilioni 4,688.3 mwaka 2009/2010. Wastani wa makusanyo ya Kodi kwa mwezi yamefikia Shilingi bilioni 390 ikilinganishwa na shilingi bilioni 177 kwa mwezi mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzishwa kwa Mfuko wa Dhamana wa Mikopo kwa Wafanyabiashara Wadogo na Kati (*SME Credit Guarantee Scheme*) ambao unaratibiwa na Benki Kuu kumeboresha mazingira ya kupata mikopo kwa wahitaji wa mitaji midogo na ya kati kutoka kwenye mabenki na taasisi za fedha. Tangu Mfuko huu uanzishwe, jumla ya SMEs 48 zimepata udhamini wa mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 6.393. Aidha, mikopo hiyo ilielekezwa katika maeneo ya kiuchumi yafuatayo: uzalishaji wa chakula, ujenzi, shughuli za hoteli na utalii, maeneo ya elimu, afya na maji, ufugaji wa kuku, uvuvi, mawasiliano na usafirishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kuboresha huduma kwa wastaifu mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuhamishia huduma ya malipo ya wastaifu kwenye Mifuko ya Hifadhi za Jamii. Wastaifu 53,600 ambao wapo kwenye daftari la pensheni la Hazina, wamehamishiwa katika Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma (*PPF*) na wameanza kulipwa Pensheni zao kupitia Mfuko huo kuanzia Julai, 2008. Wastaifu ambao ni askari Polisi na Magereza, wamehamishiwa kwenye Mfuko wa *GEPF* tangu Januari, 2009.

Aidha, viongozi wengine wa Kitaifa wanaendelea kulipwa mafao yao kuitia Hazina. Hadi kufikia Julai, 2009, idadi ya wastaifu waliokuwa kwenye orodha ya kulipwa pensheni na Wizara ya Fedha na Uchumi kuitia Mfuko wa *PPF*, ilifikia 55,051 ikiwa ni ongezeko la wastaifu 1,451. Ongezeko hili limetokana na wastaifu wapya kutoka Jeshi la Wananchi wa Tanzania (*JWTZ*), Usalama wa Taifa ambao bado hawajajiunga na utaratibu wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii pamoja na wastaifu wanaorejeshwa kwenye daftari la pensheni la Hazina baada ya kulipwa kwa mkupuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio mengine ni Wastaifu walioko kwenye daftari la Hazina kulipwa pensheni zao kuitia akaunti binafsi badala ya utaratibu wa kulipiwa kwenye kaunta za benki. Utaratibu huo umewawezesha wastaifu kuchukua fedha zao wakati wowote kwa kutumia kadi ya *ATM*. Aidha, Wizara imeendelea

kuboresha utunzaji wa kumbukumbu za wastaa fu walioko kwenye daftari la Hazina kwa kutumia mfumo wa kompyuta. Vile vile, wizara iliendesha Semina za kikanda, zilizowahusisha waajiri na maafisa wanaoshughulikia mafao na mirathi katika Wizara na Mikoa kuhusu wajibu wao wa kushughulikia mafao ya kustaa fu na mirathi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kubinafsisha Mashirika ya Umma mafanikio mbalimbali yamepatikana. Mashirika yaliyobinafsishwa na kuanza kufanya kazi sasa yanalipa kodi Serikalini badala ya kutegemea ruzuku kutoka Serikalini; Wawekezaji kutoka nje wameongezeka kwa kuwekeza katika mashirika yaliyobinafsishwa; Teknolojia katika mashirika mengi imeboreshwa kwa kuweka mifumo mipywa na hivyo kuwezesha kuongeza uzalishaji wa bidhaa bora zaidi. Watanzania wameendelea kuelimishwa na kupewa fursa ya kununua hisa na kumiliki mashirika yaliyobinafsishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akiba ya fedha za kigeni imeongezeka kutoka Dola za Kimarekani milioni 2,048.4 sawa na uwezo wa uagizaji wa bidhaa na huduma kwa miezi 4.8 kwa mwaka 2005 hadi kufikia Dola za Kimarekani milioni 3,551.3 mwaka 2009. Kiasi hiki ni sawa na uwezo wa uagizaji wa bidhaa na huduma kwa miezi 5.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa utekelezaji wa Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (*PFMRP*), Wizara imepata mafanikio makubwa yakiwemo yafuatayo:-

Kuboresha uwezo wa ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu ikiwa ni pamoja na kusomesha wakaguzi ili waweze kumudu kazi zao ipasavyo; kuhamasisha utayarishaji wa hesabu za serikali kwa kutumia viwango vya kimataifa (*IPSA*s) hatua ambayo imewezesha utoaji wa taarifa za hesabu za Serikali kwa wakati. Aidha, Kamati za Bunge za usimamizi wa fedha nazo zimevezeshwa kutathimini uwezo wa usimamizi wa fedha katika Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma. Wizara imeendelea kutoa mafunzo kwa wizara nyingine, Mikoa na Serikali za Mitaa katika kuboresha uaandaaji wa Mipango, Bajeti na utoaji wa taarifa za utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miaka minne (2006 -2009) ya utekelezaji wa MKUKUTA awamu ya kwanza, uchumi wa Tanzania uliendelea kuimari. Uchumi ulikuwa kwa wastani wa kiwango cha asilimia 6.9 ukilinganisha na shabaha ya MKUKUTA ya ukuaji wa kati ya asilimia 6 na 8. Kiwango cha jumla cha umaskini kilipungua kwa asilimia 2.2. Aidha, kwa upande wa viashiria vya kuboresha Maisha na Ustawi wa Jamii, vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano vimepungua kutoka watoto 112 kati ya 1000 mwaka 2004/2005 hadi kufikia watoto 91 mwaka 2008/2009. Lengo lilikuwa kupunguza vifo kufikia 79 kati ya watoto 1000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifo vya watoto wachanga chini ya mwaka mmoja vimepungua kutoka 68 kati ya watoto 1000 waliozaliwa hai mwaka 2004/2005 na kufikia 58 kati ya watoto 1000 waliozaliwa hai mwaka 2008/2009. Kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi katika shule za msingi kimeongezeka kutoka asilimia 96.1 mwaka 2006 hadi

asilimia 97.2 mwaka 2008, dhidi ya lengo la asilimia 99 mwaka 2010. Vile vile, kasi ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI imepungua kutoka asilimia 7.0 mwaka 2005 hadi asilimia 5.7 mwaka 2008 ikilinganishwa na lengo lililowekwa la asilimia 5.0 mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2009/2010 na Malengo ya Mwaka 2010/2011. Katika kusimamia na kutekeleza majukumu yake, Wizara inaongozwa na Mpango Mkakati ulioandaliwa kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Malengo ya Milenia 2015, MKUKUTA na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, sambamba na kutekeleza Mfumo wa Matumizi wa Muda wa Kati (*MTEF*) 2008/2009 – 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara ya Fedha na Uchumi imeendelea kutekeleza majukumu yake ya:-

Kubuni na kusimamia utekelezaji wa Sera na Mikakati ya Uchumi Jumla; Kusimamia ukusanyaji wa mapato ya ndani na ya nje, na matumizi ya Serikali; Utekelezaji wa MKUKUTA, Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na kupanga mipango ya maendeleo na kusimamia sheria, kanuni na taratibu za uhasibu, ukaguzi wa ndani Serikalini, ununuzi wa umma na usimamizi wa mali ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha majukumu haya yanatekelezwa kwa ufanisi, Wizara imegawanywa katika mafungu manne ya kibajeti. Mafungu hayo ni Fungu 50 - Wizara ya Fedha na Uchumi; Fungu 21 – Hazina; Fungu 22 - Deni la Taifa na Fungu 23 - Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali. Vile vile, Fungu 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ambayo inajitegemea, linaombewa fedha Bungeni na Waziri wa Fedha na Uchumi kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani mwaka 2009/2010. Kwa mwaka 2009/2010 Wizara ililenga kupata mapato ya ndani ya jumla ya Shilingi bilioni 5,096.016. Hadi kufikia Aprili, 2010 matokeo ya kuridhisha yamepatikana katika utekelezaji wa sera za kodi. Katika kipindi cha Julai, 2009 hadi Aprili, 2010 Serikali ilikusanya mapato ya ndani ya jumla ya Shilingi bilioni 3,821.162 sawa na asilimia 90.7 ya lengo la kukusanya Shilingi bilioni 4,211.764 kwa pindi hicho. Katika kipindi hiki, Wizara iliendelea kuboresha ukusanyaji wa Mapato ya ndani na nje kwa kutekeleza yafuatayo:-

Kuendelea kupanua wigo wa kodi, kupunguza misamaha ya kodi na kuendelea kuimarisha uchumi tulivu; kusimamia kwa karibu mageuzi yanayoendelea ndani ya Mamlaka ya Mapato (*TRA*) chini ya Mpango wa Tatu wa Maboresho wa Miaka Mitano; kuendelea kurekebisha mfumo wa kodi na kuimarisha Idara ya Walipakodi Wakubwa kwa kuboresha mifumo ya utendaji; kurekebisha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Sura 148 na Kurekebisha Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Sura 147. Mafanikio yaliyopatikana kufuatia utekelezaji wa hatua hizi pamoja na malengo ya utekelezaji kwa mwaka 2010/2011 ni kama ilivyoainishwa katika hotuba ya bajeti ya Serikali niliyowasilisha hapa Bungeni tarehe 10 Juni, 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu misaada na mikopo. Mapato kutokana na misaada na mikopo kutoka nje. Katika mwaka 2009/2010, Wizara ilipanga kukusanya mapato kutokana na misaada na mikopo kutoka nje yenye thamani ya Shilingi bilioni 3,182. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2010, misaada na mikopo iliyokuwa imepokelewa ilikuwa Shilingi bilioni 2,375, sawa na asilimia 75 ya makadirio ya Shilingi bilioni 3,182. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa, Shilingi bilioni 1,214.0 au asilimia 102 ya makadirio ya Shilingi bilioni 1,193.91 ni misaada na mikopo ya kibajeti na Shilingi bilioni 1,161 au asilimia 63.0 ya makadirio ya Shilingi bilioni 1,857.4 ni mikopo na misaada kwa ajili ya miradi ya maendeleo na mifuko ya pamoja (*Basket Funds*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara imepanga kukusanya mapato ya Shilingi bilioni 3274.553 kutokana na misaada na mikopo kutoka nje. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 821.645 ni misaada na mikopo ya kibajeti na Shilingi bilioni ni mikopo na misaada kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa pamoja wa misaada Tanzania. Katika mwaka wa fedha 2009/2010, Serikali iliendelea kutekeleza Mkakati wa Pamoja wa Misaada (*Tanzania Joint Assistance Strategy - JAST*) kwa nia ya kuongeza ufanisi wa misaada inayotolewa kwa nchi yetu. Aidha, kwa kutumia Mkakati huu Serikali iliendelea kujenga uwezo wa kusimamia na kutunza kumbukumbu sahihi za misaada na mikopo inayopokelewa pamoja na kukuza ushirikiano kati ya Serikali na wadau wengine katika mchakato wa maendeleo ya nchi yetu. Vile vile, Serikali imeendelea kuandaa Sera ya Misaada ya Kiufundi, kukamilisha Mfumo wa Mawasiliano kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo, kukamilisha mgawanyo wa majukumu mionganoni mwa Washirika wa Maendeleo na kuendelea kuboresha Mfumo wa Kumbukumbu na Takwimu za Misaada na Mikopo kwa Tanzania (*Aid Management Platform*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara inatarajia kukamilisha kazi ya kuandaa Mkakati wa Misaada ya Kiufundi, kuendeleza juhudzi za kuboresha Mfumo wa Kumbukumbu na Takwimu za Misaada na Mikopo kwa kutoa mafunzo na vitendea kazi kwa wataalamu pamoja na kuunganisha mtandao huo na mitandao katika Wizara na wadau wengine wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukuza ushirikiano na Washirika wa Maendeleo. Jukumu lingine muhimu la Wizara ni kukuza na kuboresha mahusiano kati ya Serikali na Washirika wetu wa maendeleo kupitia mikutano na mashauriano ya mara kwa mara. Katika mwaka 2009/2010, Wizara ilianda na kuendesha mikutano wa mwaka wa mapitio ya utekelezaji wa malengo ya MKUKUTA na vigezo vya kupima ufanisi wa misaada ya kibajeti (*MKUKUTA and Performance Assessment Framework Reviews*). Mkutano huo ulifanyika Mjini Dar es Salaam mwezi Novemba, 2009 kwa mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa matumizi kwa mwaka 2009/2010. Fungu 50- Wizara ya Fedha na Uchumi. Bajeti kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2009/2010 ilikuwa Shilingi bilioni 113.64. Kati ya hizo mishahara ni Shilingi bilioni 2.81, matumizi mengineyo ni Shilingi bilioni 110.83 na Shilingi bilioni 188.2 ilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Hadi kufikia Mei, 2010 Fungu hili

limepokea na kutumia Shilingi bilioni 92.71 kwa matumizi ya kawaida ambayo ni sawa na asilimia 81.58 ya makadirio ya mwaka 2009/2010. Shilingi bilioni 40.67 kwa matumizi ya maendeleo ambayo ni sawa na asilimia 21.6 ya makadirio ya mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 21-Hazina. Bajeti kwa ajili ya matumizi ya kawaida ilikuwa Shilingi bilioni 597.61. Kati ya hizo mishahara ni Shilingi bilioni 1.14 na Shilingi bilioni 68.52 ni kwa ajili ya marekebisho ya mishahara ya Kitaifa. Shilingi bilioni 365.79 ilikuwa ni kwa ajili ya matumizi maalum ikiwa ni pamoja na dharura. Shilingi bilioni 126.38 ilikuwa ni kwa ajili ya Mamlaka ya Mapato Tanzania na Shilingi bilioni 35.78 ilikuwa kwa ajili ya taasisi zilizo chini ya Wizara, michango ya Kimataifa na matumizi ya idara zilizo chini ya fungu hili. Shilingi bilioni 73.99 ilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo ambapo kati ya hizo Shilingi bilioni 63.9 ni fedha za nje. Hadi tarehe 30 Aprili, 2010 matumizi ya kawaida yalifikia Shilingi bilioni 457.85 sawa na asilimia 76.64 wakati matumizi ya maendeleo yalifikia Shilingi bilioni 44.8 sawa na asilimia 60.6 ya makadirio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 22 – Deni la Taifa. Bajeti ya Fungu 22 ilikuwa Shilingi bilioni 1,517.05. Hadi kufikia mwisho wa mwezi Aprili 2010 matumizi yote yalifikia Shilingi bilioni 1,327.69 ambayo ni sawa na asilimia 87.5 ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 23-Mhasibu Mkuu wa Serikali. Bajeti ya matumizi ya kawaida ilikuwa shillingi bilioni 97.62. Hadi mwezi Aprili 2010 matumizi ya kawaida yalifikia Shilingi bilioni 75.357 ambayo ni sawa na asilimia 77.2 ya makadirio. Bajeti ya maendeleo ilikuwa Shilingi bilioni 12.05. Kati ya hizo, Shilingi bilioni 6.0 zikiwa fedha za ndani na Shilingi bilioni 6.05 fedha za nje. Matumizi ya fedha za maendeleo hadi Aprili, 2010 yalifikia Shilingi bilioni 1.192. Kati ya hizo, fedha za ndani ni Shilingi milioni 703.8 na Shilingi milioni 488.2 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Bajeti ya Fungu 45 kwa matumizi ya kawaida ilikuwa Shilingi bilioni 19.2. Bajeti ya maendeleo kwa Fungu hili ilikuwa Shilingi bilioni 5.8 ambapo kati ya hizo fedha za ndani ni Shilingi bilioni 2.8 na fedha za nje zikiwa ni Shilingi bilioni 3.0. Hadi mwezi Aprili, 2010 matumizi ya kawaida yalifikia Shilingi bilioni 14.12 sawa na asilimia 73.7 ya makisio. Matumizi ya maendeleo yalifikia Shilingi bilioni 1.37 fedha za nje na Shilingi bilioni 1.6 fedha za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Majukumu kwa mwaka 2009/10 na Malengo ya 2010/1.1Usimamizi wa Deni la Taifa. Katika mwaka wa fedha wa 2009/10 Kamati ya Kitaifa ya Kusimamia Madeni (*NDMC*) iliendelea na kazi zake za kusimamia Deni la Taifa na kuwezesha deni hilo kuwa stahimilivu (*sustainable*). Uchambuzi wa Deni la Taifa uliofanyika mwaka 2008 unaonyesha kuwa viashiria vya Deni la Taifa vinakubaliana na vile vinavyokubalika Kimataifa. Kazi ambazo *NDMC* ilifanya ni pamoja na kuchambua mikopo kutoka nje ya nchi na ile ya ndani hususan maombi ya dhamana za Serikali kwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kufadhili miradi katika Taasisi za Umma na kumshauri Waziri wa Fedha na Uchumi kuchukua mikopo yenye masharti nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika juhudi za Serikali za kudhibiti deni la nje, Wizara ya Fedha na Uchumi ilifanya majadiliano na nchi ya Brazili ambayo ndiyo iliyokuwa hajatupatia unafuu wa deni katika Kundi la Paris ili watupatie unafuu wa deni makubaliano ya awali yameshaafikiwa. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Serikali itaendelea kujadiliana na nchi zilizobaki za *Non Paris Club* ambazo hazijatupatia unafuu wa madeni ili kuendelea kupunguza deni la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uandaaji, usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Bajeti ya Serikali, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kukamilisha rasimu ya vipaumbele vya Taifa kwa ajili ya Mwongozo na Mpango wa Bajeti 2010/2011- 2012/2013 na mwongozo huu ndio uliotumika katika kuandaa Mpango na Bajeti ya 2010/11 – 2012/13; kuratibu na kusimamia kazi ya bajeti *classification of functions of Government (CoFoG)* ambayo inatarajiwa kutumika katika kutoa taarifa za kibajeti kuanzia mwaka wa fedha 2010/2011. Aidha, Wizara ilitoa mafunzo ya uandaaji wa mipango na bajeti kwa watumishi 42 kutoka Mikoani, na watumishi 798 kutoka Halmashauri zote za Tanzania bara na mafunzo ya uandaaji wa *MTEF* yaliendelea kutolewa. Vile vile, viwango vya bajeti ya matumizi ya kawaida na maendeleo viliandaliwa na kutumika katika uandaaji wa bajeti ya mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2010/2011 Wizara itaendelea kuitia utaratibu wa uwasilishaji wa bajeti za Wizara, Idara za Serikali, Mikoa na Halmashauri; kuhakikisha sera na Mipango ya Kitaifa na ya Kisekta inaingizwa kwenye Bajeti ya Serikali na kufanya tathmini ya bajeti ya Serikali ili kuhakikisha kuwa inatenga mahitaji ya makundi yote ya jamii kwa kuzingatia uwezo wa kifedha. Aidha, Wizara itafanya marekebisho ya mpangilio wa bajeti ya Serikali kwa kuzingatia programu mbalimbali; kujenga uwezo wa Wizara, Idara za Serikali, Mikoa na Halmashauri katika uandaaji wa bajeti ya muda wa kati, usimamizi wake na utoaji taarifa za utekelezaji kwa wakati na kufuutilia pamoja na kutathmini matumizi ya fedha za umma. Vile vile, Wizara itaendelea na ukaguzi wa miradi inayotekeliza na Serikali na ile ya ubia na Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuondoa umaskini na uwezeshaji wananchi kiuchumi. Wizara iliendelea kuratibu mchakato wa maandalizi ya awamu ya pili ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA).

Maandalizi haya yalitanguliwa na tathmini ya utekelezaji wa MKUKUTA awamu ya kwanza. Aidha, tafiti na chambuzi mbalimbali zilifanyika kwa lengo la kubaini changamoto na fursa zilizopo katika kuendeleza juhudi za kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Tafiti hizo zimesaidia kuainisha maeneo ya vipaumbele katika kukabiliana na changamoto mbalimbali zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa MKUKUTA I na kupata matokeo mazuri katika maeneo yaliyoonyesha fursa za kuleta maendeleo zaidi. Matokeo ya tafiti na chambuzi hizo, pamoja na mashauriano ya wadau yamechangia katika maandalizi ya MKUKUTA awamu ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, MKUKUTA awamu ya pili ni mwendelezo wa awamu ya kwanza kimundo. Hivyo, MKUKUTA II umezingatia matokeo katika nguzo zake tatu, yaani Ukuzaji wa Uchumi na Kupunguza Umaskini wa Kipato, Kuboresha Maisha na Ustawi wa Jamii na Utawala Bora na Uwajibikaji. Maeneo yanayopewa kipaumbele

katika kuleta ukuaji wa haraka wa uchumi yanajumuisha: Kilimo, miundombinu, utalii, uzalishaji viwandani, na uchimbaji madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo haya yana mchango mkubwa katika kuongeza kipato kwa haraka, ukuzaji wa ajira, uwezo wa kuchangia katika kuongeza mapato ya Serikali, uwezo wa kuongeza ukuaji wa uchumi hasa maeneo ya vijijini, kuongeza mauzo ya bidhaa nje, na kuleta maendeleo katika viwanda. Kilimo kinaendelea kupewa kipaumbele ikizingatiwa kuwa wengi kati ya watu maskini wanaoishi vijijini wanategemea sekta hii. Katika kuhakikisha kwamba sekta hizo zinaleta matokeo tarajiwa, maeneo ya Elimu (hasa upanuzi wa elimu ya ufundi na ile ya juu), Afya (hasa kwa makundi hatarishi) na Maji yatapewa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utawala bora na uwajibikaji ni muhimu katika kujenga mazingira mazuri ya ukuaji uchumi nchini na kupunguza umaskini. Katika eneo hili, MKUKUTA II utalenga zaidi katika kusisitiza uwepo wa mazingira mazuri ya kisera ikijumuisha kulinda na kutetea hakimiliki; haki za binadamu; kuhakikisha kuwepo kwa ufanisi katika mfumo wa usimamizi wa rasilimali; kutokomeza rushwa; kuhakikisha kuwepo kwa mfumo imara wa kitaasisi ambaeo utasaidia katika kuleta maisha bora kwa watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Wizara iliendelea kusimamia Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi. Katika kusimamia utekelezaji wa Sera hii, Serikali iliendelea kutoa mikopo yenyenye masharti nafuu na elimu ya ujasiriamali. Aidha, miradi ya *SELF* na *NIGP* iliratibiwa. Hadi kufikia Aprili 2010, mfuko wa *SELF* ulikuwa umetoa mikopo yenyenye thamani ya Shilingi bilioni 5.012 kati Shilingi bilioni 5.416 zilizotengwa kukopeshwa katika kipindi hicho, mfuko ulikusanya Shilingi bilioni 4.07 kati ya Shilingi bilioni 4.17 ziliokusudiwa kukusanya kama marejesho ya mikopo. Vile vile, tangu mfuko uzinduliwe mwaka 2000, jumla ya asasi 270 zimepatiwa mikopo yenyenye thamani ya Shilingi bilioni 26.923 ambayo imewanufaisha wajasiriamali wadogo 71,065 kati yao wanawake ni asilimia 58.3

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi Aprili 2010, Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Kuongeza Ajira (*J.K Fund*) ulitoa mikopo yenyenye thamani ya Shilingi bilioni 45.4 kwa wajasiriamali 72,113 wakiwemo wanawake 26,261 na wanaume 45,852. Aidha, jumla ya fedha zilizorejeshwa ni Shilingi bilioni 35.6 ambazo ni sawa na asilimia 78.5 ya mikopo iliyoiva. Mikopo iliyotolewa na Mifuko ya uwezeshaji imeleta mafanikio makubwa kwa wajasiriamali wadogo kwa kuboresha mitaji yao. Vile vile, Mfuko wa Uwezeshaji (Mwananchi *Empowerment Fund*), hadi Aprili 2010, ulitoa dhamana kwa mikopo yenyenye thamani ya Shilingi bilioni 4.2 kwa wajasiriamali 4,437 wakiwemo wanawake 1,341 na wanaume 3,096.

Pia, Wizara iliendelea kuhamasisha uanzishwaji wa *SACCOS* kama njia muafaka ya kupata mikopo yenyenye masharti nafuu. Kutokana na juhudhi zilizofanyika, idadi ya *SACCOS* imeongezeka nchini kutoka 4,780 mwaka 2008 hadi kufikia 6,000 mwaka 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi iliendelea kutoa elimu ya ujasiriamali; ilifanya tafiti juu ya wakulima na wajasiriamali kwa lengo la kuwaunganisha na taasisi za utafiti ili wanufaikie na matokeo ya tafiti mbalimbali; ilifanya tafiti ya jinsi ya kuboresha sekta ya useremala ili kubaini namna ya kuinua viwango vya ubora wa bidhaa zinazozalishwa nchini na kuishauri Serikali na wadau wengine kununua samani za ndani badala ya zile zinazotoka nje. Aidha, zoezi la kuainisha aina za biashara zinazostahili kuendeshwa na Watanzania pekee na zile zinazoweza kuendeshwa kwa ubia na wageni lilifanyika

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara itatekeleza yafuatayo:-

Kuandaa mwongozo wa utekelezaji wa MKUKUTA II; kuandaa makadirio ya gharama kwa sekta kuu tano za MKUKUTA II; kukamilisha Mwongozo wa ufuatiliaji na Tathmini kuhusu mkakati wa utekelezaji wa masuala ya Uwezeshaji Kiuchumi; kuandaa na kuratibu utekelezaji wa mfumo wa ufuatiliaji wa MKUKUTA II; kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mradi wa *NIGP*. Aidha, Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa kuangalia maeneo yatakayoinua hali ya wananchi kiuchumi kwa muda mfupi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali; na kuifanyia marekebisho Sheria ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Namba 16 ya mwaka 2004 ili kulipa Baraza nguvu ya kubuni, kupanga, kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa mipango ya uwezeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usimamizi na udhibiti wa matumizi ya Serikali. Wizara imekamilisha majoribio ya kutumia mtandao wa Benki Kuu wa malipo ya Elektroniki wa *Tanzania Inter-bank Settlement System (TISS)*. Wizara imeandaa na kutoa miongozo ya matumizi ya mfumo huo ikiwa ni pamoja na kufanya semina elekezi kwa baadhi ya maafisa watakaotumia mfumo huo. Mfumo huu mpya utatekelezwa kwa awamu mbili kama ifuatavyo:-

Awamu ya kwanza imehusisha Wizara na Idara za Serikali zilizopo Dar es Salaam ikiwa ni pamoja na Mkoa wa Dar es Salaam ambao malipo yake yalikuwa yanalipwa kupitia Ofisi Kuu ya Malipo iliyopo Hazina makao makuu; awamu ya pili itahusisha Wizara, Idara za Serikali na Mikoa yote ambayo malipo yake yalikuwa hayalipwi kupitia Ofisi Kuu ya Malipo. Mfumo huu umeanza kutumika Julai, 2010 katika awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hesabu za mwaka za Serikali ziliendelea kuandaliwa kwa mara ya pili mfululizo kwa kutumia viwango vya kimataifa vya uandishi wa Hesabu (*IPSAs*). Hesabu za mwaka wa fedha ulioishia Juni 2009, zilitolewa moja kwa moja kutoka kwenye Mtandao wa Malipo wa Serikali (*IFMS*) na hivyo kuongeza ubora wa taarifa hizo. Ubora wa hesabu za mwaka unaendelea kuongezeka. Kwa mwaka wa fedha 2008/2009, Wizara na Idara 46, Mikoa 18 na balozi 28, sawa na asilimia 86, zilipata hati safi za ukaguzi kulinganisha na hali iliyokuwa mwaka 2004/2005 ambapo Wizara na Idara 15, na mikoa nane tu sawa na asilimia 34 ndio zilipata hati safi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Mpango na Bajeti unalenga kuendelea kusimamia udhibiti wa matumizi ya fedha katika Wizara, Idara zinazojitegemea, Mikoa na Halmashauri kuitia Mtando wa Malipo wa Serikali; kusimamia, kuimarisha na kuboresha uendeshaji na uunganishaji *IFMS*; kuimarisha mtandao kwa kuanza kushughulikia kasoro zilizoainishwa kwenye ripoti ya ukaguzi uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali; kuendelea kuimarisha kituo cha kuhifadhi kumbukumbu (*Disaster Recovery Site*); kuanzisha Idara ya Ukaguzi wa Ndani itakayowajibika kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali; kuimarisha kamati za ukaguzi (*Audit Committees*) katika Wizara, Idara zinazojitegemea, Mikoa na Halmashauri; kuboresha Kitengo cha Usimamizi wa Fedha (*Cash Management Unit*); kutayarisha majumuisho ya hesabu za Wizara, Mikoa na Idara zote za Serikali kwa viwango vya kimataifa (*IPSA*s); Kusimamia na kudhibiti mapato ya ndani na nje; na kuendeleza kada za uhasibu, ukaguzi, maafisa mipango na Wataalam wa kompyuta kutoka Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma kwa Wastaifu na Warithi. Katika jitihada za kuboresha utoaji wa huduma kwa wastaifu, Serikali imeendelea na kazi ya kuweka kwenye mfumo wa kompyuta kumbukumbu za wastaifu kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma kwa wastaifu. Kumbukumbu za majalada ya wastaifu 24,446 kati ya 45,000 yaliyokusudiwa kuwekwa kwenye mfumo wa kompyuta zimefanyika na kazi ya kuweka kumbukumbu za majalada yaliyobaki inaendelea. Vile vile, katika juhudzi za kuimarisha na kudhibiti malipo ya pensheni na kuboresha huduma kwa wastaifu, Serikali imeamua kutumia mfumo wa malipo unaoitwa Government Pension Payment System (*GPPS*) unaotumiwa na Mfuko wa Pensheni ya Mashirika ya Umma (*PPF*). Mafunzo ya namna ya kutumia mfumo huo kwa watumishi wa kitengo cha pensheni yametolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ushauri wa kisheria kwa Wizara, Idara na Taasisi. Katika mwaka 2009/2010, majukumu mbalimbali ya kisheria yanayohusu Wizara ya Fedha na Uchumi pamoja na Taasisi zake yametekelizwa ikiwa ni pamoja na:-

Kuandaa na kukamilisha Kanuni za kuwezesha matumizi ya mfumo mpya wa ukusanyaji kodi ya mapato unaotumia *Electronic Fiscal Devices* badala ya mfumo wa sasa unaotumia *cash registers*; kuandaa na kukamilisha Kanuni zinazoanzisha chombo cha ukusanyaji wa taarifa za wakopaji (*Credit Reference Bureau*); kuandaa na kukamilisha Azimio la Kuongeza Mtaji wa Mfuko wa kutoa Mikopo (*Advances Fund*) kwa Waheshimiwa Wabunge na Watumishi wa Serikali na kukamilisha marekebisho ya Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura 370 ambayo yaliwasilishwa katika Mkutano wa Bunge wa mwezi Aprili, 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu mengine yaliyotekelizwa yanajumuisha:-

Kuandaa na kukamilisha marekebisho ya Sheria ya Soko la Mitaji na Dhamana Sura 79 ambayo yaliwasilishwa katika mkutano wa Bunge wa mwezi Aprili, 2010 na kuandaa Muswada wa Sheria ya Ununuzi wa Umma wa mwaka 2010 ambao unatarajiwa kuwasilishwa katika mkutano huu wa Bunge la Bajeti unaoendelea. Aidha, Wizara katika

mwaka 2010/2011 itaendelea kuzipitia na kuzifanyia marekebisho sheria nyingine zinazosimamiwa na Wizara ili ziweze kwenda na wakati.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2009/10, Wizara kuitia Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma, ilitekeleza yafuatayo:-

Kuendesha mafunzo kuhusu utekelezaji wa Mkakati wa Kuzuia Rushwa kwenye Ununuzi wa Umma kwa taaasisi za umma 200; iliendelea na mchakato wa utafiti wa kuanzisha mfumo wa ununuzi wa umma kwa njia mtandao (*e-procurement*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, upembuzi yakinifu juu ya uanzishwaji wa mfumo huo umekamilishwa na masuala yaliyobainishwa katika utafiti huo yatashughulikiwa katika mwaka wa fedha 2010/2011; mafunzo kuhusu Sheria ya Ununuzi wa Umma na Kanuni zake yalitolewa katika kanda nne za Dar es Salaam, Arusha, Mwanza na Mbeya. Watumishi 1,901 pamoja na Wakagazi wa Ndani 100 wamefaidika na mafunzo hayo na ukagazi wa ununuzi katika taasisi za umma zipatazo 99 umefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara kwa kuitia Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma pamoja na kuendelea kutekeleza majukumu ya msingi yaliyomo kwenye Sheria ya Ununuzi, itafanya yafuatayo: kuimarisha uhusiano kati ya Mfumo wa ununuzi wa Umma na malengo ya MKUKUTA; kuendeleza harakati za kupambana na rushwa katika michakato ya ununuzi; kuongeza kiwango cha utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi kwenye Taasisi za umma kutoka asilimia 55 kufikia asilimia 80 na kuimarisha uwezo wa Mamlaka ili kuwafikia wadau wake kwa kupanua ofisi ikiwa ni pamoja na kufungua Ofisi za Kanda na kuongeza watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu rufaa za zabuni. Mamlaka iliyapitia na kutolea uamuvi mashauri 21 kati ya mashauri 23 yaliyopokelewa. Mashauri mawili yaliyobaki yanaendelea kushughulikiwa. Aidha, Mamlaka ilifanya uelimishaji umma katika mikoa ya Tanga, Tabora na Kigoma na pia katika Wilaya za Sengerema, Tarime na Korogwe ili kuwawezesha wadau kufahamu haki na wajibu wao pale wanapoona taratibu za ununuzi hazikuzingatiwa au haki haikutendeka katika utoaji wa zabuni. Pia, Mamlaka ilishiriki katika semina ya uelimishaji kwa Wabunge kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Mamlaka itaendelea kutekeleza majukumu yafuatayo:-

Kusikiliza na kusuluhisha migororo katika Ununuzi wa Umma; kuelimisha umma na wadau kwa ujumla kwa kukamilisha uelimishaji katika mikoa ambayo hajjaweza kufika; kukamilisha uandaaji wa taratibu za uwasilishaji wa Malalamiko katika lugha ya Kiswahili na kuzisambaza kama njia ya kuelimisha umma.

Mheshimiwa Spika, Huduma ya Ununuzi Serikalini. Kwa mwaka wa fedha 2009/2010 Wizara kuitia Wakala wa Ununuzi Serikalini (*GPSA*) ilianza utekelezaji wa utaratibu unaoziwesha Wizara, Idara, Taasisi za Serikali na Halmashauri kuanza kununua vifaa na huduma zitumikazo mara kwa mara (*common use items and services*)

kwa pamoja. Wakala uliitisha zabuni 13 za ununuzi wa vifaa na vyakula pamoja na zabuni tisa za utoaji huduma. Aidha, Wakala umeingia makubaliano na wazabuni 3,016 kwa niaba ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala umemwajiri Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kufanya upembusi yakinifu ili kubaini iwapo ununuzi wa mafuta ya magari ya Serikali unaweza kufanya kwa kutumia *Smart Card* ambapo kila gari la Serikali litapewa kadi kwa ajili ya ununuzi wa mafuta kwenye vituo vya mafuta vya Wakala. Aidha, Wakala umemwajiri mkandarasi kwa ajili ya kufanya kazi ya ukarabati na upanuzi wa kituo cha mafuta cha Dodoma. Zabuni ya ukarabati na upanuzi wa kituo cha mafuta Kurasini (Dar es Salaam) imeitishwa upya baada ya kukosa mzabuni mwenye sifa kwenye mchakato wa awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara imepanga kuimrisha wakala katika maeneo ya rasilimali watu, fedha, vitendea kazi pamoja na kuboresha mazingira ya kufanya kazi ili uweze kuchukua dhamana ya usimamizi wa ununuzi wa magari ya Serikali. Aidha, wakala umepanga kuimrisha mfumo wa ununuzi wa vifaa na huduma kwa pamoja kwa kujenga uwezo wa watumishi na wazabuni; kutekeleza matokeo ya upembusi yakinifu (*feasibility study*) kuhusu matumizi ya *Smart Card* na kukamilisha kazi ya kukarabati na kupanua uwezo wa visima vya mafuta Kurasini (Dar es Salaam) na Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Habari, Elimu na Mawasiliano kwa Umma. Wizara imeendelea kusimamia mawasiliano ya Habari kwa kutekeleza yafuatayo:-

Kutoa elimu kwa Umma kwa kutumia vyombo vya habari kuelezea mafanikio ya Wizara katika Serikali ya Awamu ya Nne pamoja na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 kwa kipindi cha miaka minne kuanzia Desemba 2005 – Desemba 2009; kuandaa documentary ya utekelezaji wa MKUKUTA I; kusanifu machapisho mbalimbali ya Wizara ili yasambazwe kwa wananchi wakati wa Maonesho ya kitaifa. Aidha, Tovuti ya Wizara (www.mof.go.tz) imeendelea kuhuishwa kwa kuwekewa taarifa mbalimbali za Wizara ikiwa ni pamoja na maeleo ya mgao wa fedha za matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukaguzi wa Ndani. Katika mwaka wa fedha 2009/10, Wizara iliendelea kusimamia kada ya Ukaguzi wa Ndani, kwa kuajiri na kutoa mafunzo ili kuimrisha ukaguzi wa ndani. Wizara iliendesha mafunzo yaliyohusu ukaguzi wa ununuzi na mikataba na mafunzo yaliyohusu mbinu za kubaini pamoja na kudhibiti matumizi mabaya ya fedha katika ununuzi na kandarasi; kufanya marekebisho ya Sheria ya Fedha za Umma Sura 348 kuititia Sheria ya Fedha 2010 (*The Finance Act, 2010*) ambapo inawezesha kuanzhishwa kwa Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani (*Internal Auditor General Department*); na Wizara inaendelea kukamilisha muundo wake ili kuwezesha uwepo wa Idara kamili ya ukaguzi wa ndani ambayo itaimarisha usimamizi wa kada na kazi za ukaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara itatekeleza yafuatayo:- kuijengea uwezo Idara mpya ya Ukaguzi wa Ndani kwa maana ya kuajiri watumishi ili kujaza nafasi kulingana na muundo wa Idara na kutoa mafunzo kwa watumishi wa Idara mpya ili kuendana na majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*). Katika mwaka wa fedha 2009/10, Mamlaka ya mapato Tanzania iliendelea na jukumu lake la ukusanyaji wa mapato ya Serikali chini ya Mpango wake wa *Tatu wa Maboresho wa Miaka Mitano (Third Corporate Plan)* ambao malengo yake ni pamoja na: kuziba mianya ya ukwepaji kodi; kudhibiti uvujaji wa mapato ya Serikali; kuendelea kutoa elimu ya biashara na kuimarisha namna ya ukokotoaji kodi kwa wafanyabiashara; kuboresha mifumo ya utendaji ya Idara ya Walipakodi Wakubwa; kuendelea kuboresha usimamizi na utendaji katika Idara ya Forodha kwa kuongeza uwajibikaji, matumizi ya teknolojia na kupunguza kero kwa walipa kodi; kuendelea kuimarisha usimamizi na udhibiti katika kupeleka mizigo kwenye bandari za nchi kavu (*Inland Container Depot - ICD*) ikiwemo matumizi ya teknolojia ya kisasa; na kuimarisha udhibiti wa bidhaa za mafuta ya petroli, ikiwemo kuhakikisha kuwa, mita za kupitishia bidhaa hizo (*flow metres*) zinafanya kazi kwa ufanisi wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Mamlaka ya Mapato Tanzania, imejipanga kuongeza juhudzi zaidi katika ukusanyaji wa mapato kwa kuendelea kupanua wigo wa kodi kwa kusajili walipa kodi wapya; kuendelea kusimamia kwa karibu mageuzi makubwa yanayoendelea ndani ya Mamlaka ya Mapato Tanzania chini ya Mpango wake wa *Tatu wa Maboresho wa Miaka Mitano (Third Corporate Plan)* ambayo yamekuwa msingi wa kuongezeka kwa mapato ya ndani mwaka hadi mwaka kwa kushirikiana na taasisi nyingine za Serikali; kuendelea kuchukua hatua za kuziba mianya ya uvujaji wa mapato ya Serikali na kuboresha ukaguzi wa kodi (*field and desk audits*) na usimamizi wa ukusanyaji wa malimbikizo ya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Bodi ya Rufani za Kodi ilipokea rufani 96 na maombi 23. Bodi ilisikiliza na kutolea maamuzi rufani 79. Kati ya hizo, rufani 12 zilikuwa ni zile zilizopokelewa mwaka 2008/2009. Aidha, kati ya maombi 23 iliyopokea, Bodi ya Rufani ilisikiliza na kutolea maamuzi maombi 22. Kati ya hayo, maombi sita yalikuwa ni yale yaliyopokelewa mwaka wa fedha 2008/2009. Vile vile, Wizara kupitia Baraza la Rufani za Kodi ilipokea na kutolea maamuzi rufani 23. Kati ya hizo, rufani tatu zilikuwa ni zile zilizopokelewa mwaka wa fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Bodi ya Rufani itaendelea kupokea, kusikiliza na kutoa maamuzi ya rufani za Kodi kwa wakati pamoja na kutoa elimu kuhusu taratibu za kukata rufaa katika maeneo ambayo elimu hiyo hajatolewa. Aidha, Bodi na Baraza la Rufani za Kodi, kwa pamoja zitakamilisha uchapishaji wa ripoti za kesi zote zilizoamuliwa tangu mwaka 2005 hadi 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usimamizi wa Mashirika na Taasisi za Umma. Mwaka wa fedha 2009/2010, Ofisi ya Msajili wa Hazina ilikusudia kukusanya kiasi cha Shilingi bilioni 38.4 kama maduhuli. Hadi kufikia Juni 2010 Ofisi iliweza kukusanya

maduhuli ya Shilingi bilioni 40.5 sawa na asilimia 105.5 ya makadirio. Katika kipindi hicho, Ofisi iliendelea kuchambua Miundo na Kanuni za Utumishi kwa mashirika 46, Kanuni za Fedha na Mifumo ya Mishahara ya Mashirika na Taasisi 32; kuchambua na kuidhinisha makadirio ya Ikama kwa Taasisi za Serikali 110 kwa ajili ya malipo ya mishahara na ajira mpya. Aidha, uchambuzi wa mikataba sita ya hiari kwa mashirika ulikamilishwa na uchambuzi wa mikataba miwili ya taasisi unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti kufuatia kupitishwa na Bunge kwa marekebisho ya Sheria ya Mashirika ya Umma Sura 257 na Sheria ya Msajili wa Hazina Sura 370, katika mwaka 2010/2011, Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha Ofisi ya Msajili wa Hazina ambayo ndiyo yenyewe jukumu la kusimamia mashirika na taasisi za umma kwa kurekebisha muundo wake ili iwe na mamlaka zaidi katika kusimamia kwa karibu mashirika na taasisi za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti Ukagazi wa hesabu za Serikali. Katika mwaka wa fedha 2009/2010, Ofisi ya Mdhibiti na Mkagazi Mkuu wa Hesabu za Serikali imetekeleza yafuatayo:-

Kukagua hesabu za mafungu yote ya Wizara na Idara za Serikali, Mikoa yote 21 ya Tanzania Bara na Serikali za Mitaa 133; Mashirika ya Umma 95, Balozi zote 32 nje ya nchi na Wakala za Serikali 33. Taarifa za ukagazi wa hesabu za mashirika 51 zilikamilika na kuwasilishwa Bungeni. Ukagazi wa hesabu za mashirika 105 unaendelea katika hatua mbalimbali ambapo Mashirika 10 yalikuwa hayajawasilisha hesabu zake kwa ajili ya ukagazi; Aidha, Ofisi imeendelea ujenzi wa ofisi za mikoa ya Lindi na Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Ofisi ya Mdhibiti na Mkagazi Mkuu wa Hesabu za Serikali imepanga kutekeleza yafuatayo:-

Kukagua mafungu ya Wizara na Idara za Serikali, hesabu za mikoa yote ya Tanzania Bara, hesabu za Halmashauri 133 za miji, Wilaya, Manispaa na Majiji pamoja na hesabu za mashirika ya Umma 170, Balozi zote 32 nje ya nchi na Wakala 33 za Serikali; kuendelea kuimarisha utendaji wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkagazi Mkuu wa Hesabu za Serikali; kuendelea na ujenzi wa ofisi za mikoa ya Kilimanjaro na Shinyanga pamoja na kuanza ujenzi wa ofisi za mikoa ya Dodoma na Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Pamoja ya Fedha. Katika mwaka wa 2009/10 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) zimeendelea na uchambuzi wa Taarifa mbalimbali za Tume kwa ajili ya kufanya maamuzi ya mapendekezo yaliyowasilishwa na Tume kuhusu vigezo vya kugawana mapato na kuchangia gharama za Muungano. Aidha, Tume imekamilisha mapendekezo ya Mwongozo wa Uendeshaji wa Akaunti ya Fedha ya Pamoja na Mfumo wa Bajeti utakaohusisha pande mbili za Muungano. Vile vile, Tume inaendelea na uchambuzi wa Deni la Taifa linalohusu Serikali mbili (SMT na SMZ). Hata hivyo,

kuhusu kufanya utafiti wa Mfumo wa Kodi utakaokubalika kwa pande mbili za Muungano, kazi hii inaendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Tume inakusudia kufanya yafuatayo: kukamilisha uchambuzi wa Deni la Taifa linalohusu Serikali mbili (SMT na SMZ); kufanya uchambuzi na kubainisha gharama za mambo ya Muungano; kujenga uwezo wa wataalamu wa Tume kufanya utafiti wa kufuatilia maendeleo ya kiuchumi kwa mambo ya Muungano; kufanya mapitio na kutekeleza kazi ya utafiti wa mfumo wa kodi utakaokubalika kwa pande mbili na kuendelea kutoa elimu kwa wadau na wananchi kuhusu uhusiano wa kifedha baina ya SMT na SMZ.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma za Kibenki, Benki Kuu ya Tanzania. Katika mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara ya Fedha na Uchumi kwa kushirikiana na Benki Kuu imeendelea kufanya mageuzi katika sekta ya fedha kwa lengo la kurekebisha sera na sheria mbalimbali za fedha ili kuongeza uwazi na ushindani katika utoaji wa huduma za kibenki na hivyo kurahisisha upatikanaji wa mikopo ikiwa ni pamoja na kupunguza riba kwa wakopaji. Benki Kuu ya Tanzania imeendelea kutekeleza Programu ya Awamu ya Pili ya Kurekebisha Sheria ya Fedha (*Second Generation Financial Sector Reform Program 2006 -2010*) ambapo mambo kadhaa yamefanyika yakiwemo:-

Kutungwa kwa Sheria inayoweka mazingira ya kuwezesha upatikanaji wa mikopo kwa njia ya ukodishaji vifaa, mitambo na rasilimali nyingine (*Lease Financing*); kutungwa kwa sheria ya mikopo ya nyumba ambayo inafanya marekebisho ya vipengele kadhaa vya Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 na nyinginezo ili kuweka mazingira ya upatikanaji wa mikopo ya nyumba. Aidha, Benki Kuu imeandaa Mkakati wa Kuboresha Huduma za Kifedha Maeneo ya Vijijini. Vile vile, Benki Kuu inaandaa Mkakati wa Elimu ya Fedha kwa Umma na utaratibu wa kisheria wa kuanzisha soko la dhamana za Halmashauri za Manispaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2010/11, Benki Kuu itaendelea kuimarisha sekta ya fedha ili iweze kukabili ipasavyo changamoto ya huduma na kupanuka kwa uchumi wa Taifa. Ili kufanikisha azma hii, Benki Kuu ya Tanzania itaendelea kufanya mageuzi katika sekta ya fedha ambayo yanalenga kurekebisha sera mbali mbali za fedha kwa kuongeza uwazi na ushindani katika utoaji wa huduma za kibenki na hivyo kurahisisha upatikanaji wa mikopo. Hii ni pamoja na kupunguza riba kwa wakopaji. Hatua hizi zitaenda sambamba na utekelezaji wa program ya Awamu ya Pili ya Kurekebisha Sekta ya Fedha.

Kadhalika, Serikali kupitia Benki Kuu itaanzisha utaratibu wa wa kukusanya na kusambaza taarifa za wakopaji (*Credit Information Sharing System*) ili kuwezesha wananchi kupata mikopo toka mabenki kwa urahisi. Benki Kuu imeandaa mkakati wa kuboresha huduma za kifedha maeneo ya vijijini (*Rural Financial Services Strategy*) ili kuongeza ushiriki wa wananchi vijijini katika kupata huduma za vyombo vya fedha. Benki Kuu inaandaa pia mkakati wa elimu ya fedha kwa umma (*Financial Literacy Strategy*) ili kuwahamasisha wananchi katika utumiaji wa huduma zitolewazo na taasisi za fedha na hivyo kuboresha maisha yao. Utaratibu wa kisheria unaandaliwa ili

kuwezesha kuanzishwa kwa soko la dhamana za Halmashauri za Manispaa. Uanzishwaji wa soko hili utawezesha Halmashauri za Manispaa kupata fedha za miradi ya maendeleo kwa kukopa kutoka soko hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Rasilimali Tanzania (*TIB*). Katika mwaka wa fedha 2009/2010, Benki ya Rasilimali Tanzania iliendelea kutoa mikopo ya maendeleo ya muda wa kati na mrefu, ambayo iliongezeka kutoka Shilingi bilioni 71.6 mwaka 2008 hadi kufikia Shilingi bilioni 81.8 mwaka 2009 ikiwa ni ongezeko la asilimia 14. Aidha, benki imeidhinisha mikopo ya Shilingi bilioni tano kuititia Dirisha la Kilimo, kati ya maombi ya Shilingi bilioni 31.8 yaliyopokelewa. Maombi ya mikopo mingine ipatayo Shilingi bilioni 14.3 yanaendelea kuchambuliwa. Vile vile, katika kipindi hicho amana za wateja ziliongezeka kwa Shilingi bilioni 16.3 kutoka Shilingi bilioni 88.1 hadi Shilingi bilioni 104.4 sawa na asilimia 18.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Serikali itaendelea kuimarisha mtaji wa *TIB* kwa kuwapatia fedha zaidi kwa shughuli za mikopo ya maendeleo na kwa ajili ya dirisha la Kilimo. Aidha, *TIB* inaendelea na mkakati wa kujirekebisha kwa kuunda kampuni mama (*TIB Limited*) kwa ajili ya mikopo ya maendeleo (*DFI*) na *TIB Corporate* itakayokuwa Benki ya Biashara kwa ajili ya wateja wake watakaochukua mikopo kwa muda wa kati na mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Bima la Taifa (*NIC*). Katika mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara iliendelea na mchakato wa kurekebisha Shirika la Bima la Taifa ili liweze kuongeza tija na kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. Kazi zilizotekelizwa ni pamoja na:-

Kutengeneza muundo mpya wa Shirika; kuandaa Ikama ya menejimenti na wafanyakazi wengine; imeajiri watumishi wapya katika ngazi zote; kuandaa Mpango wa Biashara na kuandaa Mfumo mpya wa TEKNOHAMA unaofaa kwa shughuli za bima. Aidha, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara itaendelea na zoezi la urekebishaji wa shirika hili pamoja na kusimamia uuzaji wa mali za shirika zilizoainishwa kuuzwa ili fedha zitakazopatikana zitumike katika kulipia malimbikizo ya madai ya bima na kuweka Mfumo mpya wa TEKNOHAMA utakaosaidia katika kuendesha shughuli za bima kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2009/10, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana iliendelea na majukumu yake kwa kufanya yafuatayo:-

Kukamilisha kazi ya kupitia Sheria ya Masoko ya Mitaji kwa kuzingatia Kanuni za Masoko ya Mitaji Duniani (*IOSCO Principles*) kwa lengo la kuiwezesha kushirikiana na wasimamizi wengine duniani. Marekebisho ya Sheria hiyo yamepitishwa na Bunge mwezi Aprili 2010. Marekebisho ya Sheria hiyo yanaruhusu kuanzishwa kwa soko la kukuza kampuni na ujasiriamali ndani ya Soko la Hisa la Dar es Salaam. Aidha, Wizara imeandaa rasimu ya Kanuni mbalimbali kuhusu utoaji wa leseni kwa washiriki wa soko la mitaji na kushughulikia maombi ya kampuni zinazotaka kuingia sokoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2010/2011, *CMSA* itaendelea kutekeleza mpango wake wa miaka mitano wa 2007/2008 - 2011/2012 kwa kufanya maandalizi ya kuanzishwa kwa Soko la Kukuza Kampuni za Ujasiriamali; kuendelea kuboresha Soko la Pili la Hatifungani za Serikali kwa kuzingatia matokeo ya utafiti uliofanyika kuhusu suala hili; kusimamia uanzishwaji wa Soko la Hatifungani za Serikali za Mitaa; kuboresha Mfumo wa Sheria ili kukidhi viwango vya Kimataifa; kuunganisha na Masoko ya Mitaji ya Afrika Mashariki pamoja na kuendelea na utoaji wa elimu kwa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi za Kitaalam na Huduma Nyinginezo. Ofisi ya Taifa ya Takwimu (*NBS*). Katika mwaka wa fedha 2009/10, Ofisi ya Taifa ya Takwimu ilieendelea kutekeleza majukumu yake ya kukusanya, kuchambua, kutunza na kuwasilisha takwimu zilizohitajika katika sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Takwimu za Pato la Taifa kwa kila nusu mwaka zilitolewa na kwa mara ya kwanza takwimu hizo zilitolewa kwa robo mwaka. Aidha, Ofisi ya Taifa ya Takwimu imeendelea kutayarisha takwimu za mfumuko wa bei kila mwezi. Kazi ya kutenga maeneo ya kuhesabia watu kwa ajili ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 inaendelea na imekamilika katika mikoa minane. Mikoa hiyo ni Pwani, Kilimanjaro, Manyara, Arusha, Morogoro na Dodoma kwa Tanzania Bara. Kwa upande wa Visiwani ni Unguja kaskazini na Unguja Kusini. Vile vile, Ofisi ya Taifa ya Takwimu imefanya majoribio ya utafiti wa Hali ya Rasilimali Watu nchini 2010 na utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada za kuboresha takwimu nchini, Ofisi ya Taifa ya Takwimu imeendelea na maandalizi ya Mpango Kabambe wa Kitaifa wa Kuboresha na Kuimarisha Takwimu nchini (*Tanzania Statistical Master Plan*) ambao umeidhinishwa na Serikali mwezi Juni 2010. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Taasisi itaendelea na:-

Maandalizi ya Sensa ya watu ya majoribio itakayofanyika Agosti 2011; kufanya tafiti zilizoainishwa katika MKUKUTA II kwa ajili ya kutoa viashiria vilivyobainishwa; kufanya uchambuzi wa Sensa ya Kilimo na Mifugo na kusambaza matokeo yake; kutoa takwimu za mfumuko wa bei kila mwezi; kutoa takwimu za Pato la Taifa kila robo mwaka na kutekeleza Mpango Kabambe wa kitaifa wa kuboresha na kuimarisha takwimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mpango wa *Millenium Challenge Account - Tanzania (MCA-T)*. Katika mwaka wa fedha 2009/10, *MCA-T* ilitekeleza kazi zifuatazo:-

Kukamilisha makabrasha ya usanifu na mipango ya fidia kwa barabara za Tanga – Horohoro, Namtumbo – Songea, Peramiho – Mbinga na Tunduma – Sumbawanga; kukamilisha zoezi la uteuzi wa Wahandisi Wasimamizi na Makandarasi; kuanza ujenzi wa barabara ya Tanga- Horohoro; kufanya upya usanifu wa barabara za Vijiji Pembra na kuandaa michoro ya kihadisi na ripoti ya athari za mazingira. Kazi zote hizi zilikamilika kama zilivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miradi ya umeme kazi zifuatazo zilifanyika:-

Usanifu, michoro ya kiuhandisi, ripoti ya mazingira na mipango ya fidia katika maeneo ya mradi wa kupeleka umeme Zanzibar kuititia chini ya bahari, kusaini mkataba kati ya *MCA-T* na kampuni ya *VISCAS* ya Japan kwa kazi ya kuweka nyaya za umeme kuititia chini ya bahari kwenda Zanzibar; kukamilisha zoezi la uchujaji wa makampuni kwa kazi ya ukarabati ya vituo vya umeme (*sub-stations*) na kutangaza zabuni na kuanza uchambuzi wa makampuni kwa kazi ya ukarabati wa mtandao wa umeme katika Mikoa ya Tanga, Morogoro, Iringa, Mbeya na Mwanza. Kwa miradi ya maji, kazi zilizofanyika ni kukamilisha michoro ya kiuhandisi na makabrasha ya zabuni za miradi ya ujenzi wa chujio la maji Ruvu Chini kwa wakazi wa Dar es Salaam na Pwani na mfumo wa maji kwa mkoa wa Morogoro.

Kwa mwaka 2010/2011 kazi ya ujenzi kwa miradi mingi chini ya *MCA-T* itaanza kutekelezwa kwani mikataba yote mikubwa itakuwa imesainiwa na wakandarasi kuanza kazi ifikapo Septemba 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio yaliyopatikana baadhi ya changamoto zilizojitokeza ni kama ifuatavyo:-

- (i) Makusanyo ya mapato ya ndani kuwa chini ya malengo ya kila mwezi na hivyo kusababisha ugawaji wa rasilimali fedha kuwa chini ya malengo;
- (ii) Ucheleweshaji wa uwasilishaji wa hati za madai Wizarani;
- (iii) Ucheleweshaji wa Majalada ya watumishi wanaotakiwa kustaafuli na kufikishwa Hazina yakiwa na nyaraka pungufu;
- (iv) Upungufu katika Sheria ya Msajili wa Hazina na Sheria zilizoanzisha Asasi na Mashirika mbalimbali;
- (v) Upungufu katika kusimamia ununuza wa Umma na udhibiti wa fedha za Umma;
- (vi) Upungufu wa Ofisi kwa watumishi wa Wizara; na
- (vii) Kuwasilishwa kwa maombi mengi nje ya Bajeti mara baada ya Bajeti kuidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na changamoto hizo, hatua zifuatazo zilichukuliwa:-

- (i) Wizara kwa kuititia *TRA* inaendelea na mikakati mbalimbali ya kupunguza mianya ya ukwepajji kodi na kurekebisha upungufu katika ukusanyaji wa mapato;
- (ii) Wizara imewashauri wadai kuwasilisha hati zao za madai kwa wakati;

(iii) Wizara imewaelimisha Maafisa Utumishi kuhusu kuandaa na kuwasilisha mapema nyaraka za watumishi wao wanaotarajia kustaifu;

(iv) Marekebisho ya sheria ya msajili wa Hazina (Sura 370) yamefanyika na Sheria imeshapitishwa katika Bunge la mwezi Aprili mwaka 2010 na Sheria zilizoanzisha Asasi na Mashirika mbalimbali zinaendelea kupitiwa;

(v) Sheria ya Fedha za Umma na ya Ununuvi wa Umma zimepitiwa na kufanyiwa marekebisho;

(vi) Wizara katika mpango wa muda mfupi, imeendelea kutafuta ofisi na katika mpango wa muda mrefu Wizara imepanga kujenga jengo la ofisi; na

(vii) Wizara imeendelea kuwakumbusha Maafisa Masuuli kusimamia upangaji wa vipaumbele vya maeneo yao na kuhakikisha fedha za kutosha zinatengwa kwa maeneo hayo pamoja na kufuata taratibu za Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza majukumu ya Wizara na kufikia malengo yaliyokusudiwa katika mwaka wa fedha 2010/2011, naomba Bunge lako liidhinishe kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Uchumi:-

- (i) Matumizi ya kawaada ni shilingi 94,271,677,000 (bilioni 94.27). Kati ya hizo, Mishahara ni shilingi 2,957,023,000 (bilioni 2.96) na matumizi mengineyo shilingi 91,314,654,000 (bilioni 91.31).
- (ii) Miradi ya Maendeleo shilingi 278,921,290,000 (bilioni 278.92). Kati ya hizo, fedha za ndani ni shilingi 7,309,135,000 (bilioni 7.31) na fedha za nje ni shilingi 271,612,155,000 (bilioni 271.61).

Fungu 21 - Hazina:-

- (i) Fedha za matumizi ya kawaada ni shilingi 962,062,861,500 (bilioni 962.10). Kati ya hizo, shilingi 1,238,047,000 (bilioni 1.24) ni mishahara na shilingi 960,824,814,500 (bilioni 960.82) ni kwa ajili ya matumizi ya Idara na Taasisi zilizo chini ya Wizara, marekebisho ya mishahara ya watumishi wa Serikali, pamoja na matumizi maalum ikiwemo dharura na michango ya Kimataifa.
- (ii) Fedha za miradi ya maendeleo ni shilingi 100,023,194,000 (bilioni 100.02). Kati ya hizo, fedha za ndani ni shilingi 50,832,264,000 (bilioni 50.83) na fedha za nje ni shilingi 49,190,930,000 (bilioni 49.20).

Fungu 22 – Deni la Taifa:-

Deni la Taifa shilingi 1,747,233,792,000 (bilioni 1,747.23).

Fungu 23 – Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali:-

- (i) Fedha za matumizi ya kawaida ni shilingi 82,344,269,000 (bilioni 82.34). Kati ya hizo, mishahara ni shilingi 2,794,013,000 (bilioni 2.80) na matumizi mengineyo ni shilingi 79,550,256,000 (bilioni 79.55).
- (ii) Fedha za miradi ya maendeleo ni shilingi 10,264,794,000 (bilioni 10.26). Kati ya hizo, fedha za ndani ni shilingi 4,185,752,000 (bilioni 4.20) na fedha za nje ni shilingi 6,079,042,000 (bilioni 6.10).

Fungu 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi:-

- (i) Fedha za matumizi ya kawaida ni shilingi 26,574,258,500 (bilioni 26.57). Kati ya hizo, mishahara ni shilingi 3,216,577,000 (bilioni 3.22) na matumizi mengineyo ni shilingi 23,357,681,500 (bilioni 23.36).
- (ii) Fedha za miradi ya maendeleo ni shilingi 10,581,010,000 (bilioni 10.58). Kati ya hizo, fedha za ndani ni shilingi 4,812,494,000 (bilioni 4.81) na fedha za nje ni shilingi 5,768,516,000 (bilioni 5.77).

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii ya Wizara ya Fedha na Uchumi inahitimisha uwasilishaji wa mapendekezo ya Serikali ya Bajeti ya mwaka 2010/2011 kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Mikoa na Serikali za Mitaa. Aidha, tunatarajia leo hii Bunge lako Tukufu litapata fursa ya kuitisha Muswada wa kuidhinisha matumizi ya Serikali kwa mwaka huu. Kama nilivyooleza katika hotuba ya Bajeti ya Serikali, Mkutano huu wa Bunge ni wa mwisho katika muhula huu wa kwanza wa Serikali ya Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi chote cha Bunge hili la Bajeti, Serikali imefarijika na maoni na ushauri kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge wa kuboresha maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika maeneo mbalimbali yakijumuisha kilimo, ufügaji, uvuvi, miundombinu ya barabara, reli, bandari, nishati, sekta za maendeleo ya jamii (Elimu, Afya, Maji), viwanda, mawasiliano na sekta ya fedha. Vile vile, Serikali imefaidika na maoni na ushauri wa Bunge hili katika kuboresha Utawala Bora na Uwajibikaji, Mazingira, Usawa wa kijinsia na Demokrasia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine tena napenda kumshukuru Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuonyesha imani yake kubwa kwangu ya kunitua kuwa Waziri wa Fedha na Uchumi Wizara ambayo ina majukumu makubwa kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wadhifa ambao kwanza namshukuru lakini pili, naamini kuwa nimeutumikia kwa uadilifu mkubwa. Napenda kumshukuru Mheshimiwa Dr. Ali Mohammed Shein, Makamu wa Rais kwa kusimamia kwa uhodari mkubwa vikao vya

mashauriano kuhusu kero za Muungano baina ya Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na masuala ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kumshukuru Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda kwa kusimamia shughuli za Serikali Bungeni kwa umahiri mkubwa ulionisaidia sana katika utekelezaji wa kazi zangu. Lakini kwa kipekee napenda kumshukuru kwa ukaribu wake na Wizara ya Fedha na Uchumi. Nisingeweza kufanikiwa kama isingekuwa ukaribu wake wa Wizara ya Fedha na Uchumi na misaada yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa ushirikiano wao mkubwa. Napenda pia kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano wao wakati wa kujadili nyaraka mbalimbali za Serikali nilizowasilisha Bungeni. Kipekee, napenda kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Kilosa kwa kunipa fursa ya kuwawakilisha katika awamu hii. Ni matumaini yangu kwamba sikuwaangusha na hivyo natarajia watanipa fursa nyingine ya kuendelea kuwatumikia ili kukamilisha kazi niliyoianza. Tumefanya mengi kwa pamoja katika kipindi hiki, mengi yamekamilishwa, mengine yanaendelea, nahitaji kipindi cha pili kuyakamilisha yote yanayoendelea. Nina hakika wananchi wa Kilosa wanansikia na watanipa nafasi ya kuwawakilisha tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwa namna ya kipekee kuwashukuru mke wangu Khalda, wanangu na wajukuu zangu kwa uvumilivu wao na kwa upendo mkubwa kwangu mimi kwa nyote nyinyi pamoja na Wabunge nasema ahsanteni sana na ni matumaini yangu kwamba wengi wetu tutakutana tena ndani ya Bunge lako Tukufu mwezi Novemba, 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi Mheshimiwa Mkullo kwa hotuba yako nzuri yenyekuti kutoa matumaini kwa Watanzania lakini pili kwa ujumbe wako kwa ndugu zangu wa Kilosa na wawakilishi wao wako hapa kwenye *gallery*. Jamani Kilosa mmesikia, bila ya Mkullo mafuriko yale....

Ahsante sana sasa nina matangazo. Mheshimiwa Kwaangw', Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii anaomba Wajumbe wake kwamba mkutane saa kama hizi ukumbi namba 227, jengo la Utawala.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Gideon Cheyo anaomba Kamati hiyo mkutane mara baada ya kikao cha jioni kuahirishwa katika ukumbi

wa *Basement*. Aidha, Mawaziri wa Wizara zetu zote za Kisekta wanaombwa wahudhurie, inaelekea hii Kamati ina mambo maalum.

Mheshimiwa Mohamed Missanga anaomba Wajumbe wa Kamati yake ya Miundombinu kwamba saa 7.00 mchana mkutane ukumbi Namba 231. Mwisho, naendelea kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kuchukua fomu zile za kutoka kwa Kamishna wa Maadili kuzijaza na kuzirudisha pale mahali panapostahili kwa sababu siku zenyeze zinakwishakwisha. Basi baada ya hapo naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi iliyopitia Makadirio ya Wizara ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Abdallah Kigoda. Mheshimiwa Kigoda karibu sana. (*Makofi*)

MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA - MWENYEKIDI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni ya 99(7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Fedha na Uchumi kwa mwaka wa fedha 2009/2010 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2010/2011:-

Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Uchumi, Fungu 21- Hazina, Fungu 22 – Deni la Taifa, Fungu 23 – Mhasibu Mkuu wa Serikali na Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ambalo linaombewa fedha Bungeni na Waziri wa Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kumalizia utangulizi huu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Handeni nichukue fursa hii kumpongeza sana Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa ushindi mkubwa alioupatata kwa kumchagua kwetu kwa kura nyingi kuwa mgombea wetu wa Urais kuptitaa Chama cha Mapinduzi. Mwenyezi Mungu amuongzee hekima, busara na afya ili azidi kutuongoza. Aidha, nimpongeze Dr. Gharib Bilal kuwa mgombea mwenza na Dr. Ali Mohamed Shein kuchaguliwa kwake kugombea nafasi ya Urais Zanzibar. Wote tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inachukua fursa hii kuipongeza Wizara ya Fedha na Uchumi kwa kutekeleza vyema malengo yake kwa mwaka uliotangulia ikiwa ni pamoa na mipango mizuri waliyojiwekea kwa mwaka huu wa fedha. Kamati inampongeza Waziri kwa umakini mkubwa iliyouchukua katika kuendesha na kusimamia uchumi hasa ikizingatiwa kwamba uchumi wetu ulipita kipindi kigumu cha mtikisiko wa uchumi duniani ulioleta mpaka hatua za kunusuru uchumi kutekelezwa. Bila ya umakini huo uchumi wa nchi ungedorora kwa kiasi kikubwa. Tunaipongeza sana Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilikutana tarehe 08 Julai 2010 na kupokea maelezo ya muhtasari wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Uchumi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011. Aidha, Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hiyo na mafungu yake kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010. Napenda kuchukua fursa hii kuipongeza Wizara ya Fedha na Uchumi kwa kutekeleza vyema malengo yake kwa mwaka uliotangulia ikiwa ni pamoa na mipango mizuri waliyojiwekea kwa Mwaka huu wa Fedha. Kamati inaipongeza Wizara kwa umakini mkubwa uliyoichukua katika kuendesha na kusimamia uchumi hasa ikizingatiwa uchumi wetu ulipitaa kipindi kigumu cha mtikisiko wa uchumi duniani ulioleta mpaka hatua za kunusuru uchumi kutekelezwa.

Bila ya umakini huo, uchumi wa nchi ungedorora kwa kiasi kikubwa. Tunaipongeza Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeendelea kutoa michango, ushauri na maelekezo ambayo Wizara ya Fedha na Uchumi imeendelea kuyazingatia katika kuboresha utekelezaji wa majukumu yake ya:-

Kubuni na kusimamia utekelezaji wa Sera na Mikakati ya Uchumi; Kusimamia ukusanyaji wa mapato ya ndani na nje na matumizi ya Serikali; Utekelezaji wa MKUKUTA, Sera ya Uwezeshaji wananchi Kiuchumi na kupanga mipango ya maendeleo; kusimamia Sheria, Kanuni na Taratibu za Uhasibu, ukaguzi wa ndani Serikalini, ununuzi wa umma na usimamizi wa mali ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2009/2010, Kamati ilitoa maoni na ushauri juu ya utekelezaji katika maeneo mbalimbali ya kukuza Uchumi. Katika kuititia Taarifa ya Wizara, Kamati iliridhika na utekelezaji wa baadhi ya ushauri iliyoutoa kwa Wizara. Hata hivyo bado yapo yanayohitaji kuangaliwa ili kuendeleza ufanisi na tija katika Uchumi wetu, kuititia utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika Kipindi cha mwaka 2009/2010, bado Wizara inakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo zinabidi kuzingatiwa katika kipindi cha 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna upungufu mkubwa katika ukusanyaji wa mapato ya ndani. Katika kipindi cha mwaka 2009/2010 Wizara ililenga kukusanya mapato ya ndani kiasi cha shilingi bilioni 5,096.016 ili kufikia lengo la asilimia 16.4 ya pato la Taifa. Hadi Aprili Wizara ilikusanya shilingi bilioni 3,821.162 sawa na asilimia 90.7 ya lengo. Hali hii bado inahitaji Wizara kufanya jitihada za kubuni vyanzo vipyta vya mapato badala ya kutegemea vyanzo vile vilivyozooleka sasa kwa muda mrefu. Kamati inasisitiza umuhimu wa kuongeza mapato ya ndani ili Serikali iweze kujidoresha kwa mapato yake yenye pamoja na mkakati wa muda mrefu wa kupunguza kutegemea misaada ya wahisani. Wizara inabidi iangalie upya eneo la matumizi katika uchumi ambayo yamekuwa makubwa kuliko kiasi kinachokusanywa pamoja na udhibiti wa matumizi ya fedha nje ya bajeti zilizoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeishauri Wizara kufanya kazi kwa pamoja na sekta nyingine hasa katika eneo la kudhibiti ukosefu wa mapato. Tatizo, kwa mfano, la uchakachuaji wa mafuta na kadhalika yanayosababisha Taifa upotevu wa mabilioni ya fedha, yanapotoka yanahitaji kushughulikiwa kwa haraka. Hatua hizi zikichukuliwa na nyinginezo kuna uwezekano wa uchumi wetu ukafikia viwango vya mapato kwa asilimia 18-20 ya Pato la Taifa. Aidha, taratibu za utekelezaji wa MKURABITA ziharakishwe (*formalization of informal sector*). Kamati vile vile inaendelea kuishauri Serikali ili kuongeza mapato ya uchumi wetu, Wizara irejee maeneo yote ya misamaha ya kodi na kupunguza yale maeneo ambayo siyo ya ulazima kupata misamaha hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaona kama vile Serikali inakinzana na azma yake ya kuiachia jukumu sekta binafsi ya kuendesha uchumi. Hali hii inajitokeza katika maeneo yafuatayo:-

(a) Uanzishwaji wa Mamlaka na Mawakala (*Authorities and Executive Agencies*).

(b) Kutokusimamia kikamilifu tatizo la kupunguza gharama za uanzishaji biashara /miradi katika uchumi wetu (*cost of doing business*). Pamoja na azma ya kuwasilisha marekebisho ya Muswada wa Manunuzi hapa Bungeni, bado rasimu inaonyesha mlolongo mkubwa wa mchakato mzima, ikilinganishwa na nchi jirani. Wakati Kenya na Uganda, mchakato wa manunuzi hauzidi siku 45, Tanzania tunachukua muda wa siku 80-100. Urasimu huu hausaidii na hauvutii sekta binafsi, marekebisho yatakayoletwa yalenge kupunguza siku za mchakato hadi 40. Aidha, rasimu ya Muswada ya PPP ambayo una lengo la kutafuta rasilimali fedha toka sekta binafsi kushirikiana na umma, nayo vilevile haukuzingatia tatizo la thamani ya muda (*value of time*) licha ya thamani ya fedha (*value for money*). Kamati kupitia Wizara inaishauri Serikali kuyaangalia upya maeneo haya ili kuboresha ushiriki wa sekta binafsi katika uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imejifunza toka Wizarani kuwa baadhi ya fedha zinazotolewa na wahisani kwa baadhi ya miradi mbalimbali hapa nchini zimekuwa zikirudishwa kwa wahisani wenyewe kutokana na urasimu wa utekelezaji wa miradi hiyo na tatizo la uwezo mdogo wa kutumia fedha hizo kwa wakati tunazopipata, (*Low absorption capacity*). *Absorption Capacity* ya nchi ya Rwanda ni kati ya asilimia 46-56 wakati Tanzania ni asilimia 23 tu. Matokeo yake ni kushindwa kutumia fedha hizo za wahisani kama zilivyopangwa kwa wakati. Hali hii inaweza kuathiri kwa kiwango fulani utekelezaji wa miradi hasa ile ya maendeleo. Aidha tunapoangalia Deni la Taifa na tunaposema linahimilika (*Sustainable National Debt*), inabidi tujulize tukilinganisha na nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Kamati kuipongeza Serikali kwa kuwajali wastaafu na kuboresha huduma zao, bado kuna tatizo katika utunzaji wa kumbukumbu za watumishi waliostaafu kwa ajili ya kupata huduma ya pensheni. Kamati inatoa wito kwa Waajiri na Waajiriwa kuhakikisha wanatunza nyaraka zao zote zinazohusika katika utoaji wa pensheni za wastaafu ili kuwapunguza makali yao ya maisha wastaafu husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia uamuzi wa Serikali wa kupandisha kima cha chini cha pensheni kutoka shilingi 21,601/= kwa mwezi hadi shilingi 50,114/= kwa mwezi kuanzia mwezi Julai 2009, bado kuna malalamiko ya utekelezaji wa nyongeza za pensheni za wastaafu katika baadhi ya Mifuko ya Jamii. Kamati inaishauri Wizara kufuatilia suala pamoja na kuharakisha mchakato wa uanzishwaji wa chombo kitakachosimamia Mifuko hii ya Jamii kwa kuwa Sheria ilishapitishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaamini kuwa hakuna nchi iliyoendelea kiuchumi hapa duniani bila ya kukopa, hata hivyo Serikali inapokopa ihakikishe kuwa

mikopo hiyo ni ya masharti nafuu na riba ndogo; matumizi ya mikopo hiyo yalenge kwenye miradi ya maendeleo inayokuza uchumi kama vile miundombinu ya reli, bandari na barabara; elimu; afya na kilimo. Kamati inaishauri Wizara isitegemee kukopa tu *IMF* na Benki ya Dunia, bali itafute vyanzo vingine. Zipo nchi zinazoweza kutukopesha kwa masharti nafuu kama vile nchi ya China na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeendelea kuishauri Serikali kwa vile sasa tunaingia katika Soko la Pamoja la Afrika Mashariki, lazima tulinde maslahi yetu katika yale maeneo ambayo tuna uwezo nayo, kwa mfano viwanda vyetu vya saruji. Hivi sasa soko letu limejaa saruji (*Cement*) kutoka nje ya nchi kwa sababu ya viwango vikubwa vya ushuru kwa bidhaa hii. Hali hii inaathiri uzalishaji katika viwanda vyetu nchini na hivyo kuleta athari katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustafa Mkullo; Naibu Mawaziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Omary Yusuf Mzee na Mheshimiwa Jeremiah Sumari, Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Wakuu pamoja na wataalam wao kwa kuwa tayari kutoa ufanuzi na kupokea maoni na ushauri wa Wajumbe wa Kamati yangu wakati wote wa mjadala wa makadirio haya. Aidha, Kamati inatoa shukrani kwa Taasisi na Idara zote zilizo chini ya Wizara hii kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati katika kipindi chote cha mwaka wa Fedha uliotangulia. Ni matarajio ya Kamati kuwa ushirikiano huu utaendelea katika mwaka ujao wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi ambao wameweza kutoa maoni na michango ya mawazo yao mbalimbali na kushughulikia katika Kamati hii na kuboresha Makadirio haya ili hatimaye yaletwe mbele ya Bunge hili Tukufu. Naomba nitumie fursa hii kwanza kuwaombea kila la kheri katika uchaguzi ulio mbele yetu na pili kuwatambua wajumbe wote kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda, Mwenyekiti; Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Elizabeth N. Batenga, Mjumbe; Mheshimiwa Andrew Chenge, Mjumbe; Mheshimiwa Fatma Abdulhab Fereji, Mjumbe; Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, Mjumbe; Mheshimiwa Athumani Said Janguo, Mjumbe; Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mjumbe; Mheshimiwa Eustace Osler Katagira, Mjumbe; Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, Mjumbe; Mheshimiwa Clemence Beatus Lyamba, Mjumbe; Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge, Mjumbe; Mheshimiwa Monica Ngenzi Mbega, Mjumbe; Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, Mjumbe; Mheshimiwa Felix C. Mrema, Mjumbe; Mheshimiwa Mossy S. Mussa, Mjumbe; Mheshimiwa Damas Pachal Nakei, Mjumbe; Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mjumbe; Mheshimiwa Dr. Omar Mzeru Nibuka, Mjumbe; Mheshimiwa Sijapata Fadhili Nkayamba, Mjumbe; Mheshimiwa Suleiman Ahmed Saddiq, Mjumbe; Mheshimiwa Mzee Ngwali Zuberi, Mjumbe; Mheshimiwa Devota Mkuwa Likokola, Mjumbe; Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mjumbe na Mheshimiwa Charles Kajege Mjumbe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kutoa shukrani kwa Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika kwa niaba ya Kamati, kwa Katibu wa Bunge Dr. Thomas Kashillilah pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake. Aidha, napenda kuwashukuru Ndugu Michael Kadebe na Ndugu Lawrence Makigi, Makatibu wa Kamati hii kwani sote kwa pamoja tumeweza kukamilisha maandalizi ya Makadirio haya kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho na sio kwa umuhimu, napenda kuwashukuru sana kwa ushirikiano mkubwa nilioupata kutoka kwa wapiga kura wangu wa Jimbo la Handeni. Ujumbe wangu bado ni ule ule “Mambo mazuri hayataki haraka”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Uchumi pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa mwaka wa fedha 2010/2011 kama alivyowasilisha mtoa hoja muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED –MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, naomba kwa idhini yako niwasilishe Maoni ya Kambi ya Upinzani. Naomba upokee shukrani zetu za dhati kwa kunipa nafasi hii ili nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Fedha na Uchumi kwa mwaka wa fedha 2010/2011 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 99(7), toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru sana Wanachama wa Chama cha *CUF* wa Jimbo la Wawi kwa kunipa ridhaa tena ya kuwania tena nafasi ya Ubunge kuitia Jimbo la Wawi. Aidha, niwashukuru sana wananchi wote wa Jimbo la Wawi kwa mshikamano na mashirikiano yao walijonipa kwa muda wote wa uongozi wangu, nawaahidi kuongeza bidii ya kuwatumikia katika kipindi kijacho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba kutoa shukurani zangu za dhati kwa wabunge wote wa Kambi ya Upinzani kwa ushirikiano wao mkubwa, wakiongozwa na Dr. Wilbrod Slaa, Naibu Kiongozi wa Upinzani kwa kuniwezesha kuiongoza vyema Kambi yetu kwa kipindi chote cha miaka mitano bila ya kutetereka katika uwasilishaji wa maoni mbadala kwa hoja zote zilizoletwa hapa Bungeni. Kazi yangu haikuwa rahisi, ilihitaji ushirikiano mkubwa kutoka kwa wenzangu. Nawashukuru sana kwa msaada wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa namna ya kipekee, niwapongeze Mheshimiwa Profesa Ibrahim Haruna Lipumba, Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Wananchi (*CUF*), Mheshimiwa Juma Duni Haji na Maalim Seif Sharif Hamad, Katibu Mkuu wote kwa kuchaguliwa kwa asilimia isiopungua 99% kugombea nafasi za Urais wa Jamhuri ya Muungano na Urais wa Zanzibar. Naamini kuwa Watanzania, kama kutakuwa

na uchaguzi ulio huru, haki na wazi watawapa ridhaa ya kuongoza Taifa letu ili na wenzetu wapate fursa ya kuwa Mawaziri vivuli na sisi tupate fursa ya kutekeleza yale tuliyokuwa tukishauri kila mwaka katika kipindi cha miaka mitano iliyopita. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwapongeze Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, Dr. Mohamed Gharib Bilali na Dr. Mohammed Ali Shein kwa kuchaguliwa kwao kuwa wagombea kwa tiketi ya CCM katika nafasi ya Urais wa Jamhuri na ile ya Zanzibar. Tunaamini timu zote mbili ile ya *CUF* na CCM, zitaingia katika uchaguzi kwa lengo moja kuu la kuwaletea maendeleo endelevu Watanzania, ambayo yameambatana na amani, umoja na utulivu wa Taifa letu. Tunashukuru kazi iliyofanywa na vyama vyetu kwa kututeulia wagombea amba ni wapenda amani, umoja na maendeleo. Naamini tutashindana kwa hoja, sera na sio matusi wala kukashifiana. Nawatakia kila la heri, naamini Watanzania watawapa ridhaa timu ya *CUF* ili waone mabadiliko katika maendeleo ya nchi yetu. *Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee naomba kuwashukuru sana wanachama wa chama cha *CUF* kwa kunipa ridhaa tena ya kuwania nafasi ya Ubunge kupitia Jimbo la Wawi. Aidha, niwashukuru sana wananchi wote wa Jimbo la Wawi kwa mashirikiano yao walijonipa kwa muda wote wa uongozi wangu. Nawaahidi kuongeza bidii ya kuwatumikia katika kipindi kijacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru wewe binafsi kwa kuliongoza Bunge letu katika kipindi hiki kwa viwango vinavyotakiwa Kimataifa na kulijengea Bunge letu heshima katika Mabunge ya dunia na hasa yale ya Jumuiya ya Madola. Aidha, naomba niwapongeze wasaidizi wako, Ofisi ya Katibu wa Bunge kwa kujitahidi kutoa utumishi ulio bora kwa wafanyakazi na Wabunge, huku tukielewa kuwa sio rahisi kumridhisha kila mtu, lakini Kambi ya Upinzani inashukuru huku ikiamini kuwa maboresho yatafanywa ili kujenga Kambi ya Upinzani iliyo imara zaidi ambayo naamini katika Bunge lijalo itaundwa na Chama Cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza Waziri wa Fedha Mheshimiwa Mustafa Mkullo, Manaibu Waziri, Katibu Mkuu na Manaibu wake, pamoja na wakuu wa vitengo na asasi zilizo chini yao kwa maandalizi ya Bajeti hii. Naelewa ugumu na uzito wa kazi yao, Mola akipenda baada ya mwezi Oktoba kazi hiyo itafanywa na Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee naomba nimpongeze Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda, Waziri Mkuu, kwanza kwa kutupa ushirikiano wa hali ya juu katika kutimiza majukumu yetu kama Kambi ya Upinzani, lakini pia kwa namna alivyoweza kusimamia shughuli za Serikali ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni shahidi namna Waziri Mkuu alivyoweza kuunganisha Bunge kama Mhimili mmoja na Serikali kama Mhimili mwingine. Misuguano na migongano imepungua kwa kiasi kikubwa kama sio kumalizika kabisa. Aidha, nampongeza kwa namna alivyohimili maswali ya papo kwa papo. Alijibu maswali

yote kutokana na ujuzi wake, lakini kwa heshima na hekima ya hali ya juu. Mungu akubariki wewe na familia yako yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani za pekee ni kwa mratibu mshauri wa Kambi ya Upinzani Ndg. Oliver Mwikila, ambaye anafanya kazi kubwa na nzito kwa Kambi ya Upinzani lakini hadi sasa tunamlipa sisi wenyewe (Wabunge wa Kambi ya Upinzani), Katibu Muhtasi Mama Salvina Mahundu na Mhudumu Grace Samuel kwa mchango wao mkubwa wa kuisaidia Kambi yetu kutimiza majukumu yake. Hawa wamekuwa watumishi wa mfano, kwani kuhudumia kambi nzima kwa kipindi chote hicho sio rahisi. Tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya fedha na uchumi majukumu yake makubwa ni kubuni na kusimamia utekelezaji wa sera na mikakati ya uchumi ikiwemo kubuni vyanzo vya ukusanyaji wa mapato ya ndani na nje pamoja na matumizi yake, utekelezaji wa MKUKUTA na kubuni sera ya uwezeshaji wananchi kiuchumi pia kuboresha usimamizi wa rasilimali fedha na uwajibikaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa za Serikali inaonyesha kuwa kulikuwa na upungufu wa asilimia 9.3% ya makusanyo ya mapato ya ndani kwa mwaka wa fedha 2009/2010 na upungufu huo ulitokana na kupungua kwa uzalishaji wa bidhaa zinazotozwa kodi hasa sigara, bia na vinywaji baridi. Pia upungufu katika mapato yasiyo ya kodi ya asilimia sita ulijitokeza kwenye ada na tozo mbalimbali. Aidha, mapato kutokana na misaada ya kibajeti na mikopo kutoka nje ina upungufu wa asilimia kumi na tatu kwa jumla. Hivyo, kuna jumla ya upungufu wa mapato ya ndani na nje ya asilimia ishirini na nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama takwimu hizi za Waziri ni sahihi (ambazo nimezitoa katika kitabu cha hotuba yake) ni vyema akatueleza ni vipi atawezeku kabiliana na bajeti ya mwaka huu tukitilia maanani kuwa kuna matumizi makubwa ya uchaguzi, vitambulisho na mishahara. Kambi ya Upinzani inapenda kupata ufanuzi wa namna gani *TRA* itaweza kabiliana na upungufu huu wa mwaka jana na mwaka huu wa 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi chote cha miaka mitano, Kambi ya Upinzani imekuwa ikiwasilisha bajeti mbadala kwa kuonyesha ni jinsi gani Serikali kuitia Wizara ya Fedha inavyoweza kupanua wigo wa mapato na wakati huo huo kudhibiti matumizi yasiyokuwa na tija kwa Taifa, kila wakati tumeambiwa kuwa ushauri wetu na wa Wabunge wengine utazingatiwa na kufanyiwa kazi. Lakini, kila uchao vianzio vyetu vimeduwa vilevile vyaa sigara na pombe tu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mapendekezo na ushauri wetu na Wabunge kwa jumla, ambao tumekuwa tukiutoa, Serikali imeishia kusema kuwa tumepokea mapendekezo, mchakato unaendelea, tutayafanya kazi, lakini kwa masikitiko makubwa hadi sasa mapendekezo ambayo yamefanyiwa kazi ni kidogo sana kulinganisha na ushauri uliotolewa kama ifuatayo:-

- Mapato kutohana na mazao ya misitu(magogo na mbao);
 - Vitalu vya uwindaji, (ada za uwindaji na gharama za umiliki wa vitalu);
 - Uvubi bahari kuu, ada ya leseni kwa meli za uvubi na mrabaha wa samaki wanaovuliwa na meli hizo;
 - Uanzishwaji wa bandari ya samaki mwambao wa bahari, (biashara ya mafuta na maji);
 - Kupunguza misamaha ya kodi;
 - Kuanzisha utaratibu wa manunuzi kwa njia ya mtandao (*electronic procurement system*);
 - *Diaspora's bond* kwa Watanzania wanaoishi nje ya nchi;
 - Kutoza kodi madini yanayopatikana katika mchakato wa uchimbaji dhahabu, kama vile fedha(*silver*) na shaba (*copper*);
 - Kuchunguza baadhi ya mikataba kandamizi kwa nchi ili wawekezaji walipe kodi stahili na kadhalika;
 - Sambamba na hayo yote tulishauri kupunguza ukubwa wa Serikali ili uendane na hali halisi ya mapato ya Serikali;
 - Kutoza kodi ya asilimia 18% ya posho wanazopata watumishi wa umma na hata makakampuni binafsi;
 - Kupitia upya mfumo wa bajeti yetu ili kuweka bayana zaidi mapato na matumizi ya Serikali; na
 - Kuanzisha utaratibu wa manunuzi kwa kutumia TEKNOHAMA (*Electronic Procurement*)(Baada ya miaka tisa leo Serikali ndio inafanya utafiti na kama hatua zingechukuliwa mapema tungepunguza rushuwa na matumizi mabaya ya fedha katika manunuzi kwa asilimia 30%).
- Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo hayo ya jumla kuhusiana na jinsi gani Serikali inashindwa kuwajibika kwa vyanzo viliviyowazi ili kuongeza mapato na kuinua uchumi wa nchi kwa ujumla, sasa naomba niende kwenye majukumu makuu ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ndiyo msimamizi na mtekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini unalenga kufanikisha kufikia malengo ya milenia. Hata hivyo, utekelezaji wa MKUKUTA umesuasua kwa sababu gharama za mkakati hazikukadiriwa mapema. Ukadiriaji wa gharama za MKUKUTA katika baadhi ya sekta muhimu ulikamilika mwishoni mwa mwaka 2006 na gharama zake

zikabainika kuwa ni kubwa mno kuliko uwezo wa Serikali, kwa hiyo, MKUKUTA hautekelezeki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, gharama za kutekeleza MKUKUTA katika sekta ya nishati ilikadiriwa kuwa wastani wa dola za Marekani milioni 911 kwa mwaka kati ya 2006/2007 mpaka 2009/2010. Sekta ya kilimo ilikuwa inahitaji wastani wa dola milioni 300 kwa mwaka. Sekta ya afya ilihitaji wastani wa dola milioni 476 kwa mwaka. Sekta ya barabara ilihitaji wastani wa dola milioni 922 kwa mwaka. Sekta nne za nishati, kilimo, afya na barabara zilikadiriwa kuhitaji wastani wa dola milioni 2,609 kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu wa bajeti ni wa mwisho wa utekelezaji wa MKUKUTA. Waziri kaeleza kwamba Serikali inaandaa MKUKUTA namba II. MKUKUTA wa kwanza haujafanyiwa tathmini ya kina ili kujifunza kutokana na mapungufu yaliyojitekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi MKUKUTA wa pili hautakamilika na kuanza kutekelezwa mwaka wa bajeti wa 2010/2011. Ikiwa Serikali ina lengo thabiti la kuwa na mpango wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini unaotekelzeza inastahili kujipa muda kutathmini MKUKUTA na kushirikisha wadau wote katika kuandaa mpango mbadala wa kukuza uchumi kuongeza ajira za uhakika na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inarudia tena kuitaka Serikali kushirikiana na Vyama vya Upinzani, taasisi zisizokuwa za Kiserikali na wananchi kwa ujumla kuitia Dira ya Taifa ya Maendeleo na MKUKUTA namba II ili kuibua dira mpya ya maendeleo na mpango wa muda mrefu unaotekelzeza utakaongoza mipango na bajeti ya Serikali. Kambi ya Upinzani inashauri kuwa MKUKUTA mpya usianze mpaka Uchaguzi Mkuu utakapokwisha ili kutoa fursa kwa wagombea uchaguzi amba hutoa ahadi nyingi nje ya program ya maendeleo, kuwapa fursa wataalam na washiriki wengine kuandaa MKUKUTA II amba umekuwa shirikishi katika kila nyanja za jamii ikijumlisha na ahadi za viongozi watakaopata ridhaa za Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uundwaji wa Tume ya Pamoja ya Fedha ambayo ipo takriban kwa kipindi cha miaka kumi sasa, hakina maana kama *formula* ya mgawo wa mapato na matumizi ya Muungano hayakuwekwa bayana. Waziri katika hotuba yake ya bajeti alisema kuwa Zanzibar imekwishawasilisha uamuzi wake kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano ambayo na senyewe ni mbia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ni jambo gani linalokwamisha utekelezaji wa matakwa haya ya kikatiba ya kila upande kuchangia Mfuko wa pamoja wa Muungano. Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri alieleze Bunge hili la mwisho ili tutakapochukua nafasi tuanje utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Udhagini wa Serikali, Hazina walitakiwa waoneshe hati za rehani iliyotolewa na kila mkopaji ili kuhakikisha kuwa dhamana iliyotolewa na Serikali ilikuwa haizidi kiwango kilichowekwa Kisheria hadi taarifa ya

CAG inaletwa Januari 2010 Serikali haikutoa majibu kwa *CAG* ambapo asilimia 100 ya udhamini wa Serikali ultolewa kuwezesha shughuli za uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 13(1)(b) cha Sheria ya Mikopo ya Serikali, Msaada na Udhamini ya mwaka 1974 na marejeo yake ya mwaka 2004 kinasema: "Kiwango cha juu kabisa ambacho Serikali inaweza kudhamini deni hakitazidi asilimia 70 ya fedha zilizokopwa".

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inajikuta ikidhamini madeni makubwa zaidi ya kiwango kilichowekwa kisheria, hali ambayo inaiweka Serikali katika mazingira hatarishi ambapo mwisho wake Serikali itahitajika kutumia kiasi kikubwa cha fedha kugharamia madeni ambayo yameshindikana kulipwa na taasisi zilizodhaminiwa kulipa madeni hayo na gharama nyinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya *CAG* inaonyesha kuwa Madeni yaliyotokana na udhamini wa Serikali kwa taasisi za umma na watu binafsi (Mashirika ya Umma kiasi kilichokopwa 454 bilioni. Kiasi chenyé udhamini wa Serikali 447 bilioni, Vikundi vya Kibishara vitano bilioni kilichodhaminiwa 2.2 bilioni, Wauzaji wa nje ya nchi kilichombwa 230 bilioni kilichodhaminiwa 182 bilioni na huduma ya Msaada wa Kifedha Serikalini kwenye Uwekezaji 65 milioni kilichodhaminiwa 65 milioni) yalikadiriwa kufikia Sh. 632,035,342,027/= (632 bilioni) ambayo ni sawa na asilimia 81% kinyume na sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 13(1)b cha Sheria ya Mikopo ya Serikali ya mwaka 1974 pamoja na marekebisho yake, kinaonesha kuwa ili taasisi yoyote au kampuni ifaidike na udhamini ni lazima iweke dhamana ya mali isiyoodosheka yenye thamani ile ile ya dhamana iliyoombwa. Baya zaidi baadhi ya taasisi na makampuni haya yamekwishaacha kufanya biashara. Sharti hili la kisheria Serikali haliheshimu kabisa. Hivyo, Waziri anaposema kuwa wanasi mamia mapato na matumizi ya Serikali wakati wao wenye we wanavunja sheria, Watanzania wasemeje juu ya Serikali yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iwaeleze Watanzania ambao ndio walipa kodi, ni utaratibu gani Serikali inatumia kufuatilia kama kweli udhamini walioutoa kwa makampuni yanayopewa udhamini, fedha hizo zinarudishwa? Aidha, ni kwa nini Serikali kupitia kwa Msajili wa Hazina isiweke mtu wa kuwa mshauri mwelekezi katika kampuni husika ili kuhakikisha fedha za walipa kodi zinafanya kazi iliyokusudiwa na zinarudishwa? Naliomba Bunge lako, kazi ya kwanza ya Kamati mpya ya Fedha na Uchumi ya Bunge la 10 iifanyie kazi taarifa hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Deni la Taifa inaonesha kwa kipindi kilichoishia Juni, 2009 limeongezeka kwa asilimia 17.66 kutoka kiasi cha Sh. 6,477,451,842,418 kwa mwaka wa fedha 2007/2008 hadi Sh. 7,621,286,730,034 kwa mwaka wa fedha 2008/2009. Deni la ndani limeongezeka kwa kiasi cha Sh. 358,846,010,302.8 (1.6 bilioni) sawa na asilimia 19.14 kutoka Sh. 1,875,794,357,188.34 (1.9 triliuni) mwaka 2007/08.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliyoitoa hapa Bungeni inaonyesha kuwa hadi Desemba 2009 Deni la Taifa limefikia dola za Marekani milioni 10,690.3 sawa na Sh. 14,966,420,000,000/= (trilioni 14.9) kati ya fedha hizo Dola za Marekani milioni 7,758.1 sawa na Sh. 10,875,340,000,000/= (trilioni 10.8) ni deni la nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Waziri inaonyesha kuwa kati ya deni hilo la nje Dola za Kimarekani 1,514.6 milioni (1.5 Bilioni) sawa na Sh. 2,120,440,000,000/= (trilioni 2.12) Serikali ilikopa kwa ajili ya sekta binafsi au ilikuwa ni udhamini wa Serikali kwa sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ina maana kuwa Serikali ina dhima kubwa katika kuwalipa wadai wa nje kuliko wadai wa ndani, hii kiuchumi ina maana kuwa kiasi kikubwa cha mtaji katika fedha za kigeni kitalipwa nje ya nchi, aidha, kukopa ndani katika mabenki ya bishara, maana yake ni Serikali kushindana na sekta binafsi, ni dhahiri benki zingependa kuikopesha Serikali, hivyo mzunguko wa fedha katika uchumi utapungua. Hii ni hatari. Dawa ni kuongeza uzalishaji, kupunguza udhamini wa kinyume cha sheria, kupunguza matumizi yasiyo na lazima, kupanua wigo wa ukusanyaji kodi kama tulivyoshauri. Vinginevyo tutakuwa tunalipia watu madeni yasiyo kuwa na manufaa kwa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kumbukumbu zilizopo inaonyesha kuwa tumekuwa tukitoa misamaha ya kodi inayoendana na misaada mbalimbali tunayoipata, mwaka 2007/2008 tulitoa misamaha ya takriban asilimia 57.77 ya misaada yote, mwaka 2008/2009 misamaha ya kodi ilikuwa ni asilimia 46.48 na mwaka 2009/2010 misamaha ilikuwa ni asilimia 30.9.

Mheshimiwa Mwenyekiti, misamaha ambayo imekuwa ikiliumiza Taifa kwa ujumla ni misamaha ambayo ina uhusiano wa moja kwa moja na uwekezaji au manunuzi na mauzo. Katika taarifa ya Waziri kwenye Kamati anaeleza kuwa idadi ya misamaha ya kodi kwa mwaka wa fedha 2009/2010 ilitarajiwu kufikia asilimia 2.1 ya pato la Taifa. Kwa kuwa pato la Taifa ni Sh. bilioni 28,212.6 hivyo inafanya misamaha ya kodi kuwa Sh. billioni 592.465.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali inaonesha kuwa misamaha ya kodi ni Sh. 752,398,800,000. Kambi ya Upinzani kwa muda mrefu tumekuwa tukitaka Serikali kuwa makini na suala zima la takwimu, sasa Mheshimiwa Mwenyekiti ni takwimu gani ipo sahihi kati ya takwimu hizo za misamaha ya kodi? Tunamtaka Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi kwa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi za Fedha na Sera ya Uwezeshaji. Taasisi na asasi za fedha ndiyo nguzo muhimu katika mchakato mzima wa kukuza uchumi wa nchi yetu. Hivyo basi, sera na mfumo ulio imara wa taasisi na asasi za fedha unatakiwa uendane na sera za kukuza na kuondoa umaskini. Vinginevyo kaulimbiu zote

zinazotolewa itakuwa ni ngonjera za kuwafurahisha wananchi ambazo haziwezi kupimwa kivitendo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti zilizofanywa na taasisi ya *Finscope* na kugharamiwa na *Financial Sector Deepening Trust Fund (FSDT)* inaonyesha kuwa ni asilimia tisa tu ya wananchi ndio wanatumia huduma rasmi za kibenki, asilimia mbili ndio wanaopata huduma zingine za asasi ndogo za kifedha, 35% wanatumia huduma ambazo si rasmi, kwa maana kwamba huduma za fedha wanapatiwa na ndugu, jamaa na marafiki. Aidha 34% ya wananchi hawapati kabisa huduma za kifedha wakati wenzetu wa Kenya ni asilimia 38 tu ndio ambao hawatumii huduma za Kibenki na asilimia 62 wanapata huduma za kibenki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu hizi zinatuonyesha kuwa hata kama Serikali itajitahidi vipi kuongeza vyanzo vya kifedha na kutengeneza mazingira mazuri kwa wawekezaji lakini tusipofanya maboresho na kuimarisha asasi/taasisi zinazotoa huduma za kifedha kwa wananchi wa mijini na vijijini, kuondoa umaskini wa kipato litaendelea kuwa ni jambo lisilowezekana kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili nchi yetu iwe na uchumi endelevu inatakiwa sekta ya viwanda kwa ujumla iwe endelevu, lakini kutokana na kutokuwepo kwa mfumo wezeshi katika tasnia ya fedha yenye Mabenki ya Maendeleo kwa mfano, Benki ya Maendeleo ya Kilimo, Viwanda, Madini na kadhalika. Hatuwezi kuwa na kiwango cha ukuaji wa uchumi endelevu wa asilimia nane na kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali ya kawaida haiwezekani kwa mfanyakishara wa kuza na kununua bidhaa nje na ndani apewe huduma za kibenki sawa na mfanyakishara anayewekeza katika miradi ya viwanda, kilimo, madini na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana Benki zetu zaidi zinawakopesha wafanyakishara ambao ni asilimia 16.5. Wakati wa uzalishaji viwandani ni asilimia 13.8%, riba wanayotozwa wawekezaji wa miradi ya viwanda, madini, kilimo na kadhalika haioani na uwekezaji wao, hivyo wanashindwa kurudisha mikopo ya taasisi na asasi za fedha kutokana na riba kuwa kubwa na mikopo ya muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaona huu ni udhaifu mkubwa kwa upande wa sekta ya fedha, kwani tunaamini taasisi hizi zina wataalam kwenye sekta ya biashara na hivyo ni moja kati ya majukumu yao kutoa ushauri ili kuhakikisha wateja wao wanafanya vizuri katika biashara zao na kurejesha mikopo kwenye asasi walizokopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo kwa asasi ndogo za fedha. Katika kusimamia na kutekeleza sera ya Taifa ya uwezeshaji kiuchumi, mwaka wa fedha 2009/2010, mradi wa *SELF* ulitoa mikopo kwa asasi ndogo za fedha na *SACCOS* yenye thamani ya shilingi bilioni 5.012 kwa asasi 41. Mikopo hiyo ilitolewa kwa wajasiriamali 71,065 na katika kipindi hicho mikopo iliyorejeshwa ilifikia shilingi billioni 4.07.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inataka Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge hili, je katika mikopo hiyo kwa asasi za fedha *SELF* ilikuwa inatoa fedha hizo kwa riba kiasi gani? Tukumbuke kuwa hizo asasi zilizopewa au kukopa fedha hizo zinafanya biashara na hivyo riba yao kwa mjasiriamali ni jumla ya ile ya *SELF* na yao, jambo linalipelekea mjasiriamali kutokusaidiwa badala yake kuibiwa. Hatima ya sera nzima ya uwezeshaji kutokufikia lengo na kumwacha mjasiriamali au mkopaji kuwafanyakazi wakopeshaji wawili tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali, ilieleze Bunge lipate urahisi wa kutathmini utendaji wake, katika takwimu za uwezeshaji kwa watu au vikundi zitakazotolewa zitolewe kwa maeneo ya Wilaya, Kata na Vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii haitofautiani na ile taarifa ya *LAAC* inayoonyesha kwenye vitabu shule imejengwa na kukamilika lakini baada ya ukaguzi haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Ununuzi wa Umma (*Public Procurement Regulatory Authority-PPRA*). Taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali inaonyesha kuwa takriban asilimia 70 ya matumizi ya Serikali ni manunuzi katika vifaa na huduma. Hii inaonyesha kwamba udhaifu wowote katika mfumo huu wa manunuzi ya umma, ni kutoa mwanya kwa mafisadi kujineemesha kuititia fedha za walipa kodi. Jambo hili ndilo limesababisha kwa kiasi kikubwa kutokuwepo kwa uwiano unaoeleweka baina ya makundi ya watu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani toka mwaka 2004 imekuwa ikisisitiza kuwepo mfumo wa kufanya manunuzi ya umma kwa njia ya mtandao (*electronic Procurement -e-procurement*), kwa kuweka kumbukumbu sawa ni kwamba Semina Maalum kwa Waheshimiwa Wabunge Kamati ya Hesabu za Serikali (*PAC*) Bunge la nane (2000-2005) na watendaji wa Wizara ya Fedha ilifanyika Bagamoyo chini ya Ufadhilli wa Kampuni ya Tejari kutoka Dubai amba ni mabingwa wa matumizi ya ununuzi wa mtandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini imetimia karibu miaka sita hadi sasa Serikali inasema ndiyo imekamilisha upembuzi yakinifu juu ya mchakato wa kuanzisha mfumo wa ununuzi wa umma kwa njia ya mtandao, ilidhihirika wazi kuwa utaratibu huu ni ufumbuzi wa kupambana na rushwa na ongezeko la gharama za manunuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kubadili *mind set* yake kuhusiana na hoja tunazozitoa kwa manufaa ya nchi yetu, kwani muda ni jambo muhimu sana katika dunia ya leo. Toka tutoe ushauri huo wa kudhibiti rushwa na kuongeza ufanisi katika mfumo wa manunuzi ya umma ni takriban miaka sita, kwa kuangalia taarifa ya *CAG* kwa kipindi chote hicho ni hasara kiasi gani nchi imekipata? Ikiwa ni mikataba mibovu na rushwa inayohusiana na mchakato wa utoaji wa zabuni za manunuzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki Kuu ya Tanzania. Chombo hiki ndio chenye dhamana ya kutunga na kusimamia sera zote za fedha na uchumi kwa ujumla wake. Uchumi kufanya vizuri au kufanya vibaya kunatokana na umakini wa chombo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufanya vizuri kwa uchumi vilevile kunategemea utendaji kazi wa Taasisi za Fedha. Benki Kuu kama ndio msimamizi wa Taasisi hizo, inawajibu wa kuangalia jinsi zinavyofanya kazi zake. Kumekuwepo na kupanda kwa gharama za kibenki (*bank charges*) kiasi kwamba wateja wanaona kuwa kuna aina fulani ya ongezeko la gharama anazotozwa mteja. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kupitia *BOT* waliangalie suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mteja siku zote ni mfalme katika kadhia nzima ya biashara, lakini inapokuja ameshindwa kuridhika na jinsi benki inavyomnyanyasa na kutoa malalamiko yake Benki Kuu, Benki Kuu inashindwa kumsikiliza. Je, kwa suala kama hilo, mteja anatetewa na chombo gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa fedha uliomalizika, Gavana aliunda Tume kutoa tathimini kuhusiana na matumizi halali ya ujenzi wa minara pacha ya *BOT*. Kambi ya Upinzani, inataka kufahamu taarifa hiyo iko wapi? Kwani Watanzania wanataka kuelewa thamani halisi ya ujezi wa jengo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka *BOT* kuangalia kwa umakini ushauri wetu wote tuliusa hapo awali kuhusiana na kubadilisha mfumo mzima wa Taasisi na Asasi za Fedha ili kuweka utaratibu maalum kwa ajili ya mikopo ya uanzishwaji wa viwanda. Aidha, kuweka utaratibu ambao fedha za Serikali kwa ajili ya uwezeshaji ziende moja kwa moja kwa asasi zinazowafikia moja kwa moja wakopeshaji badala ya asasi hizo kukopa fedha hizo kwenye mabenki ya biashara kwa riba wakati fedha hizo zinatolewa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge, baada ya kupitisha sheria ya *Financial Leasing* hadi sasa maendeleo yako vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla tunaweza kuona kuwa tumefanya vizuri katika kuinua uchumi, lakini Kambi ya Upinzani inaomba tudurusu takwimu za uzalishaji zilizopo ili tujipime kama tuna maendeleo endelevu, hasa tukitilia maanani idadi ya watu kwa mwaka 2005 ilikuwa milioni 36.2 na thamani ya Tshs.580 sawa na Dola moja ya Marekani, sasa idadi ya watu milioni 40.7 na Tshs.1500 sawa na Dola moja ya Marekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa fedha 2005/2006 tulizalisha tani 376,590 za Pamba na mwaka 2009/2010 tumefikia tani 267,004, Korosho mwaka 2005/2006 tulizalisha tani 90,385 na mwaka 2009/2010 tumefikia tani 74,169. Sambamba na hilo, taarifa ya bajeti ya kaya ya mwaka 2009 inaonesha kuwa, mwaka 2001, wananchi waliokuwa wanapata maji kutoka kwenye vyanzo salama ilikuwa asilimia 55 na mwaka 2007 ikawa asilimia 52. Anguko la 3% ni kuwa utendaji wa Serikali umeshuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo lililokuwa limewekwa katika kuzalisha mazao makuu yanayotuingizia fedha za kigeni ifikapo 2010 hata nusu yake halikufikiwa. Haya ni machache tu ya kuduruswi, lakini pia nikiri kuwa yapo maeneo mengine ya mafanikio kama ujenzi wa madarasa na kadhalika. Kambi ya Upinzani inawataka Watanzania wapime wao wenyewe hali halisi ya uchumi wao binafsi na sio maneno tu ya kujisifia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Fedha na Uchumi, ambaye pia ni Kiongozi wa Upinzani Bungeni. Sasa tunaingia katika uchangiaji kwa dakika kumi kumi. Anayetufungulia dimba, ni Mheshimiwa Peter Serukamba na Mheshimiwa Devota Likokola ajiandae, atafuatia Mheshimiwa Esther Nyawazwa.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kuwa wa kwanza kuchangia kwenye Wizara hii muhimu ya Fedha na Uchumi. Nianze kwa kumpongeza Rais wetu kwa kuchanguliwa kwa kura nyingi kuwa Mgombea wa Chama chetu. Lakini pia nimpongeze Mgombea Mwenza, Dr. Bilal na Makamu wa Rais Dr. Shein kwa kuchaguliwa kuwa Mgombea wa Urais wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, inawezekana leo ndiyo itakuwa mara ya mwisho kuongea katika mkutano huu, hivyo naaomba niwatakie Wabunge wote maisha mema na uchaguzi mwema ujao. Ni matumaini yangu kuwa, wote tutakutana hapa mnamo mwezi wa Kumi na Moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze pia Watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Uchumi, kwa kazi nzuri waliyofanya katika kuhakikisha wanasmamia uchumi wetu na shughuli za maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwapongeze sana na kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Kigoma Mjini, kwa heshima walijonipa, kwa msaada wanaoendelea kunipa na kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa. Ninafanya vyema kwa sababu ya msaada wao mkubwa. Nami niwahakikishie jambo moja tu kwamba, nitaendelea kuwatumikia kwa moyo wangu ule ule, kwa unyenyekevu wangu ule ule na nitafanya kazi bila kuchoka. Ninajua wako watu, eti nao wanadhani wanaweza lakini ninaamini bado wananchi wa Kigoma wana matumaini makubwa na mimi na nitaendelea kuwatumikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa nina machache tu ya kusema. Wizara ya Fedha na Uchumi, ni Wizara muhimu sana katika maendeleo ya nchi yetu. Ukiangalia mafanikio tuliyopata kama nchi, ni makubwa sana. Tumejenga shule, tumejenga Chuo Kikuu kikubwa, kilimo, afya pamoa na yote yaliyofanikiwa. Nilikuwa najiuliza, mafanikio haya ni makubwa sana katika kipindi kifupi sana, nilitaka watu wa

Wizara ya Fedha waje na mkakati sasa. Utaona hapa katika yote tuliyofanikiwa ni *recurrent budget* kwa sababu haya tuliyofanya si kwamba kesho hatuwezi kuyafanya tena, tunaendelea kuyafanya. Kwa hiyo, hii ni *recurrent budget* hivyo *thrust* sasa ya kwenda ni lazima tu-manage economy yetu vizuri sana, ili sasa ile *investment* ambayo tunaiingiza tuweze kupata fedha nyingi ili tuendelee kuwezesha hizi *social services* tulizozifanya ziendelee kuwa vizuri zaidi. Kwa hiyo, maendeleo haya ni makubwa lakini yanahitaji *challenge sustainability*. Tusipoya-sustain haya maendeleo makubwa tuliyoyapata kwa kipindi kifupi, tunaweza tukapata matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna matatizo makubwa ya kiuchumi *Greece*, ukisoma kwa undani kwa sababu nchi ile ilikuwa inafanya mambo makubwa sana tena kwa *ku-borrow*, lakini *ime-borrow* na imefikia hatua sasa haiwezi kulipa na *economy* *im-collapse*. Kwa hiyo, ninachotaka kusema ni kwamba, haya ambayo tumefanya ni makubwa sana na ili yaweze kuendelea na tufanye makubwa zaidi ni lazima sasa *management* ya *economy* yetu ibadilike katika kuangalia huko mbele tunakokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naangalia baadhi ya mambo katika nchi kama Tanzania, jiografia ya nchi yetu Mungu ametupendelea sana, lakini sasa ni lazima pamoja na upendeleo huo tujitahidi ili uwe na maana katika maendeleo ya watu wetu. Kwa hiyo, kuna vitu tuvisimamie kwa umakini mkubwa sana. Kuna masuala ya reli. Suala la reli siyo la kutumia mwaka au miaka miwili eti bado mnafikiria mfanye nini, ni lazima *to invest heavily* ili tuweze kupata pesa za kuweza kupeleka huko kwenye kilimo, elimu na afya na pia ili tutumie jiografia ya nchi yetu. Kuna suala la bandari, tuna badari zetu kubwa tatu (3) kwa maana ya Tanga, Dar es Salaam, Mtwara na Kigoma. Ni lazima bandari hizi ziweze kufanya kazi katika *efficiency* ili watu wanaotuzunguka waje. Tusipokuwa na utendaji mzuri, nina uhakika wenzetu watakwenda kwingine ambapo wanapata *service* nzuri na hizi bandari zetu zitakuwa hazina maana na hazitawezu kuchangia kwenye uchumi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la Shirika la Ndege la ATC. Jambo hili mimi mwenzenu linanipa shida sana, kwani pamoja na ukubwa wake, ni jambo dogo. Kama mtu binafsi ameanza na ndege moja, mbili leo ana ndege tano au sita, kuna wale *Coastal Air* walianza na vindege vidogo, leo wanafanya vizuri sana, sisi tunashindwa nini kama Serikali? Kila ukiuliza hapa unaambiwa tunatafuta Mbia, tumeongea na Mchina, tunaongea nao mpaka lini? Tufanye maamuzi kama Serikali ili sisi wenywewe tusimamie. Ukiniliza mimi *ATC* tatizo lake ni nini? Nitakwambia kwamba, tatizo lake ni mtaji na menejementi. Tuweke mtaji na tuhakikishe kuna menejementi nzuri, tuone kama vijana hawa hawawezi kuleta mafanikio. Shirika hili litakapopata faida, *then* hela hizi tunapeleka kwenye *social services*. Tukifanya hivyo itatusaidia kwenye utalii, pamoja na mambo mengi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni matumizi ya Serikali. Niiombe Serikali, jamani umefika wakati tujiangalie sana, matumizi yasiyo ya lazima tuyangalie. Watu wote walioendelea, hata katika familia ili ufanikiwe, ni lazima ubane matumizi. Hata kama Kitilya atakusanya pesa nyingi sana na anaziweka kwenye ndoo na ndoo yenywewe mmeitoboa, ile kazi yake haitakuwa na maana. Mwisho wa siku tutakuwa tunasema bado

kodi haitoshi kumbe ni kwa sababu ya matumizi makubwa ya Serikali. Hivyo, ni lazima tusaidie mapato yanayokuja kwa kubana matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni *private sector*. Ili tuendelee tunahitaji *private sector*. Wazungu wanasema, *private sector* ndiyo *engine* ya *growth*. Naombeni sana ili *private sector* ije Tanzania, ili *investors* waje Tanzania ni lazima tupunguze urasimu na ni lazima gharama za kufanya biashara Tanzania ziwe ndogo. Wenye mitaji yao mikubwa kitu cha kwanza ambacho wanaangalia ni kwamba, nikienda nchi gani gharama za kufanya biashara ni ndogo. Kama katika nchi yenu, gharama za kufanya biashara ni kubwa, hawaji, siyo kwamba, sisi ni *better than others*. Kwa hiyo, ili *investors* waje, ni lazima tuijandae vizuri sana kwenye kuhakikisha tunapunguza urasimu, lakini pia tuweke mazingira ambayo huyu *investor* ataweza kuja kujenga uchumi wetu. Leo unakwenda *TIC*, lugha unayopewa pale kama *investor*, utakapokuja tena kuanza *TRA* unapewa lugha nyingine. Ni lazima vitu hivi tuvioanishe pamoja na tuongee lugha inayofanana na hapo ndiyo tutaeleweka huko tunakoenda. Kwa hiyo, ni lazima hili tuliwekee utaratibu unaoeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la *PSPF*. *PSPF* wanafanya vizuri sana, wanatoa mafao mengi sana, ameandika Waziri hapa. Lakini, suala la *PSPF* ni lazima tuongee ukweli. Ukiangalia *actuarial valuation* ya *PSPF*, mfuko huu siyo *sustainable*. Ile *formular* ya *calucaluation* ni tofauti na mashirika yote ya pensheni. Maana yake ni nini? Ni lazima tujiulize kama kweli hiyo ndiyo *the best*, tupeleke hiyo *formular* katika mifuko yote na kama siyo *the best*, tutafute namna ya kuoanisha ili hiyo *formular* iweze kuwa *sustaible*. Ujisoma *actuarial valuation*, mfuko huu siyo *sustainable unless* Serikali ilipe deni lake la *three trillion* na inalipa lini, mimi sijui katika mazingira ambayo tuna-load kubwa ya kuendeleza nchi yetu. Kwa hiyo, lazima tuisome ile *actuarial valuation*, tufanye maamuzi magumu, kama ni *kui-revist*, *tui-revist*, maana mifuko mingine ya *PPF*, *NSSF* inatoa *formular* ndogo basi na yenyewe ibadilike ili ifanane. Ndiyo maana leo kuna migomo kwenye Vyuo Vikuu wanasema tunataka *formular* yetu iwe kama ya *PSPF*, lakini *formular* ya *PSPF* sidhani kama ni nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, ni *cash flow management*. Niombe sana watu wa Wizara ya Fedha na Uchumi, ni lazima tufikiri upya namna ya *ku-manage cash flow* za Wizara ya Fedha na Uchumi. Kwa namna unavyofanya *allocation*, kuna sehemu unapeleka pesa wakati wao hawazihitaji, wakati kuna miradi mingine inahitaji fedha kwa wakati huo. Kwa hiyo, ni lazima hapa tutafute namna ya kufanya ili *cash flow management* iwe na maana. Kuna miradi mikubwa, kuna *interest*, ukichelewa kulipa unalipa *interest* lakini kuna sehemu nyingine wameweka pesa zimekaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono bajeti ya Wizara ya Fedha na Uchumi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Peter Serukamba kwa uchambuzi wako. Huyu ni kijana ambaye ana *MBA*, kwa hiyo, anachambua mambo ki-*MBA* na mimi Mwenyekiti wenu, nina *MBA* pia. (*Kicheko*)

MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Mimi pia niungaane na Wajumbe wenzangu kupongeza kwa kweli uchaguzi ambao umefanyika katika Chama cha Mapinduzi (CCM). Chama kile kimetoa wagombea ambao hakuna wasiwasi, dola itakamatwa na CCM katika Miaka ijayo. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue nafasi hii pia kuwashukuru sana wanawake wenzangu wa Mkoa wa Ruvuma. Kwa kipindi chote tumeshirikiana vizuri sana kuleta maendeleo ya nchi yetu, maendeleo ya Mkoa wetu wa Ruvuma, lakini pia na maendeleo ya familia zetu. Wanawake wa Mkoa wa Ruvuma wamekuwa makini sana, lakini pia ninawaomba kipindi kimefika cha kuendelea kushirikiana zaidi na mimi nina uhakika kwamba tutaendelea kushirikiana vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe pongezi kwa Wizara hii na ninatoa pongezi tu kwa sababu Wizara hii jamani ni mionganini mwa Wizara sikivu. Wizara ya Fedha na Uchumi, Waziri wake ni msikivu, Naibu Waziri ni msikivu na Wataalam wake pia ni wasikivu. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi, tumetoa ushauri mwangi sana na wote wameufanya kazi. Lakini wote tumeona jinsi ambavyo pesa zimetiririka katika miradi mbalimbali ya maendeleo katika Majimbo yetu na Ilani ya Chama cha Mapinduzi imeweza kutekelezwa vizuri. Hongereni sana. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia nimpongeze Gavana wa Benki Kuu. Nampongeza Gavana Beno Ndullu kwa sababu uchumi wa dunia nzima ulidorora, lakini uchumi wa Tanzania kwa kweli umejitahidi katika kuhimili vishindo. Kwa hiyo, Gavana tunakupongeza na uendelee hivyo hivyo ili kusudi uchumi wetu usiweze kuharibika vibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza pia Kamishna wa TRA. Makusanyo yameongezeka, safari hii tumekusanya 90.7%, unaweza ukasema ni 100%. Kwa hiyo, tunahitaji kutoa pongezi kubwa sana kwa Kamishna Mkuu wa TRA, Ndugu Kitilya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niseme kuhusu maeneo machache ambayo kwa kweli ninapongeza Serikali. Kwanza, ni kwa kuongeza makusanyo. Pili, kwa kuhimili msukosuko wa uchumi, lakini kubwa zaidi la tatu ni kwa kuanzisha Benki ya Wanawake. Wanawake wa Tanzania tumefurahishwa na jambo hilo na kwa kweli, Waziri katika bao ambalo umepiga ni Benki ya Wanawake. Wanawake ndiyo wapigakura wakubwa katika nchi yetu, bila kuwawezesha kiuchumi, hatutasonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hili la kuanzisha benki linaonesha dhamira ya dharti ya Serikali yetu kuwawezesha wanawake kiuchumi. Ninachokiomba Benki yetu ya Wanawake sasa ianze kupeleka matawi Mikoani na Mkoa wa kwanza kupeleka tawi lake iwe ni Ruvuma, Kusini kabisa mwa Tanzania ili kuonesha kwamba benki hiyo itahudumia wanawake wengi. Mikoa tunayo mingi, haiwezekani wanawake wakatoka Mwanza wakaja kuchukua mikopo Dar es Salaam, hawawezi wakatoka Tunduru wakaja kuchukua mikopo Dar es Salaam, vilevile wanawake hawawezi wakatoka Namtumbo, Mbanga, Songea Vijijini, haiwezekani, ni lazima matawi sasa yashuke. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapongeza pia kwa azma ya Serikali ya kuanzisha Benki ya Kilimo *TIB* pale, sasa hivi tukiwa na benki ya wakulima itasaidia sana. Asilimia kubwa ya watu wa nchi yetu ni wakulima, wanachohitaji sasa ni mitaji. Wamelima kwa miaka mungi, wanajua kulima, tatizo sasa ni mitaji. Kwa hiyo, wakulima wakipewa mitaji, kwa kweli kilimo kitaboreka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapongeza sana Serikali na ndiyo maana ninasema Wizara hii ni sikivu. Hapa ninampongeza sana Mkurugenzi wa Kitengo cha Kuondoa Umasikini, Dada Anna Mwasha. Ni mwanamke shupavu, amepigania vitengo vyote vya uwezeshaji ili viweze kupata pesa nyingi na kufanya kazi vizuri. Tunaimani *SELF* ikipata pesa nyingi itafanya kazi vizuri, Mfuko wa JK utafanya kazi vizuri, *Mwananchi Fund* utafanya kazi vizuri na kadhalika. Lakini ninakupongeza sana Dada Anna Mwasha, kwa kupigania mpaka VIKOBA iingie kwenye ilani. Hapo ninakupa pongezi. Kwa kweli, kwa kutambua VIKOBA, ambapo ni mfumo unaowafanya wananchi wengi walio maskini waweze kupata mitaji na kuendelea, kwa kweli ninakupongeza. Niseme tu kwamba, watendaji wa Wizara ya Fedha na Uchumi, tunataka kuona matokeo rasmi katika mfumo huu wa VIKOBA. Kwa sababu Serikali ya Chama cha Mapinduzi imekubali kwamba VIKOBA inafanya kazi, ninawapongeza pia wana-VIKOBA wote kwa kazi nzuri waliyofanya mpaka Chama cha Mapinduzi kimekubali na pia Serikali imekubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, popote tunapopata mafanikio, tunapata pia changamoto. Waheshimiwa Viongozi, Waziri na Manaibu Waziri msisite, changamoto hizi ndizo zinazotupa mori zaidi wa kusonga mbele. Changamoto ya kwanza, *TRA*, Ndugu Kitilya, wajumbe wengi tumezungumza kwamba uongeze jitihada za kubuni vyanzo vipyta vya mapato. Bado mapato ya ndani hayatoshi, kwa hiyo, ongeza vyanzo vya kupata mapato. Ndugu yangu Gavana Ndullu, *BOT* kuna changamoto ya riba za mikopo. Wananchi wanalamika riba ni kubwa, hawapati faida. Kwa hiyo, wanapata tabu sana, jitahidi uone ni namna gani suala hili la riba za mikopo litarekebishwa. Lakini pia suala la mikopo midogo midogo *microfinance*, Watanzania wanahitaji mitaji, tunaomba Gavana Ndullu usimamie suala la *microfinance* na mikopo midogo midogo ili kila mtu apate pesa na afanye kazi ya uzalishaji sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaomba kutoa changamoto ya foleni kwenye mabenki. Wananchi wanalamika kwamba, kwenye mabenki kuna foleni kubwa na wanataka wapate unafuu wanapoenda benki ili wafanye kazi zao vizuri. Lakini pia tuna changamoto kubwa ya ufanyakaji biashara katika nchi yetu ya Tanzania, kwani gharama ni kubwa, tunaomba urasimu upungue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakupongeza sana, naomba Wizara hii iongeze kasi maana kauli mbiu yetu safari hii ni ‘Kasi Zaidi’ hivyo tukiongeza kasi tutafanikiwa. Naunga mkono hoja hii na ninawapongeza watu wote wanaofanya kazi katika Wizara ya Fedha na Uchumi, hongereni sana. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Devota Likokola na hasa kwa kuwatetea akina mama. Kama nilivyosema Mheshimiwa Esther Nyawazwa ndiye atakayefuata na baadaye atafuata Mheshimiwa Anna Lupembe na Mheshimiwa Kaboyonga ajiandae.

MHE ESTHER K. NYAWAZWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninamshukuru Mwenyezi Mungu kusimama leo mara ya mwisho kwa miaka hii mitano ambayo wanawake wa Mkoa wa Mwanza walinchagua kwa kura nyingi sana ili niweze kuingia ndani ya Bunge kuwatetea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Mwanza kumpongeza sana mteule wa Chama cha Mapinduzi kwa Urais, Dr Kikwete kwa kuchaguliwa katika Mkutano Mkuu tuliofanya tarehe kumi kwa kura nyingi sana na sisi wanawake wa Mkoa wa Mwanza na ni Mkoa ambao unaaminika nchi nzima kuwa na wapigakura wengi, kwa Mkoa wa Mwanza tutampa kura zote Dr. Kikwete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuwa nimpongeze sana Dr. Bilal kwa kuwa Mgombea Mwenza pamoja na Dr. Shein kushika bendera katika nchi yetu ya Zanzibar, Mwenyezi Mungu awabariki na Wazanzibar ndugu zangu Muungano ndiyo huu, Chama cha Mapinduzi sasa kimeonyesha kwamba sasa Rais anatoka Pemba. Naomba pia nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Naibu Waziri, Mheshimiwa Waziri kwanza ulikuwa na mtihani mgumu sana mwaka jana wa mtikisiko wa uchumi uliyoikumba nchi nyingi lakini Tanzania ulisimama imara na kuhakikisha kwamba Tanzania haitetereki na hatimaye tumenusurika katika mtikisiko huo. Lakini Waziri huyu, Mbunge wa Jimbo la Kilosa, akawa na mtihani wa mafuriko, mafuriko yalikuwa ni balaa Kilosa lakini Waziri alisimama kidete, wananchi wa Kilosa ninawaomba wamrudishe tena mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue nafasi hii, kuwashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Mwanza, wamekuwa na imani na mimi toka mwaka 2000-2005 na mpaka sasa na kwa kupitia kikao cha leo ninatangaza nia, niko pamoja nao na nitagombea tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa nichangie katika hoja hii ya Wizara Fedha na Uchumi. Wizara hii hapa ndipo kwenye mipango, ni Wizara tunayoitegemea sana kuhusu mipango, wana Chuo cha Mipango, kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Waziri, Chuo hiki ukisimamie zaidi ili tupate wataalamu wa mipango ili waweze kutupangia mipango yetu. Kwa hiyo, tunaomba ukiwezeshe Chuo hiki, tupate wataalamu wa kutosha ili waweze kutusaidia katika mipango ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TRA* wanafanya kazi nzuri sana na kila mtu anakubali hilo lakini napenda uendelee kuwapa motisha nzuri zaidi, uwalee ili waweze kukufanya kazi zako vizuri. Hawawezi wakawa wanakukusanya mapato yako, wewe unachukua na

kutumia wao huwezi kuwalinda. Endelea kuwajali na maslahi yao uyalinde na nina uhakika umewaweka mahali pazuri ndiyo maana wanakusanya pesa nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yako isiseme tu kwamba wewe kazi yako ni kukusanya mapato na kupeleka kwenye Wizara zingine na Halmashauri, ninaomba uwe mfuatilaji wa karibu. Wewe huwezi kuwa unakusanya pesa kwenye mlolongo wa *D by D* halafu fedha zinatumika visivyo na wewe unanyamaza tu. Nikuombe kabisa Mheshimiwa Waziri hili nalo liwe ni jukumu lako. Tutakuuliza na nina hakika wanawake wa Mkoa wa Mwanza wakinirudisha, katika Bunge la Kwanza nitakuuliza swal la kwanza umesimamiae fedha zinazoenda kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa MKUKUTA II, Mheshimiwa Waziri amesema kwamba kilimo, miundombinu, utalii, uzalishaji viwandani na uchimbaji madini vitapewa kipaumbele, ninampongeza sana kwa kuwa na mpango huu. Lakini bado nimwombe Mheshimiwa Waziri ili mipango hii uliyooanisha na nikikuthibitishia kuwa wanawake wengi wako kwenye sekta hizi sasa, uwezeshaji ni muhimu. Nikuombe sana katika lile fungu la kupeleka mafungu katika Wizara husika na hizi sekta uhakikishe kuwa unapeleka mafungu hayo mapema kwa sababu wanawake wamejikita kwenye kilimo. Kuna wanawake wanaovua sana samaki katika Mkoa wangu wa Mwanza, kuna akina mama wanauzu dagaa, kwa hiyo, nikuombe sana hizi fedha ziwafikie mapema zaidi ili ziweze kuwasaidia au kama ni mikopo basi uweze kuwapelekea mapema ili waweze kusaidiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, ninaomba nikuombe tena kwamba uhakikishe kuwa kwa sababu sasa hivi *TRA* na *TMA* wako pamoja kabisa kuhakikisha kwamba madini yetu wanayakagua na sasa migodi mingi imeanza kutoa kodi, kwa hiyo, naomba *TRA* na *TMA* uwawezeshe ili waweze kusimamia madini yetu ambayo yameanza kutuonyesha kwamba yanaweza kuongeza mapato katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ni uwezeshaji, ili katika nchi yetu tufanikiwe, hakikisha fedha nyingi unazipitisha kwenye SACCOS lakini ukisema kuwa pesa ziende kwenye mabenki haziwasaidii wananchi. Mwaka jana zile pesa za JK tulipeleka CRDB na NMB, zile ni benki za kibiashara, zinataka riba, lakini tukiwa tuna mipango maalumu kupitia Wizara hii ya Fedha na Uchumi, tukahakikisha kuwa sasa SACCOS tunaziimarisha, wewe mwenyewe Mheshimiwa Waziri unatoa fedha katika mafungu yako moja kwa moja kwenye SACCOS, wananchi wengi watafaidika na mifuko hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine niungane na wanawake wenzangu Wabunge humu ndani ya Bunge, kumshukuru sana Rais wetu kutupokelea ombi la kuwa na benki ya wanawake. Benki hii ndiyo itatukomboa lakini sasa Benki hii ninaomba kwa sababu Serikali imejieleza kabisa kuwa kila mwaka itakuwa inapeleka fedha kwenye benki hiyo ihakikishe inanufaisha wanawake nchi nzima. Sasa hivi wanawake wa Dar es Salaam ndiyo wanaonufaika. Ninajua kwamba matumizi ya kuendesha benki ni makubwa lakini kwa sababu Serikali ya Chama cha Mapinduzi inaweka fedha zake ndani ya benki hii,

ihakikishe basi tunasambaza huduma katika Mikoa yetu angalau tuanze na Kanda. Kanda ya Ziwa Mwanza na mazingira ya Mwanza ni mazuri, tuna nyumba nzuri ambazo zinaweza kupangisha akina mama wakaendesha benki yao na akina mama wa Mkoa wa Mwanza wakapata mikopo kwa karibu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo, nikushukuru sana wewe, niwashukuru sana Wabunge wenzangu, kwa ushirikiano mzuri ambao tumepeana hapa Bungeni. Niwaombe na niwatakie kheri sana Wabunge wenzangu, tunapendana na mwaka kesho turudi wote. Ninaomba ndugu zangu wa Zanzibar hasa Pemba kwa sababu tumewapa mgombea Urais, naomba mtuongozee viti vya CCM. Ninawashukuru sana na niwashukuru akina mama wa Mkoa wa Mwanza tuko pamoja. Ninaunga mkono hoja. (*Makofit*)

MHE. ANNA R. LUPEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, ninaomba nikushukuru kwa kunipa nafasi kwa siku ya leo ili niweze kuchangia Wizara yetu ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye alitupa uzima na uhai mpaka sasa hivi tuko hapa tunazungumza na kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu. Vilevile naomba nimpongeze Rais wetu, Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kupita kwa kura nyingi pamoja na Makamu wa Rais na Mheshimiwa Dr. Bilal, kwa kuwa Mgombea Mwenza wa Chama cha Mapinduzi. Tunajua wanaweza na ushindi wetu utakuwa mkubwa sana 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ninaomba niwashukuru wanawake wote wa Mkoa wa Rukwa, kwa kuniamini na kushirikiana nao kipindi cha miaka mitano. Nasema tena nitaomba ridhaa yao kwa mara nyingine ili niweze kuwatumikia. Sitachoka kuwatumikia mpaka siku hiyo Mwenyezi Mungu atakapokuja nichukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba niongelee Benki ya *NMB*. Mabenki yetu haya kwa sasa hivi huduma ni nzuri lakini kuna matatizo makubwa ambayo yanazikabili benki hizi. Leo hii unaenda *NMB* kutaka *Bank Statement* kama mteja, unachukua siku mbili kupata *Bank statement* yako, ina maana huduma imezorota. Mteja anapotaka kupata huduma ya benki anatakiwa apate huduma kikamilifu maana wewe mteja unaweka pesa zako na unayajua matumizi yako na unapoenda kuchukua hela kuna *record* ambayo inapatikana pale benki ambayo ni *statement* leo hii ukienda benki unaambiwa huwezi kupata *statement line* mbaya au mbovu subiri, kweli mteja anataka mahitaji yake unamwambia *line* mbaya ni kitu hakiwezekaniki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimefanya kazi benki ya *NBC* na *NMB*, nilipokuwa nafanya kazi wakati ule tulikuwa tuna mashine ambazo *una-post ledger* ya mteja pamoja na *statement* yake. Mteja akifika saa yoyote na dakika yoyote anapewa *statement* yake maana ni haki yake. Leo hii unakwenda Benki unaambiwa mtandao

haufanyi kazi, huwezi kupata *statement* leo hii kwa nini? Ina maana huduma imekuwa hafifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana Benki ya *NMB* au ni kutokana na wateja kuwa wengi, sijui tumewapa mzigo mzito maana mishahara yote inapitia *NMB* sasa imekuwa ni tatizo. Sasa kama imekuwa tatizo, tunaomba Serikali, huu mzigo mkubwa ambao wamepewa *NMB* ambao unawashinda basi wapunguziwe, mabenki yapo mengi mbona *CRDB* wanakwenda vizuri sana na ufanisi wao wa kazi ni mzuri sana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasi mimi ninaomba Serikali kama ni mzigo mzito mmewapa *NMB* kiasi kwamba mwananchi anaenda kutafuta *Bank Statement* yake hapati kwa siku hiyo basi muwapunguzie mzigo maana kuna Mbunge amepita hapa Mheshimiwa Devota anasema foleni zimezidi hasa *NMB* inatisha maana unakaa ile foleni mpaka kila mtu anajua yule anakwenda kuchukua pesa. Tunaomba basi kama *NMB* imeshindwa ipunguziwe mzigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kila siku ninasema hivi, ninaomba Serikali ipange mipango mikakati, jamani huko vijijini kwenye Kata zetu na Tarafa zetu, Tarafa zina wananchi wengi na wafanyabiashara wakubwa hawana mabenki, tunasema uchumi, uchumi uko vijijini, Kilimo Kwanza, wananchi kule wanalima sana, wanapata mazao mengi, wanapata fedha nyingi lakini zile fedha wanazichimbia kwenye mashimo, hakuna mabenki. Tunaomba Wizara mpange mipango mkakati ya kupeleka mabenki kwenye Tarafa na Kata. Kila siku tunazungumzia suala hili, kama *NMB* imepewa kazi nzito, kuna Benki ya Posta, wapeni mtaji mkubwa, waende kwenye Kata na Tarafa. Mimi ninaumia sana hasa Mwalimu anavyonyanyasika, tunawapeleka Walimu Vijijini, huyo Mwalimu mshahara wake aufuate Wilayani, hebu tumtizame kwanza yule Mwalimu. Kuna wafanyakazi wengine kama Mapolisi, kuna watendaji, kuna kila aina ya wafanyakazi ambao wanapata mishahara kuitia mabenki lakini atoke Tarafani, atoke kwenye Kata aje mpaka Wilayani kupata mshahara na ule mshahara mnampunja kwa sababu lazima akae gesti, atakula hoteli ili aweze kufuata mshahara wake benki kwenye foleni kubwa ya *NMB*. Ninaomba mipango mikakati ifanyike ili mabenki yafike kwenye Kata mpaka kwenye Tarafa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hazina bado wana utata hasa kwa wastaafu, hebu basi mpange utaratibu ambapo hawa wastaafu wataweza kupata haki yao jamani. Wewe mtu unastaafu, *cheque* yako inakakaa miaka miwili, mitatu unategemea huyo mstaafu anakula nini? Kwa mfano, kuna wale ma-*Driver* ambao ni wastaafu kutoka katika Mawizara, unakuta wanapunjwa, wakati mwagine Walinzi wanapunjwa mafao yao. Ninaomba sana Serikali muweke mikakati yenu vizuri au muweke kitengo maalumu kwa ajili ya wastaafu tu, ninamaanisha kuwa na deski litakaloshughulikia wastaafu tu kuanzia Mawilayani, Mikoani mpaka Hazina ili yule mtu mstaafu aweze kufanikiwa kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu umeniishia, niseme ahsante sana kwa kunipa nafasi, ninaomba niunge mkono hoja. (*Makofifi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Lupembe, kwa kweli foleni zimezidi hata kwenye ATM foleni ni kubwa sana.

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuchangia bajeti ya Wizara ya Fedha na baada ya shukrani na pongezi kwa Waziri, Naibu wake na watendaji wote, niungane na wenzangu kukipongeza Chama cha Mapinduzi, kwa kumchagua Rais Jakaya Mrisho Kikwete kama mgombea pekee atakayewakilisha Chama chetu kwenye Uchaguzi Mkuu. Nimpongeze pia Dr. Shein pamoja na Mgombea Mwenza, Dr. Ali Bilal.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami pia nadhani hii ndiyo mara ya mwisho kama nitapata nafasi tena basi itakuwa vizuri. Lakini nipende kutumia fursa hii kuwahakikishia wananchi wa Tabora, kwa mara nyingine mimi nina dhamira ya kuchukua fomu wakati ukifika ili kutetea kiti changu cha Ubunge Tabora Mjini. Kwa hiyo, zile propaganda ambazo zimekuwa zinaendelea kuwa Mheshimiwa Kaboyonga haji, ni uongo na mimi nasisitiza kwamba ninakuja kutetea kiti changu. Yapo mengi tumefanya na mengi tumetayarisha na dhamira yangu kama Waziri wa Fedha alivyosema kwa kule Kilosa, ni kuendeleza yale ambayo tumeshayawekea msingi ili tuweze kupata matokeo mazuri mwisho wa kipindi cha muhula ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichangie kwa kusema yafuatayo. Katika vitabu viliviyotangulia, tuliambiwa kuwa ukuaji wa pato la uchumi wetu baina ya miaka hii ya 2010/2013 haitofikia 8% yaani kwa sasa iko kwenye kasi ya 7.1%, itakwenda 7.3%, inakuwa 7.4% mpaka 2013. Ninachotaka kusema hapa ni kwamba kasi hii ya ukuaji wa uchumi ni ndogo ukilinganisha na kasi ambayo inahitajika ya kuondoa umaskini. Hatuwezi kuondoa umaskini Tanzania kwa ukuaji wa uchumi kwa kasi ya chini ya asilimia kati ya 8% na 10% na kwa mujibu wa takwimu zilizopo inaelekea kuwa itatuchukua muda mrefu kufikia 8% na 10% hizo ndizo kasi zinazotakiwa kuondoa umaskini Tanzania. Kwa hiyo, kazi iliyo mbele yetu, ni kuangalia ni namna gani tunautekenya uchumi wetu na kuusaidia uchumi huu ili uweze kukua kwa kasi kubwa zaidi kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika, ukiangalia uwiano baina ya mapato ya Serikali pamoja pato la Taifa kwa ujumla wake, bado ni uwiano mdogo kwa sababu sisi Tanzania tuko kwenye uwiano wa asilimia 16% wakati majirani zetu Kenya wako zaidi ya 22% hapa ninazungumzia *GDP. Revenue ratio* ya kwetu iko kwenye 16% wakati jirani zetu wako kwenye 22%. Kwa hiyo, kuna haja kubwa sana ya kuongeza mapato ya Serikali ili uchumi wetu uweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa sasa hivi tunazungumzia bajeti iliyopo, ni bajeti ambayo tayari kama ilivyo ni ndogo lakini tumejitahidi tumefika kwenye trilioni 11.6 bado haitoshi. Yapo maeneo ambayo Serikali ingeweza kwa makusudi kabisa kutumia utaratibu wa kukopa kutoka Benki Kuu kwa lugha ya kigeni ya kiuchumi tunasema *deficit financing*, ikiwa una miradi maalum hususani katika ujenzi na hasa

katika miundombinu eneo ambalo nakusudia kulizungumzia zaidi sasa. Serikali ikikopa kutoka Benki Kuu kwa ajili ya kuboresha miundombinu hususani bandari na reli, reli ikishatengenezwa maana matatizo makubwa ya reli sasa hivi ni kwamba hatuna mabehewa, hatuna injini na bila ya kuwa na injini zinazofanya kazi, hizi changamoto tulizonazo, tumesema tutumie uchumi wa kijiografia haziwezi kutuletea manufaa. Mimi niko tayari kuishauri Serikali ikope kutoka kwenye Benki Kuu yake lakini ielekeze mikopo hiyo kwenye miundombinu hususani reli na bandari kwa sababu kwa kufanya hivyo, tutatengeneza ajira nyingi sana na tutaufungua uchumi wetu. Mfumuko wa bei unaoweza kutokana na kukopa kutoka Benki Kuu utavizwa na matumizi ya hizo pesa kwenye kutengeneza miundombinu ambayo itahamasisha uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la Kitengo cha *Treasury Registrar* pale Hazina. Kitengo hiki ndicho kinachoshika mitaji katika makampuni mbalimbali ambayo Serikali ina hisa. Narudia tena, Serikali inahisa katika maeneo mbalimbali lakini lipo eneo moja mimi linaniuma sana, eneo hili ni mtaji wa Serikali katika Benki ya Twiga. Benki hii ya Twiga ni mali ya Serikali kwa asilimia 100 lakini mpaka leo Benki hii haijapata *license* ya kufanya kazi zote za benki. Inafanya kazi kama Taasisi ya Fedha kwa sababu haijawa na mtaji wa kutosha. Ili hii Taasisi ibadilike kutoka kuwa Taasisi ya Fedha iwe benki ni shilingi bilioni tano zile za chini kabisa, hivi Serikali nzima inashindwa kuweka bilioni tano? Mimi nashindwa kuamini. Ni uamu tu, mabenki yote yanayotuzunguka, mengi yaliyopo hapa nchini, ni ya kigeni, yanafanya biashara ya fedha kwa maana hiyo eneo hili la benki ni eneo la biashara. Sasa kama Serikali imeamua kutega uchumi kupitia Twiga Benki, kwa nini inashindwa kuiwekea fedha za kutosha ili na yenewe iwe benki kamili? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunaambiwa Serikali inapeleka shilingi bilioni arobaini kwa ajili ya Benki ya Wakulima, huu ulikuwa ni uamu tu, Serikali imeamua na pesa shilingi bilioni 40 zimepatakana. Hivi Serikali imeshindwa kusema shilingi bilioni kumi peleka Twiga Benki ili tuwe na benki ya biashara ya Serikali inayofanya kazi vizuri, ishindane na akina *NBC*, *ABSA*, na kadhalika, halafu mapato yote haya yawe mali ya Serikali? Ni suala la uamu tu! Kutuambia kwamba kila wakati hatuna fedha mbona kwingine zinapatikana? Ninaiomba Serikali iwekeze katika sekta ya benki, ni sekta muhimu, hatuwezi kupoteza pesa ili mradi muweke watendaji wazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la mafuta ya kuchakachua, ni tatizo kubwa sana. Dawa yake pamoja na mambo mengine yote haya ya kubadilisha sheria, tuwe wakali sana na kadhalika, dawa rahisi ni kupunguza tofauti ya bei ya mafuta ya taa na *diesel*. Kwa sababu mafuta ya taa yanatumiwa na wananchi wengi walio na vipato vyta chini basi mafuta ya *diesel* yapungue yakifuatiwa na *petrol* na mafuta ya taa yapande juu kidogo wakutane katikati. Ukipata hivyo, huna haja ya Polisi, huna haja ya kufanya nini, itaji-regulate yenewe tu. Kwa sababu ile *incentive* ya mtu kuchakachua mafuta haitakuwepo. Ili tufanye hivi, tunahitaji kutafuta mbadala wa mapato yatakayoziba pengo la yale mapato yanayotokana na kupunguza bei ya *diesel* na hii inawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba katika maelezo ambayo yamekuwa yanapatikana hapa Bungeni huko nyuma, tumeambiwa juu ya *infrastructure bond*, *bond* ambazo Serikali ikizitoa, itapata pesa na kuzielekeza kwenye miundombinu. Hatuoni hapa na wala hatuambiwi tumefika wapi juu ya hilo. Lakini lipo lile suala la *sovereign bond* ambalo tunajua mkakati bado unaendelea, ni vizuri Waziri atakapokuwa ana-*windup*, atuambie amefikia wapi juu ya hili. Kwa sababu tukitoa *sovereign bond*, tukakopa kutoka kwenye masoko ya mitaji ya nje, tutapata fedha kwa ajili ya kuendeleza miundombinu yetu. Tatizo kubwa la miundombinu ya Tanzania ni ukosefu wa fedha za kuwekeza. Kweli bajeti yetu kama bajeti yetu wenyewe haiwezi kumudu. Tuangalie namna tunavyoweza kukopa ndani na nje ya nchi kwa ajili ya miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa muda bado ninao, ninapenda vilevile nitumie fursa hii, kuishauri Serikali juu ya tatizo hili la pengo kubwa baina ya riba za kuweka kwenye benki na riba zinazotozwa tunapokwenda kukopa kwenye mabenki. Ukiweka unapewa asilimia tatu, ukienda kukopa unatozwa asilimia kumi na nane au zaidi, hii asilimia 15, haya mabenki yanaielezaje? Pamoja na kwamba wanawenza wakasema ni gherama za uendeshaji, sijui ni matatizo wanayoyapata kutokana mikopo chechefu na mambo kama hayo lakini bado kuna haja ya Serikali kupitia Benki Kuu kuona ni jinsi gani tunaweza kupunguza pengo baina ya riba tunapoweka kwenye mabenki na riba tunapokopa, vinginevyo uwezeshaji tunaouzungumzia kwamba wananchi watumie vyombo vyaya fedha ili waweze kupata fedha za kuendeshea miradi, hautowezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofî*)

MHE. DR. JUMA A. NGASONGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana kwa kunipa fursa hii na mimi nichangie hoja ya Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustafa Mkulo, mdogo wangu na rafiki yangu. Lakini pia napenda nimpongeze mdogo wetu mwininge, Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee na Watendaji wote nawapongeza kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimeshindwa kujizuia kuungana na wenzangu katika kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuteuliwa na Chama chetu kuwa Mgombea wa Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nina uhakika uteuzi huu utatupa fursa nzuri CCM kupata ushindi mkubwa wa kishindo. Lakini pia naomba nimpongeze Mgombea Mwenza, Dr. Mohammed Gharib Bilal, kwa uteuzi alioupata na nina hakika timu hii ya watu wawili ni kamilifu na itafanya kazi nzuri ili kuhakikisha kwamba ushindi wa CCM, ni wa kishindo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, naomba nimpongeze Ndugu yangu Mheshimiwa Dr. Ali Mohammed Shein, kwa kuteuliwa na Chama chetu kuwa Mgombea wa Urais wa Zanzibar. Nadhani safari hii CCM imefanya historia kubwa kwa kumteua Dr. Ali Mohammed Shein, mkazi wa Chokoch,

Mkanyageni, Mkoani Pemba, kuwa Rais. Nadhani sasa ubishi haupo tena kwamba safari hii kwa mara ya kwanza tutapata Rais wa Zanzibar kutoka Pemba, ni jambo zuri la kujivunia. Kwa hiyo, nina hakika Wazanzibari wote watampa ushirikiano Dr. Shein ili aweze kushinda kwa kishindo na tusiwe na Serikali ya Mseto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuchangia mambo manne, kwanza, jambo la wastaafu, pili, la utekelezaji wa Sera na Sheria ya Uvezeshaji Wananchi Kiuchumi na Dirisha la Kilimo katika benki ya *TIB* na *PPP* ile ya kushirikisha *private sector* ambayo Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Fedha na Uchumi ameielezea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo la suala la wastaafu la kuwalipa mafao yao baada ya miezi sita. Nimezungumza na Waziri, maoni yake nimeyakubali lakini nadhani sasa ni muhimu sana kutazama tena upya. Miezi sita kwa watu wangu wale wa Ulanga Magharibi pale unawapa matatizo makubwa sana. Kwa sababu miezi sita ile ndiyo wakati wa masika, ndipo wanahitaji pesa nyingi kwa matumizi yake binafsi. Anahitaji pesa kwa ajili ya kilimo, kupalilia mashamba yake ya mpunga, kwa mfano, sisi tunalima mpunga ambaao una kazi nyingi. Kwa hiyo, naomba sana hili jambo lifikiriwe. Wenyewe wanaomba iwe miezi mitatu angalau au kila mwezi mara moja. Sasa kama Serikali haiwezi kufanya kila mwezi basi fanyeni miezi mitatu. Najua mlitaka maoni na ushauri wa wadau wenyewe kwamba walipwe vipi na wengi wakasema miezi sita, lakini mimi nafikiri miezi sita ni mingi walipwe kwa miezi mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni utekelezaji wa Sera ya Uvezeshaji na Sheria yake. Sheria ipo na sera yake ya mwaka 2004 na mimi ndiyo nilikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Mawaziri wakati huo tulipofanya mambo hayo kwa pamoja. Mimi nadhani katika kutekeleza, suala lile halijatekelezwa vizuri. Ule mfuko mnaoitwa wa Mabilioni ya JK, una madhumuni yake mengi zaidi, ilikuwa ni kama vile kuhamasisha utekelezaji wa sera ile, lakini sera yenyewe imeunda chombo rasmi kinachoitwa Baraza la Taifa la Uvezeshaji Kiuchumi. Wajumbe wake wapo na Bodi yake ipo kama Baraza na watalaam wapo, kuna *Executive Secretary* wa Baraza lile. Juzi tuliwatengea shilingi milioni mia minne, tuliomba nyingi lakini tukapata mia nne tu, sijui mwaka huu wamepata kiasi gani, nitatazama baadaye na nitalizungumzia tena kwenye Kamati. Mimi nataka kujua kwa nini tunapata kigugumizi kuwatengea fedha, maana hiki ndicho chombo chenyewe cha uvezeshaji halisi wananchi, hizi zingine tunazozifanya hizi *SELF* mnatia humo, *SELF* inajulikana madhumuni yake ya uvezeshaji, lakini siyo wenyewe hasa, uvezeshaji wenyewe ni wa kutumia ile Sera ya Uvezeshaji Wananchi Kiuchumi na Sheria iliyounda na timu ya watu wapo pale, tulishaajiri watu, wapo pale sijui mnawafukuza? Watumieni wale mtoe pesa ya kutosha. Nchi zinazofanya uvezeshaji mzuri ni South Afrika, Malyasia na India pia, tumekwenda kule tume-study lakini hatutekelezi vizuri, fanyeni kazi hii rasmi, suala hili ni kubwa hata kwenye Ilani mpya inazungumzia jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *TIB*, nina mambo mawili ya kuzungumza, moja, ni ule mchango wa awali unaolipa wa asilimia 20, Waziri aliangalie hili. Haiwezekani watu watoe, matrekta sasa hivi ni milioni 40, asilimia ni kumi maana yake ni milioni nane mpaka milioni kumi, wakati benki binafsi inatoa milioni tano, sasa inakuwaje na huu ndiyo mfuko wa kuwawezesha wakulima? Mimi hili silielewii kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, suala hili lina urasimu mkubwa. Tunategemea *PASS*, pale *PASS* Morogoro mkubwa wake ni M-Denmark, ana matatizo makubwa, anachelewesha mambo, yanachukua muda, sasa tunapata mkopo wakati watu wanaanza tena kuvuna. Sasa mkopo wa kilimo cha trekta inatakiwa ifike mapema ili watu watumie kwa kulima. Hii *seasonality* ya kilimo ni lazima tuizingatie, hatuwezi kufanya kama vile tunakopesha wafanyabiashara, hii siyo sahihi. Mimi naomba hili nalo litazamwe, mikopo ya kilimo itolewe kwa wakati muafaka, hasa matrekta ili watu walime halafu tukianza kuvuna tusombe mazao yetu kwa kutumia matela. Sasa ninyi hamleti hii mikopo, watu tunavuna kule tunashindwa kusomba mpunga uko maporini, mambo gani haya? Mimi naomba hili jambo litazamwe vizuri na lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni *PPP*. Hili jambo ni zuri ambalo Mdogo wangu, Mheshimiwa Siraju ameliongelea vizuri.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MHE. DR. JUMA A. NGASONGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, kidumu Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika Bunge lako Tukufu. Lakini nianze pia kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa afya njema na kunipa nafasi ya kuweza kusimama asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwa asilimia 99.18 kuwa mgombea Urais kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi. Nampongeza pia Mheshimiwa Dr. Bilal, kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza kwa tiketi ya CCM bila kumsahau Dr. Shein kuteuliwa kuwa Mgombea wa Urais kwa Zanzibar. Ninaamini wananchi wote wa Tanzania watakipigia Chama cha Mapinduzi kura nydingi kwa asilimia mia moja kwa sababu tumewachagua wagombea makini na wenye uwezo wa kuendeleza nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kukusahau wewe pia nakuombea kura kwa wapiga kura wote wa Wilaya ya Kongwa au Jimbo la Kongwa. Umefanya kazi kubwa sana katika Wilaya ya Kongwa na wananchi wanaona na kutambua wajibu wako ulivyotekeleza Ilani ya CCM, wasikusahau na ningefurahi sana kama ningesikia wewe ni mgombea pekee katika Wilaya ya Kongwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Dodoma, nimefanya nao kazi kwa karibu na umakini zaidi, tumefanya mambo mengi katika Mkoa wa Dodoma. Tumetekeleza Ilani ya CCM, nawashukuru sana na kuwapongeza na kuendelea kuomba ushirikiano kutoka kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Waziri wa Fedha na Manaibu wake, Mheshimiwa Mkulo, alikuwa bosi wangu wakati tunafanya kazi Serikalini, najua uwezo wake wa kufanya kazi na uwezo wa kutekeleza wajibu na wananchi wa Kilosa pia wameona uwezo wake, namwombea kura kwa wananchi wa Kilosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona katika hotuba ya Waziri, amezungumzia juu ya madeni ya Watumishi kwamba katika mwaka huu wa fedha, madeni ya Walimu na sekta mbalimbali yatalipwa kwa mujibu madai yao. Tumechoka kusikia vitisho vyta migomo ya Walimu na baadhi ya sekta kama sekta ya afya, lakini hii inatokana pengine na uzembe wa wafanyakazi wachache waliopo katika Serikali yetu, ningeomba sana madai haya ya Walimu, posho za Walimu, posho za likizo na kadhalika, ifikie wakati sasa Serikali yetu iache kudaiwa na watumishi waliopo chini yake. Tunapanga bajeti, tunawaingiza kwenye bajeti hakuna haja ya watumishi kudai posho zao kwa Serikali yao mpaka kutishia kugoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la MKUKUTA II, kuna vipaumbele vimezungumzwa na MKUKUTA II kwamba wataweka kipaumbele katika kilimo na kadhalika lakini naipongeza Serikali kwamba kuna Dirisha la Kilimo katika benki ya *TIB*. Tukumbuke kwamba benki ya *TIB* ipo Dar es Salaam na ni wakulima wachache ambao wanaweza kufika Dar es Salaam kukopa au kufika kwenye Dirisha la Kilimo. Naishauri Serikali waangalie namna ya kuwa na dirisha lingine katika mabenki yetu au *TIB* waanzishe Dirisha la Kilimo katika Mikoa yetu la sivyo mikopo itaishia Dar es Salaam na Dar es Salaam hawana maeneo ya kulima, wana maeneo ya kujenga majumba yao lakini maeneo ya kulima hawana. Ninaomba sana suala hili pia likatazamwa upya kwamba Dirisha la Kilimo liwafikie wananchi walio wengi na waanzishe Dirisha la Kilimo katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapata uchungu mkubwa ninapokwenda katika maduka ya wafanyabiashara hasa katika Jiji la Dar es Salaam na nikaambwa bidhaa zinauzwa kwa fedha za kigeni na nilikwenda pale *Haidary Plaza* kununua *computer* na vitu vingine, wananiambia bei ni *USD*, kwa kweli niligombana na muuzaji kwa sababu niko Tanzania sioni sababu ya kuuziwa bidhaa kwa pesa za kigeni. Hili suala nadhani Serikali inalijua sijui kwa nini halifanyiwi kazi. Naomba Serikali yetu ilisimamie jambo hilo na kila bidhaa iuzwe kwa fedha ya Kitanzania. Nchi nyingine ukienda ukitoa *USD* sijui *Euro*, hawapokei mpaka utoe fedha ya nchi yao, naomba lisimamiwe hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia kuhusu *BoT*. *BoT* nawaomba sana, riba ni kubwa sana katika mabenki yetu, watu wetu wanashindwa kukopa, wana hamu ya kukopa lakini wanashindwa kukopa kutoptera na riba kubwa na inayotozwa kwa muda mfupi. Anayeweza kukopa na kupata faida kwa watu wa hali ya chini pengine awe muuza madawa ya kulevyaa lakini kama ni mfanyabiashara wa kawaada, hawezu kurudisha riba pamoja na fedha alizokopa kwa kipindi kifupi pasipo na biashara nyingine ambayo inaweza kumuingizia fedha. Muangalie suala hilo na mtajihidi kulirekebisha ili Watanzania wa hali ya chini waweze kukopa katika mabenki yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie tena suala la *CHC* ambayo inasimamia uuzaji wa Mashirika ya Umma yaliyouzwa. Mashirika mengi ya Umma yaliuzwa lakini mengine yaliyouzwa hayajawahi kuzalisha. *CHC* ipitie mashirika hayo, ifanye tathmini na yale ambayo hayajauzwa basi yarudishwe Serikalini yauzwe upya au Serikali iweze kuyahudumia. Tunaona *STAMICO* ilikuwa katika kuuzwa lakini ilirudishwa Serikalini, *STAMICO* inafanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, kwa kufanya kazi nzuri, *PPF*, *PSPF*, *GPF* wametujengea *UDOM* na sasa hivi wana mpango wa kusafirisha gasi kwenda Dar es Salaam, ninaomba Serikali iwaunge mkono na waweze kusafirisha gasi na kuendeleza nchi yetu kwa namna watakayoweza na watakavyoweza na kama wataungwa mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha nyingi za Serikali na hasa za maendeleo, zinapotea njiani au hzifikasi kwenye malengo yaliyolengwa kutokana na Halmashauri zetu kutokuwa na watalaaam hasa wa upande wa ununuvi. Fedha za Serikali zinapotea sana katika upande wa manunuvi. Mimi naiomba Serikali kuhakikisha kwamba Halmashauri zetu wana wawakilishi wa kutosha katika Halmashauri zetu. Sasa hivi fedha zinapelekwa nyingi katika Halmashauri zetu kwa mpango wa *D by D* lakini hazitafanya kazi vizuri kama hatutakuwa na Wahasibu wa kutosha katika Halmashauri zetu na watumishi katika Idara ya Ununuvi. Sasa naiomba Serikali na Wizara ya Fedha ambayo inasimamia Wahasibu wahakikishe kwamba Halmashauri zetu wanapata Wahasibu wa kutosha katika Idara zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia *CAG* kwa kazi kubwa anayoifanya na sasa *CAG* aweze kuwa na mamlaka. Mtumishi anayepatikana na makosa anakatwa asilimia 20 ya mishahara yao lakini asilimia 20 pengine ni shilingi 100 tu ambayo haimuathiri mtumishi ambaye amepatikana na makosa hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na kuwatakiwa Wabunge wote mafanikio mema na ushindi mkubwa wa kishindo katika uchaguzi wa mwaka huu 2010. Naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Felister Bura na sisi tunaomba akina mama wa Mkoa wa Dodoma wakuangalie kwa jicho la kipekee.

MHE. MOHAMMED AMOUR CHOMBOH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kwanza naanza kumshukuru Mwenyezi Mungu wa rehema, kwa kunipa uwezo wa kusimama mbele yenu, mbele ya jengo hili. Lakini pia kwa kuniwezesha kipindi chetu cha miaka mitano kuwa mzima wa afya na kutekeleza majukumu waliyonipa ndugu zangu wa Jimbo la Magomeni kule Zanzibar. Nao pia kwa nafasi ya pekee, nawapa shukrani kubwa sana kwa imani yao kwangu. *Inshallah* Mwenyezi Mungu akijalia kama nilivyokwishaahidi kwamba niko tayari kwa kipindi kingine kijacho kwa sababu nguvu ninazo, nia ninayo na uwezo, *Inshallah* Mungu atanipa kwa kushirikiana nao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo, kubwa zaidi nilikuwa nawaambia tu ndugu zangu na Wazanzibar kwa ujumla, Chama chetu cha Mapinduzi kimeshamaliza mchakato wa kuchagua viongozi wetu wakuu kwa maana Rais wa Zanzibar, Rais wa Jamhuri ya Muungano na Mgombea Mwenza. Kilichobakia sasa hivi, ni mshikamano tukijua kwanza Mwenyezi Mungu anampa amtakaye na kumkosesha amtakaye. Kwa hiyo, tusiteterere, cha msingi zaidi ushindi kwa CCM ni lazima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze Waziri wa Fedha na Uchumi, kwa hotuba yake na watendaji wote pamoja na Manaibu Mawaziri ambaye wamewasilisha leo hii. Mimi mchango wangu nafikiri ni mdogo tu. Kubwa zaidi ni ufanisi ambao tunaotegemea sana kuleta tija katika mapato ya nchi hasa ukizingatia Wizara ya Fedha ndiyo yenye dhamana ya kukusanya mapato kupitia kwa mamlaka ya *TRA*. Kwa uhakika *TRA* wanafanyakazi nzuri ya kukusanya mapato isipokuwa kila kizuri kwa kawaida huwa hakikosi kasoro. Kuna msemo mmoja aliwahi kusema Rais Mstaifu Mzee Ali Hassan Mwinyi kwamba, 'ua zuri ni la waridi lakini lina miiba'. Kwa hiyo, *TRA* pamoja na uzuri wote walijonao, pamoja na bidii walijonayo, kuna vitu fulani ambavyo kidogo vina kasoro, kwa hiyo, kuna haja ya kuweza kutafakari ili kufanya ufanisi mzuri zaidi na kuweza kukusanya mapato bila ya kuwa na mizengwe mizengwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa kabisa lililoikabili *TRA* ni urasimu. Urasimu wa maamuzi au urasimu wa utendaji wao mara nydingi sana unawakatisha tamaa wawekezaji na wafanyabiashara. Kwa mfano, mimi niko kwenye Kamati ya Biashara ya Viwanda, nilipata bahati kutembelea Mikoa tu yenye viwanda, lakini tatizo sugu katika viwanda vyote tulivyopita kuna mambo yenye usumbufu nayo ni maji na urasimu wa *TRA*. Kuna viwanda vingine wanassema sisi hatuna matatizo ya maji, lakini tatizo la *TRA* lipo. Hakuna hata mwekezaji mmoja asiyelalamikia urasimu wa *TRA*. Ndugu zangu wa *TRA* mjue mna jukumu kubwa la Taifa, jitahidini na jaribuni kutafakari ni kwa nini kila mahali wanalamika kuhusu *TRA*? Kwa mfano, kuna mtu mmoja aliwahi kuagiza bidhaa zake kutoka nje, ule mchakato wa kuagiza bidhaa zake mpaka ukafika Dar es Salaam, ikachukua wiki moja, mzigo ambao una kilogramu 400 hivi ni kama nusu tani lakini kuutoa pale bandarini, umechukua wiki tatu. Bidhaa ambayo siyo ngeni, ameshawahi kuletwa mara tatu, mara nne, si kitu kigeni kwao lakini wiki tatu ni kwa sababu tu ya *interest* ya mtu binafsi. Kuna baadhi ya wafanyakazi wanaiangusha *TRA* kwa vitendo ambavyo si sahihi na kinyume cha maadili ya kazi zao. Kuna kilio kikubwa sana katika kituo cha *TRA* cha Tanga, wahusika walifuatilie jambo hilo, *Customer Charge* ya Tanga anawasumbua sana wafanyabiashara wa Tanga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho nilikuwa nataka kuzungumzia, ni suala la *TRA* na *ZRB*, kule Zanzibar, wafanyabiashara wa Zanzibar wanalamika sana mamlaka hizi mbili kwa ulipaji wa kodi zao. Nafikiri ingekuwa jambo jema watu wa *TRA* na watu wa *ZRB* wakashirikiana, *TRA* wakawapa uwakala *ZRB*, mfanyabiashara akijua kwamba analipa kodi katika kitengo kimoja badala ya kwenda huku na huku, anakuwa na usumbufu matokeo yake ni kwamba bidhaa zinapanda bei na watu wanapata shida sana kwenye masuala hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri mchango wangu mkubwa ulikuwa ni huo. Kubwa zaidi nawasihi ndugu zangu wa Zanzibar, tushikamane na hasa wananchi wa Jimbo la Magomeni tushikamane tusitetereke, tujitahidi na tuweze kukirudisha Chama cha Mapinduzi madarakani. Naunga mkono hoja, ahsanteni. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana hasa kwa wito wako kwa wananchi wa Magomeni, turudisheeni chombo hiki. (*Kicheko*)

MHE. EMMANUEL J. LUAHULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, umenishtukiza kweli. Nilikuwa nimefikiria kwamba sitazungumza lakini acha nizungumze yale nitakayoweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nitumie fursa hii, kumshukuru Mungu kwa ulinzi wake na wema wake. Lakini pia niwapongeze Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM, kwa kazi nzuri waliyoifanya ambapo nisingependa kuielezea sana ikala muda wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitoe shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais kwa kutupa Mkoa wa Geita. Mimi ninawaomba wenzangu wa Wilaya zile tatu, Wilaya ya Geita, Bukombe na Chato, tukubali Makao Makuu yawe Bukombe na sababu zote zipo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 60 ya eneo la Bukombe ni msitu, tunawenza tukapata sehemu za kuweka kila *infrastructure* zinazotakiwa. Lakini kama sivyo, basi niwaombe Serikali ichukue ushauri wangu kwamba, tuweke Makao Makuu katikati kwa maana ya kwamba, tuchukue Kijiji cha Iparamasa kutoka Wilaya ya Chato, Kijiji cha Magenge kutoka Wilaya ya Geita na Kijiji cha Kabanga kutoka Wilaya ya Bukombe halafu hapo katikati tutaweka miundombinu yetu safi na Mkoa wetu utakuwa wa kisasa. Nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Manaibu Mawaziri na watendaji kwa ajili ya hotuba hii. Lakini ninalotaka kuzungumza ni suala la Bima ya Taifa. Bima ya Taifa, Mheshimiwa Rais aliamua kuunda *Task Force* kwa ajili ya kufanya marekebisho lakini liko suala la ulipaji madeni katika shirika hili. Tarehe 6/7, Serikali ilijibu swali langu hapa Bungeni, liliuliza kuhusiana na madai ya watu ambao bima zao zinaiva na jinsi wanavyohangaika sana kupata mafao yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wadai hawa wengi wao ni Walimu, Watu wa Afya na Maaskari, wanahangaika sana. Shirika hili limekosa uwezo wa kulipa madeni haya kwa sababu halina mtaji wa kutosha. Lakini Shirika hili lina rasilimali zake, katika kurekebisha imekubalika kuuza nyumba za wafanyakazi ili waweze kujitosheleza au *TBA* wasimamie suala hili lakini Serikali sijajua kama wamekubali kudhamini *TBA* ili waweze kusimamia na hatimaye Shirika hili liweze kupata uwezo wa kulipa madeni haya. Sasa hivi wateja wengi wa Shirika hili wanaogopa kwa sababu wanaona madeni yao hayalipiki. Siku ile wakati swali langu linajibowi nilieleza kwamba, mimi Wilayani kwangu nimekuta Walimu ambao ni wateja wa shirika hili, wako kwenye *guest house*

wanalipiwa pale na pesa wanazolipa ni zile pesa kidogo kidogo. Kwa hiyo, ninaomba sana Serikali isimamie wateja ili waweze kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini liko suala la madeni ya watumishi wa Serikali. Wako Watendaji wa Vijiji na watumishi wengine katika Wilaya yangu ambao kwa muda mrefu sana wanaidai Serikali. Kila tunapouliza kwenye vikao vya *Council*, tunaambiwa Hazina ndiyo inalipa. Tunaomba Serikali iwalipe ili wasiendelee kudai. Wapo wengine wanadai kutoka mwaka 1998 mpaka leo, tunaomba Serikali iwalipe madai yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako pia watumishi ambao hawako kwenye *payroll*, wanlipwa na Halmashauri. Wilayani kwangu wako kama watumishi 58, wameajiriwa kutoka mwaka 1994, 1997 na mpaka leo hawako kwenye *payroll*. Ni kweli wengine hawana sifa, lakini walijiriwa kipindi kirefu kabla ya utaratibu wa Sheria mpya ya mwaka 2004. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba hawa watu muwaingize kwenye *payroll* ili nao waweze kupata hata mikopo leo hawakopesheki hawa kwa sababu wanaambiwa hawana dhamana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naenda kwenye huduma za kibenki. Ninaipongeza Serikali kwa sababu ilitusaidia tukapata benki ya *NMB* katika Wilaya yetu. Lakini yako maeneo mengine kama Runzewe, ambayo yana watu wengi sana, wafanyabiashara na wakulima. Tunaomba mtusaidie tuweke pale angalau *ATM*. Lakini pia ikiwezekana tuweke tawi pale kama alivyoongea mchangiaji mmoja aliyetangulia. Watu wanapata shida kwa sababu Wilaya ya Bukombe kama tunavyojua ni kubwa halafu tunayo benki moja ya *NMB*. Nashauri ikiwezekana tuweke *ATM* pale Runzewe kwa maana ya Uyovu, lakini pia pale Masumbwe ambapo ni *centres* kubwa sana, zina watu wengi na hiyo itawasaidia sana hata katika kuchukua pesa na pia katika kuwawezesha kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ukaguzi wa ndani. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ameleeza kukiwezesha Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani, tunaomba muwasaidie kwa sababu hawana vitendea kazi. Pesa nyingi zinakwenda kwenye Halmashauri, hawana magari, bajeti yao ni ndogo, sina uhakika kama tunaweza tukadhibiti sana pesa hii. Ninaomba Mheshimiwa Waziri muangalie, muwasaidie kwa kuwapa magari ili waweze kuzungukia miradi hii, waangalia *value for money* katika miradi yao, vingenevyo pesa hizi tunashindwa namna ya kuzidhibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzugumza hayo, niwashukuru sana wananchi wa Wilaya ya Bukombe na Jimbo la Mbogwe ambalo ni jimbo jipyaa na niwaombe wachague Mbunge atakayekuwa mwakilishi mzuri, atakayesimamia kuendeleza yale niliyoyafanya kule lakini waendelee kuniunga mkono katika Jimbo la Bukombe kwani ninaamini tumefanya kazi kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninawatakia kila la kheri Wabunge wote, Mungu awarudishe kwa kadri atakavyopendezwa. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Luhahula, muda wetu hauruhusu tena mchangiaji mwagine, tutaendelea na uchangiaji jioni. Lakini Waheshimiwa Wabunge kwa kuwa Mkoa wa Geita unaleta taabu Makao Makuu yawe wapi, kwamba yawe Geita, Chato au Bukombe, mimi ninapendekeza kwa Mheshimiwa Celina Kombani, Makao Makuu ya Mkoa huu, yawe Dodoma, karibu na Ofisi ya Mheshimiwa Waziri. (*Makofî/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, jioni tutaendelea na uchangiaji, bado tuna wachangiaji kama wanne hivi. Mheshimiwa Herbert Mntangi, atafuatiwa na Mheshimiwa Godfrey Zambi. Lakini tutakuwa na Maseneta wawili wenye hotuba maalum, Mheshimiwa Paul Kimiti na Mheshimiwa Juma Nh'unga, baada ya hapo tutaendelea kumalizia hoja ya Serikali ya Waziri wa Fedha na Uchumi kuhusiana na makadirio na matumizi ya Wizara ya Fedha na Uchumi.

Baada ya hapo jioni hii hii, tutashughulikia Muswada wa Sheria ya Serikali kama *Order Paper* inavyoonesha, *The Appropriation Bill*, Sheria ya kuidhinisha matumizi ya Serikali kwa mwaka 2010, kitu ambacho ndiyo kitafunga shughuli yetu kwa maana ya suala zima la bajeti kwa kipindi chote hiki ambacho tumeanza tangu mwezi uliopita. Nitawaomba kuwahi ili tumalize mambo yetu vizuri na mapema.

Lakini kabla sijaondoka hapa, kuna matangazo mawili, moja linajirudia, lakini nilirudie pia, kwamba Waheshimiwa Wabunge amba hamjachukua na kujaza fomu za Maadili, mnakumbushwa kuchukua fomu hizo katika Ofisi ya Katibu wa Bunge.

Lakini tangazo lingine ni kwamba kuna marekebisho ya shughuli za kesho ambapo ilikuwa imeandaliwa mapema kwamba tujadili Muswada wa *Public Procurement 2010*, Muswada huo hautawasilishwa katika Bunge hili, utashughulikiwa na wenzetu watakaokuja au kama tutarudi sote, Mwenyezi Mungu ajalie, kuanzia Novemba. Sasa kesho kutakuwa na *The Written Laws Miscellaneous Amendment 2010*, kwa hiyo, tujiandae kwa Muswada huo.

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea kama nilivyosema saa 11.00 jioni, kwa hiyo, nachukua fursa hii basi kusitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00, ahsanteni.

(*Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

MwenyeKITI (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea kuhusiana na hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi kulitaka Bunge kuitisha makadirio ya matumizi ya Wizara husika kwa mwaka wa fedha 2010/2011. Sasa kama tulivyosema wakati tunaahirisha ni kwamba mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa ni Mheshimiwa Herbert Mntangi - Mbunge wa Muheza. Karibu Mheshimiwa.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nikushukuru sana wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia leo katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Lakini nikupongeze pia kwa kazi nzuri ambazo unafanya pamoja na Spika na jopo lenu lote. Bila shaka Mwenyezi Mungu atawajalia mtaweza kurudi na mwendelee na nafasi hizo tena. Niwapongeze pia Mheshimiwa Waziri, Manaibu wake wote na Watendaji wote wa Wizara hii pamoja na taasisi na sekta zilizoko chini ya Wizara hii ya Fedha. Kazi wanazofanya ni nzuri, mwelekeo ni mzuri, bila shaka uchumi wetu utaimarika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza kwa njia ya pekee ndugu zangu wanaofanya kazi pale Hazina hasa wale wanaosaidia kuangalia matatizo ya mafao ya wastaaafu. Kazi ile ni ngumu kwa sababu inahitaji kutafuta kumbukumbu ambazo ni za muda mrefu wa miaka mingi iliyopita. Idadi ya watu wanaokwenda na kulalamika pale ni wengi, lakini vijana pale wanajitahidi kuwa wavumilivu, wanajitahidi kuwa na lugha nzuri, wanawasaidia. Mimi binafsi nawapongeza sana kwa sababu zaidi ya asilimia 90 ya wananchi wangu wa Wilaya ya Muheza waliokuwa na matatizo ambayo waliyapitishia kwangu wamefanikiwa kupitia kwa vijana wale. Wapo wengi, lakini yupo mmoja ambaye anajitahidi sana na wanafanya kazi kama timu. Nawapongeza wote kwa ujumla. Kazi bado ni ngumu, bado ni nzito, madai ya mafao bado yapo, ninawaomba waendelee kuwa wavumilivu na wanawasaidia wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumie kidogo kuhusu *TRA*. *TRA* wanafanya kazi nzuri, lakini tuwatazame vizuri kwa makini *TRA* katika Mkoa wa Tanga. Inaonekana kama vile watu wanaanza kuona kama vile mapato yanashuka. Zipo sababu nyingi japo kubwa inawezekana vile vite kitaifa, mafao yale ambayo walipewa wafanyakazi wa *TRA* sasa yamekwishakuwa kama sehemu ya mazoea na hayana tena *incentives*. Basi tuangalie upya namna gani ya kuweza kutengeneza *incentive package* nyingine ya kuwawezesha wafanyakazi hawa kufanya kazi kwa bidii kama walivyokuwa wakifanya awali ili makusanyo ya mapato yaweze kuongezeka.

Lakini la pili, tutazame katika Mkoa wetu wa Tanga na mimi nazungumzia Muheza. Sasa baadhi ya viongozi, lugha wanazotumia kwa walipakodi wakati mwingine haziridhishi. Zipo kauli wakati mwingine za matusi, lugha mbaya, sio kwa viongozi wote, yupo mmoja na hili ukienda kwa mlipakodi ye yote wa Muheza atakwambia yule fulani pale anatusumbua. Kauli za namna hiyo zinawakatisha tamaa walipakodi na mimi nafikiri wajibu wa viongozi na kuwashauri walipakodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anapochelewa kulipa, wewe kama kiongozi unapashwa kuchukua fursa ya kumshauri na zipo adhabu zinazotolewa kwa wale ambao kwa bahati mbaya wanachelewa. Kwa hiyo, msitumie nafasi ya kumwona mtu amechelewa kwa bahati mbaya, basi ukamkashifu, ukamtukana, hutamsaidia mlipakodi. Wewe kama kiongozi, uwe karibu na mlipakodi, mvute mlipakodi. *TRA* wanajitahidi kutoa matangazo ya kuwakumbusha watu kulipa. Sasa haya ni ya kitaifa, tujitahidi vite vile kuwe na utaratibu mzuri wa kuwakumbusha walipakodi katika ngazi hizi za Wilaya pale pale ambapo walipakodi wapo. Huo ni ushauri wa pekee wa *TRA* ili waweze kuongeza mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba utaratibu wa kutoa fedha kutoka Hazina hasa zile zinazoelekezwa kwenye Halmashauri zetu, utaratibu uimarishwe ili kupunguza ucheleweshaji wa upelekaji wa fedha hizo. Tumeona jinsi ilivyokuwa ngumu, kwa mfano zinazotakiwa kwenda kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Muheza zianze kuitia TAMISEMI halafu ndio ziende Halmashauri ya Wilaya ya Muheza. Tumefanya mabadiliko hayo kwamba sasa fedha zinaweza zikaenda moja kwa moja katika Halmashauri zetu. Naomba hilo tuliiamarishe.

Lakini vile vile tuwe na mpango madhubuti ya kuzisimamia fedha hizi, ni fedha nyingi sana zinakwenda Halmashauri kule. Mara nyingine fedha zimekwishaingizwa katika akaunti za Halmashauri lakini ukiwaambia wataalamu, wanasema fedha zimeshaletwa, jibu rahisi wanasema fedha bado hazijaingia. Lakini ukija kutazama unakuta fedha nyingi zimeingia. Kwa hiyo, usimamizi tuuimarishe katika maeneo hayo na tuweze kuziimarishe Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tujitahidi kuhakikisha walimu wanalipwa madeni yao. Tunajua walimu wanapata uhamisho, kwa nini kwa walimu kulipwa fedha za uhamisho ni baada ya ye ye kujigharamia mwenyewe? Wafanyakazi wengine wanalipwa, halafu wanahama, lakini kwa nini walimu ni madeni tu? Ajihamishe ye ye mwenyewe, aje adai baada ya miaka miwili! Tubadilike, tubadilishe na tutenge fedha kwa ajili ya kuwasaidia walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme sasa habari kidogo za Muheza na hasa maji. Tunajitahidi kuchimba visima ili kuondoa matatizo ya maji ili kuwawezesha wananchi waweze kufanya kazi kwa bidii na kuongeza mapato. Ni matumaini yangu kwamba fedha tunazozipeleka kwa ajili ya uchimbaji wa visima zitafanya kazi ya kweli kwa ajili ya uchimbaji wa visima ili kuwaondolea matatizo wananchi.

Mimi binafsi pamoja na waasisi walionisaidia tumeweza kuchimba kisima kimoja kwa gherama ya shilingi milioni sita pamoja na pampu shilingi milioni nane, kisima kinachokwenda zaidi ya mita 30 mpaka 50. Lakini ukipeleka fedha, leo tumepata fedha shilingi milioni 50. Nina uhakika kama utaratibu nilioutumia mimi wa kuwawezesha kisima hicho kuchimbwa kwa shilingi milioni nane pamoja na pampu ukitumiwa kwa shilingi milioni 50 tutapata visima vitano.

Lakini tukiachia fedha hizo zikapita katika mkakati mwengine wa kufuata sheria ile ya manunuvi, basi kisima kimoja kitachimbwa kwa shilingi milioni 25, kwa shilingi milioni 50 na tutapata visima 2 tu. Naomba tuangalie kama tumeweza kufanya hivyo, shilingi milioni 50 hizi zilizokwenda atumiwe mkandarasi anayechimba kisima kwa kiwango tunachokihitaji kwa viwango vya fedha vilivyopo badala ya kwenda kwenye *tender* na kutumia shilingi milioni 50 kwa visima viwili badala la kuchimba visima vitatu.

Ndugu zangu wa Masuguru, ndugu zangu wa Genge, ndugu zangu wa Mjengo, Michungwani na pale Bwembwela wasiwe na wasiwasi, fedha hizo zitatumika vizuri, maji yatapatikana, tutapunguza adha hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, ninaomba niishie hapo kwa leo, nikushukuru wewe, niwashukuru wapigakura wote wa Wilaya ile ya Muheza kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa mimi. Mimi hawa mavuvuzela hawanitishi. Ninasema atakayeamua ni Mwenyezi Mungu, lakini na wananchi wenyewe wanajua kazi nzuri tunazofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mavuvuzela hawa katika jitihada za kuchimba visima, vuvuzela mmoja anakwenda kuwaambia watu wasichimbe visima vile atawapa fedha na huyo anataka Ubunge. Lakini jitihada za kuchimba visima anakwenda kuwakwamisha wasichimbe ili shida iendelee kuwakabili wananchi wa Wilaya ya Muheza. Huyu anawafaa kweli wananchi wa Muheza? Mimi nawashukuru sana na mimi naomba niseme kwamba ninatangaza nia, nitakwenda, nitaomba Mwenyezi Mungu ninajua kwa msaada wake na kwa huruma ya wananchi wa Wilaya ya Muheza nitafanikiwa kurudi tena.

Nawatakia kila la heri wote na ninawaombea wote mrudi katika eneo hili na tufanye kazi kwa jitihada kama tulivyoonesha kuzifanya mwanzo. Wale watakaokuwa wageni tunawakaribisha. Ahsanteni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia machache kufuatia hotuba ya bajeti ambayo imewasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Manaibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu kwa kazi nzuri waliofanya ya kuandaa bajeti ya Wizara yao na kuiwasilisha hapa Bungeni leo kama nilivyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwanza kuwapongeza viongozi wa Chama changu cha Mapinduzi kitaifa, Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuteuliwa na chama chetu kuwa mgombea pekee kwa ushindi mkubwa sana. Lakini pia nimpongeze sana Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein kwa ajili ya kuteuliwa kuwa mgombea Urais kwa nchi yetu ya Zanzibar, lakini pia nimpongeze sana Dr. Mohamed Galib Bilali kwa kuchaguliwa kuwa mgombea mwenza katika uchaguzi mkuu ujao. Hii ni timu makini na mimi naamini Chama cha Mapinduzi kitashinda kwa ushindi mkubwa sana ule tunaoita wa kishindo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizi kwa viongozi wangu kitaifa, naomba nianze kuchangia katika meneo machache. Kwanza mimi natoka Mbozi, wote tunajua Mbozi ni Wilaya ya kilimo, Mkoa wote wa Mbeya ni Mkoa wa kilimo. Kwa hiyo, naanza kuzungumza na suala ambalo linagusa masilahi ya wakulima kwa sehemu kubwa. Serikali na kupitia Wizara hii tumeshaambiwa mara kadhaa na utekelezaji tunauona wa kuanzisha dirisha la kilimo kupitia Benki ya Rasilimali ya Taifa (*TIB*). Suala hili mimi nimekuwa nazungumza mara kwa mara na wote tunajua kwamba azma ya Serikali ni kumkomboa mwananchi mkulima atoke kilimo cha shuruba, lakini afanye kilimo cha tija zaidi. Sasa kuna mambo ambayo yananitia wasiiasi kwa maana ya kwamba wananchi wanaweza wakafaidika na mkopo huu kutoka Benki ya *TIB*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masharti ambayo yamewekwa, nimeshazungumza na viongozi kadhaa wa Wizara ya Fedha yuko kaka yangu Raston Msongole, Naibu Katibu nimeshakaa naye lakini na viongozi wengine nikawaambia mimi nimeoneshwa kutokuridhishwa sana na masharti yaliyowekwa pamoja na kwamba nia ya Serikali ni kuwa na uhakika kwamba pesa zitakazokopeshwa zinaweza zikarudishwa, lakini wasiiasi wangu ni kwamba mabenki mengine ya kibiashara tuna *NMB*, *NBC*, *CRDB*, *BARCLAYS*, *EXIM* tuna benki nyingine nyingi.

Benki hizi zinaruhusu mtu mmoja mmoja kukopa. Mimi kinachonishangaza ni dirisha hili la kilimo kupitia *TIB* kukataa kumkopesha mtu mmoja mmoja kwa maana ya kuwa na wasiiasi kwamba inawezekana pesa zisirudi. Sasa tunataka kumsaidia Mtanzania wa namna gani? Kwa nini lazima tuwalazimishe kwamba lazima tupitie *SACCOS*, wapitie vikoba, wapitie taasisi nyingine za kifedha? Kwa nini tuwalazimishe? Mimi nadhani tungeyapeleka yote mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wakulima ambao mimi nawajua ni waaminifu, wana uwezo wao wanapokuja wanaomba Serikali ijiridhishe tu kwamba dhamana walizonazo zinajitosheleza na wanaweza kabisa kulipa kama wakikopa wao kama wao.

Kwa hiyo, naiomba sana Serikali iangalie sharti hili, vinginevyo tutaendelea tu kupiga kelele kwamba sio sharti linalolenga kumsaidia huyu mwananchi mkulima na mimi niliuliza swali hapa katika Mkutano huu wa Bunge unaoendelea nikauliza Mbozi wanatasahili kupata wangapi? Nikaambiwa walioomba watatu, nikaambiwa mmoja amekataliwa kwa sababu alikopa kwingine, lakini nikaambiwa wawili hawa maombi yao yanapitiwa. Kwa hiyo, huyu mmoja mwininge anaitwa Kenneth Mwazembe amenipigia simu wiki iliyopita anasema ameandikiwa barua kwamba anatakiwa apitishe maombi yake kutoka kwenye taasisi yoyote ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ametekeleza masharti mengine yoyote, kwa nini tuwazue kukopa na hawa ndio wakulima tunawalenga waweze kulima? Mimi naomba Mheshimiwa Waziri atueleze, lakini sharti hili halimtendei haki huyu mkulima hata kidogo. Naomba Serikali iendelee kuliangalia na *inshaallah*, Mwenyezi Mungu akinijalia kurudi hapa Bungeni nitaendelea kulipigia kelele mpaka nione kwamba wananchi hawa wanaweza kufaidika na mikopo hiyo vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine ambalo ningependa nilichangie. Ukisoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ukurasa wa 59 pale mpaka 60 kuna sentensi ambayo inasomeka kama hivi, naomna niirejee, anasema: “Benki Kuu imeandaa mkakati wa kuboresha huduma za kifedha maeneo ya vijijini, yaani (*Rural financial Services*) Strategy ili kuongeza ushiriki wa wananchi vijijini katika kupata huduma za vyombo vya fedha.”

Ninaomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha atueleze, mkakati huu unasema nini? Maana mimi sioni. Kuna taasisi nyingi zinazoendelea kukopesha huko Vijijini na maeneo mengine naona ni za kinyonyaji zaidi kuliko kuwanufaidisha wananchi, wakulima.

Nimewahi kuzungumza hapa Bungeni kwamba kuna baadhi ya taasisi zinatoza wananchi zaidi mpaka asilimia mia tatu. Kuna taasisi kama *Group Financial Services, Bayport Financial Services* na nyingine za namna hiyo, mtu anakopa *interst rate* tena wanachaji kila mwezi. Ukichukulia mpaka kipindi chote cha miaka miwili, mitatu anachajiwa zaidi ya asilimia mia tatu.

Sasa Benki Kuu wanasema wana mkakati wa kuboresha hii huduma huko vijijini naomba Mheshimiwa Waziri atuambie ni mkakati gani huu ambao Benki Kuu inaanda ambao unalenga sasa pengine kuwainulia wananchi maisha huko vijijini. Vinginevyo kama hali ndio hiyo, sidhani kama tutakuwa na mkakati wote ambao unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kingine kinachohusiana na Benki Kuu nilisema hapa Bungeni, Benki Kuu ndio inayosimamamia taasisi nyingine zote za fedha nchini, lakini nikashauri kwa sababu inaonekana sekta hizi zinafanya kazi bila kusimamiwa, basi Benki Kuu iwe na utaratibu wa kuandaa kanuni au masharti ya kazibana taasisi hizi. Lakini mpaka leo Mheshimiwa Waziri nadhani alipoulizwa ndani ya Bunge hili amewahi kusema kwamba Benki Kuu inaendelea na kutayarisha masharti haya. Masharti haya yatakamilika lini? Naomba Mheshimiwa Waziri atueleze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la mwisho, nizungumze kwa sababu ya muda ni *pension* kwa wastaafu. Bado *pension* kwa wastaafu ni ndogo, wananchi hawa wameitumikia nchi hii kwa uadilifu mkubwa sana, wengine miaka 20, wengine miaka 30, leo tunawalipa *pension* kima cha chini Sh. 51,000/=. Mimi sidhani kama tunakwenda vizuri. Ninaomba Serikali iendelee kuwaangalia na ninashauri kila tunapoongeza kima cha chini, kila tunapoongeza mishahara kwa watumishi wa Serikali na kima cha chini cha *pension* pia kipande ili watumishi hawa waliotumika vizuri sana huko zamani waweze kufaidika.

Lakini lingine ni kumbukumbu. Kumbukumbu za wastaafu ni tatizo kubwa. Tunajua mazingira ambayo wengi tunaishi, kumbukumbu zinapotea, sasa unapostaafu unakwenda Wizara ya Fedha wanakwambia lete barua uliyojiriwa, mtu ameajiriwa mwaka 1970 anakwambia barua ilipotea, huwezi kumsikiliza. Lete barua uliyopandishwa cheo, barua ilipotea, anaulizwa. Jamani hatuwatendei haki hawa. Mimi naomba Serikali iwe na wajibu mkubwa zaidi wa kutunza kumbukumbu za wasataafu inapofika wakati wa kustaafu, basi wananchi hawa waweze kustaafu bila matatizo yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, naomba nimalize kwa kuwashukuru wananchi wa Mbozi kwa ushirikiano mkubwa walionipa katika kipindi cha miaka mitano. Naomba niwahakikishie kwamba bado nina nguvu, nina akili timamu na moyo wa dhati kabisa wa kuendelea kuwatumikia. Ninaomba waendelee kunipa imani na mimi naamini, na naomba niwaahidi kwamba sitawaangusha, nitaendelea kufanya kazi kwa nguvu zangu zote na uwezo wangu wote na kwa akili zangu zote. Naomba wananchi wa Mbozi mnipe ridhaa yenu, niko tayari sana kutumika na kuishauri ipasavyo Serikali hii ya Muungano wa Tanzania. Nashukuru sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Zambi. Ni matumaini yangu kabisa kwamba wananchi wa Mbozi wamekusikia.

Sasa Waheshimiwa Wabunge wanaofuatia ni wawili. Wachangiaji hawa ni maalumu kabisa na kwa heshima yao kila mmoja wao nimempa robo saa. Ataanza Mhehsimiwa N'hunga atamalizia Mheshimiwa Paul Kimiti. Mwishoni mtanikubalia kwa nini nimefanya hivyo. Mheshimiwa N'hunga.

MHE. JUMA S. N'HUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba yetu sote naomba nichukue nafasi hii nimshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyetujalia leo tukiwa wazima na wenyewe afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina tofauti na wenzangu wanaotangaza nia. Mimi ninatangaza nia ya kutokugombea. Kwenye Bunge lako hili, nimehudhuria Mikutano 100. Kwa maana hiyo, nimeishi katika Bunge hili kwa mfululizo kwa miaka 25. Kabla ya hapo, niliwahi kuwa Mkuu wa Wilaya miaka minne, nimefanya kazi Ikulu mwaka mmoja. Karibu miaka thelathini na zaidi nimefanya kazi.

Namshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa hiari yangu bila kushawishiwa, naamua kung'atuka. Bila ya kusahau, niseme tu na ninyi wenzangu mliokuwepo ndani ya Ukumbi na wale amba hampo katika Ukumbi, kila mmoja katika nia yake Mwenyezi Mungu amjalie, basi aishi zaidi ndani ya Bunge hili mara mbili ya mimi. Nitafurahi sana nikija, nikiwakuta wenyeji wangu ninaowafahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikutakie kila la kheri wewe, umeingia kipindi chako cha pili, ni kijana mtiifu, nimekaa na wewe vizuri. Nakuombea kila la kheri na bila shaka utashinda. Namshukuru sana Mheshimiwa Spika wa Bunge letu la Jamhuri ya Muungano kwa kipindi chake hiki, ameleta mageuzi makubwa sana katika Bunge hili, Kanuni na vitu vingine vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii umeingia hapa umevaa joho, Spika wetu zamani alikuwa anavaa Mgolole. Ni vitu tofauti kabisa! Hayo ni maendeleo. Naibu Spika na Wenyeviti walikuwa hawana kitu maalum cha kucaa. Leo Bunge letu kweli ni la viwango na ninategemea kama Mungu atajaalia Mheshimiwa Spika na yeze apite katika Jimbo lake kwa kishindo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uingereza pale ukipata Uspika, Wabunge wengine wa vyama vingine hawaji katika Jimbo lako. Kwa hiyo, unapita bila ya kupingwa. Kwa sababu ukigombea na Spika pale Uingereza utakuwa huna mpango wa kuitisha hoja binafsi. Kwa maana hiyo, wana Kanuni yao hiyo kwamba ukishafikia Uspika, wewe unapitishwa tu. Sasa ningewaomba vyama vingine vya Upinzani, basi Mheshimiwa Spika kule akapite bila kupingwa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, nianze kusema kwamba mimi naunga mkono hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa asilimia mia moja. La kwanza ambalo nitalizungumzia ni suala la pensheni. Pensheni kwa wastaafu wetu, Watanzania wanafanya kazi vizuri sana. Wanaenziwa wakati wanafanya kazi. Lakini

wanapostaa fu hali zao zinakuwa dhalili sana, baadhi yao pensheni zao ni ndogo. Pensheni hazilipwi kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata leo hii ni mwezi wa saba huu, pengine ndiyo wakati wa kulipwa pensheni mwezi wa sita. Lakini mpaka leo kwa msimu huu bado wastaafu mwezi huu hawajalipwa. Nasikitika sana, lakini hivi vyombo vya pensheni ndivyo vinavyojenga Vyuo Vikuu. Vyuo Vikuu vyote vimejengwa na pesa za wastaafu, lakini wastaafu wenyewe wako hoi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kusema tu kwamba Serikali iwaangalie upya kwamba watu wanaostaafu waweze kuishi kwa kulipwa pensheni inayoweza kweli kuendeleza maisha yao, siyo kulipwa pensheni kama msaada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maneno mengine ni kwamba, nilipokuwa namsikiliza Mheshimiwa Waziri alisema kwamba kuna changamoto kwamba kila makisio yanapofanywa, basi huwa hayafikii kiwango. Hivi kwa nini makisio haya hayafikii kiwango, au makusanyo hayafikii kiwango? Kwa nini basi Serikali isingeangalia upya vyanzo vyetu viko namna gani? Viwango vyetu vya kodi viko sawa? *TRA* inafanya kazi vizuri? *TISCAN* ikoje? Kuna mwanya kiasi gani ambao unasababisha viwango visifikasiwe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza ukashangaa sana, ukienda pale *TRA* ukaangalia hali halisi utashangaa kazi inavyokwenda. Makontena yanayokuja pale, urasimu uliokuwepo pale utaudhika!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeiomba Serikali iangalie uwezekano wa kuondoa urasimu. Jambo lingine ambalo nitaliomba na lenyewe ni kuhusu suala la Bandari. Tanzania ni tajiri wa bandari. Mtwara kuna bandari, Lindi kuna bandari, Tanga kuna bandari, Dar es Salaam kuna bandari na Zanzibar kuna bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kwa nini bandari zote hizi, moja hatuteui ikawa bandari huru? Nimeambiwa hapa Pemba kuna bandari. Tuteue bandari moja iwe huru. Ukienda Singapore utakuta kuna bandari huru, wanapakia mizigo, wanashusha kwa wakati, haraka zaidi. Hong-Kong ukienda utakuta kuna bandari huru. Wanafanya kazi nzuri. Dubai wana bandari huru. Sisi kwa nini hili jambo hatulitilii maanani? Kwa mfano ukiweka bandari huru pale Zanzibar itakuwa ni bandari itakayohudumia Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii wakati mwingine unaona bora kushusha mzigo wako Mombasa kuliko kushusha Dar es Salaam kwa sababu gharama ni kubwa. Ukaushie Mombasa, uutoe Mombasa, uuingize Tanzania, bado gharama za kutoa kule kuuleta huku ni rahisi. Nini sababu? Urasimu! Ningewomba Mheshimiwa Waziri hili aliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nitakalolisemea ni la bidhaa feki. Tunaona bidhaa feki nyingi zinaingia katika nchi na kuvurugwa. Hivi nini kutufanyia uchuro

katika nchi yetu ? Unaivuruga *TV* wewe mwenyewe kuitengeneza huwezi, unasema feki. Kwa nini bidhaa hizo zisikaguliwe huko huko zinakotoka? Vikaguliwe huko huko kama mtu kaenda kununua China, China huko huko. Maana watu wanaonunua magari Hong-Kong, Uingereza, *TBS* iko kule kule. *TBS* wanakwambia kwamba gari hii haiwezi kuingia Tanzania, haina sifa, huko huko! Unalipa dola 250 kila gari huko huko, ikifika hapa ina kibali cha *TBS*. Kwa nini basi watu wetu wa *TBS* hawa wa viwango vyta hizo bidhaa wasiwe huko huko, vikafelishwa huko huko, vikarudi huko huko kuliko kutuingizia mzigo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba hilo na lenyewe liangaliwe. Pale bandari ninakumbushwa kuna uchomoaji chomoaji. Kontena nzima inapotea, vifaa vyta ndani ya magari vinapotea. Hili ni jambo la kuangalia. Linawapa shida sana Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema, wenzangu wamezungumzia sana kuhusu chama, kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano kuwa mgombea na kumpongeza Dr. Bilal kuwa mgombea mwenza. Nadhani hili halina ubishi la kumpongeza Dr. Shein kuwa mgombea wa Urais wa Zanzibar. Nadhani hili halina ubifishi. Watani zangu hapa wamesema sema hapa kwamba safari ijayo wanategemea watachukua madaraka. Hilo haliwezekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeng'atuka Ubunge, lakini nitabakia kuwa mwanachama wa Chama cha Mapinduzi. Sababu ya kung'atuka, mimi sasa sio somo tena, ni nyakanga. Nyakanga kazi yake ni kuchezesha unyago, hachezesewi. Nataka kusema kwamba mwaka 2010 mhakikishe kwamba CCM itashinda kwa kishindo, itashinda kwa kishindo Zanzibar, wala hatutazami kwa sababu Shein katoka Pemba, tunachagua Chama. Chama kwanza, mtu baadaye. Tutashinda kwa kishindo Tanzania Bara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wameshapiga kura za maoni, katika wagombea 19, saba ndio waliopata kura. Hiyo ndiyo indiketa. Hakuna sababu, kama ni pweza katabiri keshatabiri kwamba Chama cha Mapinduzi kitashinda kwa kishindo, tunaona indiketa. Sasa ndugu zangu niseme tu kwamba Chama cha Mapinduzi mwaka 2010 kitashinda kwa kishindo, na wale amba wanapenda kuwahi hili gari nafasi bado ipo, waje tunawakaribisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza hayo, nirudie tu kuwashukuru sana kama nilivyosema, mimi nimesimama hapa kwa kutangaza nia ya kutokugombea. Jimboni kwangu nimeshaaga, mpaka ninaondoka kulikuwa na vijana 24 wanataka Ubunge. Nadhani mmoja anaweza akachaguliwa akaja Bungeni. Sasa baada ya hapo, nirudie kusema naunga mkono hoja na sio mimi tu, Mheshimiwa Naibu Waziri naye nimpongeze, maana Naibu Waziri pamoja na kwamba kafanya kazi miaka mitano, lakini na ye ye ameshatangaza nia ya kutokugombea. Ameamua kwenda kuchukua *Ph.D* kwanza, akirudi huko sasa ndiyo anarudi kwa kishindo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nakutakia kila la kheri na fanaka. Niwashukuru watumishi wote wa Bunge, niwaombe radhi wale ambao pengine niliwakwaza hapa na pale, tusameheane. Sina mtu ambaye amenikosea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza hayo, nakushukuru. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITU: Ahsante sana Mheshimiwa N'hunga. Hotuba yako ni ya kipekee. Baada ya kutumikia Bunge hili mikutano 100 kwa mfululizo miaka 25, ni nadra sana kwa Mwenyekiti wa Bunge kuwaomba Wabunge wampigie makofi Mbunge mwingine. Naomba kwa hili, ahsanteni sana. Ni mfano bora kabisa. Sasa mchangiaji wa mwisho ni Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa *Senetor*, karibu.

MHE. PAUL P. KIMITI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa heshima mimi na mwenzangu Mheshimiwa N'hunga angalau tutoe nafasi ya kusema machache ambayo tutakuwa nayo. Ni heshima kubwa sana umetupatia hatuwezi kuisahau. Lakini nitumie nafasi hii kumpongeza Waziri wa Fedha ndugu yangu Mheshimiwa Mustafa Mkulo. Tunafahamiana naye wakati nikiwa Waziri wa Kazi alikuwa ndiye mtendaji wangu mkuu wa *NSSF* na ndiyo kwa kweli alikuwa chanzo cha kuibua mipango yote ya *NSSF*. Najua uwezo wake na ndiyo maana sina wasiwasi, nimekwisha mwandikia ya kwamba naunga mkono hoja yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, mkutano wangu huu ni wa 120. Namshinda mikutano 20 tu Mheshimiwa N'hunga hapa. Maana yake ndiyo nimemaliza miaka 30 ndani ya Bunge hili na kwa miaka yote hiyo sijawahi hata siku moja kukosa hata mikutano mmoja. Mikutano yote 120 nimehudhuria bila kukosa. Hivyo nina haki ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa upendo aliokuwanao juu yangu mimi kunipa afya ya kuweza kutekeleza majukumu yangu salama. Lakini pia kunipa nafasi ya kuchangia zaidi ya mara 360 katika Bunge lako Tukufu.

Pia natumia nafasi hii kumshukuru Rais wetu - Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete wakisaidiana na mwenzake upande wa Zanzibar Mheshimiwa Dr. Karume - Rais wa Zanzibar na Baraza la Mapinduzi kwa kuiweka nchi kuwa katika hali ya amani na usalama kwa kipindi chote tulichokuwanacho. Mengine nitachangia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana wapigakura wangu wa kutoka Manispaa ya Sumbawanga, wamenivumilia kwa muda mrefu sana, lakini kwa kila kipindi kilichokuwa na uchaguzi nilikuwa napata kura za kishindo. Mwaka 1995 nilishinda kwa asilimia 82; mwaka 2000 nikashinda kwa asilimia 86; mwaka 2005 nikashinda kwa asilimia 89 zaidi. Kwa hiyo, nasema kila mwaka walikuwa wanajenga imani juu yangu. Nawashukuru sana kwa hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitumie nafasi hii nimshukuru sana mke wangu Julia na watoto wangu, wajukuu zangu na wote wale waliokuwa wanabitakia mema. Wamenivumilia mengi sana. Suala la uchaguzi, wote mnafahamu Waheshimiwa

Wabunge sio suala dogo. Lina maudhi, lina kejeli, lina uchokozi, lazima uwe mvumilivu ili uweze kushinda. Nakumbuka mwaka 2000 wakati wa uchaguzi vijana waliwahi kupita pale nyumbani kwetu wakati ule na mama mzazi akiwepo ambaye alishatangulia mbele ya haki wakiimba afadhali kufa kuliko Kimiti! Afadhali kufa kuliko Kimiti! (Kicheko)

Sasa mama yangu aliposikia wanaimba afadhali kufa kuliko Kimiti, akauliza hivi Kimiti umekosa kazi gani mpaka wewe utukanwe na watoto wadogo wakati una uwezo ungeweza kufanya kazi nyingine? Nikasema mama hao watoto wameandalila tu na kikundi cha Vyama vya Upinzani. Nilichofanya wale vijana niliwakusanya, kazi ndogo tu, nikawagawia pipi, wakaanza kuimba Kimiti hoyee! Kimiti hoyee! (Kicheko/Makofi)

Sasa mama alifurahi kwa sababu akaelewa ubunge ni mchezo wa kisiasa. Nikasema ndugu zangu msije mkadharau maneno yanayopita mitaani mkaogopa, wakati mwingine mngeyafanya *home work* yanaweza kuwa ni maneno yamepandikizwa tu, hivyo katika msingi huo nataka kuwaasa msiwe na wasiwasi kama unafanya kazi vizuri utashinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitumie nafasi hii pia kuwashukuru Wabunge wenzangu wote mliopo hapa. Nikianzia na Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Wenyeviti na wote kwa kweli ambao tumeishi nao kwa kipindi cha miaka yote hiyo. Nataka niungane na nyinyi ya kwamba kwa kipindi chote hiki mmenipa nafasi kubwa na mmeniheshimu sana kwa kipindi chote hicho na mara nyingi mlikuwa mkiita Seneta mkiwa na maana ya kwamba ni kiongozi wa siku nyingi, mwenye maadili mema, mwaminifu, mpenda watu na hiyo imenipa nafasi ya kuweza kuendelea kuwashukuru sana kwa kazi nzuri mliyokuwa mmeifanya. (Makofi)

Nawashukuru pia watumishi wote wa Bunge kwa jinsi walivyokuwa wakinihudumia kwa kipindi chote. Naomba kwa kweli hata kama nikondoka msinisahau. Nitakuwa nawatembelea mara kwa mara. Tuombeane kila la kheri na uzima.

Mwisho kabisa, niwashukuru Watanzania wote popote pale walipo. Nasema hiki kwa sababu kwa kipindi changu cha miaka 30 ningeweza kukorofishana na wengi sana. Lakini napenda kuwashukuru kwa sababu wameendelea kuniheshimu popote nilipokuwa na tumejenga mahusiano mazuri sio wananchi tu wa Chama cha Mapinduzi lakini pia na wananchi wa vyama vingine, wamekuwa wakiniheshimu kwa ajili ya kusimamia haki na utendaji wa kazi. Napenda kuwashukuru wenzetu upande wa Upinzani wamekuwa wakishirikiana na sisi vizuri. Kwa sababu sio suala la kuja kupingana tu. (Makofi)

Lakini mara nyingi tumekuwa tukipingana kweli, lakini bila kupigana. Huu ni mwanzo mzuri. Nataka tuuendeleze na mimi ndiyo ombi langu kwenu wenzetu wa upande wa upinzani. Lakini pia nataka nimalizie kwa shukrani. Nataka niwashukuru Waandishi wa Habari popote walipo. Nasema hili ilifikia mahali fulani watu wakadhani waandishi wa habari wanani pigia ndogo ndogo. Ilifikia mahali fulani kwenye kila chaguzi wanasema Kimiti atakuwa Waziri Mkuu; uongo, kweli? Sasa nikaogopa nikisema hawa wanantakia mema au mabaya? Mbona hivi? Siku moja nikapigwa simu

na Tido Mhando akiwa *BBC* ambaye ni Mkurugenzi wetu wa *TBC* akasema Mheshimiwa Paul Kimiti naomba nizungumze na wewe. Nikasema kuna nini?

Nasikia umependekezwa utakuwa Waziri Mkuu. Uongo, kweli? Sasa nikasema haya mambo yanatoka wapi? Mimi nadhani pamoja na nia nzuri nataka kuwahakikishia ya kwamba kwa kipindi chote waandishi wamekuwa wazuri sana. Ni watu ambao wana nia nzuri.

Lakini mimi nataka niwaombe tu ya kwamba sasa ndiyo tunakwenda kustaafu. Tunakwenda kulima, tutaendelea kushirikiana nao na mimi nitashirikiana nao katika hali yoyote. Niwatakie kila la kheri, waendelee kufanya kazi yao vizuri hasa katika kipindi hiki cha uchaguzi ambacho kina mizengwe mingi, angalau wasaidie ili nchi yetu tuvuke salama katika suala lote la uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumalizia kwa kusema hivi, kwa nini nimeamua kustaafu? Ziko sababu nyingi sana. Kila mmoja, kila Mbunge anapoingia hapa anakuwa na malengo yake. Kila Mbunge huamua ya kwamba kwa kipindi cha miaka mitano nitafanya yafuatayo, kufuatana na ilani yetu. Unaweza kuwa na vipindi viwili, vitatu unasema kwa kipindi hicho ninategemea nitakuwa nimekamilisha yote. Mimi nilikuwa na malengo manne zaidi.

Suala la kwanza lilikuwa ni kuangalia elimu; la pili, lilikuwa ni afya, maji na barabara. Umeme nilikuja kuliingiza kwa ajili ya matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa elimu, ninashukuru na ninaondoka nikiwa kifua mbele ya kwamba wakati ninaingia kwenye madaraka ya Ubunge, tulikuwa na sekondari nne tu katika Halmashauri yetu, leo ninaondoka kifua mbele katika Halmashauri ya mji pale zipo sekondari 25. Ndio kusema kwamba ninaondoka huku nikiwa nimeweka misingi mizuri, hivyo sina wasiwasi. Lakini la muhimu katika shule za msingi, pia ninaondoka nikifurahi ya kwamba kati ya shule zetu za msingi Shule ya Chanji kwa kipindi cha miaka miwili mfululizo imekuwa kati ya shule bora za shule za msingi katika mitihani, ambapo tunajua tuna Shule za Msingi karibuni 10,000 au 11,000, lakini hii shule katika Manispaa yangu, imekuwa ni ya kwanza katika utaratibu; kwa hivyo ninamshukuru Mwenyezi Mungu, tumekwenda vizuri. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine lilikuwa ni suala la barabara. Barabara za Sumbawanga kwa kweli tulikuwa tunasema tumekosa nini kwa Mungu? Mpaka tukafikia mahali fulani tukasema labda wametusahau?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninapenda kushukuru ya kwamba nimeridhika kabisa na hatua ambayo Rais wetu - Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete amechukua hatua ya kwamba sasa kufa na kupona, barabara zote za Mikoa hasa ile ambayo ilikuwa imesahalika pamoja na Rukwa, sasa zitatengenezwa kwa kiwango cha lami. Sasa Mkoa wa Rukwa barabara karibuni zote ambazo tulikuwa na wasiwasi nazo zimeanza kutengenezwa kwa kiwango cha lami. Mungu akupe nini? Ninaondoka nikiridhika kwamba sasa misingi niliyoweka inaanza kutekelezwa. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine lilikuwa ni suala la umeme. Umeme amba tulikuwa tunaupata ulikuwa unatoka Zambia, na kutoka Zambia tulikuwa na usumbufu mkubwa sana. Baada ya kulalamika ndani ya Bunge na wote ni mashahidi, Rais ametizama tatizo letu na amekubali kutuletea jenereta nne. Mwezi uliopita ametuwekea jiwe la msingi, tunaletewa jenereta ambazo zitakuwa na uwezo wa kuweka *Megawatt* karibuni sita badala ya *Megawatt* 1.5. Ninamshukuru Rais kwa hilo. Mungu akupe nini? Msingi nimeshauweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na matatizo makubwa sana ya maji na kati ya maazimio yangu ilikuwa ni lazima nihakikishe maji yanapatikana katika mji wetu wa Sumbawanga. Ninamshukuru Mwenyezi Mungu, baada ya kilio cha muda mrefu, kwa kushirikiana na Mawaziri wetu na kwa kushirikiana na Serikali, sasa tumepata mradi wa *World Bank* amba unakuja kutandaza mabomba yote mapya katika mji wetu wa Sumbawanga na unagharimiwa na *World Bank* kwa karibu shilingi bilioni tano. Sasa nina imani kabisa kwamba kwa msingi huo, hatutakuwa na tatizo la maji katika mji wetu wa Sumbawanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ninadhani kwamba ni zuri ni la afya. Afya yetu imeboreka sana. Juzi Mheshimiwa Rais, ametuwekea jiwe la msingi na kufungua maabara ya kisasa ambayo ina vifaa vyta kisasa. Hatuna haja ya kwenda tena Mbeya, mambo yote tutayamaliza pale Sumbawanga. Mungu akupe nini? Ninamshukuru Rais kwa yote haya ambayo ametufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni suala zima la kilimo. Mimi ni mtaalamu wa kilimo. Kwa kipindi chote ninamshukuru Mwenyezi Mungu, kwamba tumekuwa tukiongoza kwa kilimo bora katika Kanda ya Nyanda za Juu. Mwaka jana katika utaratibu wetu wa kushindana katika Mikoa, mkulima wa kwanza katika Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ametoka Sumbawanga katika Manispaa yangu pale. Tena ni mwanamke, ndiye amekuwa mkulima bora kuliko wote katika Kanda yote hiyo. Mimi ninajivunia sana kusema kwamba utaalamu wangu wa kilimo haukupotea. Tumejenga misingi ambayo ninadhani nina imani nayo. (*Makofū*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninaomba sasa niseme kwamba kwa heshima kubwa ya kihistoria mimi nitakwenda kumshukuru Rais kwa kutupa heshima. Hata ninapostaafu ninafurahi kwa heshima kubwa ambayo umeiweka. Sisi tunaiona kama miujiza katika Mkaoa wetu wa Rukwa, kwa kutupatia Waziri Mkuu - Mheshimiwa Mizengo Pinda. Ni heshima ambayo hatukuitegemea, ni heshima ambayo wana-Rukwa wanasema kumbe mvumilivu hula mbivu! Tuvumilie iko siku Mwenyezi Mungu atatenda muujiza kwa Mkaoa wa Rukwa. Iko siku Mwenyezi Mungu atatufanyia maajabu katika ndani ya Mkaoa wa Rukwa. Maajabu yameshaanza kutokeea. Mimi ninamshukuru Mwenyezi Mungu, tuna imani na sisi tumemwahidi Rais, hatuna cha kumpa, tutakachompa ni kura zetu zote katika Mkaoa wetu. Tunamuhakikishia kwamba tutampa kura zetu zote kama alama ya shukrani.

Pia tumeamua tutamsaidia Waziri wetu Mkuu Mheshimiwa Pinda, ili kipindi hiki asipate wapinzani wa kijingajinga wale na kama inawezekana apite bila kupingwa. Ni heshima kubwa, haitokei, ni nani anaweza kufanya kazi zaidi? Kipindi cha miaka miwili aliyoofanya katika Mkoa wetu, umebadilika haraka sana. Halafu wanakuja watu wenye vurugu kwa sababu tu wana shida tu kutaka angalau waonekane wanashindana na wakubwa. Mimi ninaomba sana watupe heshima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuomba sana sasa nimwombe Waziri mambo mawili. La kwanza, ni ununuzi wa mahindi Sumbawanga. Miaka miwili iliyopita tumekuwa na shida sana, wakati mwengine magunia yanachelewa na wakati mwengine fedha hazitoshi. Lakini sasa ninakuomba Mheshimiwa Waziri, kuna fedha ambazo zimetengwa kwa kununua mazao katika Mkoa wa Rukwa na nchi nzima, shilingi bilioni 18. Shilingi bilioni 18 ni sawa na tani 50,000 tu. Malengo ya Wizara na Serikali ni lazima tununue angalau tani 150,000.

Ingawaje mimi ni mtaalamu wa kilimo tani 150,000 *is nothing* kwa kulisha nchi hii. Kama mtapata matatizo tu, *is nothing*. Mimi ninadhani ni vizuri mkaangalia, kuna fedha mlizokuwa mmeamua kuzitoa kwa ajili ya kulipia madeni ya chakula kilichokwenda kuwasaidia watu waliokuwa na matatizo, karibu shilingi bilioni 48. Tungependa kujua Mheshimiwa Waziri, ni kwa nini hizo fedha zisipatikane ili tuanze kununua mazao katika Manispaa zetu na katika miji yetu na katika Mikoa ambayo mwaka huu watazalisha nyingi zaidi kuliko miaka mingine yote? Isionekane fujo imetokea kwa sababu ya kipindi hiki cha uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, Mheshimiwa Waziri, ninakuomba sana. Naunga mkono hoja yako, lakini ninaomba maelezo kuhusiana na maombi haya. Ahsante sana. (*Makofi*)

MCHANGO KWA MAANDISHI

MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Waziri wa Fedha na Uchumi - Mheshimiwa Mustafa H. Mkulo na Naibu wake, Mheshimiwa Omari Y. Mzee na Mheshimiwa Jeremiah S. Sumari kwa hotuba nzuri ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya majukumu makuu ya Wizara ya Fedha na Uchumi ni kusimamia ukusanyaji wa mapato kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*). *TRA* inafanya kazi ngumu sana ya kuziba mianya ya ukwepaji kodi, kudhibiti uvunjaji wa mapato ya Serikali na kadhalika. Tatizo lililonisukuma kuchangia hoja hii ni biashara ya magendo ya sukari iliyoshamiri Mikoa ya Kusini, hasa Mbeya, Rukwa na Ruvuma. Biashara hii ya magendo imelikosesha Taifa mapato yake kwa zaidi ya miaka kumi na hali hii itaendelea kwa miaka mingi ijayo, tusipokaa chini kulitafutia tatizo hili ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiini cha tatizo hili ni gharama za uzalishaji wa sukari nchini Malawi na Zambia ziko chini, hivyo kuifanya sukari hiyo kuwa ya bei poa inapovushwa mipakani kwa magendo, yaani bila kulipiwa ushuru. Matokeo yake, sukari ya Tanzania hainunuliki!

Nakisia hati ya uzalishaji wa sukari nchini na mahitaji halisi inayojitokeza kila mwaka. Tuna upungufu wa takriban tani 200,000 za sukari kila mwaka, yaani sukari ya viwandani na sukari ya matumizi ya kawaida. Nahisi hiyo inabidi iiazwe kwa kuiagiza sukari nchini kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kukabiliana na sababu hizo mbili kwa kuruhusu sukari ya magendo. Tayari idadi kubwa ya vijana Wilayani Kyela wamejiingiza kwenye biashara hiyo na vyombo husika vya dola Polisi na *TRA* vimeshindwa kudhibiti hali hii. Badala yake, baadhi ya watendaji katika vyombo hivi wamekuwa wafanyabiashara wazuri wa sukari hiyo ya magendo, kwa kuitwaa (kuikamata) na kuiiza wenyewe. Hatuwezi kuendelea na hali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa vyema kuwa biashara ya sukari duniani kote inaendeshwa kwa taratibu maalum ili kulinda kilimo cha miwa na viwanda vya sukari ndani ya nchi. Naelewa vile vile kuwa mbali na kulinda viwanda vyetu vya ndani, nchi yetu ni wajibu kisheria kufuata masharti ya Afrika Mashariki chini ya *The East African Community Customs Management Act, 2004*. Chini ya sheria hii, Mikoa ya kusini ina fursa ya kuiomba Bodi ya Sukari kuingiza nchini sukari ya Malawi kama sehemu ya kuziba nakisi inayojitokeza kila mwaka.

Nina uhakika kuwa Kamati ya ufundi ya *Sugar Importation* haiwezi kuikatalia mikoa hii ili kulimaliza tatizo hili la magendo kwa kuwaruhusu waingizaji sukari kwa magendo, waingize sukari hiyo kwa ushuru nafuu. Kama nilivyodokeza awali, waingizaji sukari ni vijana wanaorusha sukari hiyo kidogo kidogo. Nikipewa moyo na Wizara, ni rahisi kwangu kuwakusanya vijana hawa wakaunda *SACCOS* yao ili tupate *legal personality*, *SACCOS* ambayo itapewa leseni kuingiza sukari hiyo kihalali na wanachama wake wawe askari wa kuhakikisha kuwa sukari ya magendo haipenyezwi tena Wilayani Kyela. Tukifika hapo, Serikali itapata ushuru wake na biashara ya magendo ya sukari ndani na nje ya Serikali itatoweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SACCOS* ya Kyela ikisimama, itakuwa rahisi kuanzisha nyingine Wilayani Mbozi na Mkoani Rukwa kwa sukari inayotoka Zambia. Bila kuchukua hatua hii tutaendelea na biashari hii ya magendo kwa miaka mingei sana ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mlheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Waziri, Naibu Mawaziri, Naibu Katibu Wakuu na Katibu Mkuu na

watalaam wote waliohusika katika maandalizi ya bajeti hii na kuiwasilisha hapa Bungeni. Hata hivyo, nina mambo machache ya kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanzisha dirisha la kilimo ndani ya Benki ya Rasilimali Tanzania. Hili ni jambo jema kwani linalenga kuwapa wakulima uwezo wa kuzalisha zaidi na kwa tija. Hata hivyo, jambo la kusikitisha ni kwamba masharti yaliyowekwa na benki hiyo ni magumu kutekelezwa na wakulima wengi nchini. Pamoja na ukweli kwamba riba za mikopo ziko chini (asilimia tano mpaka nane) kuliko benki nyingine. Lakini masharti ya kuwataka wakopaji kupitisha maombi yao kwa taasisi nyingine za fedha naona ni jambo ambalo limepitwa na wakati. Mkopaji pia anatakiwa awe na *statement* za benki za miaka mitatu. Sina hakika kama kweli ipo nia ya kumsaidia mkulima huyu wa Tanzania kukuza kilimo chake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mabenki (binafsi) ambayo yanatoa mikopo kwa mtu/mkopaji mmoja mmoja ili mradi ametimiza masharti mengine. Ni sababu gani hasa inayofanya benki ya *TIB*, dirisha la kilimo kushindwa kutoa mikopo kwa mtu mmoja mmoja? Je, Serikali haioni kwamba hilo likiachwa hivyo, benki hii itabaki kuwa na manufaa kwa wakulima wakubwa tu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 59 mpaka wa 60 wa hotuba ya Waziri umeeleza kwamba Benki Kuu imeandaa mkakati wa kuboresha huduma za kifedha vijijini. Nataka kujua huo mkakati wa huduma hizo za kifedha una mambo gani? Nasema hivyo kwa sababu bado huduma za kifedha kwa wananchi wa vijijini na Tanzania kwa ujumla hazipatikani kwa urahisi.

Wote tunajua masharti ya upatikanaji mikopo pamoja na riba zake ni kubwa sana. Tunaona pia jinsi ambavyo masharti ya ukopaji hata ndani ya *TIB* - dirisha la kilimo yasivyolenga kuboresha huduma ya kifedha katika maeneo ya vijijini. Je, mkakati huo wa Benki Kuu unataka kurekebisha mambo hayo ambayo mimi nayaona kama hajalengi kuboresha huduma za kifedha vijijini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo taasisi nyingi nchini ambazo hujihusisha na biashara ya fedha. Kwa uelewa wangu mdogo wa sekta ya fedha katika nchi zote duniani, masuala ya fedha husimamiwa na Benki Kuu. Lakini jambo la kushangaza nchini kwetu ni kwamba Benki Kuu inaonekana haisimamii sekta ya fedha kikamilifu. Ushahidi ni kama ule wa Taasisi za *Blue Financial Services*, *Bayport Financial Services*, *Pride Tanzania* na kadhalika kufanya biashara ya fedha huku wakitoa riba za kinyonyaji kabisa (riba kati ya asilimia 30 – 100!) Aidha, hivi karibuni Taasisi ya *DECI* ilianzishwa na kuanza kufanya biashara ya fedha nchini.

Taasisi hii ilisambaa kwa haraka karibu nchini kote na kutoa mikopo ya zaidi ya shilingi za Kitanzania bilioni 12. Jambo hili kubwa linafanyika kwa muda bila Benki Kuu kujua. Hivi Taasisi hiyo ya *DECI* ilipata wapi leseni ya kufanya biashara? Zaidi, nataka kujua Benki Kuu imefikia wapi kutunga kanuni zitakazotoa miongozo ya taasisi hizo za kifedha, kufanya biashara ya kweli, biashara isiyolenga kumnyonya Mtanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo Watanzania wenzetu ambao wamelitumikia Taifa hili kwa uadilifu mkubwa sana, lakini inapokuja kuwalipa haki zao za kustaafu inakuwa taabu kubwa sana. Pamoja na jitihada za Serikali za kurekebisha kasoro zilizopo, bado mazingira hayajawa mazuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kumbukumbu ni kikwazo kikubwa sana. Hivi Serikali yenyewe huwa haina kumbukumbu za watumishi wake mpaka imlazimishe mtumishi huyu aliyeajiriwa takribani miaka zaidi ya 20 iliyopita atoe barua yake ya kuajiriwa kwa mara ya kwanza, barua ya kupanda cheo? Mambo ya ajabu! Naomba hali hii irekebishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Nawasilisha.

MHE. FLORENCE E. KYENDESYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara hii iangalie sana kuhusu fedha za J. K. ambazo Rais alikuwa na nia njema ya kuwainua wananchi kiuchumi ambao wana hali duni kimaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba Wizara hii ifanye ufuatiliaji wa fedha hizi zikipelekwa Wilayani kwa ajili ya *SACCOS* wananchi wengi haziwanufaishi, wanaokopa kutokana na uongozi wa *SACCOS* hizo, baadhi yao sio waaminifu kwa fedha hizo za *SACCOS* kwani wengine wamelenga miradi hiyo kama zao binafsi. Sehemu nyingine wakopaji wanatozwa riba kubwa au wanacheleweshwa kupata mikopo yao. Naomba Mheshimiwa Waziri achunguze suala hili, ni la ukweli, ili faida ya fedha hizi zionekane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

MHE. ESTHERINA J. KILASI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Nampongeza Waziri - Mheshimiwa Mustafa Mkullo, Manaibu Waziri, Mheshimiwa Jeremiah S. Sumari na Mheshimiwa Omari Y. Mzee pamoja Katibu Mkuu - Bwana Ramadhani M. Kaijah na timu yake yote ya wataalamu walioko ndani ya Wizara na mashirika yaliyoko chini ya Wizara ya Fedha na Uchumi, kwa kazi nzuri zilizofanywa kwa kipindi chote tulichokuwanao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina machache ya kuchangia. Pamoja na Wizara kufanya jitihada za kusimamia uuzaaji wa mali zilizoainishwa kuuzwa ili kulipa madai ya Bima, zoezi hili linachukua muda mrefu sana na kusababisha wananchi kutumia muda wao mwangi kufuatilia madai yao. Kwa kuwa kuna nyumba au majengo ya shirika hili yamechukuliwa na Serikali, kwa nini Serikali isiyalipie majengo hayo ili wadai hawa walipwe haraka hasa waalimu na wafanyakazi wengine ambao makato yao yaliiva siku nyingi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna tatizo la ucheleweshaji na upelekaji wa pesa za maendeleo za miradi na Halmashauri hii inasababisha gharama za ulipaji wa riba kutokana na kutokamilisha malipo kutokana na makubaliano ya mikataba. Hasa hili limejitokeza sana kwa upande wa madai ya makondarasi wa ujenzi wa barabara. Sasa Serikali imeweka mkakati gani ili kupunguza tatizo hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mikopo inayotolewa na mifuko ya pensheni kwa Serikali, hakuna mikataba iliyosainiwa baina ya Serikali na mifuko hiyo ambayo imejithahidi sana katika ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma. Je, Wizara itakamilisha lini zoezi hili ili kuondoja hoja za ukaguzi kwa Wizara na mifuko hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa ulipaji na mafao ya wafanyakazi waliokuwa chini ya mashirika ya umma hadi kufikia miaka 55 umeonekana kuwa na malalamiko kwa baadhi ya wastaa fu waliopunguzwa kazi kabla ya umri wa kustaafu. Je, kuna utaratibu gani unaomwezesha kupata malipo yake mtu ambaye hajafikisha miaka 55, lakini afya yake iko hatarini na anahitaji kulipwa mapema? Nimekuwa nikiulizwa swali hili, sina jibu la uhakika ingawa umuhimu upo kama sheria/kanuni hairuhusu, basi iangaliwe upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kusimamia na kuongeza mitaji kwa Benki ya *Tunga Boncorp. Ltd.* na Benki ya Rasilimali Tanzania *TIB*. Benki hizi ni muhimu sana kwa Watanzania. Ombi ni kupeleka matawi ya benki hizi kwenvye maeneo mengi. Tuanzie kikanda hadi kimkoa ili kuongeza wigo wa huduma zinazozotolewa na benki hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Mbarali kwa sasa ina ongezeko kubwa la shughuli za kibashara na kilimo. Wananchi wanatumia *NMB* tu ambayo iko Makao Makuu ya Wilaya. Ombi ni kuanzishwa Tawi la Benki ya Posta katika maeneo ya Chimala lau Igerusi ambako ni katikati ya Wilaya na kuna idadi kubwa ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *CHC Ltd.*, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na taasisi hii, waisaidie Serikali katika kuamsha madeni yote ambayo yanalamikiwa na wafanyakazi walioachishwa kazi baada ya mashirika yao kuuzwa au kubinafsishwa. Kumekuwa na malalamiko ya kimya kimya kwa Serikali au viongozi wanapotembelea maeneo mbalimbali ambako kuna wafanyakazi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua hatua iliyofikiwa katika kuwalipa wastaa fu waliokuwa *NAFCO*, *URAFIKI* na *Kilombero Suga Ltd.* Ni vizuri kupunguza kesi za madai kwa Serikali na jitihada za kuhakikisha madeni yote ambayo hajalipwa kwa Serikali na waliouziwa makampuni na Serikali ziongozwe na *CHC Ltd.*

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri yenyeye ufafanuzi wa kina kuhusu Wizara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. Pamoja na kuunga mkono hoja hii naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kwa jitihada na mkakati mzuri wa kulipa madeni. Hii imesaidia sana kujenga na kuipa heshima nchi yetu na kuaminiwa na nchi na mashirika wanaokukopesha. Nashauri Serikali iendelee kulipa madeni. Je, madeni yaliyobaki ni Shilingi ngapi Serikali/nchi yetu inadaiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kuna sheria zinazosimamia matumizi ya fedha na manunuzi, (*The Public Finance Act*), Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa (*The Local Government Finance Act*,) *Financial Memorandum* na Sheria za Manunuzi (*The Public Procurement Act*) ushauri wangu kwa Serikali ni kwamba Wizara, Idara, Taasisi za Serikali, Mikoa na Serikali za Mitaa, wote wazingatie sheria za fedha ili kudhibiti matumizi ya fedha za umma. Je, ni watumishi wangapi wamechukuliwa hatua za kisheria kwa matumizi mabaya ya fedha za umma (Serikali na Serikali za Mitaa)?

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha utaratibu wa malipo ya pensheni ili kupunguza ufumbufuli kwa wastaafuli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa *TRA* wanafanya kazi nzuri sana ya kukusanya mapato: Je, Serikali imeweka mpango gani wa kuboresha mazingira ya kufanya kazi watumishi wa *TRA*? Je, Serikali imetenga fedha kiasi gani mwaka 2010/2011 ili kukamilisha jengo la *TRA* Mpwapwa ambalo ujenzi umeanza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

MHE. LOLESTIA J. M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Fedha na Uchumi kwa hotuba nzuri ambayo imezungumzia maeneo muhimu yanayogusa namna ya kuboresha uchumi wetu. Pia ninawapongeza Naibu Mawaziri pamoja na watumishi wote wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi bado zipo changamoto kubwa hasa katika utekelezaji wa Mkukuta katika maeneo ya vijijini. Hatuna nyenzo za kupambana na umaskini na mikopo haipatikani katika maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Wizara iweke utaratibu maalumu wa namna ya kufikisha mikopo vijijini. Mara nyingi mikopo inayotolewa na Mifuko ya Serikali mfano Mfuko wa J. K. wanaonufaika ni wananchi walioko mjini. Ili kuinua hali ya uchumi vijijini, ni vyema basi wananchi wapewe kipaumbele. Mikopo itawasaidia kuboresha kilimo, uchimbaji wa madini, uvuvi pamoja na biashara ndogo ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ukosefu wa huduma za benki vijijini. Ninaomba katika mwaka wa fedha 2010/2011 ifunguliwe benki hasa katika Makao Makuu ya Jimbo ambayo ni Katoro. Ukosefu wa benki unasababisha kushamiri kwa uhalifu katika eneo la Katoro. Mji huu umepanuka kibiashara na kwa kuwa na benki, itavutia wawekezaji wengi watakaowekeza katika mji huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni madai ya bima. Watumishi wengi wa Serikali hasa walimu wamelalamikia sana Shirika la Bima. Kumekuwa na usumbufu mkubwa wa malipo kwa wale ambao bima zao zimeiva. Ninaomba Serikali iangalie namna itakavyoweza kulipa madai hayo ya watumishi ili nao waweze kunufaika na fedha zao katika kuboresha uchumi wao. Hii ni kero kubwa sana kwa wananchi wa Jimbo la Busanda. Kila mahali nilipokutana na watumishi wa Serikali kero yao kubwa ilikuwa ni hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana Wizara iangalie namna ya kunisaidia katika mambo matatu niliyotaja hapo juu. Mikopo vijijini, Benki zifunguliwe vijijini hasa Katoro na Madai ya bima kwa watumishi yalipwe mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. BERNADETA K. MUSHASHU: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri wa Fedha na Uchumi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwanza kwa maandalizi mazuri ya hotuba ya bajeti; pili, kwa mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi hihi. Kweli kuna mambo mengi ya kujivunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepitisha bajeti hii, ili shughuli mbalimbali ikiwemo miradi ya maendeleo kuweza kutekelezwa. Uzoefu unaonesha baada ya bajeti, kupitishwa mwezi wa saba, fedha huchelewa kutoka hadi Septemba/Oktoba. Hivyo, miradi iliyopangwa na Wizara/Halmashauri/Mikoa, kutekelezwa katika *quarter* hii ya kwanza huchelewa kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine za Tanzania tangu Desemba hadi Januari, na kipindi cha Machi – Mei ni kipindi cha mvua. Hivyo utengenezaji wa miradi kama ya barabara hususua sababu ya mvua. Kipindi kizuri hasa cha utengenezaji wa barabara katika maeneo hayo ni kipindi cha jua/kiangazi ambacho ni Juni – Septemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii vile vile husababisha fedha nyingi zaidi kutolewa katika *quarter* ya mwisho wa mwaka na kusababisha miradi kushindwa kukamilika na Wizara/ Mikoa/Halmashuri kubaki na bakaa kubwa wakati wa kufunga mahesabu. Je, kwa nini hazina inachelewesha kutoa fedha?

Pili, napendekeza Bunge la bajeti lifanyike kati ya Aprili na Juni, ili ifikapo tarlehe 1 Julai, sheria na kanuni za mgawanyo wote wa bajeti unakuwepo, kusudi fedha ziweze kutoka tangu tarehe 1 Julai ya kila mwaka, kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania kama nchi nyingi, imeathirika na msukosuko wa kiuchumi. Serikali ya CCM kwa jinsi inaavyowajali Watanzania iliamua kutoa fedha nyingi. Kwa ajili ya kunusuru uchumi wa nchi usiyumbe. Serikali na Rais mwenyewe aliahidi kuwa wale wanunuzi wa kahawa, sababu ya bei katika soko la dunia kuanguka, Mkoani Kagera vyama vya ushirika na makampuni ya watu binafsi walipata hasara kwa sababu walinunua kahawa kwa bei kubwa na kuuza kwa bei ndogo. Serikali iliahidi kuwalapia madeni ya benki na kuwafidia kwa hasara walizopata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Je, kwa nini mashirika ya watu binafsi na baadhi ya vyama vya ushirika pamoja na kuwa walipeleka maombi yao, wengi hata kujibiwa hawakujibiwa na wengine wengi hawakupata fedha hizi ambazo ni ahadi ya Rais? Je, ni lini watalipwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja na nawaombea Mheshimiwa Mustafa Mkulo na Mheshimiwa Yusuf Omari Yusuf, nawapongeza kwa kazi nzuri kubwa mliyoikamilisha wakati mko madarakani. Mnao uwezo mkubwa, tunaomba Mwenyezi Mungu awajalie na wapiga kura wenu wawapigie kura nyingi za ushindi, kusudi myaendeleze hayo mazuri mliyoyaanza.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninaomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara na taasisi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu kuchangia kwa mtindo wa kuuliza maswali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa benki zote zimesongana katika Jiji la Dar es Salaam, likifuatiliwa na Arusha, ikifuatiwa na Mwanza: Je, Serikali haioni kuwa dhamira yao sio kusaidia wananchi bali ni kuvuna tu? Ni lini basi Serikali italeta Bungeni Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Fedha ya kuweka ukomo wa idadi ya matawi ya benki moja katika Mikoa hiyo mikubwa? Ninapendekeza hilo ili benki hizo ziweze kusambaa mikoa yote, ikifuatiliwa na Wilaya, *then* Tarafa Tanzania nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa maelezo ya mabenki mengi hutoza riba kubwa kutokana na wateja kukosa uaminifu wakati wa kurejesha mikopo na hivyo kusababisha hasara kwenye benki husika: Je, ni kwa nini mikopo ya wafanyakazi ambao marejesho hayana utata isipunguziwe riba ikapishana na asilimia mbili na *interest* ya *deposit*, yaani *loan interest rate 2% above deposit interest rate*?

Kwa kuwa Serikali imedhamiria kufufua Shirika la Bima la Taifa – *NIC*: Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kueleza Bunge hili kwa uhakika kabisa ni lini zoezi hilo litakamilika? Eneo hili limekuwa na shida kubwa na zile ofisi nzuri za *NIC* sasa zimekuwa kama mahame. Vijana wetu wanaomaliza *IFM* kwenye fani ya *Insurance* wanazubaa mitaani bila ajira yoyote.

Kwa kuwa Chuo cha *IFM* kinapanuka kwa kasi sana, ni lini sasa tutaelezwa mipango mahususi ya chuo kile kuhamishwa pale katikati ya mji kwa kozi za muda mrefu na kubakiza kozi za muda mfupi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Benki ya Wanawake itafungua matawi Mikoani?

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia nafasi hii kumpongeza Waziri kwa kutimiza ahadi iliyotolewa na Waziri Mkuu ya kuongeza bajeti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni nane kama nilivyoomba kama Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali. Jambo hili linaonesha jinsi gani Serikali inafanya jitihada ya kuheshimu sheria zinazotungwa na Bunge. Aidha, fedha hizi zitampa CAG kufanya kazi yake vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia nafasi hii kusisitiza umuhimu wa *Internal Auditor*. Sheria imepitishwa na Bunge lakini bila kumwezesha huyu kifedha hataweza kufikia malengo yaliyotarajiwa na Bunge kwa kutunga sheria. Pamoja na kusisitiza umuhimu wa ofisi hii na zaidi ikiwa mpya baada ya kutungwa kwa sheria, bajeti ya mwaka huu imepunguza kutoka shilingi milioni 303.7 (2009) na sasa shilingi milioni 268.62. Bajeti hii haioneshi ofisi hii itakuwa na mtandao kutoka Halmashauri hadi Wizara ya Fedha. Namwomba Mheshimiwa Waziri aeleze ni vipi ofisi hii itafanya kazi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ofisi ya *Treasury Registrar* pia imeianzishwa kisheria, lakini bajeti yake imeshuka sana kutoka shilingi milioni 64.9 mwaka jana hadi shilingi milioni 45 mwaka huu. Bajeti hii inaonesha Wizara haijaona umuhimu wa ofisi hii. Ukweli ni kwamba Serikali inawekeza sasa katika miradi na makampuni mbalimbali, nyingine zikiwa ndiyo msingi wa uchumi wetu kama vile uwekezaji katika nishati. Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge lako Tukufu ni vipi ofisi hii itafanya kazi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nawapongeza sana Waziri na Manaibu wote pamoja na wafanyakazi wote wakiongozwa na Katibu Mkuu kwa kufanya kazi vizuri na hesabu za Wizara zinazidi kuonesha matokeo mazuri ya ukaguzi. Udhaifu ni *vote* ya deni la Taifa.

MHE. CHARLES N. MWERA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuchangia machache kwenye hotuba hi muhimu. Pili, napenda kumpongeza Waziri, Manaibu Waziri pamoja na Watendaji kwa kazi nzuri ya kuletea wananchi maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza *TRA* kwa makusanyo ya kodi nchini kwa kiwango kinachoridhisha. Nawaomba waongeze juhudhi zaidi na hayo makusanyo ya kodi yapangwe vizuri kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja kwa Serikali kuwa na mkakati na maandalizi mazuri kwa ajili ya kuwalipia karo wanafunzi wote wa Shule za Sekondari. Nchi za Kenya, Uganda na Burundi, elimu ya msingi na sekondari ni bure. Wakati tunapata uhuru katika awamu ya kwanza chini ya uongozi wa Mwalimu Julius Nyerere, elimu ilikuwa bure. Kama kweli uchumi umeimarika ni kwa nini elimu isiwe ya bure? Tuna raslimali ya kutosha, sioni ni kwa nini Mtanzania asipate elimu. Kielimu Tanzania tupo nyuma ukilinganisha na nchi za jirani kama vile Kenya, Uganda, Burundi pamoja na

kwamba nchi hizo kuwa juu kielimu wao wamekuwa tayari kugharimia karo wanafunzi wake wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kuingia ubia katika uchimbaji wa madini hapa nchini. Serikali itapata faida kubwa kama itakuwa na ubia na makampuni ya nje katika shughuli za uchimbaji wa madini. Mfano, kama Serikali ingekuwa na ubia na Barrick, nchi ingepata faida kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi wanapomaliza utumishi, Serikali walipwe mapema stahili zao mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda nifahamu ni lini Waheshimiwa Madiwani watalipwa maslahi yao? Madiwani ni watu muhimu sana katika kuleta maendeleo katika maeneo yao ya Kata. Naomba wakati wa majumuisho nipate majibu ni lini hao watu watalipwa haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii.

MHE. VUAI ABDALLA KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakupongeza wewe, Spika, Naibu Spika na Mwenyeviti mwenzako kwa kusimamia Bunge na kuliongoza vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa makusudi naipongeza Wizara ya Fedha na Uchumi hasa Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake pamoja na Watendaji wa Wizara kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali katika kazi zake basi, iwe macho kusimamia uchumi wa nchi yetu, pia utumike uzalendo kwa maslahi ya nchi pamoja na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi kwa niaba ya wananchi wa Magogoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. JUMA H. KILLIMBAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Mustapha Mkullo - Waziri wa Fedha na Uchumi, niwapongeze Mheshimiwa Omary Yusuph Mzee na Mheshimiwa Jeremiah Sumari, kadhalika nitoe pongezi kwa Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii. Wizara hii ndiyo roho ya Serikali katika kutekeleza majukumu yake, ndipo kunaweza kuifanya Serikali kwenda mbele katika hatua za kimaendeleo. Umahiri wa Wizara hii unahitajika sana katika kukusanya mapato ya nchi katika kazi hiyo. Naomba juhudi ziongezwe hasa kubaini vyanzo mbalimbali ambavyo vitaleta mapato ya kutosha na kufanya shughuli za maendeleo. Naomba Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na *TRA* kutambua vyanzo vingine vya mapato vitakavyoongeza mapato ya Serikali, kwa mfano maeneo ya utalii, maeneo ya uwekezaji, maeneo ya kilimo, maeneo ya mawasiliano na kadhalika mbinu ziongezwe katika kukusanya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mianya ya kukwepa kodi idhibitiwe na adhabu zinazostahili zitolewe kwa wanaokwepa kodi. Maeneo kama ya mafuta, mfano mizuri mafuta ya taa na mafuta ya *diesel* na *petrol*, tofauti ya kodi kuwa kubwa imesababisha vitendo vya kihalifu (kuchakachua) na utofauti wa kiwango kikubwa cha kodi kinaliletea Taifa hasara na aibu machoni mwa Mataifa jirani. Vitendo hivi ni vya kuhujumu nchi kwa kukwepa kodi na uharibifu wa mitambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tozo kwenye matumizi ya bararaba ni kitu muhimu sana. Matumizi ya barabara bila tozo linalitea hasara Taifa. Naomba marekebisho yafanyike ili kuongeza mapato ya Taifa kwa uwingu wa magari tuliyonavyo, tusibaki na kodi ya mwaka (*Road licence*). Peke yake, bali matumizi ya kila siku hayaendani na kodi hiyo ya mwaka. Uimarishaji wa makusanyo maeneo ya bandari, ili kutumia vizuri soko la Burundi, Rwanda, na *Eastern Congo (DRC)* Reli iimarishe na bandari ya nchi kavu (*Dry Port*) kwa eneo la Dar es Salaam na eneo la Kahama kutarahisisha utunzji wa mawese na hivyo kuongeza ufanisi katika kukusanya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. BENSON M. MPESYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kutamka fika kuwa naunga mkono hotuba ya Waziri wa Fedha na Uchumi. Pia napenda kutumia fursa hii kumpongeza Waziri na Manaibu wake wote wawili kwa kazi nzuri wanayofanya katika Taifa letu. Nawatachia kheri kwa kazi nzuri ya ujenzi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na shukrani hizi, naomba nielekeze kilio changu kwa niaba ya Halmashauri ya Jiji la Mbeya. Tulipata maafa ya kuunguliwa na soko maarufu la Mwanjelwa, na kupoteza fedha nyingi na mali nyingi katika janga hilo, na bahati mbaya Serikali kuititia kitengo cha maafa, hakuna msaada wa aina yoyote ambao wananchi hawa wa Mbeya wameupata toka Serikalini. Kilio chetu ni juu ya *import duty/VAT- exemption on capital/deemed capital goods*. Tunajenga soko jipyaa kwa mkopo toka *CRDB*, takriban shilingi bilioni 14 na mradi huu tumeanzisha rasmi Tanzania *investment Centre* na kupata *Certificate of Incentives*. Ni kwa nini Serikali haitaki kutupa msamaha wa kodi kama makampuni/wawekezaji wa kutoka nje ya nchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali itoe upendeleo maalumu kwa Halmashauri ya Jiji la Mbeya.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Fedha na Uchumi Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Naibu Mawaziri Mheshimiwa Omari Yussuf Mzee na Mheshimiwa Jeremiah Sumari, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote walioshiriki katika kuandaa Bajeti hii nzuri ambayo imejielekeza kuboresha huduma katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitoe pole sana kwa Mheshimiwa Jeremiah Sumari, Naibu Waziri na Mbunge kwa kusumbuliwa na maradhi kwa muda mrefu sana. Ninamuombea Mwenyezi Mungu amponye ili arudi kuwatumikia wapigakura wake na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua uwezo wa Waziri Mheshimwa Mustafa Mkulo na Naibu Mawaziri wote wawili, hivyo nawaombea afya na wapigakura wao wawapigie kura za kutosha ili warudi kuendeleza gurudumu la maendeleo kupitia Bajeti waliyoandaa pamoja na miradi ya maendeleeo kwenye majimbo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma ya malipo ya pensheni. Napenda kuipongeza sana Serikali kwa huduma yake nzuri katika malipo ya pensheni. Kwa kweli malipo haya yanapatikana kwa muda mfupi sana kwani wastaafu sasa wanaletewa mikoani fedha zao na taratibu zote zinakamilika mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mkaguzi na Mdhhibit wa Fedha za Serikali (*CAG*) kujitegemea, napenda kuishukuru Serikali kwa kujenga Ofisi ya Mdhhibit na Mkaguzi wa Fedha za Serikali Singida. Ni ukweli usiofichika kuwa mchango wa *CAG* Ndugu Ludovick Utouh katika sekta hii ni mkubwa sana, kwani fedha hizi za ujenzi wa jengo zuri na la kisasa Singida alitafuta yeze kwa wahisani. Ninamuombea Mungu aendelee kumtia nguvu, afya, ari ya kazi pamoja na tabia yake ya kushirikisha watendaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali sasa imsaidie kutafuta fedha kwa kutenga kupitia Bajeti ya Serikali au kwa wahisani ili mikoa yote iwe na huduma hii kwa maana ya kujenga ofisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma ya *TRA*, naomba huduma ya *TRA* kwa upande wa ushuru wa kuingiza magari na mizigo nchini iboreshwe, bado kuna ukiritimba au usumbufu mkubwa. Vilevile pato linalokusanya na *TRA* linaweza kuongezeka wakijipanga upya kupitia vyanzo vyao na kutazama vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vyanzo vya mapato kuachiwa Halmashauri, napenda kuiomba Serikali kuwa viro vyanzo ambayo viko chini ya Halmashauri lakini leseni zake zinatolewa Wizara ya Fedha, mfano leseni za kufunga mitambo ya Televisheni na kadhalika. Naomba vyanzo vya aina hii viachiwe Halmashauri ili kukuza pato la Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu udhamini wa Serikali katika *tender* wanapewa Mashirika ya Umma. Napongeza Serikali kwa uamuzi wake wa busara wa kuyapa *tender* Mashirika ya Serikali mfano *NSSF*, *PSPF*, *PPF* na kadhalika. Hii imesaidia sana Serikali kukamilisha miradi mikubwa ilioainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005 hadi 2010 mfano ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (*UDOM*).

Naiomba Serikali kutoa hati ya dhamana kwa Mashirika haya ili Mashirika haya yasipate matatizo ya kifedha kwani fedha hizo ni za wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu malipo ya pensheni kuongezeka, napenda kuiomba Serikali kuwa viwango vya malipo ya pensheni bado ni vidogo sana kulingana na hali halisi ya maisha naiomba Serikali kuongeza viwango hivyo ili wastaafu wengi waweze kumudu hali ya maisha ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kurudia kuipongeza Bajeti hii na kutamka kwa moyo mkunjufu kuwa ninaunga mkono hoja hii.

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani kwa fursa ya kuchangia hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Fedha na Uchumi. Naipongeza Wizara chini ya uongozi thabiti wa Mheshimiwa Mustafa Mkulo na Naibu Mawaziri wake, Makatibu Wakuu wake na Maafisa Waandamizi wote kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa kusimamia vyema uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutambua mchango mkubwa wa Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Uchumi katika kuwawezesha wananchi katika masuala ya ujasiriamali na kushiriki katika uchumi wa nchi yao kwa njia mbalimbali ikihusisha mafunzo na mtaji. Lakini napenda kupata maelezo juu ya jinsi gani Wizara inaweza kuhakikisha kuwa huduma za mikopo ya mitaji ya biashara na hususani katika uchumi wa vijijini kwa maana ya kilimo, ufugaji wa wanyama, ndege na samaki zitatolewa kwa uhakika zaidi badala ya kutegemea miradi ya mara moja moja kama huduma za *NGO* na Mashirika ya nje ambayo hayakidhi mahitaji ya mikopo hii kwa wananchi wengi haswa wanawake na vijana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali haioni kuwa umefika wakati sasa wa kutoa vivutio kwa mabenki yote kuwa na dirisha la kutoa huduma hiyo. Uganda, *South Africa* na nchi kama India, Indonesia na Marekani Kusini wameweza kuwa na mipango inayounganisha huduma za benki na wazalishaji vijijni kwa kutoa huduma za kibenki ambazo ni rafiki kwa wazalishaji hao na vilevile inaingizia faida kubwa kwa benki hizi wakati zikiwaondolea wananchi umaskini kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kuwa kuna benki ambazo zipo kwa ajili ya wazalishaji na wajasiriamali wadogo lakini bado mfumo wake ni rasmi mno na ni chache sana kukidhi mahitaji ya walengwa wote nchini. Aidha, napenda kutoa rai kwa Serikali kuanzisha mfumo wa mafunzo ya ujasiriamali kwa umma ambao unaweza kuingizwa katika mitaala ya mafunzo mashulen hadi Chuo Kikuu. Aidha, kuwe na mfumo wa masomo ya jioni ya ujasiriamali katika ngazi za kata ambako Serikali inaweza kuchangia majengo na sekta binafsi ikaendesha mafunzo hayo kwa gharama nafuu ili wananchi kwa ujumla wafaidike na kuweza kumudu ushindani wa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kilimo Kwanza, bado Wizara haijaweka wazi fungu maalum litakaloiwesha hii dhana ya Kilimo Kwanza kutekelezwa. Wizara nyingi husika zimekuwa zikieleza kuwa kuna fungu maalum katika Wizara ya fedha kwa ajili hiyo, je, fedha hii iko katika fungu lipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *TRA*, pamoja na umuhimu wa Idara hii na majukumu iliyօ nayo je, kuna sababu yoyote ya kimsingi ya kuitengea Bajeti kubwa sana *TRA* ikilinganishwa na Idara nyingine zote chini ya Wizara ilhali *TRA* bado ni Idara inayolalamikiwa sana kwa rushwa? Na vilevile ukusanywaji wa kodi bado haijaboreshwa kwa kupanua wigo wa vyanzo vingine vya mapato?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Bajeti ya Matumizi, bado Bajeti ya Matumizi ya Kawaida ni kubwa sana kulinganisha na ile ya maendeleo, hakuna uwiano kati ya gharama kubwa kwenye matumizi na ukuaji wa uchumi wake. Jitihada zipi zitafanywa kupunguza matumizi ya Serikali hususani katika kutoa *benefits* zisizo za lazima kwa Maafisa wa Serikali wakiwemo Mawaziri kwenye magari, *allowance* na ruzuku ngapi nyinginezo wanazopata. Kuna ufujaji mwingi wa muda katika kutenda kazi, hii ni gharama kubwa kwa Taifa. Serikali ibadilishe utendaji kazi wake ili ufanane na ule wa sekta binafsi ili kuongeza tija na kupunguza gharama ili pesa nyingi zaidi ziende kwenye maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *JK Funds*. Tungependa kupata tathmini ya kina juu ya pesa hizi ili kuona kama mfumo uliotumiwa kutoa mikopo ulikuwa bora kuliko mingine na walengwa walinufaika na kubadilisha maisha yao kutokana na mikopo hiyo. Pendekazo langu ni kutumia taasisi za Kata kuhakikisha watu wengi zaidi hasa vijijini wanafikiwa na ndipo benki ziingie kutoa mikopo yenye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, katika ununuzi wa magari na vifaa mbalimbali vyat Serikali (*Common Use Items*) kuna haja gani ya kutumia mawakala badala ya kuagiza kwa watengenezaji moja kwa moja? Ili kuondoa muda na gharama? Ahsante na naunga mkono hoja.

MHE. JANETH M. MASSABURI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Mawaziri wake na Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu, watendaji wote walioandaa hotuba hii.

Naomba mfuko wa uwezeshaji wananchi Kiuchumi (*JK Fund*) iangalie uwezekano wa kuongeza kiwango cha mikopo katika Mkoa wa Dar es Salaam, ikizingatiwa kuwa Mkoa wa Dar es Salaam una idadi kubwa ya wakazi ambaeo wengi wao ni maskini wanajishughulisha na biashara ndogo ndogo na wengi wao ni wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, wastaifu wako katika hali mbaya pensheni ya shilingi 50,144/= kwa mwezi sawa na shilingi 1620/= kwa siku ni kidogo sana katika kupambana na kupanda kwa gharama za maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuondolewa kwa pensheni hiyo tangu mwaka 2004 hadi leo kumeleta mkanganyiko mkubwa wa kutojua haki zao wastaifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufanuzi juu ya *GN 89* ya mwaka 2006 ambayo niligusia katika Bajeti iliyopita ya mwaka 2009/2010 ambayo inaonekana sasa inatekelezwa. Naomba sana basi wakati wa majumuisho utoe maelezo yanayohusu kadhia hiyo kwa wastaifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema katika malipo yanayoendelea malimbikizo yaliyolipwa ya *GN* 89 ifahamike wazi hayaendani sambamba na viwango vyao ambapo Serikali ni vyema ikaangalia utoaji wa malimbikizo (*arrears*) za wastaifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imebainika wakati wastaifu wanapangiwa na Serikali haki yao ya mafao, kuna mapunjo ikitolewa sababu ya kukokotoa. Ripoti za *CAG* za miaka tofauti zimebainisha mapungufu hayo katika majadala yaliyokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali sasa iunde Tume ya Uchunguzi wa Pensheni itakayowahuishwa Kamati Maalum ya Wastaifu kurekebisha utata wa pensheni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana ufute kilio cha wastaifu wa *JWTZ* juu ya haki zao zinazostahili na kupatikana kwa haki zao zinazostahili.

Kuhusu upotevu wa fedha, wizi, ubadhifuru wa ujisadi, Serikali ilituambia hapa Bungeni tarehe 31 Januari, 2008 upotevu wa fedha na mali, ujisadi, ubadhilifu kuanzia mwaka 2001/2006 ni shilingi billioni nne na milioni 403 na miaka ya 2007 upotevu wa shilingi billioni 2.3, mwaka 2008 shilingi bilioni 3.5 na mwaka 2009 upotevu ni shilingi bilioni 3.2 hizi ni fedha nyingi kama taarifa ya *CAG* inavyoonesha, je, Serikali ina mkakati gani wa kukabiliana na ujisadi, ubadhilifu na wizi na hatua zipi zimechukuliwa kwa waliohusika na kadhia hiyo.

MHE. PAUL P. KIMTI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nitumie nafasi hii ya awali kumponegeza Mheshimiwa Waziri Mustafa Mkulo, Naibu Mawaziri wake wote wawili, Katibu Mkuu na watumishi wake wote kwa maandalizi mazuri ya hoja hii muhimu. Naunga hoja mkono kwa kuwa Waziri katika hali ngumu ya uchumi ameweza kuhimili mawimbi ya uchumi wa kutufikisha salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo ambayo ningeomba Mheshimiwa Waziri anisaidie kupata maelezo ili njue hatma ya mambo yanayonitatiza katika masuala kadhaa. Tatizo la kwanza ni kasi ya mfumuko wa bei na kupungua kwa thamani ya fedha yetu dhidi ya dola, je, ni kweli *BOT* imeshindwa kudhibiti kasi hii na nini mpango wa dharura katika kupunguza athari zake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la watu wabaya hapa nchini ambao wanaanza kukwatua noti za shilingi 1,000 eneo linalong'aa kwa rangi ya fedha na kuiondoa kwa madhumuni yao yasiyoelewaka. Naomba Benki Kuu ifanye uchunguzi wa kina kama kweli kuna madini au dawa fulani ambayo labda wameingundua ili kupunguza athari za uharibifu wa noti zetu hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine naomba nirudie ombi langu kwa Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Chakula kuhusu tani 25,000 za mahindi ambazo hazijaondolewa ili kupisha mahindi mapya ya msimu huu kununuliwa, suala hili ni nyeti wakati huu wa uchaguzi. Tusizue upya malalamiko wakati huu, tuanze mapema kuondoa mahindi maghalani mjini Sumbawanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi nzuri anayoifanya Mkaguzi Mkuu wa Serikali itaweza kusimamiwa vizuri zaidi kwa kuimarisha kitengo cha ukaguzi wa ndani kwa kila Halmashauri za Wilaya, Miji na Manispaa zote nchini. Katika hali ya kuzidi kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za wananchi wetu. Kazi nzuri ya Ndugu yangu Mkaguzi Mkuu Ludovick Utouh haiwezi kuzaaa matunda bila pia kuanza kuadhibu moja kwa moja wale wote wanaokiuka maadili ya kazi zao. *CAG* apewe kila aina ya uwezo wa kisheria, kiutendaji, kiusalama na kimaslahi ili heshima ya taasisi hii muhimu ianze kuogopwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri angesaidia kama atatuelezea kwa ufupi, jitihada zinazofanywa katika suala zima la kupunguza kasi ya ongezeko la watu dhidi ya kasi ndogo ya kukua kwa uchumi. Suala hili halina mjadala, lazima tulipatie ufumbuzi kwa gharama yoyote, la sivyo azma yetu ya kuondoa umaskini itafifia na kuchukua miaka mingei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sheria ya *PPP* ikipitishwa, kwa kiasi gani sisi kama nchi yetu tumejiandaa tuitumie kwa maeneo gani? Naunga mkono hoja hii na kumtakia Waziri na Naibu Mawaziri wake heri nyingi.

MHE. JUMA A. NJWAYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, Naibu Mawaziri wake na Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu kwa kazi za kila siku za Wizara yao na kujitahidi kuzikabili vyema. Aidha, nichukue nafasi kuwapongeza tena kwa kusimamia uchumi wa nchi yetu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri yafuatayo, mosi, baadhi ya watendaji wa Wizara hii ni warasimu wa mambo kupita kiasi. Hali hii imechangia miradi mingi ya maendeleo kuchelewa bila sababu za msingi kama vile mradi wa umeme wa gesi ya *Mnazibay* Mtwara. Aidha, kurudishwa kwa fedha zinazotolewa na wahisani ni dalili tosha kuwa kuna urasimu wa kutekeleza miradi. Ushauri hapa ni kubadilika kwa haraka kwa watendaji wetu. Tuache ubaguzi wa maeneo. Upo ushahidi kuwa baadhi ya maeneo miradi yake hucheleweshwa kuliko miradi ya maeneo mengine. Nchi hii ni moja na hakuna haja ya urasimu au ubaguzi wa aina yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, mkoani Mtwara kuna tawi la Chuo cha Uhasibu Tanzania ambacho kinatumia majengo ya Sabasaba na ahadi ya Serikali kupitia Waziri wa Fedha na Uchumi Mheshimiwa Mustafa Mkullo katika Bajeti ya mwaka jana 2009/2010 ilikuwa Chuo hicho kingejengewa majengo kwenye kiwanja chake nini utekelezaji wa ahadi hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu natoa rai kwa Wizara hii kutengeneza mikakati itakayofanya Benki ya *Twiga Bancorp Ltd.* kuwa Benki kamili.

Nne, wahitimu wa Chuo cha Takwimu (*EASTC*) kwa ngazi ya *Diploma* huanzia mwaka wa pili wanapoanza Shahada kwa Chuo Kikuu cha Makerere, Uganda. Lakini hapa kwetu ni lazima kuanzia mwaka wa kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri Serikali kusaidia wahitimu wote wa *Diploma* ya Chuo hicho kupewa nafasi vyuoni hapa nchini kwa kuanzia mwaka wa pili kama Uganda kwani kama wenzetu wa nchi za nje wanawatathimini hivyo, kwa nini basi wenye we tunsi jangalie na kujitathmini? Mwisho naunga mkono hoja.

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake wote wawili napenda kuunga mkono hoja kwa asilimi amia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Serikali juu ya mkopo wa mfuko wa JK na AK uweze kuwafikia walengwa vijijini zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaonekana mkopo huu unawafaidisha zaidi watu wa mjini kuliko vijijini kwa vijana na wanawake wajasiriamali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya ushauri huu naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. MWADINI ABBAS JECHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama inavyotajwa katika Sheria iliyoanzisha Mamlaka ya Mapato Tanzania jukumu lake kuu ni ukusanyaji wa mapato ya Serikali, kudhibiti uvujaji wa mapato ya Serikali, kuziba mianya ya ukwepaji kodi na kadhalika. Katika hatua za utekelezaji *TRA* inafanya ukaguzi wa mizigo katika sehemu mbalimbali hasa katika viwanja vya ndege, Bandarini na sehemu za mipakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo nyuma kulikuwa na malalamiko ya Wafanyabiashara mbalimbali kwamba utaratibu wa ukaguzi wa mizigo yao hasa bandarini pamoja na watendaji wengine *TRA* wanahusika katika kuchelewesha mizigo kutoka bandarini. Ili kutatua tatizo hilo *TRA* wamewagawa wafanyabiashara katika makundi maalum. Kuna wale wanaopitisha mizigo yao kwa mfumo wa *green belt* ambao mizigo yao haikaguliwi kwa sababu hawa ni walipa kodi wakubwa na wale wanaopitisha kwa mfumo wa *Red Belt* ambao ni lazima mizigo yao ikaguliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wananchi mbalimbali kwamba wafanyabiashara wasio waaminifu wanaingiza bidhaa zisizo na ubora unaostahili na bidhaa feki. Baadhi yake zinaelekezwa kwa *TRA* kuruhusu wafanyabiashara wakubwa kuitisha mizigo yao bila kukaguliwa. Hali hii inawanyima fursa watendaji wa *Tanzania Bureau of Standards (TBS)* kufanya wajibu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TBS* ndio wenyewe wajibu na mamlaka ya kukagua ubora wa bidhaa zinazoingia nchini. Ili kazi yao iwe ya ufanisi zaidi hapana budi kwa *TRA* kushirikiana na *TBS* kuhakikisha kwamba hakuna mizigo ya mfanyabiashara ye yole inapitishwa bandarini, uwanja wa ndege au sehemu yoyote bila kukaguliwa ubora wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Msajili wa Hazina ambayo ndiyo yenyeye mamlaka ya kusimamia Mashirika na Taasisi za Umma ikiwa ni pamoja na kurekebisha muundo wake ili iwe na mamlaka zaidi katika kusimamia kwa karibu Mashirika na

Taasisi za Umma. Bunge nalo kwa upande wake limeunda Kamati Maalum ya Kudumu ya Bunge yenye kushughulikia Hesabu za Mashirika ya Umma na Taasisi zake (*POAC*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba *POAC* katika majukumu yake inakagua Mahesabu ya Mashirika ya Umma ambayo Serikali imewekeza asilimia mia moja hadi hamsini. Kamati hii kwa sasa haina Mamlaka ya Kikanuni kukagua Mahesabu ya Mashirika ya Umma ambayo Serikali imewekeza chini ya asilimia hamsini. Hii ni kasoro kubwa kwani fedha ya Serikali ni fedha ya wananchi popote ilipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuishauri Serikali kuwasiliana na Ofisi ya Bunge ili kuiwezesha Kamati ya *POAC* kuwa na Mamlaka ya kufanya ukaguzi wa Mashirika ya Umma ambayo Serikali imewekeza hisa zake chini ya asilimia hamsini. Ni ukweli usiofichika kwa Kamati ya *POAC* imekuwa ni msaada mkubwa kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Msajili wa Hazina inafanyiwa maboresho kadhaa ili iweze kutenda wajibu wake kwa ufanisi zaidi.

Naiomba Serikali ichukue hatua za makusudi kuhakikisha kwamba ofisi hii inapatiwa ofisi yenye nafasi ya kutosha, vifaa na zana mbalimbali za kufanya kazi pamoja na mafunzo kwa watendaji. Aidha, watendaji wa kutosha wapatiwe maboresho ya mishahara na marupurupu ya watendaji yapewe kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelekezo, mapendekezo na ushauri unaotolewa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni lazima yazingatiwe ipasavyo na hatua madhubuti zichukuliwe na taasisi husika ili kudhibiti upotevu na matumizi mabaya ya fedha za Serikali. Ofisi hii inafanya kazi kubwa na hivyo hapana budi ipewe mashirikiano ya kutosha.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kupunguza matumizi makubwa ya Serikali, nashauri *strongly* Serikali kuitia Wizara ya Fedha kupunguza gharama za matumizi ya Serikali zisizokuwa za lazima. Mfano, tuache kabisa kununua/kutumia magari ya kifahari, hii ni nchi maskini, tuishi kama nchi inayoendelea. Mikogo ya maafisa wa Serikali kuishi maisha ya kusadikika katika nchi maskini ni dhambi kubwa. Fedha nyingi zaidi zielekezwe vijijini walipo wananchi wengi asilimia 85.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili kuhusu matumizi ya magari na mitambo ya Serikali baada ya kazi za ofisi. Serikali kuitia Wizara ya Fedha, isimamie kikamilifu matumizi holela ya magari ya Serikali baada ya saa za kazi. Maofisa wa Serikali wote wamekopesha magari waamriwe kuyatumia baada ya kazi. Iwe ni mwiko magari ya Serikali kuzurura nayo ovyo siku za *weekend* na usiku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ni safari za maofisa wa Serikali nje ya nchi zipunguzwe na safari ziwe zile tu ambazo zina manufaa kwa Taifa letu. Safari za mambo ya jumla jumla tu ziepukwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu juhudhi za Serikali kujenga barabara, miradi ya umeme na kuimarsha reli ya kati kwa sababu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Kikwete anaweka nguvu kubwa katika kujenga miundombinu hiyo, Wizara ipunguze matumizi yasiyo ya lazima ili pesa nyingi ielekezwe kujenga sekta hizo. Barabara, umeme na reli ya kati vitasaidia sana kuibua vyanzo vipyaa ya kodi. Juhudi za Mheshimiwa Rais ni za msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kodi za magari mfumo wa sasa urekebishwe kwa magari yanayofufuliwa. Taasisi zisizokuwa za Kiserikali (*NGO's*) na Taasisi za Dini zimekuwa kwa muda mrefu zikilalamikiwa utaratibu wa sasa wa kulipia kodi za magari wanasema. Hata kama gari lilikuwa bora kabisa kwa miaka mitano, siku ukiifufua unalazimika/kulazimishwa na *TRA* kulipia miaka yote ya uhai wa gari bila kujali miaka ambayo gari hilo lilikuwa juu ya mawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi hawa wanashauri na mimi nakubaliana nao kwamba ni kwa nini mfumo wa kulipia Bima usifuatwe maana wakati wote gari hulazimika kuwa na bima hai inapokuwa barabarani, tuondoe adha hii. Gari ikafufuliwa kodi iende sambamba na utaratibu wa leseni yake na bima yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu kwa walipakodi, kitengo hiki kimefanya kazi nzuri sana, juhudhi hizi ziendelezwe na kwa mkoa wa Kigoma na hasa Wilaya ya Kasulu, elimu hii inahitajika sana sasa. Wafanyabiashara waliopo mpakani na hasa wale wa Kigoma, Kasulu na Kibondo na ukizingatia kwamba sasa kuna soko la pamoja la *EAC* hoja hii inakuwa ya msingi sana. *TRA* njooni kutoa elimu ya kodi mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu riba za benki. Serikali kupitia Wizara hii iendelee kuangalia kwa kushirikiana na Benki Kuu kupunguza riba zinazotozwa kwa waweka akiba, wafanyabiashara na wajasiriamali na wananchi riba zipo juu sana na matokeo yake vyombo vya fedha sasa ni kwa ajili ya tabaka la watu wachache. Hii ni hatari sana kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mfuko wa Uwezeshaji Kitaifa. Mfuko huu haujafika Kigoma na hususani Kasulu, tafadhali fikeni Kasulu sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwa maandishi. Kwanza kabisa napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Fedha na Uchumi kwa hotuba yake nzuri iliyoandalisha kwa umakini kabisa na pia napenda kuipongeza Wizara kwa jitihada zake za kuimarisha uchumi na mapato ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali imeonesha mikakati mingi inayolenga kuboresha maisha ya Mtanzania, napenda nizungumzie maeneo machache ambayo ni kero kwa wananchi wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ni suala la kutokutendewa haki kwa wastaafu walio wengi ambapo baadhi yao hupunjwa mafao na wengine kutokulipwa kabisa kwa kisingizio kwamba muda wao wa kustaafuli ulikwishapita. Kweli hii si haki kwani ni matumaini yangu kwamba muda wa kustaafuli unapofika mwajiri huwa anamwandikia Mtumishi kwamba muda wake umefika. Nashangaa kuona/kusikia mtumishi anaachwa aendelee na kazi na kisha kumnyima mafao yake. Naomba Waziri atoe ufafanuzi juu ya suala hili kwani wananchi wanalamika ya kwamba Serikali imewazulumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kuhusu mfumuko wa bei ya bidhaa mbalimbali hasa mafuta ya mashine na magari. Mfumuko huu kimsingi unachangia kwa kiasi kikubwa ugumu wa maisha licha ya ukuaji wa uchumi tulio nao. Waathirika wakubwa wa tatizo hili ni ile asilimia 80 ya wananchi waishio vijijini. Ushauri wangu kwa Serikali ni kwamba Serikali sasa itoe kipaumbele zaidi kwa maendeleo vijijini kwa mfano mikopo na uwezeshaji wa kiuchumi uelekezwe zaidi vijijini kwa kutumia mawakala ili kuongeza ajira na kupunguza ugumu wa maisha. Miundombinu ya barabara iboreshwe ambapo athari za mfumuko wa bei zitapungua. Vilevile kasi ya upelekaji huduma za maji, umeme na afya iongezwe kwani hizi zitaongeza muda wa wananchi kushiriki vizuri katika shughuli za uzalishaji na kukuza uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie sasa huduma za kibenki ambazo kwa siku za hivi karibuni zinaonekana kuelemewa kwa kiasi kikubwa. Kumekuwa na msongamano mkubwa wa wateja katika mabenki yetu yote katika madirisha na hata kwenye *ATM*. Mabenki yashauriwe kuongeza matawi yake. Lakini hata hivyo *ATM* zimekuwa na matatizo ya kupoteza mtandao, kupungukiwa fedha na kuharibika ovyo. Matatizo yote haya yanaleta kero kubwa ya kupoteza muda wa wateja wa kufanya kazi kutokana na kutangatanga kutoka benki moja hadi nyingine na *ATM* moja hadi nyingine ili kupata huduma hii haraka. Tafadhali Serikali iijitahidi kulifanyia kazi suala hili kwani hizi si zama za kutunza fedha nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho napenda kuipongeza Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kazi nzuri inayofanya ya ukusanyaji mzuri wa mapato kwani mapato ya Taifa letu yameongezeka kwa kiasi kikubwa. Tatizo nililoliona au changamoto inayowakabili ni ile ya wafanyabiashara kutokutoa risiti. Hivi karibuni nimeona katika vyombo vya habari *TRA* ikihamasisha utumiaji wa mashine za utoaji wa risiti. Hili ni suala zuri sana lakini jambo la msingi ni kuhakikisha kwamba wateja wote wanapatiwa risiti baada ya kununua bidhaa kwani inashangaza kuona unapoomba risiti hasa kwenye vituo vya mafuta unajibiwa kwamba ungesema mapema. Hii inaonesha kwamba wafanyabiashara hawajui kama wana wajibu wa kutoa risiti. Hivyo ni muhimu elimu itolewe zaidi kwa wateja na wafanyabiashara wakielezwa faida za kutoa risiti na hasara za kutotoa risiti. Suala hili nimelizungumza mara nyingi, sasa lizingatiwe ahsante. Naunga mkono hoja.

MHE. FATMA ABDULHABIB FEREJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja hii kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Tume ya Pamoja ya Fedha, inasikitisha kuona kwamba tangu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kukabidhiwa ripoti kuhusu vigezo vya kugawana mapato na kuchangia gharama za Muungano, mwezi Agosti, 2006 leo hii ni miaka karibu minne Serikali hizi mbili zimeshindwa kutoa kauli ambayo wananchi wanaisubiri kwa hamu katika kupunguza malalamiko kuhusu Mapato na Matumizi ya shughuli za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri atueleze ni kitu gani kinachosababisha Serikali ya Muungano kuchukua muda wa miaka minne kutoa maamuzi kuhusu mapendekezo hayo? Wananchi wa Tanzania wanabaki kuiona Tume ya Pamoja ya Fedha kama chombo kisichokuwa na faida kwao, bali kipo kwa ajili ya kupoteza fedha za umma. Naomba Waziri atueleze ni lini Serikali itatoa tamko kuhusiana na ripoti hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matumizi ya dola za Kimarekani ndani ya nchi. Pamoja na Serikali kutoa msimamo kwamba matumizi ya dola za Kimarekani hayaruhusiwi hapa nchini, lakini inaonyesha Serikali inashindwa kusimamia maamuzi yake. Hadi leo hii baadhi ya maduka ndani ya nchi hasa maduka yanayouza vifaa vya *computer*, yanatoa *invoice* kwa wateja kwa kutumia viwango vya dola za Kimarekani na sio fedha za Tanzania. Je, kodi inayokusanywa kwenye maduka hayo inakusanywa kwa fedha za kigeni kama dola za Kimarekani? Kwa nini wenyewe gari za *Taxi* uwanja wa ndege, Dar es Salaam wanaandika bei za nauli kwa dola za Kimarekani? Ni lazima wageni wakiingia tu nchini waweze kubadilisha fedha za kigeni na waanze kutumia za Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri atueleze ana mkakati gani wa kudhibiti matumizi ya fedha za kigeni ndani ya nchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uwezeshaji wananchi kiuchumi, kutokana na takwimu alizotoa Mheshimiwa Waziri, fedha kutoka kwa *JK Fund*, ni wanawake wachache sana ukilinganisha na wanaume waliofaidika na mikopo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri atueleze kwa nini suala la jinsia halikuzingatiwa? Naomba kuwasilisha.

MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na wataalam wote wa Wizara kwa hotuba yao nzuri na yenye ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja iliyotolewa na Wizara hii ningependa kuchangia kwa kuiomba Wizara inipatie ufanuzi juu ya mambo makubwa mawili muhimu ambayo kwangu binafsi nyaona kama ni masuala hatarishi kama tu hayatapatiwa ufumbuzi wa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ambalo ningemwomba Mheshimiwa Waziri alitolee ufanuzi ni hili suala ambalo limekuwa hatarishi kwa mifuko yetu ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa ni dhahili kwamba mifuko hii yote iliyopo hapa nchini (*PPF, PSPF, NSSF* na kadhalika) bado haijawafikia wananchi ipasavyo. Asilimia kubwa ya wananchi bado haichangii katika mifuko hii, lakini hata katika asilimia hiyo ndogo ya wananchi wanaochangia katika mifuko hiyo bado kuna msuguano mkubwa baina ya mifuko kwa mifuko juu ya namna mfuko mmoja unavyoweza kupata wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya mifuko imetumia silaha ya *formular* ya namna mwanachama atakavyoweza kujipatia mafao makubwa dhidi ya mifuko mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *formular* inayotumika katika kujipatia mafao hutofautiana kati ya mfuko mmoja na mfuko mwingine. Ni dhahiri kwamba ipo mifuko inayotumia *formular* tofauti kulipa mafao makubwa kuliko kiasi halisi cha mshahara anachochangia mwananchama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili si tu linaleta msuguano baina ya wanachama na mifuko (hasa ile ambayo inatumia *formular* ambayo inalipa mafao sambamba na kiwango kinachoendana na mshahara wa mwanachama anaochangia, bali pia haileti tija yoyote ile kwa mifuko hii kwa maana ya kwamba uendelevu wa mifuko hii/*sustainability* ipo hatarini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri atueleze ni kwa nini Wizara yake imekaa kimya na haioni umuhimu wa kuja na *formular* moja (*constant formular*) kwa ajili ya mifuko yote ya hifadhi ya jamii ili kuondoa hii kero ya mifuko kushindana kwa *formular* ya mafao kwa kuitumia kama silaha ya kuiba/kuhamisha wanachama toka mfuko mmoja kwenda mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kama *formular* itakayotumika kupanga mafao itakuwa moja/sawa kwa mifuko yote basi ni ukweli usiopingika kwamba mifuko hii itajitaua/*spread* kwa maana ya kuongeza wanachama wengi zaidi kuliko sasa ambapo ime-concentrate katika kuibiana wanachama kwa kutumia utofauti huo wa *formular* itumikayo katika kutoa mafao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ningemwomba Mheshimiwa Waziri atupatie ufanuzi wa suala la *regulator* kwa ajili ya mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *regulator* ni muhimu sana kwa mifuko hii, lakini ni muda mrefu limeongelewa lakini hadi leo mifuko hii haina *regulator* jambo ambalo ni hatari sana kwa nchi na mifuko yenye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri atueleze ni kwa nini Serikali imekaa kimya juu ya kumpata *regulator* atakayesimamia masuala yote yahusuyo mifuko

hii. Tunafahamu nafasi ilitangazwa na watu waliomba hiyo nafasi sasa ni nini kimekwamisha zoezi hilo la kumpata mtu huyo muhimu kwa faida ya mifuko yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naomba kuwasilisha.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa na mimi ninataka niwashukuru wale wote ambao wameniwezesha kuwepo hapa kwa kipindi cha miaka hii mitano, kuanzia Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, wapigakura wangu, lakini pia na mke wangu na watoto wangu. Nawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme tu kwamba hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezitoa ni nyingi, nitajaribu kumsaidia Mheshimiwa Waziri wangu, lakini vilevile Mheshimiwa Waziri na ye ye atazitolea ufanuzi baadhi. Lakini pale ambapo tutakuwa hatujaweza kukamilisha, basi tutazitoa kwa maandishi na kila Mheshimiwa Mbunge atawezza kupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nianze kwa kusema kwamba jukumu kubwa la Wizara ya Fedha ni kutafuta fedha. Hilo ndilo jukumu lake la msingi na ni kubwa. Lakini ni lazima tufahamu hizi pesa au fedha zinatafutwa kwa kuangalia hali nzima au mtandao mzima wa kuimarisha uchumi. Hili nalo kwa mustakabali wa Wizara ilivyoundwa, ni jukumu la pili la Wizara ya Fedha. Kwa hiyo, pale ambapo Waheshimiwa Wabunge, walikuwa wanajadili kwa kina kwamba tuongeze juhud za kutafuta mapato, nataka niwaambie ni wajibu wenu kusema hivyo na sisi tutafanya kazi hiyo kama Wizara ya Fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge, jukumu hilo tumeshalianza. Kwanza, tumeangalia zile kodi ambazo tumeziweka, ni kwa kiasi gani tunazi-exhaust? Ni kwa kiasi gani tunakusanya? Ni kwa kiasi gani tunaziba mianya?

Waheshimiwa Wabunge, nataka niwaambie ni kwamba tunafanya juhud hiyo. Kwa kutoa mfano tu, hivi karibuni kama hamjaanza kuziona, mtaona mashine kwa kila mlipakodi ambaye amekuwa VAT Register. Kwa sababu tumegundua kwamba kuna baadhi ya wafabnyabiashara unapotaka kwenda kununua kitu wanakuuliza; ukitaka risiti ni bei hii, ukitaka bila risiti ni bei hii. Pale mapato mengi sana yanapotea. Kwa hiyo, tumeona kwamba tuanze kukamata pale. Lakini vile vile baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia kuhusu habari ya kufanyia mapitio ile orodha yetu ya misamaha au maeneo ambayo tunatoa misamaha ili kuweza kuhakikisha kwamba katika maeneo hayo, basi tutoe misamaha kwa maeneo ambayo ni muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge, kwamba hiyo kazi tumeshaianza na tutakazia zaidi ili tutoe misamaha kwa yale maeneo ambayo yana tija kwa watu na nchi yetu ili fedha itakayopatikana iweze kurudi tena na kutusaidia katika maendeleo yetu. Baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, vile vile wameelezea suala zima la *absortion capacity*. Nataka niseme tu kwamba, hilo tunaanza kuliangalia sasa hivi, ni sababu zipi hasa za msingi zinazotufanya sisi kama Serikali

tusiweze kuzitumia kwa kiwango cha asilimia 100 fedha za misaada tunazopewa? Inawezekana pengine Sheria yetu ya *Procurement* inachukua muda mrefu, hilo nalo tunalifanyia kazi ili tuweze kupunguza huo utaratibu wa *procurement*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninataka niseme kwamba juhudzi zetu za kuongeza uzalishaji, ndizo ambazo zitaweza kutusaidia katika kuongeza mapato. Lakini vile vile haya mapato yatakayopatikana, juhudzi zetu za *ku-plough back* katika *development* ndio itakayoweza kuzalisha zaidi. Kwa hiyo, mimi ninakubaliana na wale Waheshimiwa Wabunge, waliosema kuwa ujenzi wa reli, ujenzi wa barabara, ujenzi wa bandari na hizo juhudzi Serikali tutazichukua ili kuhakikisha kwamba faida inapatikana na matokeo yake yanaweza kuonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja za wastaaafu. Kulikuwa kuna hoja ambayo Waheshimiwa Wabunge wamesema *pension* ya Sh. 51,000/= kwa mstaafu kwa mwezi ni kidogo. Mimi ninataka niseme ni kweli, lakini Serikali inachukua juhudzi. Tumetoka hivi juzi tu ilikuwa ni Sh. 21,000/= tumepandisha mpaka 51,000=/. Kila hali itakapokuwa nzuri, Serikali itahakikisha kwamba na wastaaafu nao wanaongezewa *pension*; kwa sababu soko wanalokwenda wastaaafu ndilo hilo hilo tunalo kwenda sisi.

Nami ninataka niseme tu kwamba sio lazima mpaka pale ambapo tutakapopandisha mishahara kwa nchi nzima, tunaweza tukawapandishia wastaaafu tu. Sisi wengine kwa sababu mishahara yetu bado ipo katika hali nzuri, tukasubiri. Kwa hiyo, hilo tutalichukulia juhudzi ili na wastaaafu nao wajisikie kwamba wako katika jamii hii hii, wasione kama wako katika jamii nydingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *pension slip*, nataka ni wahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba kuanzia mafao watakayolipa wastaaafu Julai/Desemba, *pension slip* itatoka. Tutawalipa na *pension slip* yao ili waweze kuona kila wanapoongezewa pesa waweze kuona na kima chao waweze kukiona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utunzaji wa kumbukumbu vilevile limezungumziwa kwa kina kabisa. Sasa hivi wastaaafu watakuwa na kumbukumbu nzuri. Utunzaji wa kumbukumbu hauanzi kwa mstaafu, unaanza tokea mtu anapoajiriwa. Tunaandaa utaratibu mzuri sana. Sasa hivi kila mtu anapoajiriwa kumbukumbu zake zitunzwe mpaka siku anapostaafu. Kumbukumbu zile ziwe ziko *intact* ili asiweze kupata matatizo yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja hapa kwamba, malipo ya wastaaafu yasiwe miezi sita, yawe miezi mitatu mitatu. Hii hoja nataka kusema ni sawa na *chicken and egg* kwa sababu wengine wanaangalia muda wa kulipwa. Wengine wanaangalia kile anachokipata, kwa miezi mitatu kinakuwa ni kidogo na ni bora akipate kwa muda wa miezi sita. Lakini hili nalo vile vile tunaliangalia zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja kwamba fedha za kuwakopesha wananchi, hasa wale walioko vijijini zipitie kwenye *SACCOS* badala ya kupitia katika mabenki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kwamba hivi sasa tumeshaanza utaratibu huo. Tutaongeza *SACCOS* zaidi baada ya *SACCOS* zenyewe kuzithmini na kuweza kuziona kwamba zinakopesheka na zinaweza kurudisha na watendaji wa *SACCOS* ile sio wabahirifu. Hatuwezi tukapeleka fedha kwa *SACCOS* bila ya kuangalia uwezo wa *SACCOS* hiyo na watendaji wake. Hilo tutalifanya na tunawaahidi kwamba tumeshaanza kulifanya isipokuwa tutaliendelea zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja ambayo ilihu huduma za kibenki. Kuna wengine walisema kwamba tuongeze matawi ya benki. Suala hili nimelisema sana na nitaendelea kulisema kwamba tutajaribu kuzishawishi benki hizi ziongeze matawi. Nimeeleza katika majibu yangu kwamba *NMB* katika miaka hii mitano toka mwaka 2006, wameweza kuongeza matawi 23. *CRDB* wameweza kuongeza matawi 25, tutazishawishi na benki nyingine ili ziweze kuongeza matawi zaidi. Lakini vile vile tutawaomba wenzetu hawa wasiwe wana urasimu katika kutoa huduma kama ilivyolezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja ya malipo ya Bima. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba mchakato mzima sasa hivi umeshakamilika na kilichobakia ni kuandaa tu taratibu za kuanza kuwalipa wale wenzetu ambao Bima zao zimeiva.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kwa upande wangu nataka nieleze kuhusu habari ya matumizi. Serikali tayari imejipanga vizuri sana kudhibiti matumizi yaliyokuwa sio ya lazima. Kwa upande wa magari, tayari sasa hivi wameshaandaa orodha ya kuweza kuona kwamba ni magari gani yatumiwe na kada gani. Tutaya-*order* haya magari kwa pamoja na *directly* tuta-*order* kwa *manufacturer* badala ya *ku-order* kupitia kwa hawa mawakala. Hapo tunataka kuondoa huu urasimu wa kupoteza pesa. Lakini vile vile badala ya kwamba kila taasisi inunue vifaa vyake, tunataka kufanya kwa ujumla sasa ili kuwe na utaratibu kama ni *stationaries*, tununue kwa ujumla halafu tunazipeleka kule zinakotakiwa ziende. Hii nayo kwa kweli itatusaidia kupunguza matumizi na gharama za Seriikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile hapa kulikuwa kuna hoja ya Halmashauri kusimamiwa. Nataka niseme, kwa sababu tumeamua kupeleka fedha nyingi sana kwenye Halmashauri zetu, Halmashauri hizi tutazisimamia kwa karibu zaidi ili ziweze kutumia fedha zilivyopangiwa na Bunge hili. Vinginevyo hatua ni lazima zichukuliwe na ninadhani mmeshaona Mheshimiwa Waziri Mkuu, ameshaanza kuzitembelea hizi Halmashauri na kuchukua hatua kwa watendaji ambao wanakiuka taratibu za manunu, wanakiuka taratibu za matumizi, ili hatimaye sura nzima ya Serikali katika matumizi ionekane kwamba ni nzuri. Tukifanya hili, tutampunguzia kazi CAG; atakuwa na kazi nyepesi kuliko hata ikawa sisi tunazipeleka pesa halafu hatuzisimamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimalizie kwa kumshukuru sana Mssemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani ambaye ni kaka yangu. Hotuba yake aliyoitoa leo, kwa kweli imenifariji sana. Lakini ninataka tu nimwambie kwamba kama ana mapenzi ya kukaa

huku na sisi tukae huku, mapenzi hayo namwomba asahau kwanza. Ahsante sana.
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda nikushukuru wewe kwa kuongoza vyema mjadala wa Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka 2010/2011. Naomba nieleze kuwa maoni, ushauri na maelekezo yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, Kambi ya Upinzani na Waheshimiwa Wabunge, yatasaidia sana katika utekelezajhi wa bajeti ya mwaka huu wa fedha. Nawashukuruni wote. Pamoja na shukrani hizo, zipo baadhi ya hoja zilizotolewa na Kamati, Upinzani na Waheshimiwa Wabunge, ambazo ni muhimu nikazitolea maelezo ili tuweze kwenda pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba yangu imechangiwa na jumla ya Waheshimiwa Wabunge 11 pamoja na Maseneta wawili waliochangia kwa kuzungumza. Napenda kuwatambua Waheshimiwa Wabunge waliochangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda - Mbunge wa Handeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed - Mbunge wa Wawi (Pemba) na Msemaji wa Kambi ya Upinzani lakini vilevile Waziri Kivuli wa Wizara ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba – Mbunge wa Kigoma Mjini, Mheshimiwa Devota Likokola - Mbunge wa Viti Maalum Ruvuma, Mheshimiwa Esther Kabadi Nyawazwa – Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Anna Richard Lupembe – Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga – Mbunge wa Tabora Mjini. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Juma Ngasongwa – Mbunge wa Ulanga Magharibi, Mheshimiwa Felister Aloyce Bura – Mbunge wa Viti Maalum Dodoma, Mheshimiwa Mohamed Amour Chomboh – Mbunge wa Magomeni Zanzibar, Mheshimiwa Emmanuel Jumanne Luhahula – Mbunge wa Bukombe, Mheshimiwa Seneta Juma N'hunga ambaye anastaafu, Mheshimiwa Seneta Paul Kimiti, ambaye naye katangaza nia ya kustaafu na Mheshimiwa Omar Yusuf Mzee - Naibu Waziri wa Fedha na Uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge 25 wamechangia kwa maandishi, naomba nao niwatambue kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo – Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Janet Zebadayo Mbene - Mbunge wa Kuteuliwa, Mheshimiwa Janeth Masaburi – Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim – Mbunge wa Mtambile, Mheshimiwa Paul Peter Kimiti – Mbunge wa Sumbawanga Mjini, Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo – Mbunge wa Tandahimba, Mheshimiwa Pindi Chana – Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Faida Bakar – Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha – Mbunge wa Wete Pemba, Mheshimiwa Daniel Nicodemas Nsanzugwanko – Mbunge wa Kasulu Mashariki, Mheshimiwa Anastazia James Wambura – Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji - Baraza la

Wawakilishi na Mheshimiwa Rosemary Kasimbi Kirigini – Mbunge wa Viti Maalum.
(*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Dr. Harrison George Mwakyembe – Mbunge wa Kyela, Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi – Mbunge wa Mbozi Mashariki, Mheshimiwa Florence Essa Kyendesya – Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Estherina Julio Kilasi – Mbunge wa Mbarali, Mheshimiwa George Malima Lubeleje - Mbunge wa Mpwapwa, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba – Mbunge wa Busanda, Mheshimiwa Bernadeta Kasabago Mushashu - Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Shally Josepha Raymond – Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa John Momose Cheyo – Mbunge wa Bariadi Mashariki, Mheshimiwa Charles Nyanguru Mwera - Mbunge wa Tarime, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis – Mbunge wa Magogoni, Mheshimiwa Juma Killimbah – Mbunge wa Iramba Magharibi na Mheshimiwa Benson Mpesya – Mbunge wa Mbeya Mjini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna wengine tumewasahau naomba tukumbushwe tutawatambua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu baadhi ya hoja za Wabunge kama ifuatavyo:- Kuhusu hoja za Kamati ya Uchumi na Fedha Mwenyekiti ametoa mapendekezo na ushauri ya maeneo mengi. Nachukua nafasi hii kumshukuru yeye na Kamati yake kwa ushauri na mapendekezo walijotupa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema kwamba tumekuwa tukipata mapendekezo mazuri kutoka Kamati hii, tumeyajibu hapo awali, lakini vilevile pia ningependa nijibu kama ifuatavyo:-

Hoja moja ilikuwa ni kwamba Serikali iangalie upya eneo la matumizi katika uchumi ambayo ni makubwa na hasa yale ya nje ya bajeti. Aidha, Wizara ifanyi kazi kwa kushirikiana pamoja na nyingine hasa katika kudhibiti upotevu wa mapato. Vilevile Kamati imeshauri kwamba taratibu za utekelezaji wa MKURABITA ziharakishwe, pamoja na kwamba Serikali inasimamia kikamilifu tatizo la kupunguza gharama za uanzishaji biashara nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kwamba Serikali imepokea ushauri wa Kamati na kwamba utaufanya kazi katika mwaka huu wa fedha ili kukidhi mahitaji. Serikali imeshachukua hatua mbalimbali za kudhibiti matumizi yake kama nilivyoeleza katika hotuba ya Serikali mwezi Juni mwaka huu. Aidha, hatua za kuongeza mapato na kupunguza misamaha ya kodi pia nilizieleza katika hotuba ya bajeti ya Serikali. Napenda kuihakikishia Kamati kwamba Serikali itatekeleza kikamilifu hatua zote nilizozieleza katika bajeti ya Serikali lengo likiwa ni kuongeza wigo wa mapato na kusimamia na kukidhi ili kuwa na bajeti endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Kambi ya Upinzani, hoja zimetolewa nyingi katika maeneo mbalimbali kwa baadhi ya hoja hizo kama ifuatavyo:- Serikali iwaeleze Watanzania ambao ndio walipakodi, ni utaratibu gani Serikali inatumia

kufuatilia kama kweli udhamini walioutoa kwa makampuni yanayotoa udhamini wa fedha hizo zinarudishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naeleza kwamba kwa vile utaratibu wa dhamana unatolewa kufuatana na sheria na utaratibu, Serikali inaendelea kusimamia sheria zilizopo na kila mara taarifa sahihi zitatolewa. Majibu ya hoja za ukaguzi kuhusiana na dhamana ya Serikali yanaendelea kutolewa na hoja nyingi zimewasilishwa kwa Mkaguzi na Mdhhibitii Mkuu wa Serikali. Nataka pia kumhakikishia Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed kwamba tutaangalia yale yote na kasoro zote zilizojitokeza hasa pale ambapo dhamana zimezidi kiwango ambacho kimetamkwa kwenye sheria na kuhakikisha kwamba tunarekebisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilikuwa ni upungufu wa makusanyo ya mapato. Kambi ya Upinzani inapenda kupata ufanuzi wa namna gani *TRA* itaweza kukabiliana na upungufu huu wa mwaka jana na mwaka huu wa 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu kwamba katika mwaka 2010/2011 mkakati mkuu wa makusanyo ya kodi ni pamoja na uimarishaji wa utawala wa kodi na uboreshaji wa mfumo wa makusanyo wa mapato ya ndani. Mikakati itakayochukuliwa katika utekelezaji wa mpango huu wa tatu 2008/2009 hadi 2012/2013 katika mwaka wa fedha 2010/2011 ni pamoja na haya yafuatayo:-

Kuanza utekelezaji wa matumizi ya *register* ya *ki-electronic* za kutambua mauzo ya *electronic physical devices* kuboresha utaratibu wa kusimamia kodi kwa msingi wa vitabu vya walipakodi, yaani *block margin system*. Kuendelea kupanua wigo wa kodi kwa kusajili walipakodi wapya kutekeleza mikakati ya ripoti ya muda unaotumika kuondoa mizigo forodhani, kuboresha usimamizi na utendaji katika idara ya forodha, kuboresha na kuimarisha mfumo wa uthamini forodhani, kuimarisha uhakiki wa ukaguzi, yaani *post clearance audit*, kuimarisha matumizi ya kompyuta, kuimarisha usimamizi wa bidhaa zinazopita hapa nchini kusimamia utaratibu wa kutoa misamaha ya kodi, kuboresha ukaguzi wa kodi, kuimarisha ubora wa ukaguzi kuendelea na juhudzi za kuingiza kwenye wigo wa kodi shughuli zilizopo kwenye sekta isiyo rasmi kushirikiana na Serikali ili kuiwezesha mamlaka za mapato kunufaika na matumizi ya mfumo wa taarifa za kijiografia na vitambulisho vya Taifa, kuendelea kuimarisha mifumo yote ya ukusanyaji mapato, kuendelea na usimamiaji wa karibu na uwajibikaji na uhadilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumjulisha Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed kwamba hivi karibuni tulitembelewa na Rais Dulah wa Brazil, katika mazungumzo yake na Mheshimiwa Rais Kikwete alitueleza mbinu mbalimbali ambazo Brazil ilizitumia kupanua wigo wa mapato. Nataka nimhakikishie kwamba nakusudia kupeleka ujumbe Brazil ili kwenda kujifunza nini walichokifanya wenzetu ili huko baadaye na *ishallah*, ikiwa sote tutarudi humu Bungeni Novemba, basi tutakuja kukwambia kwamba tumejifunza nini Brazil.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ushauri wa kupunguza misamaha ya kodi, amesema yeye kwamba bado hajatekelezwa ipasavyo. Serikali imeendelea na mkakati wa kupunguza misamaha ya kodi ili kuongeza mapato na bila kuathiri uwekezaji nchini. Aidha, Serikali kwa kuitia Wizara ya Fedha na Uchumi imeendelea kupoteza kupokea mapendekezo kutoka kwa wadau mbalimbali ikiwa ni mapendekezo ya *TRA* jinsi ya kupunguza misamaha ya kodi. Hadi kufikia mwaka 2010/2011 mapendekezo ya kupunguza misamaha ya kodi yanayotekelawa na Serikali ni pamoja na haya yafuatayo:-

- (i) Kufuta misamaha ya kodi kwenye magari yanayozidi miaka kumi tangu kutengenezwa;
- (ii) Kupunguza misamaha ya VAT, kwa kupunguza vipengele kwenye *second and third schedules*;
- (iii) Kufuta *notes* zote za Serikali ambazo zilikuwa zinatoa misamaha ya kodi kwa taasisi mbalimbali; na
- (iv) Kuanzishwa kwa utaratibu wa *treasury vouchers* kwa watumishi wa Serikali na taasisi zisizo za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hizi zimesaidia kupunguza misamaha ya kodi kutoka asilimia tatu ya pato la Taifa na kufikia chini ya asilimia mbili kwa mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hoja zilizotolewa na Kamati na Kambi ya Upinzani, baadhi ya Wabunge pia walichangia hoja zao kwa kuzungumza pia kwa maandishi. Baadhi ya hoja hizo ni kusimamia matumizi ya Serikali, kusimamia manunuzi ya umma, Tume ya Pamoja ya Fedha, usimamizi wa pensheni, kudhibiti biashara, utoaji wa fedha za maendeleo, mfuko wa pensheni kutokuwa *sustainable*, urasimu katika benki ya biashara, benki ya *TIB* kuwa na kiwango kikubwa cha *advance*, Serikali inachukua ushauri huu na itaendelea kuufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumtambua Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki ambaye pia alichangia kwa kuongea. Ushauri mwingine ulikuwa ni kupunguza misamaha ya kodi kwamba bado haujatekelezwa ipasavyo. Jibu tunasema, Serikali imeendelea na mkakati wa kupunguza misamaha ya kodi ili kuongeza mapato bila kuathiri uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyininge ya Kambi ya Upinzani, ni kwanini *TRA* inawapa uwakala wa ukadiriaji wa thamani ya bidhaa bandarini *TISCAN* badala ya Bodi ya Mapato ya Zanzibar. Napenda kujibu kwamba *input duties* ni kodi ya Muungano ambayo hukusanya na *TRA* kama ilivyoainishwa kwenye Katiba. Zanzibar *Revenue Board* hukusanya kodi zisizo za Muungano Zanzibar. *TISCAN* kwa mkataba utakaoisha Desemba mwaka huu iwasaide *TRA* kukadiria kodi ya mapato, inawasaidia kukadiria

kodi ya mapato, *input duty* kwa bidhaa zinazoingia nchini. Baada ya mkataba wa *TISCAN* kwisha *TRA* itachukua jukumu hilo yenyewe.

Hoja nyingine ilihu kwa nini hadi sasa Serikali haijatekeleza suala la kufanya manunuzi ya umma kwa njia ya mtandao, yaani e'*procurement*? Napenda kujibu kwamba Serikali kupitia Mamlaka ya Ununuzi wa Umma, *PPRA* imeandaa mpango mkakati wa kutekeleza mfumo wa ununuzi kwa njia ya mtandao baada ya kukamilika kwa upembuzi yakinifu. Mpango Mkakati huo utaanza kutekelezwa katika mwaka huu wa fedha wa 2010/2011. Kama nilivyosema awali, kama tutarejea humu Bungeni, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed utakuja kuona kwamba mfumo huu umeanza kutekelezwa.

Hoja nyingine ilikuwa, ni lini uamuzi kuhusu mapendekezo ya kugawana mapato na kuchangia gharama za Muungano yaliyotolewa na Tume ya pamoja ya fedha utafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza katika hoja ya bajeti ya Serikali ya mwaka 2010/2011 ni kuwa Serikali mbili, yaani Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi inakamilisha uchambuzi wao wa taarifa ya Tume ya kugawana mapato na kuchangia gharama za Muungano. Hatua inayofuata ni kwa pande mbili kwa Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi kujadili mapendekezo hayo ili kufikia makubaliano kuwa na msimamo wa pamoja kuhusu mapendekezo hayo.

Kwa hali hiyo, utaratibu unatarajiwa kukamilika katika mwaka huu wa fedha. Nataka nikujulishe Mheshimiwa Hamad Rashid kwamba kwa kweli kiwango kimekubalika kati ya pande hizi mbili, kilichobaki tu ni kwamba wenzetu wa Zanzibar walishapitisha kwenye Baraza lao la Mapinduzi sisi hapa nadhani tutapitisha kati ya kesho na Alhamisi. Kwa hiyo, baada ya hapo ile Kamati ya Muungano ya kero za Muungano inayoratibiwa na Mheshimiwa Makamu wa Rais, Waziri Mkuu kwa upande *SMT* na Waziri Kiongozi kwa upande wa Zanzibar itakaa na kufanya maamuzi.

Baada ya Kamati ya Mheshimiwa Makamu wa Rais kufanya maamuzi kitakachobakia ni utekelezaji. Kwa hiyo, sio tena maneno matupu, tumefika mahali ambapo uamuzi unanukia na utafanyika wakati wowote. Lakini nataka uondoke ndani ya Bunge hili ukijua kwamba kiwango gani kitakuwa kwa upande wa Zanzibar, kiwango gani kwa Serikali ya Muungano, hicho kimeshakubalika. Kwa hiyo, *rubber stamp* kwamba sasa hii ndiyo inayotakiwa kutekelezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilitolewa na Waheshimiwa Wabunge kuhusu kuboresha na kuondoa udhaifu katika ununuzi wa umma. Tunapenda kujibu kwamba uboreshaji wa ununuzi wa umma kwa lengo la kuondoa udhaifu umefanywa kwa kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuanzisha na kutekeleza mpango au taratibu wa ununuzi wa bidhaa na vifaa vitumikavyo mara kwa mara kwa pamoja na kwa lengo la kupunguza gharama za ununuzi;

(b) Kuanzisha na kutekeleza mkakati wa kupambana na rushwa katika ununuzi wa umma. *PPRA* na *TAKUKURU* zimeingia makubaliano ya kutekeleza mkakati huo;

(c) Kuendelea kutekeleza mfumo wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa sheria ya ununuzi wa umma kwa kufanya ukaguzi katika taasisi za ununuzi na kufuatilia wa utekelezaji wa hoja za ukaguzi;

(d) Kuendelea kutekeleza mkakati wa kujenga uwezo kwa wataalam wa ununuzi wa kutoa mafunzo kuhusu matumizi ya sheria ya ununuzi wa umma na kanuni zake; na

(e) Kuandaa mapendekezo ya marekebisho ya sheria ya ununuzi wa umma pamoja na kanuni zake kwa lengo la kupunguza muda wa manunuzi, kupunguza gharama na kuondoa mapungufu yaliyojitokeza katika utekelezaji wa sheria tangu kutungwa kwake mwaka 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa yako, sheria hii ilikuwa ijadiliwe hapa Bunge kesho, lakini kwa ushauri wa Kamati husika wamependekeza maeneo fulani fulani ambayo inabidi yafanyiwe kazi kwa kina zaidi na kwa hiyo, Muswada huu utawasilishwa Bungeni wakati wowote tutakapokuwa tayari. Lakini nataka kuwashakikishia kwamba kero zote ambazo zimeelezwa na Waheshimiwa Wabunge ziko na zimefanyiwa kazi katika sheria hii mpya ya manunuzi itakayoletwa wakati wowote Bunge jipya litakapoanza.

Hoja nyingine ilihuhoja ya Waheshimiwa Wabunge kuhusu kupunguza gharama za biashara. Napenda kujibu kwamba hatua mbalimbali zinachukuliwa na Serikali kurahisisha mfumo wa ulipaji kodi *TRA* ili kupunguza gharama za kufanya biashara. Hatua hizo ni pamoja na kutumia mitando ya kompyuta kuwasiliaha *return* za kodi na kufanya malipo kupitia mabenki kwa mfumo wa *TC*, *TRA* itaendelea kurahisisha *business process* za ulipaji wa kodi mwaka 2010/2011 ili kupunguza gharama za kufanya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilihuhoja Serikali kuongeza mtaji wa benki ya Twiga ili uweze kukuza benki ya biashara. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imepanga kuongeza mtaji wa Benki ya Twiga kwa kuwapatia kiasi cha shilingi bilioni mbili mwaka 2010/2011. Pamoja na kufanya hivyo, gawio linalotegemewa kwa mwaka 2009 kuwa mtaji, haya yakifanyika hoja ya Mheshimiwa Kaboyonga ya kwamba benki hii iwe na kiasi kisichopungua shiligni bilioni tano kitakuwa kwa kweli kimetekelizwa.

Hoja nyingine ilihuhoja Wabunge kuhusu Chuo cha Mipango kusimamiwa vizuri ili kuwezeshe kutoa watalaam wa kutosha. Wizara inaendelea kukijengea uwezo Chuo cha Mipango katika nyanja zote za rasilimali watu na miundombinu na hivyo kukiwezesha kuwa na mazingira bora ya kujifunzia kufundishia kwa ajili yakuandaa na kutoa wataalam wa mipango ya maendeleo ya hapa nchini. Mathalan mwaka huu jumla ya wafanyakazi 21 wenye sifa wameajiriwa. Idadi hii inafanya jumla ya wafanyakazi 160

kuwa 162. Sanjari ya hilo, Wizara itaendelea kutoa fedha kwa jengo la utawala na mabweni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kukujulisha kwamba hivi karibu nilibahatika kufungua ukumbi wa mikutano mzuri kweli kweli hapa Dodoma ambao unaweza kuweka watu kati ya 2,500 – 3,000 kwa wakati mmoja. Hiyo ni katika mojawapo ya juhudhi ambazo Serikali inafanya kukiwezesha Chuo cha Mipango Dodoma.

Hoja nyine ni kuhusu Waheshimiwa Wabunge kufuatilia kwa karibu matumizi ya fedha za umma zinazokwenda kwenye Halmashauri. Naibu Waziri alijibu lakini pia naomba kuongezea majibu yake. Marekebisho yaliyopitishwa na Bunge kwenye Sheria ya Fedha kupitia *Finance Bill Act 2010* ambayo tayari yamesharidhiwa na Mheshimiwa Rais yamewezesha Serikali kusimamia kwa karibu fedha zinazopelekwa kwenye Serikali za Mitaa. Hii imefanyika kwa kuweka mamlaka hayo kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali na Mhasibu Mkuu wa Serikali. Idara mpya ya Ukaguzi wa Ndani ambayo nayo inaanizishwa kupitia marekebisho niliyoyataja nayo yanaipa mamlaka ya usimamizi wa ukaguzi wa ndani katika Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyine ya Waheshimiwa Wabunge ni kuhusu Sera na Sheria ya Uwezeshaji ya mwaka 2004 inalipa Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kama chombo pekee cha kusimamia mambo ya uwezeshaji, lakini Serikali inakipa fedha kidogo sana hasa kwa *Mwananchi Empowerment Fund* na kwamba ni muhimu mfuko huu ukapewa fedha za kutosha. Hili lilizungumzwa kwa ufasha zaidi na Kaka yangu kutoka Ulanga Magharibi Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali inatambua umuhimu wa Baraza la Uwezeshaji na Wananchi Kiuchumi na itatenga fedha kufuatana na hali itakavyoruhusu. Mwaka 2007/2008 Serikali ilitenga shilingi milioni 400, mwaka 2009/2010 tulitenga shilingi milioni 500 na mwaka 2010/2011 zimetengwa shilingi bilioni moja kwa ajili ya *Mwananchi Empowerment Fund*. Serikali itaendelea kuongeza fedha kwa *Mwananchi Empowerment Fund* mwaka hadi mwaka ili kuongeza uwezo wa Baraza kutoa mikopo kwa walengwa. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba nimeelekeza Bodi ya *National Economic Empowerment Council* ije na mkakati madhubuti ili Serikali iweze kuongeza fedha ya uwezeshaji katika mfuko huo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kutambua mchango wa aliyekuwa bosi wangu wakati mimi nikiwa Mkurugenzi Mkuu wa *NSSF Senator Paul Kimiti*. Baada ya wewe Mheshimiwa Kimiti kuzungumza nimeteta na Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, nataka nikuhakikishie kwamba Serikali itatoa pesa za kununua mahindi yote yaliyopo Sumbawanga ili kustaafu kwako kuwe kwema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho napenda kumshukuru tena Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mzuri na kwa kuniwezesha mimi kuwa Waziri wake wa Fedha na Uchumi. Wizara ya Fedha na Uchumi ni Wizara nyeti, si Wizara lelemama na si Wizara ya kutakata, inawezekana wakati mwingine usilale usingizi kwa wiki nzima matokeo yake ukaanza kuota mchana. Nashukuru kwamba

Mheshimiwa Rais ameniona mimi nafaa na kunikabidhi madaraka haya na kama nilivyosema asubuhi ni matumani yangu kwamba sikumuangusha, wala sikuiangusha Serikali na wala sikuwaangusha Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

Napenda kumpongeza Makamu wa Rais Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein kwa kuteuliwa kuwa mgombea wa nafasi ya Urais Zanzibar kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi, uteuzi huu umedhihirisha ukomavu wake kisiasa na kwamba tuna imani ya kuibuka na ushindi wa kishindo mwezi Oktoba, 2010. Lakini kwa vile tumeshardhiana kwamba kutakuwa na kushirikiana basi CCM ikishinda kusiwe na nongwa, tukubali tu kwamba Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein awe Rais na atakayeshinda *CUF* amsaidie Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein. Nina kila matumaini kwamba Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein atashinda, naona hata shemeji yangu hataki hata kuniangalia tena lakini tutashirikiana. (*Makofi*)

Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dr. Mohamed Ghalib Bilali kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mimi nimebahatika kumfahamu Dr. Ghalib Bilali kwa karibu sana kwa sababu tuna uhusiano wa kifamilia. Ni matumaini yangu kwamba ujuzi na utaalamu alionao utaongeza nguvu sana katika safu ya uongozi ndani ya Muungano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiit, pia napenda kumshukuru Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Pinda, kwa bahati nzuri katika kipindi changu chote cha takribani miaka miwili na nusu ya Uwaziri wa Fedha nimekuwa naye karibu sana, amekuwa ni mshauri mzuri, mwelekezi na asije na hasira. Namuombe Mwenyezi Mungu amjaalie aendelee kuwa hivyo, asije kuwa na hasira tena huko baadaye. (*Makofi*)

Lakini pia napenda kuwapongeza Wajumbe wote wa Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi kwa kutimiza jukumu lao kubwa na kutuletea viongozi ambao tuna imani kwamba katika nchi ambayo sasa tumekuja na demokrasia ya vyama vingi, nina imani kwamba viongozi hawa kwa kadri tunavyowafahamu wataleta amani na utulivu ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiit, lakini mwisho kabisa, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed kwamba nina kila ndoto kwamba Chama cha Mapinduzi kitatoa Serikali mwezi Novemba, 2010 na ni matumani yangu kwamba ikiwa hivyo ndivyo kwa hiyo tutaomba Mheshimiwa aendelea kuwa Kiongozi Mkuu wa Kambi ya Upinzani na upande wetu utatoa Waziri wa Fedha na Uchumi. (*Kicheko*)

Lakini la mwisho kwa namna ya kipekee naomba kumshukuru sana Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed kwa hotuba yake ya leo, kwa kweli ilikuwa ni ya kiusuluhishi, haikuwa hotuba ambayo ni *confrontational*, imekuwa ni hotuba ambayo ina mawazo mengi ambayo yanaweza yakafanyiwa kazi, ni matumaini yangu kwamba kweli na kwa pamoa mawazo yale yote ambayo umeyatoa mengine sikuyajibu kwa sababu yalikuwa mengi na hayo ambayo nimeyajibu nadhani yanaweza yakutupeleka mbele. Ni matumaini yangu kwamba wakati wa kampeni lugha yako itakuwa ya namna hiyo hiyo ya kiusuluhishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niliwashukuru wote asubuhi, sina haja ya kurudia, bali naomba tena kukushukuru kwa kuendesha kikao hiki cha leo vizuri sana na ni matumaini yangu kwamba nimejitahidi kujibu yale yote ambayo kwa kweli yalikuwa ni ya kiujumla zaidi. Lakini yale yote ambayo sitakuwa nimeyajibu ama yatajibiwa wakati wa Kamati au tutayaleta kwenye kibango kitita ili kila mmoja aone kwamba alihoji nini na Serikali tumejibu nini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki!

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi Mheshimiwa Mustafa Mkulo kwa kupitia hoja za Waheshimiwa Wabunge na kwa kutoa hoja ambayo imeungwa mkono. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa kabla hatujasogea hatua inayofuata nitoe tangazo dogo kwa Wabunge wote kwamba Mheshimiwa Waziri wa Fedha ametawanya *addendum* ya kitabu cha pili, natumaini tumepata nakala zake. Kwa hiyo, tuzingatie marekebisho hayo wakati wa kupitisha vifungu.

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 50 - Wizara ya Fedha na Uchumi

Kifungu 1001 - *Administration and General*Sh. 9,885,474,500

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *Vote 50 programme* ya 10 *sub vote 1001*, mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini Serikali inakuwa na kigugumizi katika kutafuta vyanzo vingine vya mapato bado inang'ang'ania juu ya vinywaji vikali, pombe, sigara na kadhalika yaani vitu ambavyo vina athari kwa Watanzania? Je, itakapofikia wakati Watanzania kuacha kunywa na kuvuta Serikali itaendeshwa kwa pesa gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi Kambi ya Upinzani katika Bajeti ya mwaka 2009/2010 ilieleza vyanzo vingi tu vya mapato vitakavyoisaidia Serikali na hotuba hii ya sasa hivi Wizara vilevile kama vile imeelekeza vyanzo 13 vya mapato. Ni

kwa nini Serikali inakuwa inakwepakwepa kufuata ushauri wa bure ambao inapewa na Kambi ya Upinzani?

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoleza kwenye hotuba yangu ya Bajeti, kwanza sisi wenyewe tumesema tunatafuta vyanzo vipyta vya mapato na hivi punde nimeeleza kwamba tumepata hata ushauri mwingine wa bure kutoka kwa mtu mkubwa sana duniani, na nimesema kwamba tunapeleka ujumbe kwenda kujifunza nini wenzetu wanafanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli sikutaka kueleza pale mwanzo kwamba Rais Laurent alipoingia madarakani alikuta *tax revenue* ilikuwa 8% ya Bajeti ya Serikali lakini mwaka huu *tax revenue* imefika 37% ya Bajeti, sasa hiyo ni *miracles* ndiyo maana nikasema kwamba ni vizuri tukapeleka wataalamu kwenda kuangalia. Lakini pia Kambi ya Upinzani kama nilivyosema tuliletewa mapendelezo yenu ile siku niliposoma Bajeti, sasa hata kama yangetuwa mazuri vipi haingeweze kana siku ile Serikali ikae na ije na kubadili hiki na kile ili tuje kusema kwamba tunakubali hiki mapato yaweje.

Kama nilivyosema ni kwamba tunarudia kusema kwamba tumepokea mawazo yote mliyoyatoa, yatafayiwa kazi na yale mengine ambayo mlisyayatoa yameshaanza kufanyiwa kazi. Sasa kwa hiyo, nadhani tusubiri mwezi Novemba, 2010 na Bajeti ya mwakani tuone hali halisi itakavyokuwa lakini si kwamba Serikali inasuasua au haitaki kufanya, hapana! Serikali yenye we ina mkakati na ushauri ambayo mmetupa yote tutafanya kazi. (*Makofi*)

MHE. JUMA A. NJWAYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Uhasibu Tanzania Tawi la Mtwara imekuwa ina mazingira mabaya sana ya mahali palipo, kwanza ilikuwa tu jengo la Sabasaba lakini ilikuwa imepata kiwanja na mwaka jana hapa Mheshimiwa Waziri aliahidi kwamba baada ya marekebisho yaliyofanyika Singida ilikuwa zamu ya Mtwara. Lakini kwenye Bajeti hii sioni mahali ambapo pana makusudi maalumu ya kufanya ujenzi wa maana na wa msingi katika chuo kile cha Uhasibu Tanzania tawi la Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata *commitment* ya Waziri kwenye jambo hili.

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli na Mheshimiwa Njwayo alishaninong'oneza hata kabla ya leo. Bajeti ya mwaka huu kama unakumbuka wakati naiwasilisha tulipunguza mambo mengi sana kwa sababu nilizozieleza. Sasa nakuhakikisha tu kwamba katika Bajeti ya mwaka ujao kwani mwaka huu haiwezekani kwa sababu Bajeti ndiyo imeshapita lakini mwaka ujao tutahakikisha kwamba hilo linatekelezwa.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mimi napenda kuishukuru Serikali kwani ni muda mrefu nilikuwa nimeomba tujengewe jengo la *TRA* Wilaya ya Mpwapwa lakini kwa kuwa Serikali yetu ni siki hivi sasa jengo hili limeanza kwa hiyo naishukuru sana Serikali na Mheshimiwa Waziri nakushukuru na kwa kuwa njia ya kwenda Kilosa ya mkato ni kupitia Mpwapwa – Godegode - Lumuma na kwenda Kilosa naomba upite uone kazi nzuri inayofanyika pale ya kujenga jengo la *TRA*.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Lubeleje.

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuzipokea pongozi kwa niaba ya Serikali, lakini pia ni kweli kwamba Mheshimiwa Lubeleje tunapakana, ni jirani yangu, mimi niko Kilosa pale na yeze yuko Mpwapwa huku Bonde la Lumuma. Nataka kukuhakikishia kwamba kesho kutwa wakati tunaondoka hapa Dodoma nitapita njia hiyo kuelekea Kilosa. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Na mimi nikwambie tu mafuriko yote ya Kilosa maji yanatoka Mpwapwa na Kongwa. Mheshimiwa Godfrey Zambi!

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwenye michango yangu yote miwili ya kuandika na kuzungumza hapa Bungeni na siku za nyuma nimewahi kuiuliza Serikali imeanzisha dirisha la kilimo ndani ya *TIB* kwa ajili ya kuwakopesha wakulima, lakini nikawa naeleza wasiwaso wangu kwamba kuweka masharti ya kuwataka wakopaji kwamba lazima wapitie kwenye vyombo vingine vya fedha nadhani si sharti zuri sana. Nikasema wapo wakulima ambao wana uwezo wao mzuri, wana hati zote ambazo wanaweza kukopa bila matatizo. Lakini pia nikasema zipo benki ambazo zinafanya biashara na nikazitaja kuwa ni *NMB*, *CRDB*, *NBC* na nyinginez, hizi zinaamini mtu mmoja mmoja ili mradi awe ametimiza masharti. Kwa nini sisi tunaweka sharti hili la kumfunga mtu mpaka apitie taasisi nyingine? Waziri haoni kwamba ni wakati mwingine sasa turuhusu taratibu zote mbili kupitia vikundi lakini pia na mtu mmoja mmoja aweze kukopa?

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza lazima tukiri kwamba dirisha la kilimo katika Benki ya *TIB* ni kitu kipy, *TIB* ilikwa haijihusishi na kilimo, ni benki ambayo tangu iundwe imekuwa ikishughulikia viwanda. Sasa tumeipa kazi nyingine ya kilimo na inabidi tuwape muda wa kuweza kuja na mfumo ambao utaweza kusaidia. Sasa hayo yote ambayo yamezungumzwa tumeyasikia, tumeyapokea na tutayafanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa wakati huu ambao tunarekebisha Benki ya *TIB* ningependa kuwashauri wakulima wadogo wadogo kwamba ziko benki ambazo tayari zinatoa mikopo ya kilimo ikiwa ni pamoja na *NMB*. Kwa hiyo, tusidhani kwamba ni lazima sana twende kwenye dirisha la *TIB*. Dirisha la *TIB* lina *only 19 billion*. Tukilipelekea zile pesa nyingine sawa lakini *NMB is the most liquid bank* sasa hivi hapa nchini, wanatoa mikopo ya kilimo, *micro finance*. Kwa hiyo, ningeshauri kwamba kwa wakati huu ambapo tunajengwa *TIB* jamani twendeni kwenye zile benki nyingine ambazo

Serikali yenewe imezianzisha na imeanzisha mifumo ili tuweze kupata kule, baadaye *TIB* itakapoimarika ndiyo twende huko.

MHE. ARCHT. FUYA G. KIMBITA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii. Ni jambo dogo, ambalo rafiki yetu Mheshimiwa Waziri wa Fedha tumeshazungumza naye, nilitaka tu atuhakikishie na kutupa matumaini mazuri sisi Wabunge tunaotoka maeneo yanayolima kahawa twende na jibu lipi kuhusu lile ombi letu la Chama Kikuu cha Ushirika kule Kilimanjaro (*KNCU*) kuhusu ule mporomoko wa uchumi?

MWENYEKITI: Ni ombi gani Mheshimiwa Kimbita ili tufaidike sote?

MHE. ARCHT. FUYA G. KIMBITA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kudorora kwa uchumi wa dunia, Chama cha Ushirika Kilimanjaro (*KNCU*) ni mionganoni mwa vyama vyaa ushirika vilivyopata hasara. Sasa tumeleta maombi Serikalini, yamefanyiwa kazi na Mheshimiwa Waziri, tumeshazungumza hilo jambo. Sasa kwa sababu ndiyo tunaelekeea katika maeneo yetu, Mheshimiwa Waziri anatupa neno lipi la faraja kwamba *KNCU* watarajie kupata huo msaada kutoka Serikalini lini?

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakiri kupokea barua ya Mheshimiwa Kimbita na viongozi wa *KNCU*. Mheshimiwa anataka nimfahamishe kwamba tunalishughulikia suala lake na si yeze peke yake tu, kuna *KNCU*, *corperative* ya Kagera, kuna *corperative* ya Karagwe ambaa wote wanahuksika na haya mambo ya Kahawa. (*Makofi*)

Ninachotaka tu kueleza ni kwamba ule mfumo wa *rescue package* ambaa tulikuwa tumeuanzisha unatakiwa upitie kwenye benki yako maana yake ndiyo inajua nini kilipelekea mpaka wewe ukapata hasara. Wale wa benki yako wakiridhika, wanapeleka Benki Kuu, Gavana wa Benki Kuu akiridhika ndio wanapeleka kwa Waziri. Sasa tumepata yale maombi yake, yanashughulikiwa katika mfumo huo nilioueleza, nadhani Mheshimiwa Kimbita tunaomba usubiri tu, tutakujulisha mara tu baada uchambuzi utakapokuwa umekamilika.

MHE. CHARLES N. MWERA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Waheshimiwa Madiwani wametumikia Taifa hili karibu miaka mitano sawa na sisi Wabunge. Katika mchango wangu nilitaka nifahamu ni lini hawa Waheshimiwa Madiwani watalipwa mafao yao?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Charles Mwera ameuliza swali hili. Kama tulivyosema ni kwamba masuala yalikuwa ni mengi, lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mwera kwamba ni jana Halmashauri zote tayari tumeshawapelekea fedha ili waweze kuwalipa madiwani. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Jamani Madiwani nchi nzima mmesikia huko? Fedha imeishatumwa. (*Makofi*)

MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD: Mheshimiwa Mwenyekiti, nililotaka kuuliza limepata ufanuzi na nimeridhika nao, nasubiri kifungu 1002.

MWENYEKITI: Ahsante sana, tumalizie na Mheshimiwa Baba Askofu.

MHE. BENSON M. MPESYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kifungu hicho hicho mshahara wa Waziri, lakini sina shida nao kwa sababu ninafahamu fika kwamba wana Kilosa wanamhitaji na Taifa hili pia linamhitaji. Kusudi langu nilikuwa nataka anisaidie katika kilio tulichonacho, Halmashauri ya Jiji la Mbeya tuliunguliwa na soko kubwa maarufu linaloitwa soko la Mwanjelwa na jitihada kubwa zimefanywa na Halmashauri ya Jiji la Mbeya kukopa mkopo wa shilingi bilioni 14 ili kujenga soko la kisasa. Lakini bahati mbaya baada ya kuusajili mradi huu *Tanzania Investment Centre (TIC)* tumeomba tupewe msamaha wa ushuru wa forodha kwa ajili ya bidhaa muhimu za ujenzi, lakini mpaka sasa naona bado Serikali haitaki au haijafikiria namna ya kutusaidia Wanambeya. Ikumbukwe wazi wakati soko hili linaungua Serikali haikutoa msaada wowote na wananchi wameumia sana, wamepoteza bidhaa zao. Nilikuwa naomba kwa jicho la huruma, Kaka yangu Mustafa Mkulo ultazame hili katika mtazamo mpya, tupate msamaha, tuwajengee soko wafanyabiashara wale wadogo wadogo ili wainue uchumi wao. Ahsante. (*Makofti*)

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakiri kwamba hili pia nalifahamu. Linashughulikiwa ila nimweleze tu Mheshimiwa Mpesa kwa sababu upande mmoja Wabunge wanasema dhamana zimezidi na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed asubuhi alitueleza kuwa Sheria inasema isizidi asilimia 70, imevuka sasa iko asilimia 82.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna upande mwininge Baba Askofu anataka tumpe msamaha kule Mbeya. Tunatambua lile tatizo, mimi sijalionia lile soko tangu liungue lakini watu wangu walikwenda wakaliangalia, nataka nikuhakikishie Baba Askofu kwamba tutalizungumza na wenzangu na hasa *TRA* na baadaye ile Kamati ya Madeni na pia wenzetu wa *TIC* ili tuone jinsi gani tunaweza tukawasaidieni.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts*..... Sh. 14,644,548,000

MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD: Mheshimiwa Mwenyekiti, muda mchache uliopita Mheshimiwa Naibu Waziri, alieleza kwamba kazi kubwa ya Wizara hii ni kutafuta misaada na kufuatalilia. Lakini kifungu 221100 *Travel Out of Country* hakuna fedha hata shilingi moja, kazi hii wataifanya vipi?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli maelezo ambayo ameyaeleza Mheshimiwa Soud, lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa kwamba kifungu alichokieleza 221100

hatujakiwekea fedha lakini hizo shughuli alizozieleza fedha zake zitatoka katika kifungu cha *travel foreign*, fedha zake ziko hapo. (*Makofi*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1003 - <i>Policy and Planning</i>	Sh. 6,546,720,200
Kifungu 1004 - <i>Legal Services</i>	Sh. 621,704,100
Kifungu 1005 <i>Information Education and Communication</i>	Sh. 1,305,130,500
(<i>Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote</i>)	
Kifungu 1006 - <i>Internal Audit Unit</i>	Sh. 268,628,500

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Hiyo *internal audit unit* na kifungu kidogo *travel in country* ambacho kimepunguziwa fedha zake na ambazo zilikuwa ndogo kwanza, zilikuwa shilingi bilioni 19 na sasa ni shilingi bilioni 15. Nataka kumuuliza Waziri, juzi hapa tumepitisha sheria ya kuhakikisha kwamba tuna *internal audit* yenye nguvu ili imsaide *CAG* kutayarisha mazingira ambayo yanawezesha zisiwepo hoja nyingi. Lakini nikiona fedha kama hizi kwanza hata *title* yenye *internal audit unit* inaashiria ni kama *ka-department* kadogo sana ambako hakaendani na uzito uliowekwa ndani ya sheria.

MWENYEKITI: Mheshimiwa John Cheyo kama nia yako ni *CAG*, ye ye yuko ukurasa 231.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, *I know what I am talking about*, nazungumzia juu ya Sheria ya *Internal Audit* ambayo tuliiitunga juzi juzi hapa na ipo chini ya *Vote 50*. *CAG* atakuja *Vote 45* kwa hiyo, fedha inayoonekana hapa haileti uzito ule ambao Bunge hili lilionesha kwamba sasa wakati umefika tuimarishe hii *department* ya *Internal Audit* na itaanza chini katika Halmashauri mpaka juu kwamba itakuwa chini ya *Permanent Secretary* wa Wizara. Hii hai-reflect kabisa hali halisi, kwa hiyo, ningependa maelezo.

MWENYEKITI: Maneno ya Mheshimiwa John Cheyo yanajaribu kuzungumzia punguzo la shilingi 3,400,000 kwamba ndiyo maelezo yanayohitajika, kama nimemuelewa vizuri nafikiri niko sahihi.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE): Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie tu Mheshimiwa Cheyo kwamba hii *unit* tunayoizungumza hapa ya *Internal Audit* ni ya Wizara, siyo ile ambayo ni ya Taifa. Ile ya Taifa ina fedha za kutosha, ziko kwa *Accountant General* ile ambayo inazunguka zunguka. Hii ni kwa ajili ya Wizara tu. (*Makofi*)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu 1007 - *MCC Tanzania*..... Sh. 506,653,000
Kifungu 1008 - *Procurement Management Unit*Sh. 535,711,500
Kifungu 1009 - *Public Procurement Policy Unit (PPU)*.....Sh. 4,602,150,700
Kifungu 2003 - *Treasury Registrar*.....Sh. 45,004,242,900
Kifungu 5001 - *Government Asset Management Division*.....Sh. 6,594,629,600
Kifungu 6001 - *Financial Mgmt Information Systems Division*Sh. 1,710,099,000
Kifungu 6002 - *Tax Revenue Appeals Board*.....Sh. 822,297,500
Kifungu 6003 - *Technical Audit Unit*..... Sh. 632,218,300
Kifungu 6004 - *Tax Revenue Appeals Tribunal*.....Sh. 591,468,600

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 22 – Deni la Taifa

Kifungu 1001 - *Administration and General*.....Sh. 1,747,233,792,000

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 21 – Hazina

Kifungu 2001 - *Government Budget Division*.....Sh. 803,037,498,500

MHE. MWADINI ABAS JECHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, *vote 21, sub vote 2001* katika dhana ile ile ya kudhibiti matumizi ya Serikali fedha iliyotengwa katika kifungu kidogo cha 229900 *other operating expenses* ni burungutu kubwa mno hili. Lakini maelezo yake hayafahamiki. Ningependa kupata ufanuzi burungutu hili la fedha lililotengwa katika kifungu hiki hasa lina madhumuni gani?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha kwamba hapa tumetenga shilingi bilioni 129. Lengo la fedha hizi ni pamoja na kugharamia ushauri elekezi, vilevile pamoja na kugharamia fidia itokanayo na mikataba.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *Sub vote 2001 item 290700 contingency non-emergence* pamoja na marekebisho ambayo mmetupa kutoka shilingi bilioni 378 na sasa ni shilingi

bilioni 370 fedha hizi naona ni nyingi sijui mtatumia vipi. Inakuwaje, naomba mtupe ufanuzi zaidi ni dharura gani hiyo?

MWENYEKITI: Anazungumzia ongezeko la shilingi milioni kama 90 naomba ufanuzi Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE): Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi ni pamoja na kugharamia michango ya Serikali katika zile taasisi za Kimataifa ambazo sisi Hazina tunatakiwa kulipia.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

Kifungu 2002 – <i>Policy Analysis Division</i>	Sh. 150,350,673,000
Kifungu 2003 – <i>Treasury Registrar</i> ...	Sh. 0
Kifungu 4001 – <i>External Finance Division</i>	Sh. 6,230,667,000
Kifungu 7001 – <i>Poverty Eradication and Empowerment</i>	Sh. 2,444,023,000

(*Vifungu vilivytajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

Fungu 23 – Mhasibu Mkuu wa Serikali

Kifungu 3001 - *Public Debt Management* Sh. 534,729,800

MHE. MWADINI ABBAS JECHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naangalia *sub vote* zote zilizofuatana hapa lakini katika *sub vote* hii 3001 ukiangalia 210200 *Basic Salaries Non-pensionable* inaonekana hakuna *basic salaries* hapa. Sasa sijui kama hakuna wafanyakazi au inakuwaje naomba ufanuzi.

MWENYEKITI: Hebu rudia tena, tuko 3001.

MHE. MWADINI ABBAS JECHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, 210200. Nilikuwa naangalia katika *sub vote* nyingine zote hapa zote zimetengewa fungu la mishahara lakini hii *sub vote* pekee ambayo haikutengewa mishahara nilikuwa naomba ufanuzi.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Jecha. Lakini watumishi wote walioko katika *department* hii mishahara yao iko katika fungu 3003.

MHE. MOHAMED RAJAB SOUD: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu lilikuwa linalingana na la Mheshimiwa Jecha, nilifikiria kwamba wafanyakazi wamejitelea kufanya kazi ya kujenga Taifa. Ahsante.

MWENYEKITI: Mwaka mzima bila mshahara!

(*Kifungu kilichotwaja hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

Kifungu 3002 - *Expenditure Management* Sh. 26,119,960,000

MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa na angalizo kidogo katika kifungu hiki kwamba wakati wa mikutano na hasa ya Bunge kuna gharama kubwa sana ya wafanyakazi wa Serikali wanaoacha shughuli zao Dar es Salaam na kuja Dodoma. Lakini pamoja na hiyo gharama ya kuwasafirisha kuwaleta hapa kwa kila mmoja ni gharama kubwa sana na gharama za kujikimu ni kubwa sana. Kwa sababu tunaangalia mapinduzi ya *IT* kwa nini Serikali kupitia Wizara hii isibuni mkakati ambao utapunguza kuleta watendaji wengi Dodoma badala yake tupunguze gharama kwa ku-*invest* kwenye *IT* na kama kuna maswali wajibu wakiwemo ofisini kwao badala ya ku-*mobilize* ofisi zao na kuja hapa Dodoma.

Mimi nafikiri lengo la Serikali ni kupunguza zaidi gharama ambazo tunatumia katika kuendesha Serikali yetu. Naomba pengine Waziri atoe mwelekeo wa Wizara yake kwamba je, ni lini au anaonaje, wanaweka mkakati gani wa kupunguza gharama za uendeshaji wa Serikali kupitia njia hii?

MWENYEKITI: Mimi nilidhani sisi Wabunge ndio tunahitaji watu hawa ili watujibu mambo yetu. Kama sisi Wabunge *option* yetu ni hiyo kwamba wasije na tushughulike na *IT*, Mheshimiwa Waziri ufanuzi.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE): Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo la Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni sio bayu, ni zuri na ndiyo moja ya jitihada za Serikali katika kuhakikisha inapunguza gharama. Lakini na wewe kama ulivyosema wazo lako nalo Waheshimiwa Wabunge wanahitaji wataalamu ili kuweza kupata majibu ya masuala yao. Lakini ushauri tunaupokea na tutaufanya kazi katika kupunguza gharama za Serikali. (*Makofi*)

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Nakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti, *item 270800. Current Grant to Non Financial Public Units (General)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zimetengwa shilingi bilioni 25 na ni mwaka huu tu. Kwa nini iwe mwaka huu na tunaelekea Uchaguzi Mkuu naona kidogo nina wasiiasi hapa?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama alivyoona Mheshimiwa Masoud, nadhani Waheshimiwa Wabunge wote ni mashahidi katika Bunge lililopita linakuja na ombi kutoka wa Wabunge kuongeza fedha katika ule mfuko ambao Wabunge pamoja na watumishi wa Serikali wanakopa na ndiyo kwa maana kwamba tukaidhinisha hizo fedha za mikopo ili Wabunge watakaokuja pamoja na watumishi wa Serikali waweze kukopa.

Kwa hivyo huu ni ule mfuko wa kukopa Serikalini kwa ajili yetu pamoja na watumishi na watendaji.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

Kifungu 3003 -	<i>Financial Management</i>	Sh. 45,802,318,000
Kifungu 3004 -	<i>System and Internal Audit</i>	Sh. 4,690,031,200
Kifungu 3005 -	<i>Sub Treasury Arusha</i>	Sh. 247,325,000
Kifungu 3006 -	<i>Sub Treasury Coast</i>	Sh. 209,456,000
Kifungu 3007 -	<i>Sub Treasury Dodoma</i>	Sh. 277,207,000
Kifungu 3008 -	<i>Sub Treasury Iringa</i>	Sh. 217,400,000
Kifungu 3009 -	<i>Sub Treasury Kagera</i>	Sh. 217,807,000
Kifungu 3010 -	<i>Sub Treasury Kigoma</i>	Sh. 216,444,000
Kifungu 3011 -	<i>Sub Treasury Kilimanjaro</i>	Sh. 229,616,000
Kifungu 3012 -	<i>Sub Treasury Lindi</i>	Sh. 234,635,000
Kifungu 3013 -	<i>Sub Treasury Mara</i>	Sh. 226,532,000
Kifungu 3014 -	<i>Sub Treasury Mbeya</i>	Sh. 230,129,000
Kifungu 3015 -	<i>Sub Treasury Morogoro</i>	Sh. 271,572,000
Kifungu 3016 -	<i>Sub Treasury Mtwara</i>	Sh. 223,726,000
Kifungu 3017 -	<i>Sub Treasury Mwanza</i>	Sh. 235,847,000
Kifungu 3018 -	<i>Sub Treasury Rukwa</i>	Sh. 240,717,000
Kifungu 3019 -	<i>Sub Treasury Ruvuma</i>	Sh. 225,444,000
Kifungu 3020 -	<i>Sub Treasury Shinyanga</i>	Sh. 222,744,000
Kifungu 3021 -	<i>Sub Treasury Singida</i>	Sh. 224,644,000
Kifungu 3022 -	<i>Sub Treasury Tabora</i>	Sh. 238,880,000
Kifungu 3023 -	<i>Sub Treasury Tanga</i>	Sh. 220,718,000
Kifungu 3024 -	<i>Sub Treasury Manyara</i>	Sh. 223,889,000
Kifungu 7001 -	<i>Pension and Gratuity</i>	Sh. 562,498,000

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

Kifungu 1001 - *Administration and General*Sh. 9,661,240,000

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kifungu hiki kwa niaba ya Kamati ya PAC nataka kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa Waziri Mkuu pamoja na Waziri wa Fedha kwa kukubali ombi la PAC waongeze fedha za CAG mpaka shilingi bilioni 8 hii ni uungwana mlifanya kama mlivyoahidi.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*.....Sh. 1,500,026,000
 Kifungu 1003 - *Internal Audit Unit*.....Sh. 241,550,000
 Kifungu 1004 - *Ministerial Audit Division*.....Sh. 4,942,024,000
 Kifungu 1005 - *Regional and Local Govt.
Audit Division*.....Sh. 5,793,295,500
 Kifungu 1006 - *Value For Money Audit Division*.....Sh. 1,531,873,000
 Kifungu 1007 - *Treasury Audit Division*.....Sh. 1,775,112,000
 Kifungu 1008 - *Techn. Support, Research and
Consultancy*.....Sh. 1,129,038,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 21 - Hazina

Kifungu 2001 - *Government Budget Division*.....Sh. 45,701,010,000
 Kifungu 2002 - *Policy Analysis Division*.....Sh. 47,291,062,000
 Kifungu 2003 - *Treasury Registrar*.....Sh. 0
 Kifungu 4001 - *External Finance Division*.....Sh. 303,430,000
 Kifungu 7001 - *Poverty Eradication and
Empowerment*.....Sh. 6,727,692,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 23 – Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali

Kifungu 3003 - *Financial Management*.....Sh. 10,264,794,000

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

Kifungu 1001 - *Administration and General*.....Sh. 4,812,494,000
 Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*.....Sh. 5,768,516,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 50 - Wizara ya Fedha na Uchumi

Kifungu 1001- *Administration and General*Sh. 2,526,063,000

MHE. ATHUMANI S. JANGUO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kasma 50, kifungu 1001. Tangu mwaka jana na mwaka huu nilikuwa nikizungumzia juu ya ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Kisarawe na Mheshimiwa Waziri aliahidi kwamba mwaka huu atajenga Mahakama ya Kisarawe na vilevile kukarabati Mahakama za Wilaya. Nimeangalia katika kasma 40, 41, 64 na 71 sioni wapi fedha zimetengwa kwa ajili ya Mahakama hii, labda Waziri aniambie fedha hizo ziko mahali gani?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe maelezo kuhusu ujenzi wa Mahakama ya Kisarawe na ukarabati wa Mahakama ya Mwanzo pale. Pesa za kufanya kazi hiyo ziko chini ya *Legal Sector Reform Programme* na ipo katika ule utaratibu wetu wa kujenga Mahakama 20 Kisarawe ikiwa ni mojawapo.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts*.....Sh. 3,316,000,000

MHE. MASOUD ABDULLAH SALIM: Nakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti, item 6321 *Construction of IAA Modern Library Project*. Kuna shilingi bilioni 1.5, taarifa ambazo ninazo ujenzi huu umeshakamilika. Sasa hizo fedha zitapelekwa wapi au ni za nini?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli anavyosema Mheshimiwa Masoud, lakini tuna madai ambayo hatujakamilisha baada ya wajenzi kutoa *certificate* zao na sisi kuridhika kwamba wanahitaji kulipwa ndiyo kwa maana tumeweka hii hela hapa ili tuweze kukamilisha malipo hayo.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1003 - *Policy and Planning*.....Sh. 1,250,000,000

Kifungu 1004 - *Legal Services*.....Sh. 0

Kifungu 1005 - *Information Education and Communication*.....Sh.100,000,000

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1007 - *MCC Tanzania*.....Sh. 268,750,097,000

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, sub vote 1007 item 4156, *Zanzibar Rural Roads - Road Construction*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hizi zinajengwa na MCC. Tulikuwa na ahadi ya Mheshimiwa Waziri katika Bajeti ya Wizara ya Afrika Mashariki alituahidi kwamba barabara yangu ya Kenya - Chambani itajengwa. Hadi leo barabara hii haikujengwa, sasa

nilitaka kujua pesa hizi ni kwa ajili ya barabara gani, zile zile ambazo Mheshimiwa Waziri aliahidi hapo nyuma? Je, barabara yangu imo au haimo?

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, haya tuliyoyaweka humu ni ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa tuna miradi ya Afrika Mashariki. Sasa ile inakuwa kwenye Bajeti tofauti kabisa katika hizi ni kwa ajili ya barabara ambazo zinashughulikiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Sasa kama ukitaka tupate majibu kwamba hiyo ipo katika Bajeti ya Afrika Mashariki kwa kweli ningeomba niwasiliane na mwenzangu Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala ili kuweza kujua ni kiasi gani kimetengwa, lakini hizo nilitaka *nikuhakikishie* ni zile ambazo zimetolewa kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa kama barabara yako Mheshimiwa Waziri aliahidi kwamba iko ndani ya Afrika Mashariki itakuwa kwa kweli katika Bajeti ya Afrika Mashariki kwa sababu kuna miradi ambayo inaitwa *Regional Intergration* na inashughulikiwa Kiafrika Mashariki.

MWENYEKITI: Maalim Salim barabara yako haimo humo bwana.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

Kifungu 2003 - *Treasury Registrar*.....Sh. 850,000,000

Kifungu 6001 - *Financial Management*

Information Systems Division.....Sh. 2,129,135,000

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

(*Bunge linarudia*)

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Fedha na Uchumi na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa mwaka 2010/2011 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila ya mabadiliko yoyote. Hivyo naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali Makadirio haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. (*Makofi*)

MWONGOZO WA MWENYEKITI

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 68(7) wakati Waziri anajibu hoja ya Mheshimiwa Salim alisema kwamba Bajeti hii ni

kwa ajili ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nilifikiri Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni pamoja na Zanzibar au ni tofauti? Naomba ufanuzi wako. (*Makofit*)

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Tanzania Bara na Tanzania Visiwani. Lakini ndani ya Afrika Mashariki kuna nchi tano ambazo zinaunda *East African Community*. Sasa kwa sababu ya *efficiencies* tumekubaliana kwamba iko miradi ambayo itashughulikiwa na Bajeti ya Afrika Mashariki, sasa Bajeti ya Afrika Mashariki ina vyanzo vingi, ukiondoa hii ya Wamarekani kuna Wajerumani wanasadida kule, kuna nchi kadhaa chungu nzima ambazo zinasadida kule. Kwa hiyo, sikuwa na maana kwamba Zanzibar sio sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ielewewe kwamba Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed tunapozungumza Bajeti hii, ni Bajeti kwa kweli ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo ni pamoja na Zanzibar. Lakini tunazo pesa kwa sababu sisi wenye kama Tanzania tunachangia pia Bajeti ya Afrika Mashariki. (*Makofit*)

(*Hoja ilitolewa Iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Fedha na Uchumi kwa mwaka wa fedha 2010/2011 yalipitishwa na Bunge*)

MWENYEKITI: Nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Waheshimiwa Naibu Mawaziri wa Wizara hii, Katibu Mkuu, watumishi wote, Mkaguzi Mkuu wa Serikali na wataalamu wote tunawataenia kila la kheri katika kazi zao katika kutekeleza Bajeti hii kwa sababu Wizara hii ni muhimu sana na ni nguzo muhimu ya maendeleo ya nchi yetu.

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Fedha za Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2010 (*The Appropriation Bill 2010*)

(*Kusomwa Mara ya Pili*)

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali ya kiasi cha shilingi 11,609,557,584,000 kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya Matumizi ya Kawaada na Miradi ya Maendeleo itakayotekeliza kwa mwaka wa fedha 2010/2011 na kutumia fedha zitakazotolewa na Serikali kwa ajili hiyo sasa usomwe kwa mara ya pili. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kwamba hotuba ya Bajeti ya mwaka 2010/2011 ilibainisha shabaha na malengo ya Serikali ya kutumia shilingi 11,609,557,584,000 kwa mwaka wa fedha 2010/2011 kama ifuatavyo:-

Kwanza, Matumizi ya Kawaida shilingi 7,790,506,521,000 na pili, Matumizi ya Miradi ya Maendeleo shilingi 3,819,051,063,000. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako Tukufu limekwishajadili na kuitisha hoja mbalimbali na Waheshimiwa Mawaziri wakati walipowasilisha Makadirio ya Wizara zao hivyo basi madhumuni ya Muswada huu ni kuliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe Matumizi ya Serikali ya mwaka 2010/2011 ya jumla shilingi 11,609,557,584,000 kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo iliyokubaliwa na Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kwa mara ya mwisho kwa sababu hapa ndipo tunahitimisha mjadala wa Bajeti ya mwaka 2010/2011 kuwashukuru wote Spika, Naibu Spika, Wenyeverti, Wenyeverti wa Kamati na hasa Kamati yetu ya Fedha na Uchumi kwa michango yao na msaada wote ambao wametupa katika kipindi hiki ambacho mimi nimekuwa Waziri wa Fedha na Uchumi. Nawatakieni wote kheri na tuombe Mola atujalie wengi wetu turudi katika jumba hili tukufu mwezi Novemba mwaka huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(*Hoja ilitolewa Iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Nifafanue kidogo kinachoendelea ni nini. Kinachoendelea kinatawaliwa na Kanuni yetu ya 105 ambayo kwa faida ya wote nitaisoma kwa haraka; “Baada ya Bunge kukamilisha kazi ya kujadili na kuitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara zote kwa mwaka unaohusika, Muswada wa Fedha za Matumizi utawasilishwa Bungeni na kuitishwa mfululizo katika hatua zake zote.”

Sasa ndicho kitakachofuata baada ya muda si mrefu. Lakini fungu dogo la pili linasema; “Kwa madhumuni ya Kanuni hii Muswada wa Fedha za Matumizi maana yake ni Muswada wa Sheria wenye Makadirio na Mapato na Matumizi ya fedha za Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata.”

Fungu la tatu, Muswada wa Fedha za Matumizi hautapelekwa kwenye Kamati yoyote ya Kudumu wala Kamati ya Bunge zima na masharti kuhusu Muswada kusomwa mara ya kwanza hayatatumika. Kwa hiyo, ndiyo maana hakutakuwa na maoni ya Kamati na maoni ya Kambi ya Upinzani na wala hapatakuwa na Kamati ya Bunge Zima. Mwisho Muswada wa Fedha hautatangazwa kwenye Gazeti kabla haujawasilishwa Bungeni. Kwa kuzingatia Kanuni hiyo Katibu hatua inayofuata.

Muswada wa Sheria ya Fedha za Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2010 (*The Appropriation Bill 2010*)

(*Kusomwa Mara ya Tatu*)

(*Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa na Bunge*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kazi aliyoitaja Katibu hapa inakamilisha shughuli nzima ambayo tulianza tangu mwezi uliopita wa Juni kupitia Bajeti ya Serikali, kwa kupitisha Wizara kwa Wizara tumemaliza zote na tumetunga sasa ile Sheria ambayo inawezesha Matumizi ya Serikali kufanyika kama taratibu zinavyotaka. Kwa hiyo, naomba nichukue fursa hii kuwapongezeni sana kwa kazi kubwa na nzito ambayo tumeifanya katika kushughulikia Bajeti ya mwaka 2010/2011 na katika wakati mfupi amba ni rekodi haijapata kutokea. (*Makofî*)

Sasa tumewasikia Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga na wengine wakiaga hapa na kwamba yamebaki masaa machache na siku ya Ijumaa Mheshimiwa Rais atakuja hapa kwa ajili ya kufunga Bunge hili na mimi na Wenyeviti wenzangu tumekuwa tukikaa hapa kumsaidia Spika na kwa kuwa tunafika hapa mwisho mwisho ni vizuri nikasema maneno mawili, matatu kwa dakika mbili kwa niaba yangu mwenyewe na kwa niaba ya Wenyeviti wenzangu wawili Mheshimiw Jenista Mhagama na Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid. (*Makofî*)

Naomba tuwashukuruni sana, hasa mimi kwa kuniamini na kunichagua pamoja na wenzangu ili tumsaidie Mheshimiwa Spika na Naibu Spika katika kuendesha mambo katika meza hii kuu. Mambo hapa huwa si mepesi, ni mazito lakini nawashukuruni sana kwa vile ambavyo imani yenu na ushirikiano wenu, umoja, upendo umekuwa mkubwa sana kwetu. Namshukuru kipekee Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge, Kambi zote mbili na hasa Kambi ya Upinzani mlitupa ushirikiano wa kila aina, kwa kweli nawashukuruni sana sana sana. Lakini pia kipekee namshukuru sana Spika, Mheshimiwa Samuel Sitta na Naibu Spika Mheshimiwa Anne Makinda hasa kwa kunipa fursa kadhaa za kujifunza mambo mengi ya Bunge ndani ya nchi na nje ya nchi. (*Makofî*)

Mwaka 2006 niliongoza Kamati Ndogo ya kupitia Masuala ya Kanuni ambayo ilikuwa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Athuman Janguo, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mheshimiwa Nimrod Mkono na kwa kweli kazi yetu kubwa ndio ilipelekeea kutoka kwa Kanuni za mwaka 2007 ambazo zilibadili mambo mengi katika Bunge letu ambalo sasa linaitwa za viwango, mchango wetu ulikuwa mkubwa katika jambo hilo nashukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kazi hiyo ndipo kipindi cha Maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kilianza, masuala ya *CDCF* yalitokea na mabadiliko mengine yalitokea hapo. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge, lakini pia nawashukuru Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wote ambavyo nilipata nafasi ya kuliwakilisha Bunge

hili katika Jumuiya ya Madola ambako mimi ni Mjumbe wa *CPA International* Kamati ya Utendaji nikiwa nawakilisha nchi za Rwanda, Uganda, Kenya, Tanzania, Mauritius na Seychelles. Mjumbe wenu katika Kamati hiyo ya Umoja wetu wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola ni mimi na kwa hiyo, ninakaa na Maspika wengi kule wa India, Canada, Uingereza na sehemu nyingine kwa maana hiyo nimejifunza mambo mengi sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, lakini mwisho naomba nimshukuru Katibu wa Bunge na watumishi wote wa Bunge kwa kurahisisha kazi yangu na wenzangu hasa Wenyeviti tulipokuwa hapa Bungeni. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, mwisho nimwombe Mwenyezi Mungu azibariki nia zenu nyote hasa mnaogombea, nawaombeeni kura kwa wapigakura wenu nyote na wale ambaao hawagombei nawaombea maisha marefu na kila la kheri. Nimesema maneno haya si kwamba sitarudi hapa tena lakini nimeona niseme mapema maana tupo mwisho mwisho. Nawashukuru sana na kwa kipekee. (*Makofi/Kicheko*)

Mwisho kabisa tangazo, Waheshimiwa Wabunge wa Mikoa ya Manyara, Arusha na Kilimanjaro wanaombwa na ndugu zetu waandishi wa habari kutoka *Radio Kili FM* ambayo iko Kanda ya Kaskazini waonane nao kesho kwa ajili ya kutengeneza vipindi maalum ambavyo vinaweza vikawasaidia vilevile katika kufikisha ujumbe kwa wapigakura wetu wote. (*Makofi*)

Baada ya maelezo hayo Waheshimiwa Wabunge niwahakikishie *Order Paper* ya leo imekamilika na mambo yote yaliyopangwa tumeshayafanya kazi, kwa jinsi hiyo naomba sasa kuahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

(*Saa 1.30 usiku Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Jumatano, Tarehe 14 Julai, 2010 saa tatu asubuhi*)

